
	<p style="text-align: center;">JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI</p>	
<p style="text-align: center;">Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora Machel Na. 16, S.L.P. 9080, 11101 Dar es Salaam. Simu ya Upepo: „Ukaguzi“ D“Salaam, Simu: +255(022)2115157/8, Tarakishi: +255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz</p>		

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. FA.27/249/01/2016/2017/42

28 Machi 2018

Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 9120
Barabara ya Barack Obama, Na.1
11400, DAR ES SALAAM.

**YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI
MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA
YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mabadiliko na kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya 11(4) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuiwasilisha Bungeni kulingana na matakwa ya sheria.

Wako Mwaminifu,



Prof. Mussa Juma Assad.

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(Kama ilivyoanzishwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) Majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi ya Umma, Na. 11 ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Dira ya Ofisi

Kuwa Taasisi ya Hali ya juu katika ukaguzi wa sekta ya umma.

Dhamira ya Ofisi

Kutoa huduma za ukaguzi wa sekta ya umma zenye ubora wa Hali ya juu zinazoimarisha utendaji, uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Misingi Yetu

Kutopendelea: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki bila upendeleo.

Ubora: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ukaguzi.

Uadilifu: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha maadili ya kazi ya kiwango cha juu na kuheshimu sheria.

Kujali Watu: Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa

na watumishi wenye uwezo na kuongeza tija.

Ubunifu:

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.

Matumizi bora ya Rasilimali za Umma:

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI	iv
DIBAJI	vii
MUHTASARI.....	viii
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA.....	1
SURA YA PILI	6
AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA	6
SURA YA TATU.....	9
MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILİYOPITA	9
SURA YA NNE	28
MASUALA YALIYOPEWA UZITO KATIKA UKAGUZI.....	28
SURA YA TANO	102
MAPITIO YA MIKAKATI NA UENDESHAJI WA KIUFANISI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA	102
SURA YA SITA	141
UKAGUZI MAALUM.....	141
SURA YA SABA	168
UKAGUZI WA UFANISI WA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA NCHINI	168
HITIMISHO	190
VIAMBATISHO	191

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Kuondolewa kwa Mzabuni Mwenye Gharama Ndogo	68
Jedwali 2: Dhamana Pungufu zilizowekwa dhidi ya mikopo..	70
Jedwali 3: Makato ya kodi pamoja na michango kwenye Mfuko Mkuu.....	99
Jedwali 4: Ukokotozi wa uwiano wa ukwasi	143
Jedwali 5: Kutolipa Madeni yenye Riba kwa Wakati (katika mamilioni ya Shilingi)	156
Jedwali 6: Udhaifu katika kusimamia madeni	156

SHUKRANI



Ninalazimika kuanza dibaji hii kwa maneno ya shukurani kwa Ofisi, watu na wafanyakazi mbalimbali ambao kwa kiasi kikubwa wamechangia kwenye mafanikio ya Ofisi yangu kutimiza matakwa ya Kikatiba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake ya mwaka kwa Rais mwisho wa mwezi Machi kila mwaka.

Kwa furaha kubwa natumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dk. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa msaada wake mkubwa na juhudi binafsi kuhakikisha Ofisi yangu inatimiza jukumu lake kikatiba.

Rasilimali za kifedha, kimfumo na watu ni muhimu sana katika jitihada za kitaasisi, hivyo, nalazimika kutoa shukurani zangu za dhati kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kamati za Bunge kwa kutimiza wajibu wao wa kuwezesha uwepo wa rasilimali kwenye Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha wa 2016/17. Kwa namna yoyote, haya yasingewezekana bila ushirikiano na juhudi za pekee za Wizara ya Fedha ambao tunawashukuru kwa namna ya pekee.

Mwisho, sina budi kushukuru kazi nzito inayofanywa na askari wetu wa miguu ambao ni wakaguzi waliopo katika ngazi za chini kabisa za taasisi yetu pamoja na wafanyakazi wengineo. Nimeweza kutoa ripoti hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwasababu wakaguzi hawa walifanya kazi yao katika kiwango cha juu na kuwasilisha ripoti zao kwa wakati na wakati mwingine katika mazingira magumu.

Nilipowasilisha ripoti zangu mwezi Machi mwaka jana Rais alimuelekeza Waziri Mkuu kuhakikisha yaliyowakilishwa kwake

siku ile yanafikishwa pia kwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa. Kufuatia juhudi za Waziri Mkuu hili liliwezekana na naamini mwamko ambao nimeuona katika kaguzi za Halmashauri na Wilaya kwa mwaka huu wa ukaguzi umechangiwa kwa karibu na kujitoa kwa hali ya juu kulikoonyeshwa na Wakuu wa Mikoa.

Kwa Wabia wetu wa Maendeleo, ningependa kutambua mchango wao mkubwa wa kuendelea kuzifanya kazi za ukaguzi katika Ofisi yangu kuwa za kisasa kwa kudhamini mafunzo na kutoa zana muhimu za na msaada wa kiufundi.

Tukiwa tunajitahidi kudumisha viwango na ubora wa ripoti zetu, napongeza michango ya makampuni binafsi ya ukaguzi ambayo yamekuwa yakifanya kazi nasi kwa bidii na kwa weledi. Mchango wao kuelekea maandalizi ya ripoti hii ni muhimu na wenye thamani kubwa.



Prof. Mussa Juma Assad

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

28 Machi 2018

DIBAJI

Ninayo furaha na heshima kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka 2016/2017. Hili linatekeleza matakwa ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sura ya 34 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Ripoti hii ni mkusanyiko wa masuala muhimu yaliyojitokeza katika kaguzi za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017. Pia, ripoti hii imejumuisha mapendekezo yaliyotolewa kwa wasimamizi wa mashirika haya ili kupunguza mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi.

Nimekagua masuala ya kimkakati na ufanisi katika utendaji wa Mashirika ya Umma sita (6) kwa lengo la kujibu maswali muhimu ya kisera au changamoto muhimu na vikwazo vya kiutendaji ambavyo vinaathiri mikakati, mipango, na ufanisi. Matokeo ya kaguzi hizi yamejumuishwa katika Sura ya Tano ya ripoti hii.

Ripoti pia inajumuisha matokeo ya kaguzi maalumu na kaguzi za kiuchunguzi (forensic audit) kwa Mashirika ya Umma sita (6) zilizoombwa na wadau mbalimbali. Muhtasari wa matokeo ya kaguzi hizi yamejumuishwa katika Sura ya Sita ya ripoti hii.

Kama ilivyokuwa kwa mwaka uliopita, katika Sura ya Saba ya ripoti hii, nimekagua na kutathmini ufanisi pamoja na changamoto za sekta ya mafuta na madini na gesi Tanzania.

MUHTASARI

i. Utangulizi

Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi masuala mahususi yaliyojadiliwa kwa kina katika ripoti hii na ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti ya Taasisi husika ili kuhakikisha kuna ongezeko la ufanisi katika utendaji wa Mashirika ya Umma.

ii. Aina na Muelekeo wa Hati za Ukaguzi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 2016/2017 nilikagua na kukamilisha kaguzi za mashirika 188 ikijumuisha maoni 52 ya kaguzi za miaka ya nyuma yaliyotakiwa kukaguliwa. Hata hivyo, niliweza kutoa maoni ya ukaguzi kwa mashirika 105 pekee. Kati ya kaguzi za mashirika 105 zilizokamilika na kutolewa hati ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, mashirika manne (4) yalipata hati yenye mashaka wakati mashirika 101 yalipata hati zinazoridhisha. Hati isiyoridhisha na hati mbaya hazikutolewa kwa shirika lolote au taasisi nyingine za umma katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha.

iii. Muhtasari wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita

Katika kufuatilia utekelezaji wa kaguzi za miaka iliyopita nilibaini kwamba, kati ya mapendekezo 33 ni mapendekezo 15 (sawa na asilimia 31) ndio ambayo yametokelezwa wakati mapendekezo 12 (sawa na asilimia 25) hayakutekelezwa; hivyo, kubakiza mapendekezo 21 (sawa na asilimia 44) yakiwa katika hatua za utekelezaji. Mapendekezo haya yanapatikana katika sura ya tatu (3) ya ripoti hii.

Miongoni mwa mapendekezo ya kaguzi zilizopita ni: Benki ya Azania kutokuwa chini ya usimamizi wa Msajili wa Hazina, Msajili wa Hazina hajaweza kuonyesha uhalali wa kisheria katika umiliki wa PRIDE; Kukosekana kwa mkataba na dhamana kwa mkopo wa Shilingi bilioni 44.29 uliotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF); Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) kutofikia

kiwango cha chini cha mtaji; Kuporomoka kwa wa ufanisi kibiashara kwa Shirika la Posta Tanzania (TPC); tatizo la uendelevu wa Benki ya Twiga, kuchelewa kutekeleza mpango mkakati kuhusiana na ujenzi wa nyumba za walimu; Wizara ya Nishati kutokulipa deni la pango la Shilingi bilioni 1.117 kwa Kampuni ya Umeme Tanzania (TANESCO); Pamoja na upunjifu katika ulipaji wa kodi ya pango uliofanya na Mlimani City Holding Limited kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

iv. Maswala Yaliyopewa Uzito katika Ukaguzi

Katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS), nimebaini vyeti halisi vya ufanisi 3,911 vilivyotolewa na SGS ambayo vimeisha muda wake wa matumizi. Hata hivyo, TBS haikufanya uchunguzi wa jambo husika kuona kama wanunuzi wenye kumiliki vyeti hivyo waliingiza bidhaa nchini; na kama vyeti hivyo vilifanyiwa Ukaguzi wa Mwisho (Destination Inspection) na adhabu kutolewa. Pia, nimebaini kutokuwapo kwa maafisa wa TBS katika vituo zaidi ya 18 vya uingizaji bidhaa ili kuangalia ubora wa bidhaa zinazolingia nchini.

Nimebaini kuwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kuna ankara za malipo za kiasi cha Shilingi bilioni 1.86 zilizokataliwa na kampuni za bima, pamoja na ankara za malipo za kiasi cha Shilingi milioni 241.97 ambazo zilipelekwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa ajili ya dawa ambazo wagonjwa hawakupewa.

Kwenye Shirika la Posta Tanzania (TPC), nilibaini ofisi 83 za posta ikijumuisha ambazo zimekwishapewa kibali hazijaunganishwa kwenye mfumo wa mapato wa Netsmart; Hivyo, mapato kurekodiwa kwa njia ya kawaida (manually). Kutokana na kukosekana kwa upatanisho kati ya fedha zinazopokelewa, ankara zilizotolewa kwa wateja na mapato yanayoripotiwa makao makuu, mapato ya EMS kwa mujibu wa mfumo wa Netsmart yametofautiana na mapato yaliyoripotiwa kwenye taarifa za fedha za TPC kwa kiasi cha Shilingi milioni 607.

Nimebaini kuwa waingizaji bidhaa kutoka nje, wamefanikiwa kuingiza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1.94 kupitia vituo mbalimbali vya uingizaji bidhaa kwa kutumia vibali feki bila kubainika na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), hali inayoonyesha kuwapo kwa mapengo katika taratibu za udhibiti au kuwapo kwa hujuma ndani ya Mamlaka ya Chakula na Dawa.

Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) ni moja ya wanahisa wa Star Media Tanzania Limited, lilimiliki asilimia 35 ya mtaji. Asilimia 65 iliyobaki inamilikiwa na kampuni ya kichina ya Star Communication Network Technology Limited. Nimebaini kuwa TBC haikuwahi kupokea gawio kutokana na uwekezaji wake katika Star Media tangu mwaka 2013, ambayo inapingana na malengo ya uwekezaji katika kampuni husika.

Kampuni Hodhi ya Reli (RAHCO) ilifanya upembuzi yakinifu kwa baadhi ya miradi yake inayopangwa kufanyika kwa gharama ya Shilingi bilioni 20.1. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi hiyo haukuwa wenye mafanikio kutokana na kukosekana kwa fedha. Pia, RAHCO imetumia kiasi cha Shilingi bilioni 1.61 kwenye miradi isiyotekelezeka ambayo haijakamilika na imetelekezwa.

Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ina kiasi cha dawa kilichoisha muda wake chenye thamani ya Shilingi bilioni 4.43 ambacho ni sawa na asilimia 3.4 ya gharama za mauzo ikilinganishwa na kiwango stahiki cha asilimia 1. Kwa mujibu wa Menejimenti ya MSD, kuwapo kwa dawa zilizoisha muda wake kumesababishwa na kubadilika kwa teknolojia, kupita kwa wakati, kubadilika kwa miongozo ya matibabu, uwezo mdogo wa manunuzi wa wateja wa MSD pamoja na washirika wa maendeleo/wahisani kununua dawa zinanazofanana na zilizopo.

Pia, nimebaini Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imenunua hekta 500 kutoka kwa iliyokuwa Mamlaka ya Uendelezaji wa Makao Makuu (CDA) katika eneo la Ihumwa kwa ajili ya ujenzi wa

bandari kavu kwa makadirio ya gharama za Shilingi bilioni 12.6 bila kufuata taratibu sahihi, ikiwa ni pamoja na ruhusa (approval) ya Bodi ya Wakurugenzi na uthaminishaji wa ardhi iliyonunuliwa. Nimebaini kuwa, Machi 2017, TPA ilifanya malipo ya awali ya Shilingi bilioni 6.3 ikiwa ni asilimia 50 ya mauzo husika ambayo ni kinyume na makubaliano kati ya CDA na TPA. Katika mkutano uliofanyika tarehe 4 Novemba 2016 ilikubalika kuwa ardhi ithaminishwe kabla ya fedha kulipwa.

Mikopo Chechefu (NPL) ya Benki ya Maendeleo ya TIB imeongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha mwaka mmoja. Kufikia tarehe 31 Desemba 2016, uwiano wa mikopo hiyo ulifikia asilimia 35 ikilinganishwa na asilimia 14 kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2015. Ongezeko hili ni kubwa ikilinganishwa na ongezeko la kisekta la asilimia 24 kama ilivyoripotiwa na Taarifa ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iliyotolewa mwezi Juni 2016 na uwiano elekezi wa mikopo chechefu wa asilimia 5. Kuongezeka kwa mikopo chechefu kunaonyesha kupungua kwa ubora wa mikopo ambayo imetolewa na Benki.

Benki ya Maendeleo ya TIB ilidhamiria kubatilisha mikopo mingi yenye thamani ya Shilingi bilioni 94 inayohusiana na miradi isiyofanya vizuri ambayo ilitakiwa kulipwa ndani ya siku 30 tangu kupokea barua ya kubatilisha mikopo hiyo. Ukubwa wa mikopo iliyobatiliswa unaonyesha kukosekana kwa ufuatiliaji wa miradi isiyofanya vizuri ambayo ingeweza kugundulika katika hatua za awali. Mpaka nafanya ukaguzi mwezi Machi 2017, ni kiasi cha Shilingi bilioni 2.9 tu ambazo zimepatikana, ikiwakilisha asilimia 3 tu ya kiasi kilichobatiliswa.

v. **Tathmini ya Ufanisi wa Kimkakati na Uendeshaji wa Mashirika ya Umma**

Ukaguzi niliofanya kutathmini ufanisi wa utendaji wa Mashirika ya Umma ulibainisha masuala makuu yafuatayo:

Katika Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kupitia kampuni ya Biotech, nimebaini kuwa jumla ya lita 236,420 zenye thamani ya Shilingi bilioni 3.12 zilisambazwa kwenye mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kati ya mwezi Agosti na Novemba 2017, ambapo kila Halmashauri ilitengewa kiasi maalum cha lita za viudadu. Kutoka kwenye sampuli ya Halmashauri 57 nilizozitembelea, nilibaini kuwa ni lita 25,609 tu ambazo zimepuliziwa kati ya lita ambazo zilisambazwa, ambazo ni sawa na asilimia 28 ya jumla ya viudadu vilivyosambazwa.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inatekeleza mradi wa Mfumo wa Kuhakiki Mapato ya Kampuni za Simu (Telecom Revenue Assurance System)(TRAS) ambao unatarajiwa kutoa uhakika wa mapato ya kampuni za simu kwa Serikali. Mradi ulitarajiwa kuwa umekamilika kufikia tarehe 27 Septemba 2017. Hata hivyo, mpaka nafanya ukaguzi mwezi Oktoba 2017, mradi haukuwa umekamilika na hakukuwa na mabadiliko ya tarehe ya kukamilisha kwa mradi. Hali hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama kwa TCRA na Serikali.

Kwenye Kampuni ya Umeme Tanzania (TANESCO) nimebaini kuwa, eneo la Ubungo Complex lilipewa Songas mwaka 2004 wakati Songas ilipoanza shughuli zake nchini Tanzania. TANESCO ilipatiwa hisa 10,000 katika kampuni ya Songas kama malipo kwa ajili ya Ubungo Complex; pia, Songas ilichukua yaliyokuwa madeni ya TANESCO yaliyotokana na ununuzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa gesi pamoja na mitambo husika iliyopo Ubungo Complex. Hata hivyo, hakuna ushahidi unaoonesha kuwa Ubungo Complex pamoja na mali nyingine ilizopewa Songas Limited zilithaminishwa kabla uhamishaji haujafanyika.

Nimebaini kuwa Serikali imeingia mkataba wa kukopa na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na kampuni ya Songas Limited. Mkataba ulielekeza kuwa gharama za mradi zilikuwa Euro milioni 392. Kwa mujibu wa mkataba, Serikali ilitakiwa kukopa Euro milioni 235.1 na kuwekeza katika mradi; pia kutoa kiasi cha Euro milioni 0.6 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato. Pia, Serikali ilichukua mkopo wa Euro milioni 50 kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na kuikopesha Songas. Uwekezaji uliofanywa na Serikali katika mradi ni Euro milioni 285.7 ambayo ni asilimia 73 ya gharama za mradi ingawa hakuna sehemu katika mkataba inayoonyesha stahiki ya Serikali katika mradi husika.

Nimebaini kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa dhamana kwa mkopo uliotolewa kwa kampuni ya Tanzania Finance Development Limited ili iweze kujipatia hisa kwenye kampuni ya Songas Limited. Hata hivyo, nimeshindwa kupata uhusiano uliopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Tanzania Finance Development Limited, usajili wa kampuni husika pamoja na umiliki wake ambavyo vilipelekea Serikali kutoa dhamana ya mkopo huo.

vi. Kaguzi Maalumu na Kaguzi za Kiuchunguzi

Katika mwaka wa ukaguzi, mambo yafuatayo yalibainika katika kaguzi maalum na kaguzi za kiuchunguzi:

Katika Star Media, imebainika kuwa katika Makubaliano ya Utendaji, mali zitakazotumika kwenye mradi zitapata msamaha wa kodi. Ukaguzi wa Kitabu cha Orodha ya Usajili wa Mali kwa mwaka 2014, sampuli ya vifaa vya mtandao imebaini vifaa vyenye thamani ya Shilingi bilioni 34.4 viliingia nchini na kufungwa. Hata hivyo, vifaa hivyo havikuonekana nilipotembelea maeneo husika; ingawa katika Orodha ya Mali vinaonekana vimefungwa.

Zaidi, Star Media imekuwa ikitengeneza hasara kwa zaidi ya miaka 7 mfululizo ambayo imekuwa ikichangiwa na kutoza uchakavu kwenye ving'amuzi vilivyouzwa kwa wateja tofauti na

sera za makampuni mengine ambayo yanafanya biashara hiyo kama vile Azam Media na DSTV. Hii ni kwa kuwa ving'amuzi vikiuzwa, Star Media haiingii gharama za matengenezo wala haiwajibiki kumpatia mteja king'amuzi kipya pindi cha kwanza kinapopata matatizo. Jumla ya Dola za Marekani milioni 30.11 zimetozwa kutoka kwenye faida kwa jumla ya miaka 6 kuanzia 2010 mpaka 2015.

Pia, kifungu cha 1.4 na 1.5 cha Randama ya Makubaliano kati ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Star Times kinaainisha mtaji wa ushirikiano kuwa ni Dola za Marekani milioni 1 utakaotokana na hisa 10,000 zenye thamani ya Dola za Marekani 100 kila moja. Mgawanyo wa mtaji ulikuwa ni asilimia 35 kwa TBC na asilimia 65 kwa Star Times. Mtaji wa Dola za Marekani milioni 1 ulipanga kupatikana kwa TBC kutoa Dola za Marekani 350,000 na Star Times kutoa Dola za Marekani 650,000. Nimebaini kuwa Star Times haikutoa fedha za mtaji kama sehemu yake ya umiliki wa Star Media.

Nimebaini pia kuwa Star Media ilijipatia mikopo ya Dola za Marekani milioni 10.5 bila TBC kufahamu na mikopo hiyo haikuwekwa wazi katika taarifa za fedha za Star Media kwa mwaka 2014. Ukaguzi wa Makubaliano ya Mkopo umebaini kuwa mikopo hiyo ilipatikana kutoka Star Times International Holdings of China, ambayo ni kampuni dada ya Star Times. Mikopo hiyo ilitolewa ili Star Media ipate mtaji wa kujiendesha kwa riba ya asilimia 8.5 ambapo mali za Star Media ziliwekwa kama dhamana ya mkopo huo.

Ukaguzi maalum wa Mfuko wa Hisani wa Kuendeleza Sekta ya Korosho (CIDTF) umebaini kutokuwasilishwa kwa tani 837 za Salfa zenye thamani ya Shilingi milioni 803.52 zitokanazo na mkataba ulioingwiwa na kampuni ya Hammers Incorporation Ltd kwa ajili ya kusambaza tani 3,000 za Salfa. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji wa mkataba, mzabuni alisambaza jumla ya mifuko yenye jumla ya uzito wa tani 2,307 na kuacha kuleta mifuko yenye jumla ya

uzito wa tani 693. Pia, nimebaini kuwa ujazo wa baadhi ya mifuko ulipunguzwa na kusababisha upungufu wa tani 144. Ubadhirifu huu umesababisha upotevu wa Shilingi milioni 837 na hasara ya tani 803.52. Pia, nimebaini kuwepo kwa viwatilifu vilivyoisha muda wake vyenye thamani ya Shilingi milioni 594.03 vilivyopo kwenye maghala ya Mtwara Mjini, Naliendele na Tandahimba.

Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) iliingia mkataba na kampuni ya Wallis Trading Inc. Ili kukodi ndege aina ya AIR BUS A-320. Nilibaini kuwa, ingawa kipengele cha 4.5 cha mkataba kinaelekeza ukaguzi wa ndege ufanyike kabla ya kuingia kwenye mkataba, ukaguzi uliofanyika uligundua kuwepo kwa matatizo makubwa ya kiufundi, hivyo kutakiwa kufanyiwa matengenezo makubwa kwa kipindi cha miezi saba kwa gharama ya Dola za Marekani 370,000 kwa mwezi; hivyo, kufikia jumla ya Shilingi milioni 2.59 kwa kipindi chote cha matengenezo. ATCL ililipa gharama hizo kwa kuwa ilishaingia mkataba wa kukodisha ndege.

Ukaguzi wa Vocha za Malipo kwa miezi mitatu (2014, 2015 na 2016) umebaini kuwa TANCOAL imelipa gharama za Shilingi milioni 940.34 kwa shughuli ambazo hazihusiani moja kwa moja na uchimbaji wa makaa ya mawe na shughuli nyingine za uendeshaji kwa mujibu wa Makubaliano ya Ubia. Uchambuzi zaidi wa Vocha hizo umebaini jumla ya kiasi cha Dola za Marekani milioni 3.36 kimetumika kwenye shughuli za uchimbaji ambazo hazihusiani na TANCOAL.

vii. Ukaguzi wa Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Madini

Ukaguzi wangu wa Sekta ya Madini umebaini mambo muhimu yafuatayo:

Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017 na Sheria ya Mamlaka ya nchi Kuhusu Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017 hazina kanuni ambazo zingerahisisha utekelezaji wa sheria hizo.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana nafasi finyu ya kupata taarifa mbalimbali kutoka kwa makampuni ya Mafuta, Gesi na Madini kwa kuwa Sheria mama za Madini na Gesi hazijampa nguvu na mamlaka ya moja kwa moja ya kupata taarifa zinazohusiana na uzalishaji na mauzo ya maliasili hizo.

Matumizi ya kimtaji ambayo yanaruhusiwa kupunguzwa wakati wa kukokotoa kodi kwa mujibu wa mikataba iliyoingiwa na makampuni ya madini na Sheria ya Kodi ya mwaka 1973 hayakuwahi kukaguliwa na Tume ya Madini ili kuangalia usahihi wa gharama za uzalishaji wakati wa kutoa leseni maalum za uchimbaji kama inavyotakiwa na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

Kifungu cha 22(a) cha Mfano wa Makubaliano ya Uzalishaji wa Pamoja wa Mafuta na Gesi (MPSA) kinataka mali zote zinazomilikiwa na mwekezaji na kutumika katika shughuli za uchimbaji mafuta na gesi kuwa mali za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kadri TPDC litakavyoona inafaa baada ya mkataba kuisha au kuvunjika au pale gharama zote za mali zinapokuwa zimerudishwa na mwekezaji kutegemea kipi kitaanza. Hata hivyo, Ukaguzi wa Mikataba ya Madini umebaini kuwa hakuna uhamishaji wa mali kwa serikali pale ambapo gharama zote za mali zilikuwa zimerudishwa na wawekezaji. Zaidi ya hayo, hakuna ushahidi unaoonesha kuwa misamaha ya kodi na marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inaisaidia Serikali katika kukusanya kodi na mirabaha kutoka kwa makampuni ya madini.

Nimebaini kuwa uchambuzi na uthaminishaji wa madini ya vito unafanya na TANSORT na maafisa wa wizara ya madini bila kuwa na muongozo na viwango vya uchambuzi na uthaminishaji ili kuwa na kuwa na matokeo yenye kufanana na kuondoa makosa ya kibinadamu.

Pia, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) haina mfumo unaoweza kuwasaidia kufanya uchambuzi wa gharama na kubaini ikiwa miamala iliyofanyika kati ya makampuni yanayohusiana ilifanywa kwa taratibu wa kibiashara na hakukuwa na upangaji wa bei kwa nia ovu.

Ukaguzi wa Kampuni ya Tini ya Kyerwa umebaini kuwa uchambuzi na usafishaji wa madini ya Tini wakati wa kununua unafanywa kwa njia ya mikono, hivyo kuongeza uwezekano wa kuwapo kwa makosa ya kibinadamu na kupata thamani isiyo sahihi kwa madini ya Tini ghafi yaliyonunuliwa. Kwa mfano, mwezi Oktoba 2016, wakati Kampuni ya Kyerwa ikiuza Tini kwa kampuni ya African Top Minerals, ilibainika kuwa ilikuwa imenunua Tini ghafi ambayo imesafishwa tani 26.739 lakini uchambuzi na uthaminishaji uliofanyika wakati wa mauzo ulionesha tani 18.0652 pekee za Tini ghafi ndizo safi, na tani 8.3138 zilizobaki zilionekana kuwa chafu. Bei ya kuuzia Tini ghafi ilikuwa Shilingi 18,000 kwa kilo ambayo ilileta hasara ya Shilingi milioni 150.

Nimebaini kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) haina mfumo unaoiwezesha kufanya ulinganisho wa gharama ili kuweza kubaini kama miamala iliyofanyika kati ya kampuni husika haijazidisha au kupunguza faida za makampuni ya madini.

Tume ya Madini imepewa mamlaka ya kukagua mitaji iliyowekezwa na kampuni za madini na gharama za uendeshaji kwa ajili ya kupata taarifa za kodi na kuipatia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili iweze kuchukua hatua. Hata hivyo, nimebaini kuwa hakuna mwongozo unaotoa maelekezo ya namna TRA wanavyotakiwa kufanyia kazi matokeo ya ukaguzi ya Tume.

Ukaguzi wangu wa Sekta ya Gesi na Mafuta umebaini mambo muhimu yafuatayo:

Wizara ya Nishati iliweka vitalu 4/1B na 4/1C kwa ajili ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kupitia Tangazo la Serikali Na.

184 la tarehe 20 Mei 2016. Hata hivyo, leseni ya utafutaji wa gesi imetolewa kwa TPDC lakini mpaka sasa Serikali haijatoa pesa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Pia, hakuna makubaliano rasmi miongoni mwa wadau ambayo yangesimama kama mwongozo wa uendeshaji wa vitalu hivyo.

Kampuni ya British Group Plc inapinga kutozwa kodi ya ongezeko la mtaji ya Shilingi trilioni 1.4 kufuatia kampuni hiyo kununuliwa na kampuni ya Royal Dutch Shell Plc tarehe 27 Januari 2016. Pia, kampuni hiyo imepinga kulipa moja ya tatu ya kodi iliyokokotolewa ya Shilingi bilioni 381.

Mfano wa Makubaliano ya Uzalishaji wa Pamoja wa Mafuta na Gesi (MPSA) wa mwaka 2008 na 2013 unatambua uhitaji wa kuwepo kodi itokanayo na faida ya ziada (Windfall Tax). Hata hivyo, Sheria ya Kodi haina vifungu vyenye kushughulikia kodi itokanayo na faida ya ziada hivyo kufanya utekelezaji wa matakwa ya mkataba kushindikana.

Ukaguzi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) umebaini kuwa, kinyume na kifungu cha 44(5) cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 ambayo inataka kampuni ya mafuta ya nchi kuwa na ushiriki usio chini ya asilimia 25, Shirika husika limekuwa na ushiriki wa chini ya asilimia 25 kwenye haki za uchimbaji ambazo zimeshatolewa. Pia nimebaini ibara ya XII ya Makubaliano ya Uzalishaji wa Pamoja wa Mafuta na Gesi (PSA) ya Songosongo inataka mrabaha kukokotolewa kutoka kwenye gawio la faida ya Serikali kinyume na kifungu cha 113 cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 inayotaka wamiliki wa leseni na wachimbaji kulipa mrahaba kwa serikali.

Ukaguzi wa ununuaji wa asilimia 40 katika kampuni ya Pan African Energy Tanzania (PAET) uliofanywa na kampuni ya Swala Oil & Gas Tanzania umebaini kuwa Makubaliano ya Uzalishaji wa Pamoja wa Mafuta na Gesi PAET Songosongo yamekuwa na mapungufu mengi. Serikali inashauriwa kuendelea na msimamo

wake wa kusimamisha mauzo hisa za PAET kwa Swala Oil & Gas Ltd mpaka pale mapungufu hayo yatakapotatuliwa.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

1.0 Uanzishaji wa Ofisi ya Ukaguzi Kisheria

Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebisha mara kwa mara). Ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 na kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya Mwaka 2011 inamtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma angalau mara moja kwamwaka wa fedha.

Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu ana mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha au kaguzi nyingine katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kama ilivyoainishwa kwenye vifungu Na. 26, 27, 28 na 29 vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008. Kifungu cha 12 cha Sheria hiyo kinampa mamlaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa maoni kwa nia ya:

- Kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyokuwa na tija;
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya umma;
- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu, udanganyifu, au rushwa kuhusiana na fedha na rasilimali za umma;
- Kuongeza uchumi, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma.

Mashirika na Taasisi Nyingine za umma nchini zinafanya kazi kwa kutumia mifumo ya uhasibu ambayo inayalazimu kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSASs). Miongozo zaidi ya kisheria inayotumika kuandaa hesabu ni pamoja na Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 au sheria yeyote iliyopitishwa na Bunge ya kuanzishwa kwa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008.

Sheria namba 418 ya Msajili wa Hazina na kifungu cha 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma namba 16 ya mwaka 1992 zinahusiana na majukumu ya Msajili wa Hazina katika Mashirika ya Umma. Sheria hizo zinaelezea kuwa Msajili wa Hazina ana kazi na jukumu la kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika husika. Vyombo vyote hivyo vinafanya kazi katika kusimamia na kuongoza kwa ukaribu Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa ufanisi na kwa kutoa maelekezo ya kiusimamizi.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Katika kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, ripoti hizo zinatakiwa kuwasilishwa kwa Rais ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka. Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais atawataka wahusika kuwasilisha ripoti hizo Bungeni ndani ya siku saba tangu kuanza kwa kikao cha kwanza cha Bunge.

Kama Rais hatachukua hatua zozote za kuwasilisha taarifa hizo Bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha nakala za ripoti hizo kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano (au Naibu Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yeyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye

atawasilisha ripoti hiyo Bungeni. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayohusu Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma itajadiliwa kwanza na Kamati za Bunge za Hesabu (PAC) kwa niaba ya Bunge na kuandaa ripoti ambayo itawasilishwa Bungeni.

1.1 Wigo wa Ukaguzi na Viwango vya Ukaguzi Vinavyotumika

1.1.1 Wigo na Madhumuni ya Ukaguzi

Madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutimiza jukumu la kutoa maoni huru kuhusu hesabu za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma ili kuona iwapo zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu. Ukaguzi huu unahusiana na hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Desemba, 2016 na tarehe 30 Juni 2017.

Wigo wa ukaguzi wangu unajumuisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kahasibu na udhibiti wa ndani katika shughuli za taasisi husika. Pia, unahusisha ukaguzi na uhakiki wa hesabu, ripoti za utekelezaji, na taratibu nyingine za kikaguzi ambazo ni muhimu katika kukamilisha ukaguzi. Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia viashiria vya hatari na kiwango cha juu cha miamala kinachokubalika.

Kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi yanatokana na kiwango ambacho kumbukumbu, nyaraka, na taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi na zikawasilishwa kwangu.

1.1.2 Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (INTOSAI), Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Afrika (AFROSAL) na Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi kwa Nchi za Afrika Zinazoongea Kiingereza (AFROSAL-E). Hivyo, Ofisi inatumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (ISSAI) vinavyotolewa na “INTOSAI” na

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu (ISA) vilivyowekwa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC).

1.2 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma

Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyingine za umma zina jukumu la kutayarisha kwa usahihi hesabu kama inavyotakiwa katika Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSAS). Majukumu hayo yanajumuisha:

- Kuhakikisha taarifa za hesabu zinaandaliwa kwa kiwango cha kimataifa ikiwa ni pamoja na kubuni, kutekeleza, na kudumisha mifumo thabiti ya ndani itakayoweza kuandaa hesabu zilizo huru, zisizo na makosa, wala mapungufu yatokanayo na udanganyifu;
- Kuchagua na kutumia sera sahihi za uandaaji wa mahesabu; na
- Kufanya makadirio ya mahesabu yanayoendana na mazingira halisi.

Kiwango cha Kimataifa cha Kihesabu Na. 1 (IAS 1) na Kiwango cha Kimataifa cha Utayarishaji wa Hesabu za Taasisi za Umma Na. 1 (IPSAS 1) vinaainisha aina za hesabu zinazotakiwa kuandaliwa na taasisi hizi.

1.3 Mpangilio na Uteuzi wa Makampuni Binafsi kwa Kazi ya Ukaguzi

Ili Ofisi yangu iweze kutimiza majukumu ya ukaguzi kwa ufanisi katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma nchini, kitengo cha ukaguzi wa Mashirika ya Umma kimegawanywa katika vitengo vinne ambavyo ni Ukaguzi wa Taasisi za Fedha, Ukaguzi wa

Taasisi za Elimu ya Juu, Ukaguzi wa Taasisi za Usimamizi na Ukaguzi wa Taasisi za Huduma.

Pia, kaguzi za baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma yamekaguliwa na makampuni binafsi ya ukaguzi kwa niaba yangu. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, ambacho kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kumruhusu mtu au kampuni yeyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na. 33 ya Mwaka 1972 iliyorekebishwa mwaka 1995 kufanya ukaguzi kwenye Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa niaba yake.

Wakaguzi watakaoteuliwa watafuata sheria kama inavyotakiwa; pia hawatatoa siri za mashirika wanayoyakagua.

Wajibu wa kutoa hati ya ukaguzi unabaki kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kaguzi zitakazofanywa na Makampuni binafsi zitahakikiwa ubora wa kazi zake na yangu.

SURA YA PILI

AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.0 Utangulizi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Namba 200 (ISA 200), lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya Shirika na kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango na mfumo unaokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji wa hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika. Hivyo, kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

2.1 Aina za Hati za Kaguzi Zilizotolewa

2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika.

2.1.2 Hati zisizoridhisha

(i) Hati Yenye Shaka

Aina hii ya hati hutolewa pale (a) mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuhitimisha ukaguzi na kuona athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa taarifa za fedha; au (b) mkaguzi anapokuwa ameshindwa kupata uthibitisho wa kutosha kumuwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho kwa ujumla wake si za kimsingi katika usahihi wa taarifa za fedha.

(ii) Hati Isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zina makosa, na zikiangaliwa kwa

ujumla wake zinakuwa hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

(iii) Hati Mbaya

Hati hii hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri taarifa za fedha kiasi cha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na taarifa za fedha hizo.

2.1.3 Aya za Msisitizo wa Jambo Kwenye Ripoti ya Mkaguzi

Kama mkaguzi ataona umuhimu wa kuvuta umakini wa wasomaji wa taarifa za fedha kuhusu suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha, na ambalo limeonekana kuwa ni muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo kwa ajili ya kufanya maamuzi yenye tija, ataweka Aya za Msisitizo. Aya hii itawekwa tu pale ambapo mkaguzi amepata vielelezo vya kutosha kuwa taarifa za fedha hazijakosewa kwa kiasi kikubwa na inatakiwa itokane na suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za hesabu pekee.

2.1.4 Aya ya Mambo Mengineyo ya Ukaguzi

Kama mkaguzi ataona umuhimu wa kuwasilisha mambo mengineyo zaidi ya yale ambayo yameoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha na kwa maono ya mkaguzi ni muafaka kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili waweze kufahamu ukaguzi, majukumu ya mkaguzi au ripoti ya ukaguzi, ataweka Aya ya Mambo Mengineyo katika ripoti yake.

2.1.5 Uwasilishaji wa Mambo Muhimu ya Ukaguzi

Kuwasilisha Mambo Muhimu ya Ukaguzi kunatoa taarifa za ziada kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili kuwasaidia kuelewa mambo hayo ambayo katika maono ya kiweledi ya mkaguzi ni muhimu katika ukaguzi wa taarifa za fedha za mwaka huu. Kuwasilisha mambo muhimu ya ukaguzi kunaweza kuwasaidia watumiaji wa taarifa za fedha kuelewa taasisi na mambo

yanayohusisha zaidi maono ya menejimenti katika maamuzi kwenye taarifa hizo, pia mambo hayo huwekewa mkazo katika ukaguzi.

2.1.6 Maoni ya Ukaguzi yaliyotolewa katika kipindi cha mwaka

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, kulikuwa na jumla ya hati za ukaguzi 104, kati ya hizo; zinazoridhisha 101; Pia, kulikuwa hati nne (4) zenye mashaka zilitolewa; na hapakuwa na hati yoyote mbaya au isiyoridhisha. *Angalia Kiambatisho Na. I.*

2.2 Muelekeo wa Hati za Ukaguzi

Uchambuzi wa mielekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma kwa muda wa miaka mitano kuanzia 2012/2013 mpaka 2016/2017 ni kama ifuatavyo:-

Aina ya Hati ya Ukaguzi	Ripoti Kuu ya Mwaka					
	Mwaka wa fedha	2012/2013	2013/2014	2014/2015	2015/2016	2016/2017
Zinazoridhisha		92	117	107	108	101
Zenye mashaka		1	3	5	4	4
Zisizoridhisha		0	1	0	0	0
Mbaya		0	0	0	0	0
Jumla		93	121	112	112	105

SURA YA TATU

MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA

3.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha kwa ufupi muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti ya Ukaguzi wa miaka iliyopita; baadhi ya mapendekezo hayajatekelezwa na mengine yakiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji hadi ilipofikia wakati wa kuandaa taarifa hii.

Mwezi Julai 2017, nilipokea majibu ya Serikali ya ripoti ya mwaka uliopita kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Ninapenda kutambua juhudi zilizofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kujibu na kuandaa mpango wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa Mashirika ya Umma.

Tathmini ya majibu imeonesha kuwa mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa na mengine yapo kwenye hatua za utekelezaji. Kwa hali hiyo, hatua za ziada zinahitajika katika utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Napenda kurejea mapendekezo yote niliyoyatoa katika ripoti zilizopita ambayo hayajatekelezwa au yametekelezwa kwa kiwango kidogo na Mashirika ya Umma husika kama ifuatavyo:-

3.1 Hadhi ya utekelezaji wa Mapendekezo yaliyopita

3.1.1 Benki ya Azania (2012/2013)

Benki ya Azania inatakiwa iwe chini ya Msajili wa Hazina. Hivyo, Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 9(a) (iii) na (iv) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 inaitaka Benki hii kuwasilisha hesabu kwenye Ofisi yangu kwa ajili ya kukaguliwa.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Wizara ya Fedha iliandika barua kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yenye kumbukumbu namba TYC/A/400/765 ikieleza kuwa Wizara imeomba ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya swala hili, ambapo Mwanasheria Mkuu alishauri kwamba marekebisho yafanyike katika ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma sehemu ya 418, itakayompa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua chombo kilichosajiliwa na kuanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni. Hivyo, tafsiri ya “Mamlaka ya Umma” imebadilishwa kiasi cha kubeba upekee fulani, ambapo inasisitizwa kuwa kama chombo kimesajiliwa chini ya sheria ya Makampuni ikiwa Serikali inamiliki sehemu kubwa ya hisa itatakiwa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Maoni ya Mkaguzi;

Ni matarajio yangu kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atasaidia namna ya mabadiliko ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kunipa mamlaka ya kukagua vyombo vyote vya umma.

3.1.2 Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo vijijini (PRIDE Tanzania Limited) (2012/2013)

Ninaendelea kusisitiza kuwa Msajili wa Hazina anapaswa kufuatilia kwa karibu juu ya umiliki wa kisheria wa hisa za PRIDE Tanzania zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali na baadaye kuhamishiwa kwa wamiliki binafsi.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Maoni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yamezingatiwa, Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, imeandaa waraka kwa Baraza la Mawaziri na kuainisha mambo yafuatayo;

- Itaweka wazi hali ya umiliki wa PRIDE Tanzania;
- Usajili wa PRIDE Tanzania kama Kampuni inayomiliki hisa, na

- Kusajiliwa kama Benki ndogo ya utoaji mikopo iliyosajiliwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Maoni ya Mkaguzi

Nimeyapokea majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya ufuatiliaji, ijapokuwa juhudi nyingi zinapaswa kuelekezwa kwenye suala la umiliki wa kisheria wa hisa za PRIDE Tanzania zinazomilikiwa na Serikali.

3.1.3 Kukosekana kwa Mkataba na Uthibitisho wa Udhadini Kutoka kwa Serikali kwa Mkopo wa Shilingi bilioni 44.29

Menejimenti ya NHIF inashauriwa kuhakikisha mkataba wa mkopo unaingiwa kati yake na mkopaji. Pia, ihakikishe uthibitisho wa udhamini unapatikana kutoka Serikalini. Pia, NHIF inashauriwa kuhakikisha inaingia katika mkataba kabla ya kutoa mkopo wowote mbeleni.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Tarehe 15 Desemba 2015, NHIF ilimepokea barua kutoka Wizara ya fedha na Mipango yenye kumbukumbu namba CJA.452/479/01 kuonyesha nia ya kugeuza mkopo kuwa Bondi itakayotumiwa kufuta madeni yote ya muda mrefu ya Serikali kwa mifuko ya jamii.

Maoni ya Mkaguzi

Nitafatilia utekelezaji wa majibu ya Mlipaji Mkuu.

3.1.4 Kukosekana kwa hati ya umiliki wa Ardhi yenye thamani ya Shilingi milioni 550.71

Ninaushauri uongozi wa NHIF kuongeza juhudi za kupatikana hati halali za umiliki wa ardhi kwa ardhi wanazomiliki.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

- Hati miliki ya kiwanja cha Tabora imepatikana na ipo chini ya usimamizi wa Mfuko.

- Ufuatiliaji wa hati miliki ya viwanja vya Geita na Kagera unaendelea, ambapo upo katika hatua za mwisho za kusainiwa na Kamishna Msaidizi wa Ardhi.
- Manispaa ya Bariadi imechelewesha utoaji wa hati miliki ya kiwanja cha Simiyu; mnamo mwezi wa kumi na mbili 2016 NHIF iliandika barua ya kuikumbusha Manispaa kupitia kwa Kamishna wa Ardhi na kujibiwa tarehe 07/02/2017 kumbukumbu namba LD/288181VOL.1/60 juu ya utekelezaji.
- NHIF inasubiri majibu kutoka Ofisi ya Rais, Ofisi ya Mkoa, na Serikali za Mitaa juu ya utekelezaji.

Maoni ya Mkaguzi

Ninapenda kutambua juhudi zilzofanywa na NHIF. Hata hivyo juhudi zaidi inahitajika kufanywa ili kufanikisha upatikanaji wa hati miliki za viwanja vyote vilivyosalia.

3.1.5 Kutokidhi matakwa ya kiwango cha chini cha mtaji

Menejimenti ya Benki ya Wanawake inashauriwa kuhakikisha inafuata matakwa ya kiwango cha chini cha mtaji kwa kufuatilia mwenendo wa mtaji (monitoring capital position) kila siku na kuchukua hatua thabiti za kudumisha kiwango cha chini cha mtaji.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ilisajiliwa kama Benki ya Kijamii (community Bank) kwa mtaji stahiki wa chini wa Shilingi bilioni 2.5. Mwaka 2014 Benki kuu ya Tanzania ilitoa mamlaka halali ya utoshelevu wa mtaji (Capital Adequacy Regulation) ambayo ilibadilisha Benki ya Wanawake kuwa Benki ndogo ya Kifedha (Micro Finance Bank) yenye mtaji stahiki wa chini wa Shilingi Bilioni 5. Benki ya Wanawake ilipewa muda wa msamaha wa miaka mitatu ulioishia Agosti, 2017; hadi kufikia kipindi cha ukaguzi, Benki ya Wanawake ilifikia nafasi stahiki ya mtaji wa Shilingi bilioni 2.6 tu.

Maoni ya Mkaguzi

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali nimeyazingatia, ijapokuwa pendekezo langu halijatekelezwa, hivyo naendelea kusisitiza mapendekezo yangu yaliyopita kwamba Menejimenti ya TWB inashauriwa kuhakikisha inafuata matakwa ya kiwango cha chini cha mtaji.

3.1.6 Kudorora kwa Mwenendo wa Biashara wa Shirika la Posta Tanzania (TPC)

Shirika la Posta linahitaji Mageuzi makubwa ya kimkakati likilenga watu, michakato, teknolojia, na fedha. Pia, Serikali inatakiwa kulirejeshea Shirika kiasi cha Shilingi bilioni 3.87 kilichotumika kuwalipa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Menejimenti inafanya jitihada kukabiliana na changamoto kwa kuanzisha mfumo mpya. Ni kweli Shirika lina uhitaji wa kurejeshewa gharama zilizotumika kuwalipa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Serikali inafanyia kazi jambo hili pamoja na maswala mengine ya viinua mgongo.

Maoni ya Mkaguzi

Majibu ya Serikali nimeyapokea kwa ufuatiliaji zaid wa utekelezaji wake.

3.1.7 Kushindwa Kuilipa TCRA Mirahaba na Ada za Mwaka Shilingi bilioni 1.38

Menejimenti ya Shirika la Posta inashauriwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zote na kuhakikisha kwamba deni lote linalipwa kwa Mamlaka ya Udhubiti wa Mawasiliano (TCRA).

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Menejimenti imekubali mapendekezo ya Mkaguzi Mkuu, hadi sasa Menejimenti inalipa TCRA Shilingi milioni 10 kila mwezi ili kutekeleza matakwa ya sheria.

Maoni ya Mkaguzi

Naomba kutambua juhudi za Menejimenti, huku nikisubiri uthibitisho wa malipo hayo kwa ufuatiliaji zaidi wa kumbukumbu.

3.1.8 Tatizo la Uendelevu wa Benki ya Twiga Bancorp Ltd (TBCL)

Naishauri menejimenti ya benki kufanya uchunguzi na kuainisha sababu zilizopelekea benki kufanya vibaya. Pia, kubuni mikakati itakayosaidia kuokoa utendaji wa benki.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu yaliyotolewa.

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kuisitza mapendekezo yangu ya awali.

3.1.9 Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kujenga Nyumba za Walimu (TEA)

Serikali inashauriwa kuweka fedha za kutosha katika muda sahihi kwa Mamlaka ya Elimu ili kukamilisha miradi yake na kuondoa tatizo la makazi kwa walimu.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Tarehe 16/06/2016 Mamlaka ilisaini mkataba na kampuni ya Watumishi Housing wa kujenga nyumba 40 za walimu katika maeneo yanayofikika kwa ugumu Tanzania bara kwa jumla ya gharama ya Shilingi bilioni 6.52 ikiwa imejumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kati ya nyumba 40, 10 zimekamilika na 30 zipo katika hatua mbalimabali za ukamilishwaji.

Tarehe 10/05/2016 mkataba wa pili ulisainiwa wa kujenga nyumba za walimu 18 katika shule ya msingi Kakuni Wilaya ya Milele kwa jumla ya gharama ya Shilingi milioni 540 ikiwa imejumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Nyumba zote bado hazidakamilika.

Maoni ya Mkaguzi

Majibu ya Serikali yamepokelewa kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji.

3.1.10 Hasara Iliyopatikana Kufuatia Ukiukwaji wa Mkataba na Mfuko wa Pensheni wa LAPF Shilingi Milioni 473.76 (AICC)

Menejimenti ya AICC inashauriwa kutafuta msaada wa kifedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ili kutekeleza mradi huo.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Kituo kimeandika kwa wapangaji kuelezea nia ya mradi wa maduka, pia kinaendelea kutafuta wawekezaji kwa makubaliano ya ushirikiano wa kibinafsi na umma ambao watakuwa na nia.

Maoni ya Mkaguzi

Majibu ya Serikali nimeyapokea kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji.

3.1.11 Mapato Yaliyopotea kwenye Mali za Uwekezaji Shilingi Bilioni 1.53 (AICC)

Menejimenti inatakiwa kuanzisha kampeni kabambe kutafutia soko sehemu za ofisi zilizopo wazi kwa kukodishwa.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Mpango wa kituo cha biashara upo katika hatua za utekelezaji kwa kupunguza kiasi cha gharama za mwezi za nyumba na ofisi. Kiwango cha umiliki wa nyumba za makazi kwa sasa kipo kati ya asilimia 90 na 100, kwa nafasi zilizo wazi za ofisi kituo kimeweza kutoa 1500 sqm kwa wapangaji wapya ikiwa ni pamoja na makampuni binafsi/ Taasisi za kimataifa na Serikali kutoka Julai 16 hadi Februari 2018.

Maoni ya Mkaguzi

Majibu ya Serikali nimeyapokea kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji.

3.1.12 Ukosefu wa Maendeleo ya Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya ADS-B (TCAA)

Naishauri menejimenti kufanya utafiti mpya na wa kina wa Kampuni juu ya uwezo wa kifedha na uendeshaji wa COMSOFT GmbH. Hii inaweza kuhitaji kuuhusisha Ubalozzi wa Tanzania nchini Ujerumani kwa maelezo ya kuaminika.

Menejimenti inashauriwa kufanya tathmini ya changamoto za utekelezaji wa mradi na kuchukua hatua sahihi ili kuboresha shughuli za udhibiti wa anga.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Sehemu muhimu ya kukamilisha mradi inatarajiwa kufungwa (installed) sambamba na rada mpya ya uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ili kuunganisha taarifa za rada na taarifa za ADS-B kwenye kidhibiti cha taarifa (monitor) ili kutumiwa na Mdhibiti wa anga (Air Traffic Controller).

Maoni ya Mkaguzi

Ipo katika hatua za utekelezaji, nitaendelea kufuatilia utekelezaji kamili.

3.1.13 Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Usalama na ICAO(TCAA)

Mamlaka inashauriwa kumalizia utekelezaji wa Mipango Sahihi ya Utekelezaji (CAPs) kama ilivyopendekezwa kutoka kwenye ukaguzi wa ICAO na kuweka ushahidi unaohitajika ili kudumisha wastani wa kimataifa kwa ajili ya Utekelezaji Madhubuti.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Taarifa zilizopatikana kutoka tawi la Uchunguzi wa ajali za Anga (AAIB) ziliwasilishwa kwa Mkaguzi. AAIB ni taasisi iliyo chini ya Wizara; na Mamlaka haiwezi kulidhibiti isipokuwa utoaji wa fedha kama ilivyoagizwa na Wizara.

Mamlaka inalisaidia AAIB kwa suala la kujenga uwezo na rasilimali, lakini haina uwezo wa kulidhibiti. Aidha, kulingana na mahitaji ya ICAO, Mamlaka haiwezi kufanya kazi za AAIB.

Maoni ya Mkaguzi

Ipo katika hatua za utekelezaji, nitafuatilia utekelezaji wake kamili.

3.2 Hali ya Utekelezaji wa Ufanisi wa Mikakati na Uendeshaji wa Mashirika ya Umma

3.2.1 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

i. Usimamizi wa Kampuni Binafsi za Uzalishaji Umeme Gharama zake

Ili kulihuisha Shirika la TANESCO na kulifanya lipate ufanisi, ninapendekezo yafuatayo; Bei za umeme zinazopitishwa na EWURA zizingatie gharama halisi zinazotumiwa na TANESCO kuzalisha umeme au kununua toka kwa makampuni binafsi ya uzalishaji umeme. Vile vile, bei itakayopitishwa izingatie gharama za uendeshaji wa shirika na uwezo wa kufanya uwekezaji kwenye miundombinu ili huduma ya umeme iendelee kuwa ya uhakika.

Manunuzi ya umeme toka kwenye makampuni binafsi ya uzalishaji umeme yafanywe kwa uwazi na ushindani kama ianvyotakiwa na sheria ya manunuzi ili kuwezesha TANESCO kupata bei nafuu.

Serikali iwezeshe TANESCO fedha ili iweze kuwekeza kwenye uzalishaji umeme wa bei, nafuu hivyo kusaidia kuepukana na utaratibu wa kununua toka vyanzo vya gharama kubwa.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

i. Ongezeko la bei kutokana na matumizi ya EPPs na IPPs litasababisha athari tofauti kwa uchumi wa Nchi. Badala yake, Serikali imetoa ruzuku kwenye umeme ili kuwezesha kufikia

majukumu yake ya kifedha na kutoa huduma zinazohitajika kwa wateja wake;

- ii. Serikali tayari imeelekeza chini ya GN No.292 ya tarehe 21/10/2016 kwa IPPs zote zishiriki katika zabuni za ushindani. Hata hivyo, Serikali imetoa msisitizo juu ya maendeleo ya mradi wa uzalishaji umeme.
- iii. TANESCO imekuwa ikihusishwa katika mchakato wa manunuzi, majadiliano na utoaji zabuni.

Maoni ya Mkaguzi

Majibu ya Menejimenti nimeyapokea kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji.

ii. Ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme Eneo la Songwe

Naishauri Serikali kupitisha Makubaliano ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe kuwezesha mradi kufanyika kwa ufanisi. Pia, Serikali ilihusishe Shirika kwenye ujenzi wa bwawa na ununuzi wa mitambo ya uzalishaji ili liweze kutoa ushauri wa kitaalamu pindi utakapohitajika.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Ushiriki wa TANESCO katika shughuli ya uwekezaji wa mkondo wa chini hasa katika kuhamasisha rasilimali za utekelezaji wa mradi na msaada wa kiufundi.

Tumeafiki wazo la TANESCO kushiriki mchakato wa ujenzi wa bwawa dogo na mtambo wa umeme (hydropower) na kutoa ushauri wa kiufundi wakati unapohitajika.

Maoni ya Mkaguzi

Majibu ya serikali nimeyapokea kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji.

iii. Uhalisia wa Bei ya Umeme Inayotozwa na TANESCO

Ninaishauri EWURA kupitia kwa umakini gharama za umeme ili kuhakikisha kuwa gharama zote za uzalishaji wa umeme zinahusishwa, ili hatimaye, kusaidia upatikanaji wa faida baada ya uwekezaji wenye lengo la kuboresha huduma na kuongeza matokeo chanya kwa TANESCO.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Tumekubaliana na mapendekezo ya Mkaguzi, na TANESCO itaendelea kufuatilia kwa karibu na kuhakikisha EWURA inapitia upya gharama za umeme na kufanyia marekebisho kila robo muhula.

Maoni ya Mkaguzi

Majibu ya serikali nimeyapokea kwa ajili ya ufuatiliaji.

iv. Wizara ya Nishati na Madini Kutolipa Deni la Kodi ya Pango Shilingi Bilioni 1.117

Menejimenti ya TANESCO inashauriwa kuongeza jitihada za kufuatilia Wizarani ili deni hilo lilipwe. Pia, Wizara ya Nishati na Madini, ambayo ni Wizara mama ya TANESCO, ihakikishe haiwi chanzo cha ukata wa fedha unaoikumba kampuni yake.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna jibu

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kuisisitiza mapendekezo yangu.

3.2.2 Mamlaka ya Ukanda wa Kutengeneza Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (EPZA)

i. Kutokujitosheleza kwa Ufuatiliaji na Tathmini za Leseni za Wawekezaji wa EPZA

EPZA wanashauriwa:-

- 25rKufuatilia na kutathmini wawekezaji ili kuhakikisha maendeleo na utendaji wa jumla wa EPZA kwa uchumi wa Taifa.
- Kuanzisha Idara ya ufuatiliaji na tathmini ili kutekeleza jukumu la usimamizi, udhibiti, na ufuatiliaji wa shughuli za kila siku.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Mapendekezo ya mpangilio mpya wa Shirika ulipelekwa kwa Msajili wa Hazina ili kuidhinishwa mnamo mwezi Februari 2017. Kwa kuongezea tunasubiri kibali cha kuajiri watumishi 34. Mapendekezo haya yakiidhinishwa, kutakuwa na wafanyakazi ambao watapewa majukumu ya tathimini na ufuatiliaji wa wawekezaji.

Maoni ya Mkguzi

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali nimeyazingatia, ijapokuwa pendekezo langu halijatekelezwa, hivyo naendelea kusisitiza mapendekezo yangu.

ii. Utendaji Duni wa Wawekezaji Wenye Leseni

EPZA inashauriwa kuanzisha mfumo wa kuwashawishi wawekezaji kuzingatia mapendekezo yao yaliyowasilishwa wakati wa maombi ya leseni na kusaini mkataba wa utendaji na wawekezaji.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Wafanyakazi wenye jukumu la ufuatiliaji wa utendaji wa wawekezaji wanasubiri muundo mpya wa shirika uliopendekezwa ambao ulitumwa tena kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya

kuidhinishwa mnamo mwezi Februari 2017. Kwa kuongezea, tunasubiri kibali cha kuajiri watumishi 34. Mapendekezo haya yakiidhinishwa, kutakuwa na wafanyakazi ambao watapewa majukumu ya kutathimini na kufuatilia ufanisi wa wawekezaji.

Maoni ya Mkaguzi

Pendekezo langu lipo katika hatua za utekelezaji, nitafuatilia utekelezaji wake kamili.

3.2.3 Mfuko wa Pensheni wa LAPF

i. Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Uwekezaji

Menejimenti ya LAPF inashauriwa:

- Kuongeza nyanja za kufuatilia na kutathmini uwekezaji ili kuwa na ufanisi katika utendaji na kufikia malengo yake; na
- Kuipitia sera yake ya uwekezaji kuhusiana na ufuatiliaji na tathmini ili kuongeza mawanda na kujumuisha vipengele vinavyoathiri zinaathiri utendaji wa Mfuko katika utekelezaji wa bajeti ya uwekezaji, tathmini ya asilimia ya ukamilifu wa malipo kwa wakandarasi dhidi ya ukamilifu wa miradi husika ya ujenzi na kuongelea urejeshaji wa mikopo na ulipaji wa kodi wa wapangaji.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu.

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kuisitza mapendekezo yangu.

3.2.4 Mfuko wa Pensheni PPF

i. Utoaji wa Mikopo kwa SACCOS Zaidi ya Ukomo

PPF inashauriwa kuhakikisha mikopo yote inatolewa katika kiwango kinachostahili kufuatana na sera ya mikopo ya Mfuko.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali
Hakuna majibu.

Maoni ya Mkaguzi
Ninaendelea kuisitiza mapendekezo yangu.

3.2.5 Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF)

i. Tathmini ya uwezo wa Mfuko

Menejimenti inashauriwa kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kuhakikisha Serikali inalipa madeni yake na kutoa dhamana sisizo za kifedha ili kuimarisha hali ya kifedha ya mfuko.

Ili kuweka mkazo na kuipa nguvu barua tajwa hapo juu pamoja na makubaliano mbalimbali na Serikali, ninashauri Sheria ya sasa ibadilishwe ili kutambua hali ya sasa ya madeni ya kabla ya mwaka 1999 (pre-1999 employee liabilities) kisheria.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Serikali imeahidi kushughulikia suala hili, wakati huo huo Mfuko unapiga hesabu ya kiasi kinachohitajika kila mwaka na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango ili kuingizwa katika bajeti ya Serikali. Mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imeshalipa kiasi cha Shilingi bilioni 150 ili kufidia uhaba (finance the actuarial shortfall); hata hivyo, kuna mpango wa kuiunganisha mifuko yote ya pensheni ambapo suala hili litashughulikiwa katika Mfuko mpya.

Maoni ya Mkaguzi

Pendekezo langu lipo katika hatua za utekelezaji, nitafuatilia utekelezaji wake kamili.

3.2.6 Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)

i. Mitambo Michache Inayohamishika ya Kusimamia Masafa

Kutokana na umuhimu wa mitambo hiyo, ninashauri kwamba, ni muhimu kufanya tathimini ya mahitaji katika kila kanda ili

kuhakikisha idadi ya mitambo inayohitajika inapatikana ili kuongeza ufanisi na ubora katika usimamizi wa masafa.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kusesitiza mapendekezo yangu ya awali.

ii. Kuwapo kwa Makampuni ambayo Hayajaandikishwa Kwenye Mfumo wa ‘dot (.).tz’

TCRA inashauriwa kuanzisha kanzidata ya kuhakikisha idadi ya taasisi zinazohitajika kubadilisha mifumo ya tovuti zao zinatambuliwa na kuhakikisha makampuni ya umma na ya binafsi yanajitokeza kujiandikisha na kuhakikisha TCRA inashirikiana na taasisi nyingine kama tzNIC, BRELA na TRA ili kuhakikisha makampuni yote yanajisajili kwenye mfumo wa ‘.tz.’

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kusesitiza mapendekezo yangu.

iii. Kutojulikana kwa Thamani ya Mchango wa Kiufundi

Ni maoni yangu kuwa, uthaminishaji wa michango ya wadau wote wawili ni muhimu kwa ajili ya uwazi na kutambua juhudi zinazofanywa na kila mmoja katika kuhakikisha operesheni za tzNIC zinaendeshwa vizuri. Hivyo, nashauri TCRA na TISPA kujadili na kutathmini mchango wa kiufundi unaotolewa na TISPA ili kuwezesha kujua thamani ya michango kwa ujumla.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kusesitiza mapendekezo yangu.

iv. Muingiliano wa Masafa kwa Watumiaji

Ninashauri TCRA iandae mwongozo wa watumiaji ambao utatumika kama njia ya kuongeza ufahamu wa namna bora ya kufanyia kazi masafa yaliyotolewa. Aidha, mara kwa mara iwakumbushe watumiaji namna bora ya urushaji wa matangazo ndani ya mipaka ya masafa waliyopewa ili kupunguza muingiliano kwa watumiaji.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kuisitiza mapendekezo yangu.

v. Shughuli za Mkongo wa Taifa Kutosimamiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Ninaishauri Mamlaka ya Mawasiliano nchini kufanya mazungumzo na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili kuweza kuweka wazi shughuli, usimamizi na majukumu yake kwenye sekta ya mawasiliano.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kuisitiza mapendekezo yangu.

3.2.7 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Mradi wa Mlimani City

i. Ucheleweshwaji wa Utekelezaji na Ukamilikaji wa baadhi ya Miradi

Menejimenti ya Chuo Kikuu inashauriwa kuuangalia upya mkataba ilioingia na Mlimani City Holding ili kuharakisha umaliziaji wa miradi.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Tarehe iliyopangwa ya kukamilisha mradi ilisogezwa kupitia mkataba wa utendaji kutoka tarehe 1 Septemba 2006 hadi tarehe

31 Desemba 2019 ambapo utamalizika. Wakati wa mkutano wa pamoja uliofanyika tarehe 20 Aprili 2017 kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mlimani Holdings Ltd. (MHL), MHL alisema kuwa wanataka kuweka bustani ya mimea (botanical garden) kabla ya mwisho ya kipindi cha maendeleo lakini hakuna mipango ya kujenga hoteli ya nyota 4. Hata hivyo, UDSM na TIC walimwomba MHL kutafakari upya juu ya Hoteli kulingana na mkataba uliopo na MHL aliahidi kufanya hivyo.

UDSM tayari imeanzisha mchakato wa kupitia upya mkataba wa kukodisha ardhi (Ground Lease Agreement).

Maoni ya Mkaguzi

Pendekezo langu lipo katika hatua za utekelezaji, nitafuatilia utekelezaji wake kamili.

ii. Ukiukwaji wa Malipo ya Kodi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Nashauri menejimenti ya chuo kufanya yafuatayo:

- Kufanya upya hesabu za gawio lake la asilimia 10 kutokana na mkataba na kuomba kulipwa na mpangaji kiasi kilichokuwa kimekosewa.
- Kuwasiliana na mpangaji na kufikiria kubadilisha mkataba ili kuweka vifungu ambavyo vitaruhusu idara ya Ukaguzi ya ndani ya chuo kuangalia mapato na gharama za uendeshaji za mradi.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Menejimenti imeyapokea mapendekezo na hatua stahiki zinachukuliwa ikiwa ni pamoja na kutengeneza ankara za ada iliyokuwa imekosewa ikifuatiwa na ripoti ya mahitaji ya malipo ya tofauti kati ya jumla kuu na kiasi kilichokwisha lipwa chuoni (UDSM). Wakati huo huo, UDSM inafuatilia mambo yanayohusiana

na MHL ili kuanzisha njia bora ambayo itakuwa na manufaa ya pamoja na kiwango kikubwa cha kukubalika katika mkataba ambao ni hati inayoongoza kazi pande zote mbili kuhusiana na mradi wa Mlimani City.

Maoni ya Mkaguzi

Pendekezo langu lipo katika hatua za utekelezaji, nitafuatilia utekelezaji wake kamili.

iii. Udhaifu wa Ufuatiliaji na Usimamizi wa Mapato kutoka kwa Wapangaji Wadogo

Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inashauriwa kutekeleza vifungu na vipengele vyote vya hati ya makubaliano ya upangaji kikiwemo kifungu 11.2(l) cha hati ya makubaliano ambacho kinakitaka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kuwathibitisha wapangaji wadogo wadogo.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hivi sasa, UDSM inapaswa kuidhinisha wapangaji kabla ya makubaliano rasmi ya kukodisha na kusainiwa ili kuongeza uwazi juu ya makubaliano ya kimkataba. Hadi sasa, UDSM imeimarisha mahitaji haya ya kiutaratibu.

Maoni ya Mkaguzi

Pendekezo langu lipo katika hatua za utekelezaji, nitafuatilia utekelezaji wake kamili.

iv. Kukosekana kwa Haki ya Kujua Kazi Zinazofanywa na MHL

Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kinashauriwa kuwasiliana na Mlimani Holding Limited ili kupata haki ya kukagua shughuli za miradi kwa manufaa ya pande zote mbili.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Afisa Uhusiano wa UDSM ameshahakiki taarifa zote, hadi sasa hakukuwa na kizuizi na MHL.

Maoni ya Mkaguzi

Pendekezo langu lipo katika hatua za utekelezaji, nitafuatilia utekelezaji wake kamili.

3.2.8 Mamlaka ya Bandari Tanzania

i. Kupungua kwa ufanisi katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mamlaka inashauriwa kuweka juhudi katika utekelezaji wa miradi yote ili kufanikisha malengo yaliyowekwa.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu.

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kuisitiza mapendekezo yangu ya awali.

ii. Tathmini ya ukusanyaji wa mapato ya uhifadhi wa mizigo Bandarini (Wharfage) kati ya Mamlaka ya Bandari na Mamlaka ya Mapato Tanzania

Nashauri Mamlaka ya Bandari kukubaliana na Mamlaka ya Mapato juu ya namna ya kutekeleza majukumu yaliyobainishwa kwenye Memoranda ya Makubaliano baina yao ili kuhakikisha kila upande unatekeleza majukumu yake ipasavyo ili kuisaidia Mamlaka ya Bandari kufikia malengo yake ya kimkakati ya uanzishwaji.

Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Hakuna majibu

Maoni ya Mkaguzi

Ninaendelea kuisitiza mapendekezo yangu ya awali.

SURA YA NNE

MASUALA YALIYOPEWA UZITO KATIKA UKAGUZI

4.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine pamoja na mapendekezo ya nini kifanyike ili kutoa ufumbuzi wa masuala hayo. Masuala hayo yamegawanyika katika sehemu mbili, yale yaliyozihusu taasisi moja moja na yale yaliyozihusu taasisi mbalimbali kwa pamoja.

4.1 Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

4.1.1 Mwenendo Usioridhisha wa Hali ya Kifedha

Kwa miaka kadhaa, TANESCO imekuwa na mwenendo usioridhisha kwa kupata hasara mfululizo. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hasara iliyopatikana ilikuwa Shilingi bilioni 346.40; na kwa hesabu za miezi 18 hadi mwaka wa fedha ulioishia Juni 2015, hasara ilikuwa Shilingi bilioni 124.46. Mwenendo wa hasara umekuwa ukichangiwa na hali isiyoridhisha ya maji ya kuzalisha nguvu ya umeme pamoja na ongezeko la gharama za uzalishaji.

Mfululizo wa hasara hizo una athari kubwa kwenye Mtaji wa Shirika, hivyo kulifanya kutokopesheka ili kukidhi mahitaji yake ya kifedha.

Pia, kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2016, madai yameongezeka kwa asilimia 23, hadi Shilingi bilioni 958 kutoka Shilingi bilioni 738 zilizoripotiwa kwenye hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2015. Kwa upande mwingine, thamani ya wadaiwa ilipungua hadi Shilingi bilioni 330.55 kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2016, kutoka Shilingi bilioni 440.66 zilizoripotiwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2015. Hali ya uwiano wa mali na madeni hairidhishi, na kuna viashiria vinavyoonesha kwamba Shirika haliwezi kugharamia mahitaji yake ya kifedha.

Naishauri TANESCO kuboresha mahitaji yake ya kifedha ili kufanikisha azma ya Mkakati wa Kitaifa wa Ukuaji wa Uchumi kupitia Viwanda.

4.1.2 Fidia ya Ucheleweshaji wa Malipo ya Kampuni ya Pan African Energy yenye Thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 10.43

Kwa mujibu wa Mkataba wa Usambazaji wa Gesi (Gas Supply Agreement) baina ya TANESCO na Kampuni ya Uzalishaji Gesi ya Pan African (PAET), endapo kutatokea mgogoro wa kiasi chochote cha malipo, kiasi hicho kinatakiwa kuwekwa kwenye Akaunti ya Pamoja (Escrow Account) hadi pale mgogoro utakapotatuliwa. Kinyume na hapo, fidia ya ucheleweshaji wa malipo itatozwa. Kutoka mwaka 2011 hadi 2016 TANESCO imekuwa na mgogoro dhidi ya baadhi ya malipo ya usambazaji wa gesi ya PAET yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 6.48.

Hadi tarehe 30 Juni 2016, TANESCO ilikuwa inadaiwa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 71.38 na PAET; na hadi wakati wa ukaguzi ilikuwa haijaweka fedha hizo kwenye akaunti ya pamoja. Kuchelewa kulipa deni hilo kwa wakati kutapelekea TANESCO kulipa fidia ya ucheleweshaji kwa PAET yenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 10.43.

TANESCO inashauriwa kutatua mgogoro huu mapema iwezekanavyo ili kujiepusha na ongezeko la madai.

4.1.3 Hospitali ya Tumaini Kutolipa Kodi ya Pango lenye Thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 9.4

TANESCO imepangisha jengo lake kwa kampuni ya Tumaini Comprehensive Infirmary Limited tangu mwaka 1998. Hata hivyo, kumbukumbu zinaonesha kuwa mpangishwaji hajalipa kodi ya pango kuanzia mwaka 1998 hadi 2016 licha ya kampuni ya Tumaini Comprehensive Infirmary Limited kufungua kesi ya kupinga malipo hayo mwaka 2008 ambayo iliamuliwa kwa TANESCO kushinda na mlalamikaji kuamuliwa kulipa kodi ya pango pamoja na fidia ya usumbufu na uharibifu zenye thamani ya jumla ya dola za kimarekani milioni 9.4. Sambamba na hilo,

kampuni ya Tumaini Comprehensive Infirmary Limited ilitakiwa kuondoka kwenye jengo mwezi Januari 2016.

Hata hivyo, hadi tarehe 30 June 2017 mpangishwaji hajatii maamuzi ya Mahakama, na hakuna hatua nyingine zozote zilizochukuliwa na TANESCO.

TANESCO inashauriwa kuhakikisha uamuzi wa Mahakama unatekelezwa bila kucheleweshwa zaidi.

4.1.4 Deni tarajiwa baina ya SCBHK na TANESCO lenye Thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 148.4

Mnamo mwezi Septemba 2010, TANESCO ilishtakiwa na Benki ya Standard Chartered ya Hong Kong (SCBHK) kulipa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 258.7 kilichotokana na madai ya malipo ya uzalishaji wa umeme pamoja na fidia ya kutolipa madai ya uzalishaji umeme na uharibifu uliosababishwa na TANESCO kutoilipa IPTL kwa wakati.

Maamuzi ya mwisho yaliyotolewa tarehe 12 Septemba 2016 yaliitaka TANESCO kulipa SCBHK, ikijumuisha fidia ya kiasi cha Dola za Kimarekani 148.4. Baada ya hukumu hiyo, TANESCO ilipinga maamuzi hayo kwa kukata rufaa Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kibiashara (ICSID) kisha kuwasilisha utetezi wake tarehe 21 Agosti 2017, ambapo baadaye SCBHK iliwasilisha pingamizi juu ya utetezi huo wa TANESCO.

Tangu kipindi hicho, TANESCO imekuwa ikitumia gharama kubwa za uendeshaji wa kesi hiyo, ambapo jumla ya Shilingi bilioni 7.58 zimetumika ikiwa ni jumla ya Shilingi bilioni 3.65 kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Shilingi bilioni 3.93 kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Hata hivyo, suala hili litarejeshwa kwa mamlaka za kisheria za ndani ambapo utekelezaji wake kisheria utazingatia uwezo wa kulipa wa TANESCO.

Licha ya kiasi kikubwa cha fedha zinazotumika kwenye kesi hiyo, hakuna uhakika wa kushinda.

Ninaishauri TANESCO kuandaa mpango wa utafutaji wa fedha za ziada ili kujiandaa ikitokea maamuzi ya kesi yakiipa ushindi SCBHK, TANESCO iwe tayari kulipa fedha hizo kwa wakati.

4.1.5 Kuchelewa Kuhamisha Wateja kwenye Madaraja ya Tozo Wanayostahili

TANESCO inatoza wateja wake tozo tofauti kulingana na matumizi yao ya Umeme.

Ukaguzi wa wastani wa matumizi ya miezi mitatu ya tozo za jumla ya wateja 14,099 wa kiwango cha Tariff 4 (Eclipse) na jumla ya wateja 40,148 wa kiwango cha Tariff ECO (Hiaffinity) ulibaini kuwa, watumiaji hao wanatumia wastani wa zaidi ya 75 Kwh, ambapo walitakiwa kuhamishiwa kiwango cha Tariff 1.

Hii inaashiria kuwa kuna wateja ambao tozo zao hazijahamishwa kwenye kiwango cha madaraja wanayostahili, hivyo wanaendelea kutozwa kiwango cha chini na kuikosesha mapato inayostahili TANESCO. Jambo hili ni kinyume na matakwa ya Kanuni za EWURA.

TANESCO inashauriwa kuweka mifumo bora ya udhibiti ili kuhakikisha wateja wanahamishwa katika kiwango cha tozo wanachostahili kulingana na matumizi yao. Sambamba na hilo, mfumo maalumu wa moja kwa moja (automatic system) unaweza kutumika kuhakikisha mabadiliko ya moja kwa moja ya tozo hizo.

4.1.6 Zabuni ya Thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 1 Kutolewa kwa Mzabuni Asiye na Vigezo

Ukaguzi wa mkataba wa usambazaji wa nguzo za umeme ulibaini kwamba nyongeza ya mkataba wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1 ilitolewa kwa kampuni ya M/s Farm

Equipment Tanzania Limited (FETL) katika mwaka wa fedha 2015/2016. Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:-

- i) Wakati wa utoaji wa sabuni hiyo, FETL ilikuwa na leseni yakuagiza na kuuza pembejeo na vifaa vya kilimo, hivyo utoaji wa zabuni hiyo kwa FETL ulikuwa kinyume na Kifungu Namba 3 cha Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1972 ambayo inazuia mtu yoyote kufanya biashara kama wakala bila kuwa na leseni halali aliyopewa kwa ajili ya biashara hiyo; na
- ii) Wasifu wa kampuni ya FETL ulionyesha kuwa na uzoefu kwenye uuzaji wa mashine ndogo za kulimia, matrekta na mafuta. Utoaji wa zabuni hii ulikwenda kinyume na sifa zilizoainishwa kwenye zabuni, ambapo muombaji alitakiwa kuwa na uzoefu kwenye huduma ya usambazaji nguzo au kazi ya namna hiyo kwa miaka mitano.

Hali hiyo inaashiria mapungufu kwenye mapitio ya waombaji, kiasi cha kusababisha jambo lililopelekea zabuni kutolewa kwa kampuni isiyokuwa na vigezo vya biashara.

TANESCO inashauriwa kutotoa zabuni kwa muombaji asiyemiliki leseni ya biashara husika na mwenye uzoefu mdogo wa biashara iliyopo kwenye zabuni.

4.1.7 Upungufu kwenye Vipuri vya Mitambo ya Ufuaji Umeme wa Gesi wa Warstila (Ubungo) na Tegeta

Mapitio ya mkataba wa usambazaji wa vipuri wenye thamani ya Euro milioni 6.85 kwa ajili ya mitambo ya kufua umeme ya 12W20V345G Wartsila uliopo Ubungo na ule wa usambazaji wa vipuri vya mitambo ya Warstila wenye thamani ya Euro milioni 0.67 uliyopo Tegeta yalibaini yafuatayo:-

- i) Ripoti ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya tarehe 6 Julai 2016 ya mapitio ya mkataba baina ya TANESCO na M/s Warstila

uliosainiwa tarehe 21 Machi 2016 ilibainisha mambo 14 ambayo yalihatijika kuwamo kwenye mkataba huo. Moja ya mambo hayo ni TANESCO kupata ruhusa kutoka PPRA kutokana na kuwapo na tofauti ya Masharti ya Ujumla ya Mkataba baina ya ule unaotolewa na PPRA na ule wa TANESCO. Hata hivyo nilibaini kuwa, maombi ya ruhusa ya PPRA yalicheleweshwa kwa miezi minne hadi tarehe 4 Novemba 2016 jambo lililopelekea kuchelewa kusainiwa na kutekelezwa kwa mkataba.

ii) Tarehe 6 Desemba 2016, PPRA ilielekeza kwamba Masharti ya Ujumla ya Mkataba yasibadilishwe na ikaishauri TANESCO kuandaa Standard Bidding Document inayoonyesha Masharti Maalumu ya Mkataba na kuyawasilisha PPRA kwa mapito ya uthibitisho. Hii inamaanisha kuwa kulikuwa na uthibitisho zaidi uliotakiwa kufanywa na PPRA kabla TANESCO haijasaini mkataba. Mnamo tarehe 6 Juni 2017 TANESCO iliamua kuandika barua kwa Msajiri wa Hazina ili iruhusiwe kutozingatia mapendekezo na maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA).

iii) Pia, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mkataba huu mnamo mwaka wa fedha 2015/2016 ni Shilingi bilioni 1.88 wakati kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilikuwa Shilingi bilioni 3, ilihali mkataba halisi una thamani ya euro milioni 6.85 (bilioni 17). Bajeti isiyotosha ina athari kubwa kwenye manunuzi na inaweza kupelekea Shirika kulipa gharama zaidi ya ilivyopangwa kutokana na ucheleweshwaji wa kulipa.

Kuchelewa kwa taratibu za manunuzi kunaweza kusababisha hitilafu kwenye mitambo pindi matengenezo yatakapoacha kufanyika kwa wakati kutokana na kukosekana kwa vipuri. Pia, kunaweza kupelekea ongezeko la gharama za vipuri na muda wa usambazaji wake.

Naishauri TANESCO kuzingatia maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kwa kuongeza kasi ya taratibu za manunuzi; na pia kuongeza bajeti ya manunuzi hayo ili kufanikisha utaratibu huo kwa wakati bila ongezeko jingine la gharama.

4.2 Chuo Kikuu cha Ardhi (AU)

4.2.1 Kutolipwa kwa Maslahi ya Watumishi Shilingi Bilioni 2.9

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Chuo Kikuu cha Ardhi hakijalipa maslahi mbalimbali ya watumishi wake kama posho ya nyumba (housing allowance), posho ya majukumu (responsibility allowance), kiinua mgongo (gratuity) na posho ya madaraka kwa zaidi ya miaka mitatu (3) yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 2.9 kinyume na matakwa ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Chuo Kikuu cha Ardhi.

Hali hii inapunguza mori wa kazi na kuwanyima watumishi haki zao za msingi na kwa wakati.

Nashauri uongozi wa Chuo hicho kulipa madai hayo ya watumishi ili kuongeza ufanisi kazini.

4.3 Shirika la Viwango Tanzania (TBS)-2016

4.3.1 Ukiukwaji wa Taratibu za Manunuzi

Mapitio ya manunuzi ya TBS yalibainisha idara zenye uhitaji zinajitafutia wazabuni, zinajadiliana na wazabuni na kutoa maoni juu ya njia gani ya manunuzi itumike kufanikisha manunuzi, hivyo kuacha Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU) kuwezesha utaratibu wa manunuzi tu. Nilibaini kuwa bidhaa na huduma zenye thamani ya dola za kimarekani 177,526.50 na Shilingi milioni 135 zilinunuliwa chini ya utaratibu huo ulio kinyume na Sheria za Manunuzi.

Pia, nilibaini kuwa mkataba wa huduma wa usafiri baina ya TBS na kampuni ya G4S wenye gharama ya Shilingi 120,000 kwa kila safari na Shilingi 150,000 kwa kila usafirishaji uliongezewa muda kwa mwaka mmoja bila kuhusisha Kitengo cha Manunuzi na Bodi ya Zabuni.

TBS Ilikiuka kifungu namba 38 na 39 vya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011, jambo lililopelekea manunuzi yasiyofuata thamani ya fedha.

4.4 Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

4.4.1 Kutofanyika kwa Uchunguzi wa Hati Zilizoisia Muda wa Matumizi kutoka SGS

Aya namba 2.2.2 ya Masharti ya Kudumu ya mkataba baina ya TBS na mawakala wa Ukaguzi inataka kabla ya mzigo kusafirishwa, upatiwe Hati ya Awali ya Uhalali wa Ufanisi yaani ‘Pre-shipment Verification of Conformity (PVoC),’ pia inahitaji kuambathishwa kwa Hati ya Uhalali wa Ufanisi kwa bidhaa zilizothibitishwa kwa matumizi ya Tanzania yaani ‘Certificate of Conformity (CoC)’. Vyeti hivi vinaihakikishia TBS kutokuwapo kwa hatari ya bidhaa husika kutokidhi vigezo, hivyo kuathiri uchumi.

Aya namba tano ya mwongozo wa utaratibu wa kuagiza bidhaa toka nje ya nchi inataka bidhaa yoyote isiyo na Hati ya Uhalali wa Ufanisi wa Bidhaa zilizothibitishwa kwa matumizi ya Tanzania, lakini ilipatiwa Hati ya Awali ya Uhalali wa Ufanisi kufanyiwa Ukaguzi mara utakapofika nchini (Destination Inspection). Mzigo wowote wenye thamani zaidi ya Dola za Kimarekani 5,000 utakapofanyiwa Ukaguzi baada ya mzigo kufika nchini unatakiwa kutozwa faini isipokuwa kama bidhaa hiyo ilipata msamaha wa faini.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa Jumla ya Hati 3,911 za Uihakikisho wa Ubora wa Bidhaa zilizothibitishwa kwa matumizi ya Tanzania kutoka kampuni ya SGS zilikaa zaidi ya siku 90, hivyo kuisha muda wake wa matumizi bila kuchukuliwa na waagizaji. Hata hivyo, TBS haikufuatilia wala kuchunguza kama waagizaji ambao walilipa hati hizo waliagiza bidhaa kuja nchini au la; na ikiwa waliagiza, kama walifanyiwa Ukaguzi wa mwisho baada ya mzigo kufika nchini na kutozwa faini.

Kuna hatari kwamba ankara zilizowasilishwa kwa Wakala kwa ajili ya ukaguzi zilibadilishwa kwa udanganyifu kwa kupunguza ankara hizo. Hati ya Uhalali wa Ufanisi kwa bidhaa zilizothibitishwa kwa matumizi ya Tanzania hazikukusanywa na bidhaa ziliingizwa nchini.

Nashauri TBS ichunguze kwa nini hati 3,911 za uhakikisho wa ubora wa Bidhaa zilizothibitishwa kwa matumizi ya Tanzania hazikuchukuliwa, na kujiridhisha kama bidhaa zilizoagizwa zilifanyiwa Ukaguzi baada ya kufika nchini au la.

4.4.2 Misamahama Inayotolewa Bila Kufuata Sheria

Majukumu ya TBS yameainishwa kwenye Kifungu Namba 4 cha Sheria ya Viwango ya mwaka 2009. Kifungu hicho kinataka kuwe na msamaha wa ukaguzi wa biadhaa zinazoingizwa nchini.

Aya namba 5.1.4 ya Mwongozo wa Utaratibu wa Ukaguzi uliofanyiwa Marekebisho ya 4 na kutolewa tarehe 30 Agosti 2017 inatoa msamaha wa ukaguzi kwa bidhaa za msaada, miradi ya Serikali, miradi ya uwekezaji ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), bidhaa za mitaji na bidhaa za Ukanda Maalumu wa Uwekezaji (EPZA). Katika mwaka wa fedha 2016/2017 TBS ilitoa jumla ya misamaha 744.

Mwongozo huu uko kinyume na malengo ya TBS hivyo kuongeza uwezekano wa nchi kuwa kwenye hatari ya kutumia bidhaa zisizo na ubora.

Naishauri TBS kutathmini maamuzi yake ya kutokagua bidhaa za msaada, miradi ya Serikali, miradi ya uwekezaji ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania, bidhaa za mitaji na bidhaa za Ukanda Maalumu wa Uwekezaji ili kujiridhisha bidhaa pekee zenye vigezo ndizo zinazoingizwa nchini.

4.4.3 Kutokuwapo kwa Maafisa wa TBS kwenye Vituo vya Mipaka ya Nchi

Moja ya malengo ya TBS ni kuhakikisha kuwa bidhaa za ndani na zinazoagizwa kutoka nje ni zenye viwango na ubora unaostahili kwa kufanya ukaguzi maeneo yote yanayoweza kuingiza bidhaa nchini.

Ukaguzi ulibaini kuwa hakuna maafisa wa TBS kwenye maeneo kadhaa ya mipakani niliyoyafanya sampuli ya ukaguzi. Maeneo haya ni Borega, Kogaja, Kilongwe na Gorogonja mkoani Mara. Mengine ni Bandari za Bukoba na Kemondo, mkoani Kagera; Kiseke, Kitobo na Chumvini, mkoani Kilimanjaro; pamoja na Kigombe, Kipumbwi, Mkwaja, Kwale - Jasini, Chongoleani, Sahare, Mwambani, Dumi na Mnyanjani mkoani Tanga.

Kutokuwapo kwa maafisa wa TBS kwenye vituo vya mipakani kunaongeza uwezekano wa athari ya bidhaa zisizo na ubora kuingizwa nchini.

Nashauri vituo vyote vya mipakani nchini viwe na maafisa wa TBS ili kuhakikisha bidhaa zenye ubora tu ndizo zinaruhusiwa kuingizwa nchini.

4.5 Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA)

4.5.1 Makusanyo ya Mapato yasiyoridhisha yatokanayo na Urukaji wa Puto

TANAPA ilianzisha huduma ya Utalii kwa Urukaji wa Puto kwa mbuga za Tarangire na Serengeti. Huduma hii inatolewa na kampuni binafsi kwa makubaliano ya TANAPA kupata asilimia 10 ya gharama iliyotozwa kwa kiasi kilicholipwa kulifanya puto kuruka.

Hata hivyo, nilibaini kwamba, kwenye ukokotoaji wa asilimia 10 ya kiasi kilicholipwa kulifanya Puto kuruka, TANAPA inategemea hati za madi zinazotolewa na kampuni inayotoa huduma ya kurusha Puto bila ya kuwa na namna nyingine ya kuthibitisha

kiasi tajwa kama ni sahihi. Kwa namna hii, TANAPA inaweza kuwa inapoteza sehemu kubwa ya mapato yanayotokana na mauzo ya bidhaa ya Puto kwa watalii mbalimbali. Sambamba na hivyo, ukokotoaji wa asilimia 10 unafanywa kwenye gharama halisi baada ya kutoa punguzo kwa mteja (net amount) badala ya jumla kamili (gross amount).

TANAPA inashauriwa kuhakikisha malipo yote yatokanayo na bidhaa ya urushaji wa Puto yanalipwa kwenye magezi ya kuingilia mbugani, na siyo baada ya kuingia ndani ya hifadhi. Pia, uongozi utengeneze kitabu cha kurekodi safari za puto (flight manifest logbook) ambacho kitakuwa kinahifadhiwa na Afisa Utalii wa mbuga husika. Kabla ya safari, kitabu hicho kitahitaji kusainiwa na rubani wa Puto na Afisa Msimamizi wa TANAPA.

4.5.2 Kutokuwapo kwa Namna Nyingine za Kufanya Malipo ya Utalii

TANAPA ilianzisha mfumo wa malipo ya kielekroniki ili kuongeza udhibiti wa mapato ya utalii. Chini ya mfumo huu watalii wanatakiwa kuchanja kadi za malipo kwenye mfumo wa mashine za malipo zinazoratibiwa na benki za Exim na CRDB.

Hata hivyo, nilibaini kuwa hakuna namna nyingine ya malipo inayoweza kufanyika zaidi ya mtalii kuchanja kadi ya malipo kutoka benki ili kufanikiwa kuingia hifadhini kufanya utalii. Kwa namna hii mfumo, huu una kizuizi.

Pamoja na kupongeza jitihada za TANAPA kwenye kuboresha makusanyo ya mapato ya utalii, nashauri uongozi wa mamlaka kufikiria njia mbadala za malipo kama kutumia malipo kwa njia ya mtandao wa simu (mobile money transfer) ili kuondokana na adha ya kutumia namna moja ya watalii kufanya malipo.

4.5.3 Mapungufu ya Mfumo wa Kuweka Nafasi za Watalii (Reservation System)

Mpango Mkuu wa Usimamizi wa TANAPA's umebainisha uongozi wa kila hifadhi kutekeleza kwa ufanisi mfumo wa kuweka nafasi

za watalii (reservation) kwenye malango yote ya kuingia hifadhini ili kupunguza uwezekano wa kuweka nafasi za watalii zaidi ya inavyostahili (overbooking), usumbufu kwa wateja na kupunguza gharama kwa makampuni ya Utalii.

Mapitio ya mfumo wa uwekaji nafasi kwa watalii (booking) yalibainisha kuwa TANAPA bado haijaboresha mfumo huo kwenye malango ya kuingilia hifadhini, hivyo kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa kwenye Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Mamlaka (GMP). Nilibaini kuwa uwekaji wa nafasi bado unafanywa nje ya mfumo, hivyo kutoshahibiana na matumizi ya mfumo wa malipo wa 'Point of Sale'. Pia, kutokuwapo kwa mfumo wa uwekaji nafasi mtandaoni (online booking system) kunaondoa ufanisi na uwazi kwenye zoezi zima la uwekaji nafasi za watalii, hivyo kupunguza jitihada za uongozi kukusanya mapato na kuyasimamia.

Nashauri TANAPA kuanza kutumia mfumo wa kuweka nafasi wa kielektroniki kwenye hifadhi utakaokidhi viwango vinavyostahili na kuondoa mapungufu ya mfumo wa sasa.

4.5.4 Mapungufu ya Ufanisi katika Usimamizi wa Mapato ya Vibali Vilivyoisha Muda

Kanuni za Fedha za TANAPA zinataka malipo ya ziada yatozwe kwa vibali vilivyoisha muda wake kwa mtalii aliye ndani ya eneo la hifadhi baada ya muda wa awali aliyopatiwa kuisha.

Mapitio yangu yalibaini kuwa vibali vingi haviondolewi ndani ya mfumo kwa wakati kipindi ambacho watalii wanatoka. Jambo hili linasababishwa na mfumo usioridhisha wa intaneti au kufeli kwa mfumo kipindi watalii wanapakuwa wanatoka hifadhini. Pia, nilibaini kuwa hakuna utaratibu uliowekwa na Mamlaka unaotofautisha kati ya vibali vilivyoisha muda kwa kufeli kwa mfumo na vile vinavyotokana na kutotoka hifadhni kwa wakati.

Swala hili linaashiria mapungufu kwenye udhibiti wa vibali vilivyoisha muda, hivyo kupelekea upotevu wa mapato.

TANAPA inashauriwa kuandaa na kutekeleza namna bora ya usimamizi wa vibali vinavyoisha muda wake kama mashine ya 'QR Scanner' ambayo itahakikisha usimamizi bora na kulipiwa kwa vibali vyote vilivyoisha muda wake.

4.5.5 Kutokuwapo kwa Mfumo wa Kudhibiti Mali

Nilibaini kuwa TANAPA haina mfumo mmoja wa kudhibiti mali za mamlaka kwa kuunganisha gharama za manunuzi ya mali hizo, gharama za matengenezo na gharama za mafuta kwa ajili ya kufanya maamuzi. Sambamba na hilo, nilibaini pia mamlaka haina sera ya usimamizi wa mali kwa ajili ya udhibiti na usimamizi wa aina zote za mali.

Kutokana na ukuaji wa uhitaji wa magari na mitambo kwa mamlaka, mfumo wa udhibiti wa mali unahitajika kuanzishwa ili mali husika zifuatiliwe mara kwa mara kwa madhumuni ya udhibiti na kufanya maamuzi.

TANAPA inashauriwa kuandaa sera ya usimamizi wa mali na kufanya tathmini ya kina juu ya umuhimu wa mfumo wa kudhibiti mali ili kurahisisha ufuatiliaji wa gharama za manunuzi ya mali, gharama za matengenezo na mafuta, hivyo kusaidia uongozi kwenye maamuzi na kuongeza ufanisi wa uzalishaji kwa kupunguza gharama za usafirishaji.

4.6 Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Mwanza (MWAUWASA)

4.6.1 Malipo kwa Mkandarasi bila Uthibitisho wa Kazi Shilingi Milioni 420.10

MWAUWASA iliingia mkataba na kampuni ya M/s D.F Mistry kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya MWAUWASA. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, MWAUWASA ilimlipa mkandarasi tajwa jumla ya Shilingi milioni 420.10 bila ya uthibitisho wa kazi iliyofanyika (certificate for works executed) kinyume na Sharti

namba 7.2 (h) la mkataba baina ya MWAUWASA na M/s D.F Mistry ambalo linataka kabla ya malipo kufanyika, mhandisi mshauri afanye tathmini ya kazi na kuthibitisha kiwango kilichofanyika.

Jambo hili lilitokea kwasababu MWAUWASA ilimpa kazi mkandarasi wakati ikiendelea na taratibu za manunuzi za kumpata mhandisi mshauri.

Nilibaini kuwa, ni kazi yenye thamani ya Shilingi milioni 628.93 tu iliyothibitishwa na mhandisi mshauri, hivyo kuacha kiasi cha Shilingi milioni 420.10 kikilipwa licha ya kazi husika kutofanyika.

Malipo kwa kazi ambayo haijaanza au kuthibitishwa huongeza hatari kwa mamlaka kushindwa kupata chochote ikitokea jambo linaloweza kumfanya mkandarasi asitekeleze majukumu yake.

MWAUWASA inashauriwa kuhakikisha kiasi cha Shilingi milioni 420.10 kilicholipwa kwa mkandarasi kinarejeshwa bila kuchelewa, na kilipwe pale tu kazi husika ikithibitika kufanyika.

4.6.2 Ukosefu wa Mfumo wa Usimamizi wa Viashiria vya Hatari kwa Taasisi

Suala la kuhakikisha viashiria vya hatari kwa taasisi vinatambulika na kutafutiwa ufumbuzi ni mbinu mojawapo ya kuhakikisha malengo ya taasisi yanafanikiwa. Hatua hii inahusisha utambuzi wa viashiria vya hatari, mapitio ya viashairi hivyo, uchambuzi wa viashiria hivyo pamoja na kutafuta ufumbuzi kwa viashiria vinavyoonekana kuathiri kufikiwa kwa malengo ya taasisi.

Hata hivyo, MWAUWASA haijaandaa mfumo wa namna ya kufanya utambuzi wa viashiria vya hatari kwa taasisi, jambo ambalo lingesaidia kuepukana na viashiria vinavyoweza kupelekaa kuathiri utendaji wa mamlaka na malengo mapana ya taasisi.

4.6.3 Kuchelewa Ukamilishaji wa Mradi wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 6.66

Tarehe 25 Mei 2015 MWAUWASA iliingia mkataba na kampuni ya M/s Jassie& Company Limited wa Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Safi na Majitaka katika Mji wa Geita wenye thamani ya Shilingi bilioni 6.66. Mradi huu ulipangwa kuanza mwezi Juni 2015 na kumalizika ndani ya siku 360.

Hata hivyo, hadi muda wa ukaguzi, mwezi Novemba 2017, mradi ulikuwa haujakamilika na mkandarasi ameshaondoka eneo la kazi.

4.7 Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Babati (BAWASA)

4.7.1 Upotevu wa Maji wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.5

Ukaguzi wangu ulibaini upotevu wa maji wa asilimia 48 wenye thamani ya Shilingi bilioni 1.5 katika Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka ya Babati, kinyume na kiwango kilichokubaliwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji cha asilimia 31. Upotevu huu umesababishwa na kuvuja kwa mabomba na matumizi ya maji nje ya mita za upimaji wa matumizi ya maji.

Naishauri BAWASA kupunguza kiwango cha upotevu wa maji kwa kuongeza usimamizi, ukaguzi na kuondoa hitilafu kwa wakati pindi litokeapo tatizo kwenye mfumo wa miundombinu ya maji.

4.8 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CARMATEC)

4.8.1 Mapungufu kwenye Ongezeko la Mkataba

CARMATEC ilipangisha eneo la ofisi kwa makampuni ya M/s Life Fitness Club Ltd na M/s Perfect Choice Supermarket Ltd kwa gharama ya Dola za Kimarekani 4 kwa kila mita za mraba. Hata hivyo, mapitio yangu yalibaini kuwa kiwango hicho ni kidogo ikilinganishwa na wastani wa gharama ya bei ya soko katika jiji la Arusha. Bei halisi ya soko ipo kati ya Dola za Kimarekani 7 hadi 10 kwa kila mita ya mraba. Pia, kupitia mikataba nilibaini kuwa kiwango cha kubadilishia fedha za kigeni kiliwekwa Shilingi 2,193

kwa kila dola kwa miaka sita kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2022.

CARMATEC inapoteza mapato kutokana na kiwango kidogo cha kodi inachotoza na viwango vya kubadilishana kubadili pesa kinachotumika kua kimoja kwa kipindi cha miaka mitano.

Ninapendekeza mapitio ya mkataba ili kuweza kubabili viwango vya kodi yafanyike na kile cha kubadilishia fedha kuwa kile cha soko la wakati husika.

4.9 Mfuko wa Pensheni wa LAPF

4.9.1 Madai ya Muda mrefu ya kodi ya pango

LAPF inawadai wapangaji wake kiasi Shilingi bilioni 3.5, kati ya hizo, Shilingi milioni 887 imekuwa ikidai kwa kipindi cha zaidi ya miezi 9. Madeni haya yanatokana na wapangaji kukiuka kifungu 4.7.1 cha makubaliano ya mkataba wa kupanga, ambao unahitaji kodi ya kulipwa kila mwaka, nusu mwaka au robo mwaka kabla.

Hii inapelekea kiasi kikubwa cha fedha kuwa katika mikono ya wapangaji, hivyo kukwamisha mipango ya taasisi.

LAPF inashauriwa kuweka mikakati ya kukusanya madeni yote; pia wapangaji wazingatie kifungu cha mkataba kinachotaka kodi kulipwa kabla.

4.9.2 Malipo ya awali yamelipwa ilihali kazi haijafanyika Shilingi Milioni 258.22

LAPF ililipa malipo ya awali ya Shilingi milioni 258.22 kwa M/s African Focus & H Consult mwaka 2013 kwa ajili ya kazi za ujenzi. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe ya ukaguzi huu, Oktoba 2017 kazi hizo zilikuwa hazijafanyika.

LAPF imelipeleka suala hili mahakamani kudai kurejeshewa fedha zake lakini maamuzi ya mahakama bado hayajatolewa.

Kuchelewa kukamilika kwa kesi hiyo kunaathiri shughuli za Mfuko; hivyo napendekeza Mfuko kufuatilia suala hili kwa karibu ili kuweza kupata fedha hizo.

4.10 Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

4.10.1 Kuongezeka kwa Madai na kutokuwapo kwa jitihada za ukusanyaji madeni

Ukaguzi wangu umebaini kuwa kumekua na ongezeko la madai ambayo Hospitali inadai toka kwa taasisi mbalimbali. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2016, madai yalikuwa yamefikia Shilingi bilioni 30.8, ikilinganishwa na mwaka jana yalipokuwa Shilingi bilioni 17, ikiwa ni ongezeko la asilimia 45.

Kuongezeka kwa wadaiwa kunachangiwa na kutokuwapo kwa jitihada za ukusanyaji madeni.

Ninashauri Hospitali kuandaa mikakati na mbinu zitakazowezesha kukusanya madeni hayo.

4.10.2 Madai ya bima za afya yaliyokataliwa Shilingi Bilioni 1.86

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) hutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa walio na Bima za afya za Makampuni mbalimbali ya Bima. Chini ya mpango huo, Hospitali hutoa huduma za matibabu kabla ya malipo, kisha hudai gharama kutoka kwa Makampuni husika ya Bima.

Katika kipindi cha ukaguzi, nilibaini madai yanayofikia Shilingi bilioni 1.86 ambayo yalikalaliwa kulipwa na Makampuni ya Bima.

Mapitio zaidi yalibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulikataa madai ya Shilingi milioni 241.97 ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, ikidai ni madai ya madawa ambayo NHIF ilibani hayakutolewa kwa wagonjwa, udanganyifu huu ulidaiwa kufanywa na watumishi wa hospitali.

Hali hii inaashiria kuwapo kwa udanganyifu katika mfumo mzima wa kutoa huduma kwa wagonjwa wanaotumia Bima ya Afya. Hali hii isipodhibitiwa inaweza kupelekea hasara kubwa kwa hospitali.

Ninashauri Hospitali kuchunguza udanganyifu huo na wahusika watakaobainika wachukuliwe hatua stahiki. Pia, kuupitia mfumo mzima wa kuudumia wagonjwa wenye bima za afya ili kubaini mapungufu na kutafuta ufumbuzi.

Pia ninashauri Hospitali kuandaa mikakati na mbinu zitakazorahisisha ukusanyaji wa madeni hayo.

4.11 Watumishi Housing Real Estate Investment Trust (WHC-REIT) - 2016

4.11.1 Fedha ambazo hazijatolewa kwenye mradi- Shilingi bilioni 8.9

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, wamiliki wa kampuni ya Watumishi Housing Real Estate Investment Trust (WHC-REIT) waliahidi kutoa Shilingi bilioni 22.3 ili kuchangia miradi wa ujenzi. Hata hivyo, kiasi walichotoa ni Shilingi 13.4 bilioni (asilimia 60), hivyo Shilingi bilioni 8.94 hazikutolewa.

Kutotoa kiasi kamili kilichoahidiwa kumesababisha miradi ya ujenzi kutofanyika kwa wakati kama ilivyopangwa, hatimaye kuzua malalamiko ya wateja ambao tayari wamekamilisha malipo yao.

Ninashauri kuwa wamiliki wa kampuni watoe michango yao kwa wakati ili kuweza kuondokana na malalamiko ya wateja.

4.11.2 Miliki za majengo ambazo hazikukatiwa Bima Shilingi Bilioni 1.96

Kanuni Na.51 (8) ya Masoko ya Mitaji na Usalama, 2011 inataka majengo yanayomilikiwa kukatiwa Bima za majengo.

Ukaguzi umebani kuwa, majengo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.96 yaliyotelekezwa na wahandisi wa ndani hayakuwa yamekatiwa Bima. Hii najumuisha majengo ya Mkundi (Shilingi

bilioni 1.43), Gezaulole (Shilingi bilioni 0.433), na Mabwepande (Shilingi bilioni 0.092). Hii ni kinyume na kanuni tajwa hapo juu.

Miliki za mali zipo kwenye hatari pindi majanga yatakapotokea na kupelekea hasara kubwa isiyokuwa na fidia.

4.12 Kampuni ya Maendeleo ya Nishati ya Geothermal Tanzania (TGDC)

4.12.1 Kutokuwapo kwa waraka wa bei elekezi kati ya kampuni Tanzu TANESCO inamiliki 100% ya Hisa za Kampuni ya Tanzania Geothermal Development Limited (TGDC) iliyoanzishwa tarehe 19 Desemba 2013.

Kanuni za Bei elekezi baina ya makampuni tanzu ('TP Regulations') zilianza kutumika mwezi Februari 2014, ikizitaka Taasisi zinazohusiana kuandaa nyaraka zinazoonesha biashara iliyofanyika baina yao kila mwaka.

Imebainika kuwa TGDC haikuandaa nyaraka za kuonyesha biashara iliyofanyika na makampuni dada kwa kutumia bei elekezi kinyume na kanuni husika.

Kanuni zinahitaji Kampuni itakayoshindwa kuandaa nyaraka tajwa, itatozwa faini ya Shilingi milioni 50 au kifungo kwa Wakurugenzi au Maafisa wake, au vyote kwa pamoja.

TGDC na TANESCO wanashauriwa kuhakikisha kwamba nyaraka zinaandaliwa kabla ya tarehe zilizopagwa ili kuepuka faini na adhabu.

4.13 Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi

4.13.1 Kuchelewa kukamili kwa Mradi Shilingi Bilioni 1.18

Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi (UWASA) inatekeleza mradi wa kuboresha mfumo wa maji katika Manispaa ya Moshi wenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.18 unaofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya usimamizi wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia WSDP. Mradi una awamu mbili; Awamu ya kwanza ilikuwa

kubuni michoro pamoja michakato ya zabuni na ilikamilika mwaka 2015; awamu ya pili ni kwa ajili ya ujenzi. Hadi 30 Juni 2017 awamu ya pili ilikuwa haijanza.

Mamlaka inashauriwa kuwasiliana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji juu ya utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi.

4.14 Shirika la Nyumba la Taifa(NHC)

4.14.1 Malipo Yasiyo na Vielelezo Shilingi Milioni 111.25

NHC ilikuwa inatekeleza Mradi wa ujenzi wa nyumba 300 kwenye kata ya Iyumbu Dodoma. Mradi ulianza tarehe 5 Desemba 2016 kwa kutumia wataalamu wa ndani kwa kiasi cha Shilingi bilioni 12.78, na ilipangwa mradi ukamilike tarehe 4 Desemba 2017.

Katika ukaguzi wa nyaraka mbalimbali, nilibani kuwa malipo ya Shilingi milioni 111.25 hayakuwa na nyaraka za kuthibitisha uhalali wa malipo.

Nashauri NHC kuwasilisha nyaraka hizo kwa ajili ya ukaguzi.

4.15 Baraza la Walaji la Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA-CC)

4.15.1 Sheria ya TCAA kwenda Kinyume na Katiba ya Jamhuri

Kifungu 52 (4) cha Sheria ya TCAA (2006) kinasema kuwa, Taarifa za Fedha za Baraza zitakaguliwa na mkaguzi yeyote aliyeainishwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wakaguzi na Wahasibu (1972).

Sheria hii inaleta mkanganyiko juu ya mamlaka ya ukaguzi wa Baraza pale inapohusishwa na ibara ya 143 (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) ambayo inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Taasisi zote za Serikali.

Ninapendekeza TCAA ianische kifungu cha 52 (4) ya Sheria ya TCAA (2006) na matakwa ya ibara 143 ya Katiba.

4.16 Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)

4.16.1 Mgogoro wa Kutokabidhiwa Nyumba Zilizonunuliwa

BAKITA ilinunua nyumba nane kutoka Shirika la Bima la Taifa zilizopo Kijitonyama kwa Shilingi bilioni 1.5. Baadhi ya nyumba hizo hazidakabidhiwa kwa BAKITA.

Nimebani kwamba, wakazi wa nyumba hizo (wafanyakazi wa zamani wa NIC) walikataa kuondoka kwenye nyumba hizo, wakidai kuwa hawakupewa kipaumbele wakati wa zoezi la kuuzwa kwa nyumba hizo.

Ninashauri ufuatiliaji ufanyike ili hili swala liweze kufika mwisho, na nyumba hizo ziweze kutumiwa na BAKITA.

4.17 Shirika la Posta Tanzania- 2016

4.17.1 Tofauti katika Mapato Yaliyoripotiwa Shilingi Milioni 607

Ofisi 83 za posta hazijaunganishwa na mfumo wa mapato wa Netsmart. Hivyo mapato ya ofisi hizo yanarekodiwa nje ya mfumo.

Kutokana na ukosefu wa usuluishi fedha taslimu zilizopokelewa, bili za kawaida, mapato yanayowasilishwa Ofisi Kuu, pamoja na mapato ya EMS, kumekuwa na tofauti kati kilichoripotiwa katika mfumo wa Netsmart na kwenye Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kwa Shilingi milioni 607 .

TPC inahitaji kuunganisha Ofisi zote kwenye mfumo wa mapato, kufanya usuluishi wa mapato yote, pamoja na kuchunguza tofauti zinapojitokeza.

4.17.2 Kutofanyika Usuluishi wa Fedha zilizoko Benki Shilingi Bilioni 12.52

TPC imeripoti katika vitabu vyake kuhusu kuwapo fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 12.52 kufikia 30 Juni 2016. Hata hivyo, nilibaini yafuatayo:

- i. Kulikuwa na cheki zilizokwisha muda wake, Shilingi milioni 12.84;
- ii. Malipo yaliyofanywa na TPC kupitia hundi au TISS katika akaunti saba kiasi cha Shilingi milioni 152.26 hayakuvingizwa kwenye Kitabu cha fedha;
- iii. Fedha zilizoingizwa benki zinaonekana katika taarifa za kibenki Shilingi bilioni 4.60 lakini hazionekani katika Kitabu cha fedha.
- iv. Fedha zimerekodiwa kupokelewa katika kitabu cha fedha kiasi Shilingi bilioni 4.66 lakini hazionekani katika taarifa za kibenki. Taarifa hizi zinarejea Januari 2013.

Matatizo yaliyotajwa hapo juu yanatokana na kutofanyika kwa usuluhishi wa kibenki kwa wakati. Hali hii husababisha ugumu wa kuthibitisha usahihi wa taarifa za fedha zilizoonyeshwa kwenye vitabu vya mizania.

TPC ihakikishe usuluhishi wa kibenki unafanyika ipasavyo.

4.17.3 Madai na Matumizi Yaliyokosa Vielelezo

Mapitio ya Taarifa za Fedha na vielelezo vya msingi yalibaini kuwa:

- i. Shilingi bilioni 2.4 ziliziripotiwa kama madeni yanayodaiwa wateja ambazo hazikuwa na nyaraka za uthibitisho kutoka kwa wateja hao. Aidha, Shilingi milioni 623.86 walizokuwa wanadaiwa mawakala pia hazikuwa na nyaraka za uthibitisho.
- ii. Kiasi cha Shilingi milioni 739,41 hazikuambatishiwa ushahidi wa kutosha ili kuthibitisha kama ni sehemu ya biashara zilizofanywa na TPC.
- iii. Matumizi ya utawala Shilingi milioni 290.37, hayakuwa na nyaraka za uthibati.

Kwa kuzingatia mapungufu yaliyotajwa hapo juu, kiasi kilichoripotiwa katika vitabu vya mizania hakiwezi kuthibitika.

TPC lihakikishe madai yote kwa wateja na matumizi yana vielelezo vinavyojitosheleza.

4.18 Shirika la Posta - 2017

4.18.1 Mapungufu Katika Usimamizi wa Mapato ya Shirika la Posta

Ukaguzi wa mapato ya Shirika ulibaini usimamizi dhaifu wa mapato yatokanayo na huduma za mtandao, ikiwa ni pamoja na Shirika kutofanya uwianishaji wa taarifa kati ya mfumo wa Global Netsmart na mfumo wa Watcher. Pia hakuna ushahidi kuwa wasimamizi wanapitia ripoti ya fedha inayowasilishwa kila siku na mtunza fedha (cashier), na zile zinazotoka kwa mwangalizi wa ripoti za kila siku. Zaidi ya hayo, Shirika haitunzi kumbukumbu rejeshi za muda wa uangalizi wa mfumo wa matandao.

Pia, nimebaini kiwa hakuna mfumo unaosimamia uegeshaji wa magari, idadi ya magari yaliyoegeshwa na muda uliotumika. Shirika linatumia kitabu (manual register) kinachorikodi kwa mkono kumbukumbu za idadi ya magari yaliyoingia na kutoka. Na hakuna sera inayoongoza upangaji wa bei ya uegeshaji wa magari.

Kwa kuongezea, nilibaini pia kuwa shirika halina orodha ya tozo za masunduku ya posta hivyo hakuna utambuzi wa mapato kwenye mfumo wa kiuhasibu (accrual basis). Sera ya Shirika inamtaka mteja kulipa tozo la sanduku la posta kwa mwaka kati ya mwezi Januari hadi Machi; na endapo mteja atashindwa kulipia, ataondolewa huduma na kupewa mteja mwenye uhitaji. Hata hivyo, nilibaini kuwa baadhi ya wateja wa Global Netsmart hawalipi ada za masanduku ya posta wanayomiliki kwa muda mrefu. Pia shirika halitoi risiti za kielektroniki wakati wa ukusanyaji wa mapato.

Ninalishauri Shirika:

- a. Kufanya suluhisho ya taarifa kati ya Time Watcher na Poastal Global Netsmart, na kuhakikisha kuwepo kwa utunzaji na uidhinishaji wa kumbukumbu rejeshi (backups).
- b. Uwekaji wa mfumo utakaosimamia uegeshaji wa magari na idadi ya saa za kuegesha gari, kutambua uwezo wa eneo la kuegesha magari na utoaji wa risiti za kielektroniki kwa mapato yote yatayokusanywa.

4.19 Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)

4.19.1 Kutokuwepo kwa Udhibiti wa kutosha Dhidi ya Bidhaa za Zinazoingizwa Nchini

Aya Na. 6.1.3 na 6.1.4 ya Taratibu za uendeshwaji wa TFDA zinahitaji kuhakikiwa kwa taarifa za bidhaa bandarini kabla ya kuingizwa ili kuhakiki taarifa zake.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kwamba baadhi ya waagizaji waliweza kupitisha bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani 1,944,499 bandarini kwa kutumia vibali vya kughushi bila kugundulika. Hali hii inaashiria uwapo wa mapungufu katika taratibu zilizopo za udhibiti wa mifumo.

Kutokana na udhaifu huo, upo uwezekano wa kuingizwa kwa bidhaa ambazo hazina sifa ya kuingizwa nchini, hatimaye kuhatarisha afya za Watanzania.

Ninashauri TFDA kuchunguza mapungufu yaliyotajwa hapo juu na kuchukuwa hatua stahiki za kuleta marekebisho.

4.20 Mamlaka ya Kanda Maalum ya kuzalisha Bidhaa za Nje (EPZA)

4.20.1 Utendaji Usioridhisha wa wawekezaji waliopewa leseni

Taratibu za kutoa leseni zinahitaji Wawekezaji kuwasilisha Mapendekezo ya Mradi ambayo yanajumuisha mtaji unaotarajiwa kuwekezwa na ajira zitakazo tengenezwa na mradi. Hii huwa sehemu ya mkataba wa utendaji na mwekezaji baada ya tathmini kufanyika.

Katika kupitia mapendekezo yaliowasilishwa ya miradi 11 kati ya 57 yafuatayo yalibainika:

- i. Shilingi bilioni 43.41 (asilimia 33) zimewekezwa kati ya Shilingi bilioni 131.52 zilizopangwa kuwekezwa; na
- ii. Jumla ya ajira 3,850 (asilimia 87) zimetengenezwa badala ya 4,425 ambazo zilitegemewa kutengenezwa.

Hali hiyo inaweza kuzuia kufikiwa kwa malengo ya EPZA kuhusiana na ajira na ukuzaji uchumi.

Nashauri EPZA kuchukua hatua za kuboresha hali hii kwa kuhakikisha kuwa wawekezaji wanazingatia mikataba yao ya utendaji. Pia, EPZA inapaswa kufanya ufuatiliaji mara kwa mara ili kujua utekelezaji wa makubaliano.

4.21 Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)

4.21.1 Mapungufu katika Usimamizi wa Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi

Serikali zimetenga Shilingi bilioni 2.5, kupitia NEEC, ili kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji wa mwananchi (MEF) ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Fedha hizo ziliwekwa kwenye akaunti za amana za kudumu kwenye benki tatu ambazo ni Benki ya CRDB, Benki ya Posta ya Tanzania na Benki ya Uwekezaji Tanzania ili zitumike kama dhamana.

Benki hizo hutoa mikopo kwa Makundi ya Kiuchumi na kibiashara kwa kutumia taratibu za mikopo za kawaida. Hata hivyo, ilibainika kwamba Shilingi bilioni 1.05 zilitumika kulipa fidia CRDB kwa ajili ya mikopo chechefu ambapo mapungufu yafuatayo yalibainika:

- i. Hapakuwa na ushahidi wa SACCOS kusajiliwa. Kati ya SACCOS saba nilizozipitia, hapakuwa na ushahidi wa kusajiliwa kwa SACCOS mbili ambazo zilikopa Shilingi milioni 634.10 kutoka CRDB.

- ii. CRDB ilitoa Shilingi milioni 260 kwa kampuni binafsi iitwayo Matiri Company Limited kinyume na Aya 6.1 na 6.2 ya Mkataba wa Dhamana. Kampuni hiyo ilishindwa kurudisha Shilingi milioni 104.90; na CRDB ilitaka kukata fedha hizo kutoka kwenye fedha za dhamana.
- iii. Benki ya CRDB ilitoa mkopo kwa baadhi ya SACCOS zaidi ya kikomo kilichowekwa. Awali, kikomo cha mkopo kilikuwa Shilingi milioni 400; na mwaka 2012 kikomo kilibadilishwa kuwa Shilingi milioni 100.
- iv. Zaidi ya hayo, CRDB imekuwa ikitoza riba ya kiwango kimoja badala ya riba inayopungua kadri mkopo unavyolipwa, kinyume na kifungu cha 5.1 cha Mkataba wa Dhamana.

Mapungufu yaliyoainishwa hapo juu yanaonesha kushindwa kwa NEEC kutokana na usimamizi hafifu wa mfuko na kutoa mikopo kinyume na madhumuni yaliyokusudiwa na mkataba. Matokeo yake, kiasi kikubwa cha fedha za Umma kimepotea kutokana na kutoa mikopo kinyume na makubaliano.

Ninashauri NEEC kuchukuwa hatua zinazofaa ili kuhakikisha fedha zilizokopwa zinarejeshwa na zinatumiwa ipasavyo kulingana; na malengo yaliyokusudiwa.

4.22 STAMIGOLD

4.22.1 Mapungufu katika Udhibiti wa Mifumo na Hasara

Nimebaini mapungufu katika mifumo wa udhibiti wa mgodi wa STAMIGOLD ambayo yamesababisha mapungufu yafuatayo:

Kuna malipo yalifanyika mara mbili, kiasi cha Shilingi milioni 32.68, kwa M/s Afrimak kwa utoaji huduma za chakula. Malipo ya kwanza yalifanyika tarehe 21 Juni 2014, na ya pili yalifanywa tarehe 21 Julai 2014 kwa kutumia nyaraka zilizotumika katika malipo ya awali.

Hapakuwa na ushahidi wa nyaraka za mapokezi ya bidhaa zenye thamani ya Shilingi milioni 142.25. Malipo yalifanyika kwa M/s Afrimak kwa utoaji wa huduma za chakula. Ushahidi uliopatikana ulionesha kupokelewa kwa bidhaa zenye thamani ya Shilingi milioni 45.20 tu.

Kulifanyika manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni ya Randi za Afrika ya Kusini milioni 3.5, Euro 192,000, Shilingi milioni 41,000 za Kenya, Shilingi milioni 471 na Dola za kimarekani milioni 1.3 kinyume na kifungu Na. 33 (1) (d) & (e) cha Sheria ya Manunuzi (2011). Pia kulifanyika manunuzi ya Dola za kimarekani milioni 1.69 yaliyofanyika bila mkataba kwa bei iliyozidi mipaka ya jedwali la 6 na 7 la PPR,2013. Kwa mujibu wa jedwali la sita kima cha juu cha manunuzi madogo kinachoweza kufanywa ni Shilingi milioni 750.

Mazingira dhaifu ya udhibiti yaliyotajwa hapo juu yanaweza kutoa fursa ya udanganyifu.

Ninashauri STAMIGOLD kuchukuwa hatua zinazofaa ili kuboresha mazingira yake ya udhibiti na kuchukua hatua stahiki kwa ubadhirifu uliotokea.

4.23 Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)

4.23.1 Makusanyo ya Mapato chini ya Malengo Shilingi Bilioni 11.53

Shughuli za TBC zinaendeshwa kwa kutumia vyanzo viwili vya fedha, kutoka kwa Serikali pamoja na mapato kutokana na shughuli za biashara.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, TBC ilikusanya mapato ya Shilingi bilioni 8.91, sawa na asilimia 44 ya bajeti iliyoidhinishwa ya TZS 20.44 bilioni. Pia, nilibaini kuwa TBC ilitumia bajeti ya matumizi kama msingi wa bajeti ya ndani ya mapato bila kujali uwezo wa vyanzo vyake. Mfumo huu wa kuandaa bajeti ya mapato kwa kuangalia matumizi unaweza kupelekea kujumuishwa katika bajeti kiasi ambacho hakikusanyiki. Taratibu

hizi zimepelekea upungufu wa makusanyo wa Shilingi bilioni 11.589 mwaka huu.

Ninashauriwa TBC kuweka bajeti za mapato halisi, kisha kuweka bajeti halisi ya matumizi ili kupunguza upungufu wa mapato. Pia, shirika linapaswa kuwa na ubunifu katika kuzalisha na kukuza programu za redio na televisheni ambazo zingevutia zaidi wa dhamini wa matangazo kwa lengo la kuongeza mapato.

4.23.2 Uwekezaji Usio na Tija

TBC ni mmoja wa wanahisa wa Star Media Tanzania Limited kwa kumiliki hisa za asilimia 35 ya mtaji. Sehemu nyingine ya asilimia 65 zinamilikiwa na Star Communication Network Technology Limited (kampuni ya Kichina).

Ufuatiliaji wangu wa uwekezaji wa TBC katika Star Media Tanzania Limited ulibainisha kuwa Taarifa za Fedha za Kampuni zilizokaguliwa zilikuwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2013; ambapo ziliripoti hasara za Dola za Kimarekani milioni 3.39 (takribani Shilingi bilioni 5.34).

Taarifa za Fedha za mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2014, ambazo hazijasainiwa na Mwenyekiti wa Bodi na Wakaguzi wa nje (Ernst & Young) zinaonesha hasara ya Dola za Kimarekani milioni 8.63; na jumla ya hasara ya Dola za Kimarekani milioni 12.02 (takriban Shilingi bilioni 20.75 bilioni). Hadi Juni 30, 2016 iliripotiwa hasara za takribani Shilingi bilioni 61.14.

Kufuatia hasara hii kubwa, TBC haijawahi kupokea gawio lolote katika uwekezaji huu tangu 2013. Hali hii ni kinyume na lengo la uwekezaji.

Ninaishauri TBC kuchukua hatua ambazo zitahakikisha kwamba shughuli zote za kifedha zinafuatiliwa na kusimamiwa kwa ukaribu.

4.23.3 Tofauti ya Deni Lililoonyweshwa kwenye Vitabu vya TBC Shilingi Milioni 922.05.

Hadi kufikia Juni 30, 2017, TBC imeripoti deni linalotokana na huduma zinazotolewa na TTCL linalofikia kiasi cha Shilingi bilioni 1.25. Kuthibitisha deni hili TTCL, ilibainika kuwa inaidai TBC kiasi cha dola za Kimarekani 974,638.55 (sawa na Shilingi bilioni 2.17) tofauti ya Shilingi milioni 922.05.

Mapitio yangu ya barua kutoka TTCL ya tarehe 27 Oktoba 2017 yanaonesha kuwa pande hizi mbili zinatofautiana juu ya deni la kiasi cha Dola za Kimarekani 473,772; ambapo zipo kwenye majidiliano juu ya kiasi hicho.

Naishauri TBC kufuatilia jambo hili kwa ukaribu na kutafuta muafaka ili kuweza kuweka kumbukumbu sahihi katika vitabu vyake vya hesabu.

4.24 Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO)

4.24.1 TRA Kutowasilisha Ushuru wa Maendeleo ya Reli ya Shilingi Bilioni 194.31 kwa RAHCO

Mwaka 2014 yalifanyika marekebisho ya Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usimamizi wa Forodha ya Mwaka 2004 (EAC Customs Management Act (2004)) kwa kuweka ushuru wa miundombinu ya asilimia 1.5 kwenye bidhaa zote zinazolingizwa nchini. Kiwango hicho kinatakiwa kutozwa kwenye thamani ya forodha ya uingizaji bidhaa ndani ya Jumuiya.

Tanzania, kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2015, ilipitisha kiwango cha asilimia 1.5 kama Ushuru wa Maendeleo ya Reli kwenye bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje isipokuwa kwa bidhaa zenye msamaha kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Namba 5 la Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usimamizi wa Forodha ya Mwaka 2004.

Kiasi kinachokusanywa kinatakiwa kuhifadhiwa kwenye akaunti ya RAHCO iliyopo Benki Kuu. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha

2016/2017. Mamlaka ya Mapato (TRA) ilikusanya Ushuru wa Maendeleo ya Reli wa Shilingi bilioni 194.31 bila kuwasilisha RAHCO kama invyotakiwa na sheria.

Ninashauri Mamlaka ya Mapato kuwasilisha kwa wakati kiasi chote cha makusanyo ya Ushuru wa Maendeleo ya Reli kwa RAHCO.

4.24.2 Kushuka Thamani kwa Miradi ambayo Haijakamilika ya Shilingi Bilioni 1.61

Ukaguzi ulibaini kuwa miradi ya Shilingi bilioni 1.61 haijakamilika kwa muda mrefu.

Miradi hiyo kwa sasa haina thamani tena kwa sababu mbalimbali kama vile, mabadiliko ya Sera za Serikali, Makao Makuu ya RAHCO kuhamishiwa Dodoma, pamoja na Kubadilika kwa Mpango Mkakati wa Kampuni kwenda kwenye ujezi wa reli kiwango cha Standard Gauge Railway (SGR).

Mapitio ya hesabu za RAHCO zinazoishia tarehe 30 Juni 2017 yanaonesha kuwa miradi hiyo imeondolewa kwenye miradi inayoendelea hadi kuwa miradi isiyo na thamani.

Kwa hali hiyo, fedha iliyotumika kwenye miradi hiyo haikutekeleza malengo ya muda mrefu ya kampuni, hivyo kuiletea RAHCO hasara.

Nashauri kampuni ya RAHCO ifanye uchunguzi wa aina ya miradi na kufanya uamuzi sahihi kuhakikisha miradi inamalizika au kuwachukulia hatua viongozi wote waliohusika kuisababishia hasara kampuni hiyo.

4.24.3 Kutoanza kwa Miradi licha ya Upembuzi Yakinifu Kufanyika kwa Jumla ya Shilingi Bilioni 20.1

Nilibaini kuwa katika kipindi kilichoishia 30 Juni 2017, RAHCO ilishafanya upembuzi yakinifu wa miradi ifuatayo:- Arusha-Musoma, Mtwara-Songea-Mbambabay, Uvinza-Musongati-Mpanda-

Karema na Tabora-Kigoma-Kaliua-Mpanda kwa kutumia gharama ya Shilingi bilioni 20.1.

Hata hivyo, licha ya kumalizika kwa upembuzi yakinifu wa miradi hiyo kipindi kirefu kilichopita, utekelezaji wa miradi hiyo haujafanywa hadi kipindi cha ukaguzi unakamilika kwa sababu ilielezwa ilielezwa kuwa ni ukosefu wa fedha.

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2017, gharama za upembuzi huo zimeripotiwa kama miradi inayoendelea licha ya kutokuwapo kwa bajeti ya miradi hiyo, hivyo kufanya malengo ya kampuni kutotimizwa na gharama zake kutokuwa na thamani ya fedha.

Nashauri RAHCO kutafuta namna ya kupata fedha ili kutekeleza miradi husika ili kufikia malengo yaliyotazamiwa. Pia, siku zijazo RAHCO ihakikishe haifanyi upembuzi yakinifu kama fedha za utekelezaji wa miradi husika hazipo.

4.24.4 Usimamizi wa Mikataba Usioridhisha

Ukaguzi wangu wa RAHCO ulibaini yafuatayo kutokana na usimamizi usioridhisha wa mikataba:

(i) Mapungufu kwenye Mikataba ya Ukodishaji kati ya RAHCO na Wakodishwaji

Nilibaini kuwa, mkataba baina ya RAHCO na wakodishwaji wake una vigezo na masharti yaliyowekwa tangu enzi za mabadiliko ya TRC kwenda RAHCO na TRL. Hii inaonesha kuwa masharti mengi yamepitwa na wakati na hayaendani na hali ya sasa ya soko. Pia, nilibaini kuwa wakodishaji wengi hawana mikataba hai kutoka RAHCO licha ya kulipa gharama za ukodishwaji kwa wakati.

Pia nilibaini kuwa hakuna makubaliano ya kisheria kati ya RAHCO na wakodishaji yanayoonesha vigezo na masharti baina yao.

Nashauri RAHCO ifanye mapitio ya mikataba ili iendane na hali ya sasa ya soko, kisha kusaini mikataba mipya na wapangishwaji wake mapema iwezekanavyo.

(ii) Mapungufu kwenye Malipo ya Pango baina ya RAHCO na Wapangaji

Nilibaini kuwa wapangani wa RAHCO wa eneo la Chuda, jijini Tanga, hawajalipa malipo ya pango kwa muda mrefu.

Nilibaini kuwa katika miji ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga kuna maelekezo yenye mkanganyiko juu ya nani anayetakiwa kukusanya malipo ya pango, hivyo kupelekea baadhi ya wapangaji kulipa Tanzania Railway Limited (TRL) au Tanzania Building Agency (TBA), na siyo kwa RAHCO. Nilijulishwa kuwa, timu ya watu kutoka TRL iliwatembelea na kuwataka wapangaji hao wawe wanalipa malipo ya pango kwenye akaunti ya TRL au Ofisi ya Mkuu wa Stesheni badala ya kulipia RAHCO.

Sikupata ushahidi wa kutosha wa sababu za msingi zilizofanya malipo haya yawe yanalipwa TBA na TRL na siyo RAHCO ambaye ndiye msimamizi wa mali hizo.

Naishauri RAHCO kufuatilia swala hili ili kuhakikisha malipo ya pango yanalipwa kwa kampuni hiyo. Pia, malipo yote yaliyolipwa na wapangishwaji hao TRL na TBA yaombwe na kurejeshwa RAHCO.

(iii) Mapungufu Yaliyobainika kwenye Mkataba wa Ukodishaji kati ya RAHCO na Kampuni ya Monaban Trading and Farming

Mwezi Agosti 2015, RAHCO ilisaini mkataba wa ukodishaji wa eneo la Kitalu Namba 121/E lililopo barabara ya Factory jijini Arusha na kampuni ya Monaban Trading and Farming Co. Hata hivyo, nilibaini kampuni ya Monaban ilijenga uzio wa kudumu na maduka ambayo imepangisha

watu wengine bila ridhaa ya RAHCO, kinyume na masharti ya mkataba. Ujenzi wa uzio ulijengwa mita sita ndani kutoka kwenye mpaka halisi wa eneo hilo.

Pia nilibaini kuwepo kwa biashara nyingine kama vile maduka na sehemu ya kuoshea magari kinyume na masharti ya ukodishwaji wa eneo.

Nashauri RAHCO ichukue hatua ya kisheria dhidi ya kampuni ya Monaban Trading and Farming ili kusimamia makubaliano ya mkataba wa ukodishaji.

(iv) Mapungufu kwenye Ukodishaji wa Klabu ya TRC Bombo Tanga

RAHCO ilikodisha klabu ya TRC iliyopo eneo la Bombo jijini Tanga kwa Bw. Carlistus Z. Livigha kwa kiwango cha Shilingi 354,000 kwa mwezi kwa kipindi cha miezi mitatu.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kuna mgogoro wa mpaka baina ya majirani wa eneo la klabu na mkodishwaji. Mgogoro huu ulisababisha uongozi wa klabu kukatazwa kuingia na kutumia eneo la klabu kwa maelezo kuwa eneo hilo liliuzwa kwa jirani huyo na TRC. Nyumba hiyo inayosemekana kuuzwa kwake na TRC ina uzio wake binafsi, na iko nje ya eneo la klabu ya TRC.

Nashauri RAHCO ichukue hatua ya kisheria dhidi mhusika ili kulinda rasilimali zake.

4.25 Bodi ya Pareto Tanzania

4.25.1 Hali Dhoofu ya Bodi ya Pareto

Ukaguzi wangu wa Bodi ya Pareto ulibaini kuwa, kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2017 bodi ilifanikiwa kukusanya mapato ya Shilingi milioni 170.82, sawa na asilimia 17 ya bajeti ya mapato iliyopanga kukusanya ya Shilingi milioni 834.29. Licha ya

hivyo, matumizi ya bodi yalikuwa zaidi ya mapato kwa asilimia 52.

Bodi imepata hasara mfululizo katika kipindi cha miaka miwili mfululizo ambazo ni Shilingi milioni 7.94 katika mwaka wa fedha 2014/2015 na Shilingi milioni 226.97 katika mwaka wa fedha wa 2015/2016. Hali hii inaleta hali hasi ya mtaji wa kazi (negative working capital) ya Shilingi bilioni 1.17.

Hali ya ukata wa bodi imechangiwa kwa kiwango kikubwa na kutofikiwa kwa malengo ya mapato na kutodhibitiwa kwa matumizi yanayoenda na mapato yaliyopatikana mwaka huu.

Kutokana na hayo, hali ya bodi inatia shaka kwa kushindwa kuwa na fedha za kutekeleza majukumu yake hivyo kuelekea kufilisika.

Bodi ilishindwa kufikia malengo yake makuu ya kuwahamasisha wakulima mashamba ya pareto kwa kutumia teknolojia bora na njia na mbinu za kisasa za ukaushaji, kulima, kutunza viatlu na mashamba.

Nashauri Serikali kupitia upya Sheria Namba 1 ya Pareto ya mwaka 1997 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Mazao Namba 20 ya mwaka 2009 kwa lengo la kuanzisha tozo kwa wanufaika wa pareto ili kupatikana kwa fedha zitakazosaidia bodi kuendeleza na majukumu yake.

4.25.2 Kutolipwa kwa Madai ya Watumishi ya Shilingi Milioni 310.24

Nilibaini kuwa Watumishi wa Bodi ya Pareto wana madai ya jumla ya Shilingi milioni 310.24 yaliyokaa zaidi ya mwaka mmoja bila kulipwa. Madeni hayo yanahusisha mishahara, likizo, kiinua mgongo na mafao ya kustaafu. Hali hii inawanyima watumishi haki ya msingi, na inaweza kupelekea morali ya kazi kushuka.

Nashauri Serikali iingilie kati kuisaidia Bodi ya Pareto kulipa madeni ya watumishi wake kwa wakati.

4.26 Kituo cha Mahusiano ya Kimataifa (CFR)

4.26.1 Bajeti ya Shilingi Bilioni 14.53 Kutolipwa kwa Asilimia 100

Nia ya Kituo cha Mahusiano ya Kimataifa ni kutoa mafundisho ya kitaaluma na kimkakati, kufanya utafiti, kufanya utetezi wa sera na kukuza mahusiano ya kimataifa, pamoja na kuweka msisitizo kwenye shughuli za kidiplomasia kwa mawanda ya kitaifa na kikanda. Shughuli zilizotajwa hapo juu zinaweza kukamilika ikiwa kuna fedha za kutosha kwa ajili ya upatikanaji wa vifaa vinavyohitajika.

Mapitio yangu yalibaini kuwa, katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2017, CFR ilipitishiwa bajeti ya maendeleo ya Shilingi bilioni 14.53 huku bajeti ya matumizi mengineyo ikiwa Shilingi milioni 882, hivyo kufanya bajeti nzima kuwa Shilingi bilioni 15.414.

Hata hivyo, katika mapitio ya utendaji ya taasisi nilibaini kuwa malengo ya mwaka hayakufikiwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha kutoka Wizara ya Fedha. Nilibaini kuwa ni asilimia 49 tu ya bajeti ya matumizi mengineyo iliweza kupelekwa kwenye kituo hicho, huku fedha za maendeleo zilizopitishwa wakati wa bajeti hazikupelekwa.

Nashauri Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, sambamba na Wizara ya Fedha na Mipango kujadiliana na kukubaliana ni namna gani Kituo cha Mahusiano ya kimataifa kinaweza kuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa usahihi, ikiwemo kupewa fedha zake za bajeti kwa wakati.

4.27 Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)

4.27.1 Udanganyifu Ulioleta Hasara ya Shilingi Milioni 130.6

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ilipoteza kiasi cha Shilingi milioni 130.6 kutokana na ubadhirifu uliofanywa na mlipa fedha (cashier) kutokana na mapungufu kwenye mifumo ya uthibiti.

Ubadhirifu huu umeipunguzia taasisi uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mpango wa utekelezaji wa mwaka.

Mapitio yangu yalibaini ubadhirifu huu umeripotiwa Polisi kwa hatua zaidi za utekelezaji.

Nashauri Taasisi ya Moyo ya Jakaya kuendelea kufatilia hii kesi ili kuhakikisha maamuzi ya mwisho yanapatikana ili waliouhusika wachukuliwe hatua inayostahili. Pia, taasisi iongeze udhibiti wa mifumo ya ndani itakayopunguza uwezekano wa ubadhirifu kwa kugawanya majukumu ya watumishi, kuhamisha watumishi mara kwa mara, na kufanya mapitio ya mara kwa mara ndani ya taasisi.

4.28 Chuo cha Mabaharia Dar es Salaam (DMI)

4.28.1 Ubadhirifu katika Malipo ya Dola za Kimarekani 26,356.65 na Euro 2,500

Nilibaini kuwa tarehe 8 Desemba 2016, Chuo cha Mabaharia kiliamisha kiasi cha Dola za Kimarekani 26,356.65 na Euro 2,500 kutoka akaunti namba 012105004460 iliyopo Benki ya Biashara ya Taifa (NBC) kwenda akaunti namba 83261395 yenye jina la VIKING Life-Serving equipment (SA) iliyopo benki ya Barclays PLC badala ya kupitia FNB Bank ya South Afrika kwenye akaunti namba 62009015050 kwa lengo la kununua vifaa vya uokozi na huduma ya mafunzo kutoka Kampuni ya VIKING South Africa.

Pia nilibaini kuwa, mawasiliano ya barua pepe baina ya mtumishi wa Chuo cha Mabaharia na kampuni ya Viking SA yalidukuliwa na watu wasiojulikana, hivyo kupelekea ubadhirifu huo. Ankara ya malipo namba 95701885 kutoka kwa mdukuzi ilitumwa kupitia barua pepe binafsi ya mtumishi wa DMI ikiwa na akaunti feki ya malipo. Idara ya Uhasibu ilipata Ankara ya malipo kupitia mtumishi huyo na kufanya utaratibu wa malipo bila kuifanyia mapitio ya kina. Sambamba na hilo, chuo kiliripoti udanganyifu

huu kwa Kitengo cha Makosa ya Mtandao ila kupata uthibitisho wa mwenendo na hatua iliyofikiwa.

Nilibaini pia kwamba, matumizi ya barua pepe binafsi kwa mawasiliano ya kiofisi ndiyo chanzo cha ubadhirifu wa fedha hizo sambamba na mapungufu makubwa kwenye mifumo ya ndani ya udhibiti wa malipo.

Nashauri Chuo kufuatilia kwa umakini mwenendo wa ubadhirifu huo kwa kitengo cha Makosa ya Mtandao cha Jeshi la Polisi ili kujua hatua iliyofikiwa ili kufanikisha upatikanaji wa fedha hizo. Pia, nashauri chuo kihakikishe mifumo ya ndani inawezesha upitiaji wa usahihi wa nyaraka za malipo ili kuhakikisha fedha zote zinalipwa kwenye akaunti halali.

4.28.2 Kutokuwapo kwa Kanzidata ya Wanafunzi wa Kozi Fupi

Wakati wa kaguzi wa mapato yaliyotokana na kozi fupi, nilibaini kuwa hakuna kanzidata ya kuhifadhi taarifa za kozi fupi kama idadi ya kozi zilizofanyika kwa mwaka na idadi ya wanafunzi waliojiunga kwa mwaka. Pia, nilibaini kuwa, taarifa ziliandaliwa nje ya mfumo baada ya kuziomba kwa ajili ya ukaguzi. Sambamba na hayo, hakukuwa na taarifa ya uwanishaji wa idadi ya wanafunzi waliodahiliwa dhidi ya ada iliyolipwa kwa muhula wa masomo.

Kwa utaratibu huu, ni vigumu kubainisha usahihi wa malipo ya ada ya wanafunzi yaliyotokana na mafunzo ya muda mfupi.

Nashauri Chuo kuwa na kanzidata ya wanafunzi wa mafunzo ya muda mfupi ili kuwa na taarifa sahihi za idadi ya wanafunzi waliohudhuria mafunzo, idadi ya mafunzo yaliyofanyika kwa mwaka na idadi ya wanafunzi waliopata mafunzo. Sambamba na hilo, kitengo cha uhasibu kiwe kinafanya uwanishaji wa ada iliyolipwa kwa kila kozi fupi na idadi ya wanafunzi waliohudhuria ili kuleta usahihi wa taarifa za fedha.

4.29 Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

4.29.1 Kutokusanywa kwa Mikopo Yenye Thamani ya Shilingi Milioni 303

Vifungu 2.5.1 (a) na Kifungu 2.5.4 (vii) vya Mwongozo wa Uwekezaji wa Mamlaka ya Elimu Tanzania wa mwaka 2008 vinataka waombaji wa mkopo kuwasilisha mapendekezo ya mradi (project proposal) katika utaratibu unaotakiwa na TEA ili kubaini uwezo wa muombaji wa kulipa mkopo kwa kuwasilisha tathmini ya mtiririko wa fedha kwa kipindi chote cha mkopo; pia, waombaji wenye historia ya kutorejesha mkopo kutopewa mikopo hadi itakapoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka.

Mapitio yalibaini kuwa mamlaka ilifanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi milioni 830 katika sampuli ya mikopo yenye jumla ya Shilingi bilioni 1.69, hivyo kupelekea kiasi ambacho hakijakusanywa kuwa cha Shilingi milioni 303 katika mwaka wa fedha 2016/2017 kutoka katika shule na taasisi za elimu na Shilingi milioni 560 ni kiasi ambacho muda wake wa marejesho bado haujafika.

Mamlaka inapoteza fedha nyingi kutokana na kutorejeshwa kwa mikopo mingi iliyokopeshwa kwa taasisi za elimu na shule ambazo hazirejeshi mikopo hiyo.

Ninaishauri Mamlaka ya Elimu Tanzania kuboresha mbinu ya kutathmini wakopaji kabla ya kutoa mikopo au kubadili Kanuni za msingi za Uwekezaji. Pia, kuandaa mkakati wa namna ya kukusanya mikopo ambayo haijarejeshwa.

4.29.2 Miradi Kuchelewa Kuanza

Ukaguzi wa miradi ulibaini kuwa Shilingi bilioni 28 zilipitishwa na Bodi ya Wakurugenzi kutekeleza miradi. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2017, nilibaini hakuna malipo yaliyofanywa kwenye utekelezaji wa miradi. Hii ni kwasababu baadhi ya miradi ilikuwa haijaanza na iliyoanza haijakamilika. Licha ya hivyo, kiasi tajwa

kilionyeshwa kwenye orodha ya wadeni kwenye hesabu za mamlaka.

Kati ya Shilingi bilioni 28, Shilingi bilioni 16 zinahusika na miradi ambayo haijaanza kutekelezwa, huku kiasi cha Shilingi bilioni 14.72 kikihusisha na miradi iliyotakiwa kutekelezwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2017. Shilingi bilioni 12 zilizobaki, inahusika na miradi iliyokwisha kuanza ila haijakamilika. Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi kunachelewesha malengo yaliyokusudiwa kutoka kwenye miradi hiyo.

Nashauri mamlaka kuendelea na mipango ya miradi ambayo haijatekelzwa huku ikizingatia uwezekano wa ongezeko la gharama. Pia, nashauri waje na namna sahihi ya kurekodi gharama halisi za mradi.

4.29.3 Mkataba Usioridhidha baina ya TEA na Kampuni ya Watumishi Housing

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, TEA iliingia mkataba na kampuni ya Watumishi Holding mnamo tarehe 16 Juni 2016 kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za Walimu kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi kwa mkataba wa awali wa Shilingi bilioni 4 ambako ilielekezwa gharama ya kila nyumba isizidi Shilingi milioni 126. Tarehe 29 Juni 2016, Ongezeko Namba 1 la mkataba lilisainiwa kwa kuelekeza ni nyumba 40 tu zitajengwa kwa bei ya Shilingi milioni 126 kwa nyumba. Gharama hizo ziliongeza thamani ya mkataba kufikia Shilingi bilioni 5.04. Hata hivyo, sikuweza kupata uthibitisho wa Bodi ya kuiidhinisha ongezeko la Shilingi bilioni 1.04.

Sambamba na hayo, mnamo tarehe 21 Aprili 2017, ongezeko Namba 2 la mkataba lilisainiwa huku likibadilisha gharama ya ujenzi wa nyumba kutoka Shilingi milioni 126 hadi Shilingi milioni 145.57 kwa nyumba 40; Hata hivyo, pia sikupatiwa uthibitisho uliobariki maamuzi hayo.

Zaidi ya hayo, Ongezeko Namba 2 la mkataba lilibadilisha namna ya ulipaji kutoka kuanza na 40% ya gharama ya nyumba ikifuatiwa na 30%, 20%, 5% na baadaye 5% baada ya kipindi cha uangalizi hadi malipo ya awali ya 80% na 20% baada ya kukamilika kwa mradi. Hata hivyo, mkataba uliondoa kipengele cha kuwapo kwa kipindi cha uangalizi, na hakukuwa na kumbukumbu ya maamuzi yaliyobariki mabadiliko hayo. Kampuni ya Watumishi Housing ilikamilisha ujenzi wa nyumba 15 kwa kutumia kiasi cha Shilingi bilioni 2.01 na kushindwa kumaliza ujenzi wa nyumba nyingine 5 na kurudisha kiasi cha Shilingi milioni 687.12 kwa TEA kama fedha za nyumba ambazo hazikujengwa.

Naamini mkataba kati ya TEA na kampuni ya Watumishi Housing una viashiria vya kutokuwa na maslahi kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania.

Nashauri mamlaka kuchunguza matukio yote yaliyoufata baada ya mkataba wa kwanza.

4.30 Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA)

4.30.1 Udhhibiti Usioridhisha wa Gharama za Matumizi ya Umeme na Maji

Nilibaini kuwa katika eneo la makao makuu ya Chuo kuna jumla ya mita za umeme 21 zenye matumizi ya Shilingi milioni 504 kwa mwaka huku kukiwa na mita za maji 5 zenye matumizi ya Shilingi milioni 46 kwa mwaka; wakati kampasi ya Solomoni Mahlangu ina jumla ya mita 5 za umeme zenye matumizi ya Shilingi milioni 380 kwa mwaka na mita moja ya maji yenye matumizi ya Shilingi milioni 499 kwa mwaka.

Pia niligunda kuwa gharama za umeme na maji za wapangaji wa chuo zinatozwa kwa bei isiyobadilika na isiyotegemeana na matumizi halisi ya Shilingi 45,000 kwa mwezi kwa umeme na Shilingi 25,000 kwa mwezi kwa maji.

Chuo kinatumia gharama kubwa za umeme na maji ambazo zinachangiwa kwa kiwango kidogo na watoa huduma za maduka, migahawa, na nyumba za wafanyakazi.

Ninashauri SUA kufanya tathmini ya matumizi ya umeme, maji kisha kufunga mita tofauti kwa kila mtumiaji jambo litakalosaidia uongozi wa chuo kufanya maamuzi sahihi kulingana na matumizi.

4.31 Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Songea (SOUWASA)

4.31.1 Kuondolewa kwa Mzabuni Mwenye Gharama Ndogo Bila Kufata Taratibu

Kanuni ya 17 (1-4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inaitaka taasisi inayofanya manunuzi kuomba ufafanuzi kutoka kwa mzabuni, kuthibitisha taarifa kutoka kwa mzabuni, kuhifadhi uthibitisho na ufafanuzi huo kwa maandishi, kupata idhini kabla ya kumuengua mzabuni mwenye bei ya chini zaidi ikiwa bei yake ni ndogo sana kuliko bei ya soko, na kumjulisha mzabuni.

SOUWASA iliwaalika wazabuni kwa ajili ya uchimbaji wa mitaro, ulazaji wa mabomba, na uwekaji wa mita za maji. Wazabuni wanne walijitokeza kwa kuanisha gharama ya kazi hizo kama ifuatavyo:

Jedwali 1: Kuondolewa kwa Mzabuni Mwenye Gharama Ndogo

Na	Wazabuni	Kiasi (TZS)
1	M/s Msae General Supplies Ltd	209,704,585
2	M/s Shilo Construction Company	179,000,000
3	M/s Almasi General Supplies	211,062,824
4	M/s Matonga Civil Engineering Contractors and General Supplies	230,736,020

Wazabuni wote walifanikiwa kuvuka hatua ya tathmini ya awali na tathmini ya kina. Hata hivyo, kampuni ya M/s. Shilo Costruction ambayo ilikuwa mzabuni mwenye bei ya chini zaidi

iliondolewa kwa sababu sehemu moja ya nyaraka zake ilinukuliwa kwa kiwango cha chini kuliko kiwango cha soko, lakini hakukuwa na ushahidi kuwa taratibu sahihi zilifuatwa kuthibitisha hili kama Kanuni za Manunuzi ya Umma zinavyotaka.

Zabuni hiyo ilitolewa kwa kampuni ya M/s. Msae General Supplies Ltd kwa Shilingi milioni 209.70 licha ya kampuni ya M/s. Shilo Costruction kupeleka malalamiko kwa SOUWASA juu ya ukiukwaji wa taratibu za manunuzi.

Ukiukwaji uliobainika unaweza kuwa ni dalili ya udanganyifu, hivyo kufanya manunuzi yaliyofanywa kutokuwa na thamani ya fedha.

Ninatoa wito kwa taasisi za kiuchunguzi kufanya uchunguzi wa Kamati ya Tathmini, Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU), na Bodi ya Zabuni kama hakukuwa na udanganyifu kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

4.32 Benki ya Biashara ya TIB

4.32.1 Uwiano wa Mtaji Usioridhisha

Kanuni namba 9 ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Utoshelevu wa Mtaji) inaitaka benki au taasisi ya fedha, wakati wote kudumisha kiasi cha chini cha mtaji usiopungua asilimia kumi na mbili na nusu ya jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa hesabu (off-balance sheet exposure) na mtaji wa jumla usiopungua asilimia kumi na nne na nusu ya jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa kimaheسابu. Hata hivyo, kwa mwezi wa Desemba 2016, utoshelevu wa mtaji wa msingi na mtaji wa jumla wa benki ya Biashara ya TIB ulikuwa asilimia 12 ambayo ni chini ya kiwango cha chini cha mahitaji ya mtaji.

Kushindwa kwa benki kuzingatia kanuni zilizowekwa kunaweza kuisababishia benki adhabu, ikiwa ni pamoja na kupokonywa leseni.

Naishauri Benki ya Biashara ya TIB kupitia upya viwango vya chini vya mtaji na kuchukua hatua thabiti kudumisha kiwango hicho kwa lengo la kuboresha hali ya benki na uendeshaji.

4.33 Benki ya Maendeleo ya TIB

4.33.1 Dhamana Pungufu zawekwa Katika Mikopo

Katika ukaguzi imebainika kuwa baadhi ya dhamana zilizowekwa rehani kwenye mikopo zilikuwa chini ya asilimia 125 ya jumla ya mikopo ambayo ni kinyume na Kanuni namba 9 ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2011. Jedwali la hapa chini linaonyesha orodha ya mikopo pamoja na dhamana zake ambazo zimewekwa rehani:

Jedwali 2: Dhamana Pungufu zilizowekwa dhidi ya mikopo

Na	Jina La Mteja	Kiwango cha Mikopo TZS 'm	Dhamana ya Mikopo TZS 'm	Asilimia ya dhamana ya Mikopo
1	Mzinga Corporation	90,518	0	0
2	Kampuni ya Hodi (Usimamizi wa Hoteli)	5,459	6,710	123
3	Kampuni ya Konecct Wires na Cables	4,560	5,122	112
4	Kampuni ya Iron 2011	1,610	1,589	99
5	Kampuni ya Kilimanjaro Roses	129	0	0
6	Kampuni ya uwekezaji wa Allvess	20	18	90

Benki itapata hasara endapo mikopo haitarudishwa. Pia, kuna uwezekano wa Benki Kuu ya Tanzania kutoza faini na adhabu.

Benki ya Maendeleo ya TIB inashauriwa kufanya uchunguzi wa kina wa dhamana zilizoahidiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha

dhamana zote za mikopo zinatoshwa kuepukana na hasara itokanayo na kutorejeshwa kwa mikopo.

4.33.2 Mapungufu katika Utoaji wa Mikopo

Katika ukaguzi wangu nilibaini mapungufu yafuatayo ambayo yanaonyesha dalili za mapungufu kwenye mchakato mzima wa utoaji mikopo na ufuatiliaji wa mikopo hiyo:

- i) Benki ya Maendeleo ya TIB ilitoa mkopo wa Shilingi bilioni 2.9 mwezi wa Desemba, 2014 kwa ajili ya kufadhili ujenzi wa kiwanda cha Kaboja kilichoko Kijiji cha Kihangaiko, Bagamoyo-Msata. Mkopo huo ulidhaminiwa na mali za kampuni mama ya kiwanda cha Kaboja iitwayo Syscorp pamoja na ardhi ya ekari 2,500 ambayo ndiyo eneo lililopendekezwa kujengwa kiwanda hicho. Hata, hivyo Mkopo huo ulifutwa kwenye vitabu vya benki kwa kiasi cha Shilingi bilioni 3.8 baada ya mkopo huo kuonekana kuwa chechefu hadi kufikia robo ya nne ya mwaka ya 2016.

Pia, sikuweza kuona hati ambazo zilikuwa zimewekwa kama dhamana wala ushahidi wowote ambao unaonyesha kuwa dhamana hizo zilikuwa zinatambuliwa na benki.

- ii) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilipata Mkopo wa dola milioni 27.18 kwa ajili ya kulipia hati ya madai ya 80mmscf/d ya gesi. Dhamana zilizoahidiwa dhidi ya mkopo huu zilijumuisha malipo ya TPDC kwenye Gharama za Gesi na Faida za Gesi kama ilivyo kwenye makubaliano ya Mkataba wa Mnazi Bay ambao unaonyesha TPDC ina maslahi ya asilimia 20 ya faida. Hakuna ushahidi wowote wa benki wenye kuhakikisha kuwa dhamana hizo zipo kamilifu.
- iii) Shirika la nyumba Tanzania (NHC) lilipewa mkopo wa muda mrefu wenye thamani ya Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kujenga Golden Premier Upanga ambayo baadaye ilihamishwa Kawe kama Golden Anniversary. Kutokana na

mpangilio huu, NHC iliendeleza utaratibu mwingine wa muda mfupi wa kuomba mkopo wa kugharamia ujenzi wa daraja lenye thamani ya Shilingi bilioni 7 kwa Mradi wa Morocco Seven Eleven. Mkopo huo ulidhaminiwa na taarifa ya mali, madeni na mtaji wa shirika la Nyumba na malipo yatakayofanyika ndani ya miezi miwili.

Hakukuwa na ushahidi unaoonesha kuwa Benki ya maendeleo ya TIB ilifanya tathmini ya awali ya Mradi wa Morocco Seven Eleven kabla ya kupitisha na kulipa Mkopo huo wa Shilingi bilioni 7. Pia, sijaona makubaliano au ushahidi wowote unaoonesha kuwa mkopo huo wa Shilingi bilioni 7 ulirejeshwa au kuelekezwa upya kwenye ujenzi ule wa kawe wa Golden Anniversary.

Kutoa mikopo bila ukamilifu wa usalama wa dhamana huongeza hatari ya kuokoa fedha zilizokopwa ambazo huathiri utendaji wa benki kutokana na mikopo chechefu.

Benki hiyo inapaswa kuimarisha udhibiti wake juu ya tathmini ya mikopo na kuhakikisha kwamba mikopo haitatolewa kabla ya kujihakikishia ukamilifu wa dhamana.

4.33.3 Ongezeko katika Mikopo Chechefu

Nilibaini kuwapo kwa ongezeko kubwa la madeni chechefu kufikia kipindi cha mwisho wa mwaka.

Kufikia tarehe 31 Desemba 2016, kiwango cha madeni chechefu kilifikia asilimia 35 kulinganishwa na asilimia 14 kilichoripotiwa mwaka 2015. Ongezeko hili la asilimia 24 ni la juu ikilinganishwa na mikopo chechefu kwenye sekta ya benki. Pia, kulingana na taarifa za sera za fedha kwa Benki kuu ya Tanzania zilizotolewa mwezi Juni, 2016, uwiano uliopendekezwa kwa mikopo chechefu katika sekta ya benki ni wa asilimia 5.

Ongezeko la mikopo chechefu linanesha kuzorota kwa ubora wa huduma za kibenki.

Ninapendekeza Benki ya Maendeleo ya TIB inapendekezwa iongeze jitihada zaidi za kuimarisha udhibiti juu ya taratibu za utoaji wa mikopo ili kuepuka hatari ya mikopo chechefu.

4.33.4 Mapungufu kwenye utoaji na Ufuatiliaji wa ulipwaji wa Mikopo.

Katika mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2016, Benki ya Maendeleo ya TIB ilifuta idadi kubwa ya mikopo hadi kufikia kiasi cha bilioni 94 ambayo imetokana na miradi yake kuwa chechefu. Hivyo, benki ilitoa notisi ya siku 30 kwa wadeni hao na kuwataka walipe mikopo hiyo. Upitiaji wa mikopo hii unaonesha mapungufu kwenye ufuatiliaji wa ulipaji wa mikopo hiyo hadi kufikia hatua ya kuwa chechefu. Hadi wakati wa kumaliza ukaguzi wangu mwezi machi, 2017, kiasi cha Shilingi bilioni 2.9 tu ndicho kilichokusanywa ambacho ni sawa na asilimia 3 ya mikopo yote.

Pia, Ukaguzi wangu ulibaini kuwa makusanyo kwenye mikopo yaliyofutwa ilikuwa chini sana ya matarajio ya ukusanyaji ambao benki uliwekeana na wadaiwa hao. Benki iliweza kukusanya Shilingi bilioni 6.2 ambayo bado ni chini ya malengo yaliyowekwa ya Shilingi bilioni 10.

Ingawa wakopaji walipewa onyo kali endapo watashindwa kulipa mikopo hiyo kwa kipindi walichopangiwa, bado niliweza kuwa kubaini ukusanyaji ni wa kiwango cha chini, hivyo kuna uwezekano mkubwa wa benki hii kupoteza fedha zake.

TIB inashauriwa kuboresha taratibu zake za kufuatilia na kurejesha mikopo ili kuzuia udhaifu ulioonekana na ambao unaweza kuathiri utendaji wa benki.

4.34 Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)

4.34.1 Kiasi Kikubwa cha fedha kimewekwa kwenye amana za kudumu Shilingi bilioni 54.70

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilianzishwa mnamo Septemba 2011 chini ya Sheria ya Makampuni, 2002. Kazi kuu ya

Benki ni kuhamasisha utoaji wa huduma za fedha na huduma zisizo za kifedha kwa sekta ya kilimo Tanzania ikiwa ni pamoja na:

- Kutoa vifaa vya muda mfupi, vya kati na vya muda mrefu kwenye sekta ya kilimo.
- Kuchochea utoaji wa mikopo kwa sekta ya kilimo, hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo.
- Kuwa benki kuu inayofadhili sekta ya kilimo, yenye mikakati ya kujenga uwezo, na mipango ya kuimarisha mnyororo wa thamani kwenye sekta hiyo.
- Kufadhili shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji nyuki na shughuli za mifugo.
- Kuimarisha mnyororo wa thamani kwa njia ya mafunzo, utafiti na ushauri.

Mnamo Septemba 2014, Serikali ilitoa mtaji wa Shilingi bilioni 60 kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania.

Nimebaini kwamba, Benki haijatimiza kwa ufanisi malengo ya kuanzishwa kwake. Badala ya kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo ambayo ndiyo shughuli kuu, Benki imekuwa ikiwekeza sehemu kubwa ya fedha zake katika amana za kudumu. Kufikia tarehe 31 Desemba 2016, jumla ya Shilingi bilioni 54.70 zilikuwa zimewekezwa kwenye amana za kudumu, ambayo ni karibu asilimia 91 ya mtaji.

Mapitio yangu zaidi yalibainisha kuwa, kati ya Shilingi bilioni 3.95 bilioni jumla ya mikopo iliyotolewa, Shilingi bilioni 1.71 ni mikopo kwa watumishi na Shilingi bilioni 2.23 tu ndio zimetolewa mikopo kwenye sekta ya kilimo.

Kuweka kiasi kikubwa kwenye amana za kudumuna na mikopo kwa wafanyakazi husababisha kudhoofisha uwezo wa Benki kufikia malengo mkakati yake.

Ninashauri TADB kuzingatia kufanya shughuli zinazoendana na malengo makuu ya kuanzishwa kwake, yaanikuwekeza sehemu kubwa ya fedha zake katika kukopesha sekta ya kilimo, badala ya kuweka amana za kudumu kwa lengo la kupata riba.

4.35 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

4.35.1 Dawa zilizoizisha Muda wake Shilingi bilioni 4.43

Aya ya 3 ya mwongozo wa usimamizi wa dawa wa MSD wa Januari 2017 inaitaka Bohari kujitahidi kudhibiti kiwango cha kuwa na dawa zilizoisha muda wake, hivyo imeweka kiwango cha dawa hizo zinazoisha muda wake kutozidi asilimia 1 ya gharama ya mauzo ya mwaka.

Ukaguzi wangu ulibainisha kuwa wakati wa mwisho wa mwaka, Bohari ya dawa ilikuwa na dawa zilizoisha muda wake za kiasi cha Shilingi bilioni 4.43 ambacho ni juu ya uwiano stahiki ambao unawakilisha asilimia 3.4 badala ya asilimia 1. Kwa mujibu wa Menejimenti, dawa hizi zilizoisha muda wake zilisababishwa na mabadiliko ya teknolojia, dawa zilizoharibika, mabadiliko katika miongozo ya matibabu, uwezo mdogo wa wateja wa MSD, Pamoja na upokeaji wa dawa zinazofanana kutoka kwa wahisani.

Bohari ya dawa inashauriwa kuweka mpango mkakati wa ununuzi na usambazaji wa dawa ili kuepuka kiwango kikubwa cha dawa kuisha kwa muda wake kwa wakati mmoja. Pia, Bohari inapaswa kufuatilia mara kwa mara tarehe za kuisha kwa muda wa dawa ili kuhakikisha zinasambazwa na kugawiwa kwa muda unaopaswa.

4.35.2 Kutokuwapo kwa Kiasi kikubwa cha dawa wakati wa Uhitaji wa dawa kwa wateja

Shabaha ya Bohari ya Dawa ni kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana muda wote zinapohitajika na kwa gharama nafuu na zenye ubora wa hali ya juu. Ili kuhakikisha shabaha hii inafikiwa,

Bohari ilianzisha ofisi za kanda, vituo vya mauzo pamoja na maduka ya dawa ya Bohari ambavyo kwa pamoja vinawezesha kuhifadhi na kusambaza dawa hizo.

Ukaguzi ulibaini kuwa uwezo wa Bohari kukidhi mahitaji ya wateja sio wa kuridhisha. Sampuli iliyochukuliwa kwenye hati za maombi za wateja ikilinganishwa na kiasi cha dawa ambacho hakijapatikana kutoka Bohari ni kati ya asilimia 45 hadi 87 ya mahitaji yote yaliyooombwa.

Bohari inashauriwa kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya wateja wakati wote .

4.35.3 Manunuzi ya dawa chini ya muda wake wa matumizi

Aya ya 5.3 ya usimamizi wa mwongozo wa Bohari wa Januari, 2017 unamtaka ofisa wa ghala kupokea na kuhesabu muda wa dawa uliobaki na kuhakikisha kuwa, bado zina asilimia 80 ya muda wake au uwe zaidi ya miaka 2. Pia, mfumo wa Bohari umeundwa ili kuhakikisha kuwa dawa zote zenye muda wa chini ya miezi mitatu haziruhusiwi kutoka isipokuwa zile dawa zenye maisha mafupi ya chini ya miezi mitatu.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa baadhi ya dawa zilizonunuliwa zilikuwa na chini ya umri wa asilimia 80 wa muda wake wa matumizi au chini ya miaka miwili kinyume na miongozo. Hivyo, kupelekea muda uliobaki wa dawa hizo kuwa mfupi, hatimaye, kuisha muda wake kwa haraka.

Hali hii inasababisha dawa hizo kuisha muda wake kabla ya kutumika. Pia huongeza uwezekanao wa zahanati kutoa dawa ambazo zimeisha muda wake.

Bohari inatakiwa kuwa kuhakikisha dawa zinazonunuliwa zina umri wa zaidi ya asilimia 80 ya maisha yake. Pia, menejimenti inashauriwa kuhakikisha hakuna dawa zilizo chini ya miezi mitatu zinatolewa kwa wateja.

4.36 Chama cha Hati miliki Tanzania (COSOTA)

4.36.1 Madeni ya Mirabaha ya Shilingi mlioni 987.86 kwa vituo vya Televisheni na Redio

Chama cha Hati Miliki Tanzania kina mpango wa kukusanya mirabaha kutoka kwenye vituo vya televisheni na redio ikiwa ni kama moja ya kutekeleza kanuni namba 3 ya COSOTA ya mwaka 2003. Hati za madai zilizotolewa na chama cha hati miliki Tanzania kwa televisheni na redio zilizotolewa kwa ajili ya mwaka 2015/2016 zilikuwa zina thamani ya Shilingi milioni 928.68, Kati ya hati hizo, zilizotolewa, ni Shilingi milioni 3.19 tu ndizo zilizokusanywa, ambayo ni sawa na asilimia 0.34. Pia, nilibaini kuwa, COSOTA haikuweza kutoa hati mpya za madai kwa vituo vya televisheni na redio kwa mwaka 2016/2017.

Chama cha Hati Miliki kinashauriwa kuongeza jitihada kwa kuvikumbusha vituo vya televisheni na redio kuwa vina wajibu wa kulipa mirabaha hiyo.

4.37 Bodi ya Rufaa ya Mapato ya Kodi.

4.37.1 Kesi za Rufaa za mapato ya kodi kutoamuliwa kwa wakati

Sheria inahitaji kesi zote za rufaa za mapato ya kodi zilizowasilishwa, ziamuliwe bila upendeleo, kwa uwazi na kwa wakati.

Ukaguzi ulibaini kuwa rufaa hazijakamilika kwa wakati. Katika mwaka 2016/2017 kulikuwa na jumla ya maombi na kesi 356 za rufaa zilizosajiliwa; kati ya kesi hizo, ni 99 tu, sawa na asilimia 28, ndizo ziliamuliwa na kuacha kesi 257, sawa na asilimia 72, kuwa hazijaamuliwa. Vizuizi hivi vinapelekea Bodi kutofikia malengo yake iliyoyakusudia.

Bodi inashauriwa kuhakikisha kesi zote za rufaa zinaamuliwa kwa wakati kama sheria inavyotaka.

4.38 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)

4.38.1 Mapungufu Katika Kuripoti Uwekezaji katika Mfuko wa Kulinda Uhifadhi (NPF)

Mapitio yangu yalibaini kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro iliripoti hasara ya uendeshaji wa Mfuko wa Uhifadhi wa Ngorongoro (Ngorongoro Protection Fund) ya Shilingi milioni 117. Hata hivyo, hakuna uthibitisho wa kisheria wa uanzishwaji wa mfuko na wamiliki wake hawajulikani, hivyo, nilishindwa kuthibitisha uhusiano uliopo kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mfuko wa Uhifadhi.

Pia, nilibaini kuwa mali zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.46 zinazomilikiwa na Mfuko wa Uhifadhi wa Ngorongoro zilijumuishwa kwenye taarifa za hali ya fedha za Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Mali hizi ni pamoja na amana isiyohamishika (fixed deposit) ya Shilingi milioni 597, fedha zilizopo benki Shilingi milioni 467, madeni yenye thamani ya Shilingi milioni 316, na bidhaa (stock) zenye thamani ya Shilingi milioni 80.

Aina hii ya uandaaji wa taarifa za kihasibu inaonesha kuwa Mfuko wa Uhifadhi wa Ngorongoro ulijumuishwa kama kampuni tanzu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kinyume na matakwa ya uandaaji wa taarifa za kihasibu baina ya kampuni mama (parent company) na mshirika wake (associate company). Hata hivyo, nilibaini kuwa hesabu za Mfuko wa Uhifadhi wa Ngorongoro hazijakaguliwa kama Mfuko unaojitegemea.

Naushauri uongozi wa mamlaka kufuatilia na kupata nyaraka zinazothibitisha umiliki wa Mfuko wa Uhifadhi kwa kuainisha uhusiano uliopo baina ya Mamlaka na Mfuko huo. Kufanya hivyo kutarahisisha kujua ni kwa namna gani uwekezaji wa kwenye Mfuko unaweza kuonekana kwenye hesabu za mamlaka.

4.38.2 Uwekezaji kwenye Maswala yaliyo Nje ya Majukumu Makuu ya Taasisi

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilianzishwa mwaka 1959 kwa lengo la kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za asili za Eneo la Uhifadhi, kukuza utalii ndani ya Eneo la Uhifadhi, kutoa na kuhamasisha utoaji wa vifaa muhimu kwa ajili ya kukuza utalii; na kulinda na kukuza maslahi ya Wamaasai wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaojihusisha na ufugaji wa ng'ombe na maziwa ndani ya Eneo la Uhifadhi.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, kinyume na majukumu makuu ya taasisi, Mamlaka iliwekeza kiasi cha Dola za Kimarekeni milioni 17 kwenye ujenzi wa nyumba jijini Arusha katika eneo la barabara ya Makongoro Jirani na jengo la Benki Kuu ya Tanzania, tawi la Arusha. Gharama zilizotumika kwenye mradi huo katika mwaka wa fedha ni Shilingi bilioni 20. Sambamba na hayo, mapitio ya mpango wa biashara wa mamlaka yalibainisha kuwa, makusanyo ya pango yaliyotarajiwa kutoka kwenye uwekezaji yamepungua kutoka kiwango cha wastani wa dola 14 kwa mita za mraba hadi dola 10 huku upangishwaji ukiwa umefanywa kwa asilimia 80.

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inapaswa kuelekeza juhudi na rasilimali zake kwenye shughuli za msingi za uwanzishwaji wa mamlaka. Uwekezaji wowote kwenye maswala yasiyokuwa makuu kwa mamlaka yanapaswa kufanyika baada ya kufanyika kwa uchambuzi wa kina kuhusu mategemeo ya faida na hasara za mradi husika na kuthibitishwa na mamlaka husika.

4.38.3 Ujenzi wa Mradi ambao Hakuna Thamani Iliyopatikana

Tarehe 30 Juni 2017, Mamlaka iliripoti kazi za ujenzi wa majengo unaoendelea (WIP) wa Shilingi milioni 860 zinazohusiana na mradi wa Ramat.

Hata hivyo, mradi huo ulipigwa marufuku na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira Tanzania (NEMC) Oktoba 2010 kutokana na kutofanya tathmini ya athari za mazingira.

Baadhi ya sababu ambazo zilipelekea mradi kukatazwa ni;

- i. Mradi huo ulianzishwa kwenye ukanda wa wazi wa wanyamapori kinyume na Sheria ya Wanyamapori ya 2009.
- ii. Uzio uliozungushiwa katika shamba husababisha majeraha kwa wanyama wanaohama hasa wakati wa usiku.
- iii. Kuenea kwa magonjwa kutoka kwa wanyama pori kwenda kwa wanyama wa kufugwa; na kiasi kikubwa cha Floraidi kutoka kwenye mashimo yaliyochimbwa.

Nimebaini katika kipindi cha kati ya mwaka 2013 na 2014 NCAA iliingia gharama ya Shilingi milioni 52 ili kuzungusha wigo wa kulinda wanyama pori. Nilibaini kuwa taratibu za manunuzi hazikufuatwa kwenye mradi huu kwa sababu kulikuwa hakuna mkataba uliosainiwa kati ya NCAA na mkandarasi LL-M-APIFAT.

Kwa kuwa mradi ulitelekezwa, NCAA haikuweza kupata faida kutokana na thamani ya fedha ambayo imewekezwa kwenye mradi huo.

Mamlaka inapaswa kufungua njia ya wanyama iliyokingwa ili kuwezesha utaratibu wa kawaida wa maisha ya wanyama katika Hifadhi ya Ngorongoro na pia kuzingatia ushauri wa NEMC.

Pia, inatakiwa kuwa inafuata sheria za manunuzi ikiwa ni pamoja na kuingia mikataba na wazabuni ili kuepuka hasara zinazoweza kutokea.

4.39 Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

4.39.1 Malipo kwa manunuzi ya Ardhi yaliyo kinyume na Utaratibu.

Kanuni namba 55 ya Manunuzi ya Uma inahitaji taasisi za Umma kupata idhini ya Mkurugenzi Mkuu na bodi ya zabuni. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, Mamlaka ya Bandari ilianza na mazungumzo na iliyokuwa Mamlaka ya Uendelezaji wa Makao Makuu kwa ajili ya ununuzi ya heka 500 za ardhi katika eneo la Ihumwa Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu kwa gharama ya wastani wa Shilingi bilioni 12.6 mnamo tarehe 22 Septemba 2016 bila kufuata

utaratibu ikiwemo kutopata idhini ya Bodi ya manunuzi pamoja na ardhi hiyo kutofanyiwa tathmini kabla ya ununuzi huo.

Pia, nilibaini kuwa mnamo Machi,2017, Mamlaka ya Bandari ilifanya malipo ya awali ya Shilingi bilioni 6.3 ikiwa ni asilimia 50 ya gharama ya Ardhi yote.

Hii ni kinyume pia na makubaliano yaliyofanyika tarehe 4 Novemba 2016 kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na iliyokuwa Mamlaka ya Uendelezaji wa Makao Makuu.

Mamlaka ya Bandari Tanzania inashauriwa kufuata taratibu zilizowekwa na sheria ya Manunuzi ya Umma ikiwemo kuhakikisha inapata idhini ya Bodi pamoja na kuhakikisha ardhi hiyo tajwa inatathminiwa kabla ya kulipa gharama zilizobaki.

4.39.2 Usimamizi Usioridhisha wa Mapato kutoka TICTS

Mamlaka ya Bandari (TPA) ina makubaliano na Kituo cha Huduma za Makontena ya Kimataifa (TICTS) yanayoruhusu TICTS kutoa huduma ya makontena kwa niaba ya Mamlaka hiyo huku ikilipa mrahaba na tozo ya kupitisha mizigo bandarini (wharfage) kwa kila kontena lililopokelewa. Ili kuimarisha ufuatiliaji, Mamlaka ilianzisha Kitengo cha Ufuatiliaji wa TICTS (TICTS Monitoring Unit (TMU) ambacho kilikuwa na jukumu la kufuatilia makontena yote yaliyofanyiwa kazi na TICTS bila majukumu yake kuingiliwa.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, hakuna ufuatiliaji uliofanywa na TMU kwenye makontena yanayoenda nje ya nchi. Aidha, hakukuwa na ushahidi kwamba uwainishaji unafanyika kati ya makontena yaliyofanyiwa kazi na TICTS dhidi ya yale yaliyoripotiwa na TMU.

Kutokuwapo kwa taarifa ya uwainishaji kunaifanya TPA kushindwa kuthibitisha kwa usahihi mapato yanayopatikana kupitia TICTS.

TPA, kupitia TMU, inashauriwa kuhifadhi taarifa za makontena yaliyoingizwa nchini na yanayoenda nje ya nchi, Na mara kwa

mara kufanya usuluhishi wa taarifa zinazotolewa na Mfumo wa Pamoja wa Forodha wa Tanzania (TANCIS); na endapo kutakuwa na tofauti uchunguzi ufanyike mapema. Bili ya mwisho kwenda TICTS inatakiwa kutolewa baada ya mapitio ya taarifa ya usuluhishi wa mapato.

4.40 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

4.40.1 Utata wa Umiliki wa Kituo cha Mafuta cha COPEC Kilichopo Eneo la Makumira

TPDC, kupitia kampuni yake tanzu ya COPEC, ina makubaliano ya umiliki na makampuni mawili ya Makeru Filling Station Limited (MSFL) na Skyone Petroleum na Transport Limited (SPTL) yenye lengo la kuendesha kituo cha mafuta kilichopo Makumira, Arusha. Makampuni hayo yalianza kufanya kazi tarehe 12 Julai 1999 kwa MSFL na tarehe 1 Julai 1999 kwa SPTL. Kwa mujibu wa makubaliano, COPEC ina hisa 7,700 zenye thamani ya Shilingi 10,000 kila moja kwenye kampuni ya MSFL na hisa 5,700 zenye thamani ya Shilingi 10,000 kila moja kwenye kampuni ya SPTL.

Nilibaini kuwa, hapakuwa na mapato yaliyotokana na uwekezaji huu kwa miaka ya fedha 2015 na 2016. Zaidi ya hayo, ziara yangu ilibaini kuwa kituo hicho kinatumiwa na mpangaji binafsi ambaye alidai kukodishwa na Engen na siyo TPDC. Hata hivyo, kituo hicho kilionekana kuwa na nembo ya Engen.

TPDC inashauriwa kufuatilia umiliki wake katika makampuni hayo mawili ili kujua hali ya uwekezaji wake na kuchukua hatua zinazofaa.

4.40.2 Malipo ya Mshahara Nje ya Mfumo wa LAWSON yenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.4

PDC inatakiwa kulipa mishahara ya wafanyakazi kupitia mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimaliwatu wa LAWSON kama ilivyokumbushwa na Wizara ya Nishati na Madini (MEM) kupitia barua mbili za tarehe 18 Septemba 2014 na 25 Septemba 2014.

Mapitio yangu ya malipo ya mishahara yalibaini kiasi cha Shilingi bilioni 1.04 kililipwa nje ya mfumo kwa LAWSON. Kiasi hiki kililipwa kama ongezeko la mishahara (top up salary) mbali na malipo halisi ya mishahara ya watumishi 110 ambayo yamelipwa ndani ya mfumo wa LAWSON.

Kulipa mishahara nje ya mfumo wa LAWSON kunakiuka udhibiti wa malipo uliowekwa, hivyo kutoa mwanya wa malipo yenye udanganyifu kufanyika.

TPDC inashauriwa kuhakikisha kuwa mishahara yote inaandaliwa kupitia mfumo wa LAWSON.

4.40.3 Malipo Yasiyostahili kwa Kampuni ya Maurel & Prom ya Dola za Kimarekani Milioni 27.18

Kifungu cha 15.1 cha Makubaliano ya Mauziano ya Gesi (GSA) kati ya TPDC na Maurel & Prom (M&P) kinataka TPDC kuweka dhamana ya fedha kwa kuweka kiasi cha fedha kwenye akaunti ya pamoja (Escrow) au kwa Barua ya Mkopo kutoka Benki (letter of credit) au kwa mkataba wa dhamana ya malipo (payment guarantee agreement).

Hata hivyo, nimebaini kuwa, TPDC ilitoa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 27.18 (sawa na Shilingi bilioni 56.70) kwa kulipa akaunti ya M & P kinyume na masharti tajwa hapo juu huku ikichukulia fedha hizo kama malipo ya awali (prepayment). Pia, ilibainika kuwa fedha zilizolipwa kwa M&P zilikopwa kutoka Benki ya Maendeleo ya TIB.

Ukosefu wa makubaliano rasmi juu ya namna fedha za dhamana zinavyotakiwa kuhifadhiwa unaiweka TPDC kwenye nafasi mbaya endapo kutatokea mgogoro wowote. Pia, kukopa fedha kwa lengo la kuweka dhamana kunaongeza gharama kwa taasisi kwa sababu ya riba.

TPDC inashauriwa kuzingatia makubaliano ya mauziano ya gesi na kutumia kwa makini rasilimali zilizopo chini yake ili kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

4.41 Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO)

4.41.1 Matumizi Yasiyoridhisha ya Fedha Zilizotengwa Kufanikisha Uunganishaji wa Maji kwa Wateja Wapya

Ibara ya 36 ya Mkataba wa Ukodishaji wa Maji na Miundombinu ya Maji (Water and Sewerage Lease Contract) kati ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) na Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO) inaitaka DAWASCO kutoza ushuru wa kuunganisha maji kwa mara ya kwanza kwa wateja wake wote na kuwa na akaunti maalum ya kuhifadhi fedha hizo kwa lengo la kufanikisha uunganishaji wa bure wa maji kwa wateja wapya.

Ukaguzi wangu ulibaini DAWASCO haikufuata masharti ya mkataba kwa namna zifuatazo:

- i. Makusanyo yaliyotokana na ushuru wa kuunganishiwa maji kwa mara ya kwanza yaliyofikia Shilingi bilioni 1.82 (FTNDWSCF) yalihifadhiwa kwenye akaunti ya kawaida ya DAWASCO;
- ii. DAWASCO ilitumia Shilingi milioni 536.84 kwa matumizi yake ya kawaida bila kuihusisha DAWASA kinyume na mkataba;
- iii. DAWASCO ilitumia akaunti ya mfuko (FTNDWSCF) kuchukulia mkopo kutoka benki ya CRDB hivyo kusababisha gharama za maombi ya mkopo kufanyika kwenye akaunti hiyo.

Matumizi yasiyoridhisha ya fedha yamesababisha kutofikiwa kwa malengo ya mwaka wa fedha 2016/17 ya kuunganisha wateja wapya 50,000, hivyo kufanikiwa kuunganisha wateja 38,386 tu. Kwa sasa, wateja wapya wa maji wanatozwa kiasi cha Shilingi 26,000 huku wakitakiwa kujilipia vifaa vya uunganishaji wa maji ili hali vilitakiwa kutolewa bure.

Naishauri DAWASCO kufuata masharti ya mkataba baina yake na DAWASA.

- 4.41.2 Kushindwa Kununua Kifaa cha Utambuzi wa Uvujaji wa Maji**
Ibara ya 18.3 (b) ya Mkataba wa Ukodishaji wa Maji na Miundombinu ya Maji kati ya DAWASA na DAWASCO unaitaka DAWASCO kununua kifaa cha utambuzi wa uvujaji wa maji kama njia ya utatuzi wa haraka.

Nilibaini kuwa DAWASCO bado haijanunua kifaa cha utambuzi wa uvujaji wa maji kama masharti ya mkataba yanavyotaka. Pia, kumekuwa na agizo kutoka kwa Kamati ya Bodi ya Ufundi na Utekelezaji kuharakisha ununuzi wa kifaa hicho, lakini maagizo hayo hayajafanyiwa kazi.

Jambo hili linapunguza kasi ya kusimamia kupunguza upotevu wa maji kufikia asilimia 28 hadi mwaka 2018/2019. Kwa hali ya sasa, upotevu wa maji ni asilimia 47.

DAWASCO inashauriwa kuhakikisha kifaa cha utambuzi wa uvujaji wa maji kinanunuliwa na kufungwa.

- 4.41.3 Ufutaji wa Deni la Shilingi Bilioni 24.9 bila Kuishirikisha DAWASA**

bara ya 33 (5) ya Mkataba wa Ukodishaji wa Maji na Miundombinu ya Maji kati ya DAWASA na DAWASCO unaitaka DAWASCO kuweka wazi orodha ya wateja wanadaiwa kwa muda mrefu, na kujadiliana na DAWASA kabla madeni hayo hayajafutwa kwenye orodha ya wadeni.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, kiasi cha Shilingi bilioni 24.90 kilifutwa na DAWASCO kwenye orodha ya wadaiwa bila kuishirikisha DAWASA. Ufutwaji huo wa madeni ulifanywa kinyume na utaratibu na kuna uwezekano ukaleta mgongano na kuathiri shughuli za DAWASCO.

Naishauri DAWASCO kuheshimu masharti ya mkataba ili kuepuka matatizo yanayoweza kutokea kutokana na kwenda kinyume na utaratibu uliopangwa.

4.41.4 Makusanyo ya DAWASCO yaliyochelewa Kuwasilishwa na MAXCOM

Mnamo tarehe 22 Novemba 2016, DAWASCO iliingia mkataba na kampuni ya MAXCOM kama wakala wa ukusanyaji wa mapato.

Hata hivyo, mapitio yangu yalibainisha mambo yafuatayo: MAXCOM haikuweka kiasi cha Shilingi milioni 500 kupitia Benki ya CRDB kama ilivyotakiwa na Kifungu namba 7.3 cha mkataba baina yake na DAWASCO.

- i. Mkataba haukubainisha muda unaotakiwa kutozidi kwa MAXCOM kukaa na fedha za makusanyo. Hadi mwisho wa mwaka kiasi cha Shilingi milioni 431.77, kikihusisha makusanyo ya kuanzia tarehe 22 Juni 2017, kilikuwa bado hakijawasilishwa na kampuni ya MAXCOM.
- ii. MAXCOM imekuwa na mwenendo wa kutowasilisha makusanyo yote kwa mkupuo. Kwa mfano, tarehe 3 Juni 2017 MAXCOM ilikuwa na Shilingi milioni 242 lakini iliwasilisha Shilingi milioni 200 tu. Tarehe 21 Juni, 2017 ilikuwa na makusanyo ya Shilingi milioni 511 lakini iliwasilisha Shilingi milioni 250 tu; na tarehe 30 Juni 2017 ilikuwa na makusanyo ya Shilingi milioni 756 lakini iliwasilisha milioni 400.

Kiasi kikubwa cha fedha kinakuwa mikononi mwa kampuni ya MAXCOM hivyo kuathiri utendaji wa DAWASCO.

Kuna uwezekano kuwa ucheleweshaji huu unaotoa mwanya wa matumizi kinyume na utaratibu kwa upande wa MAXCOM.

DAWASCO inatakiwa kuhakikisha masharti ya mkataba wake na MAXCOM yanafuatwa kwa kampuni husika kuweka kiasi cha Shilingi milioni 500 sambamba na makusanyo yote yaliyopo

mikononi mwa MAXCOM. Pia, mkataba unatakiwa kufanyiwa mapitio na kuweka ukomo wa muda tangu fedha zimekusanywa hadi kuwasilishwa DAWASCO.

4.41.5 Matumizi ya Njia ya Manunuzi Isiyostahili

DAWASCO iliingia mkataba wa ununuzi wa pikipiki na kampuni ya M/s City Motors wenye thamani ya Shilingi milioni 210 kupitia chanzo kimoja bila kushirikisha wazabuni wengine (single source) kinyume na Kanuni namba 159 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 (Marejeo 2016) na Jedwali Namba Saba la kanuni hizo.

Njia iliyotumika haikuwa ya ushindani na hivyo kuna uwezekano wa kusababisha taasisi kufanya manunuzi yasiyo na thamani ya fedha.

DAWASCO inashauriwa kuzingatia sheria za manunuzi ili kupata thamani inayostahili kwenye manunuzi yake.

4.42 Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA)

4.42.1 Kukosekana kwa Mpango wa Kudhibiti Viashiria vya Hatari

Kudhibiti majanga kwenye Mamlaka ni moja kati ya majukumu muhimu ya Taasisi.

Wakati wa ukaguzi wangu, nilikuta matumizi ya Shilingi milioni 42 kwa ajili ya mafunzo yanayohusiana na mambo hayo ambapo Bodi ya Wakurugenzi, Utawala na watumishi wote walihusika kwa kipindi cha mwezi wa Februari na Machi 2017.

Nawashauri DAWASA watengeneze sera za kudhibiti viashiria vya hatari ili kuweza kubaini na kudhibiti uwezekano wa kutokea majanga.

4.42.2 Kuchelewa kukamilika kwa Miradi

Baada ya kufanya marejeo na ukaguzi wa utekelezaji wa miradi, nilibaini kuwa kuna ucheleweshaji wa miradi unaofanywa na

wakandarasi. Miradi hiyo ni kama vile utafiti wa visima 8 na uchimbaji wa visima 20 katika eneo la Mpera na Kimbiji.

Nilibaini kuwa, DAWASA waliingia mkataba na Kampuni ya NSPT Limited JV Serengeti Limited wenye thamani ya Shilingi bilioni 18.48 kwa ajili ya uchimbaji visima 20; na kazi ilipaswa iwe imekamilika tarehe 31 Desemba 2015. Lakini tulitembelea mradi mwezi Septemba 2017, tulikuta visima 11 kati ya visima 20; na ni viwili tu nilivyovikuta vimekamilika, visima tisa vikiwa bado havijakamilika.

Uchelewaji huo ulisababisha kupanda kwa gharama za mradi. Kwa mfano, kazi za mradi wa uchimbaji visima 8 kazi zilikuwa zinafanywa na mkandarasi aitwae CDM International Inc., ambapo gharama za mradi zilipanda kwa aslimia 211.3 kutoka Dola za Kimarekani milioni 1.29 mpaka Dola za Kimarekani milioni 2.73.

Naishauri DAWASA watoze fidia kwa mkandarasi kwa kuchelewa kumaliza kazi kwa wakati.

4.43 Shirika la Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO)

4.43.1 Upungufu wa Kamera za CCTV katika kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro

Wakati wa ukaguzi na ziara ya kutembelea eneo la kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro, nilibaini uchache wa kamera za CCTV katika uwanja huo. Nilibaini kuwa, kamera zipo kwenye maeneo ya maegesho ya magari, geti namba moja la kuingilia na eneo la kukaa watu mashuhuri tu; wakati maeneo mengine yaliyobaki yakikosa kamera kwa ajili ya ulinzi.

Wakati wa mahojiano na kiongozi, walikiri kuwapo kwa kamera chache, na wakasema kuwa mchakato wa manunuzi ulisitishwa kutoka kwenye kikao cha bodi ya zabuni kutokana na mapungufu ya kiufundi yaliyojitokeza. Hata hivyo, Menejimenti imeshaanza

mara moja mchakato wa manunuzi kwa ajili ya usambazaji na ufungaji wa kamera za CCTV.

Naishauri Menejimenti ya KIA iharakishe mchakato wa zabuni na kumpata mshindani halisi kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo.

4.43.2 Kutokuwapo kwa Vifaa vya Kuzimia Moto

Ukaguzi niliufanya kwenye rejista ya mali za Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro umebaini seti mbili za kuzimia moto zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.63 hazikuonekana kwenye rejista. Baada ya kupitia mawasiliano kati ya Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro na uwanja wa ndege wa kimataifa wa Dar es Salaam, nilibaini kuwa hivi vifaa viliuzimwa na kiwanja cha ndege cha Mwalimu Nyerere, pamoja na hatua za ufuatiliaji uliofanyika bado hakuna majibu ya kuridhisha.

Naishauri Menejimenti ya KADCO wafanye mawasiliano na Wizara ya Mawasiliano ili kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo.

4.44 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

4.44.1 Kutofanyika kwa marekebisho ya Mazingira katika Mgodhi wa Buhemba

Mnamo mwaka 2011 STAMICO, walichukua mgodi wa dhahabu wa Buhemba ambao hapo awali ulikuwa unaendeshwa na kampuni ya Meremeta Limited kutoka mwaka 2003 mpaka 2011. Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Shirika halikupata fedha kutoka kwa mwekezaji wa awali kwa ajili ya kufukia mashimo yaliyoachwa. Hii ni kutokana na kutotengwa fedha kwa ajili ya shughuli hiyo.

Kutotengwa kwa fedha kwa ajili ya marekebisho ya eneo la machimbo na kuliacha eneo baada ya uchimbaji kuna athari kubwa kwa mazingira.

Nashauri STAMICO wawasiliane na Wizara ya Nishati kwa ajili ya kupata suluhisho la kurekebisha mazingira ya mgodi huo.

4.44.2 Uwekezaji katika Kampuni ya Madini ya Itetemia

Mnamo tarehe 12 Julai 1994, STAMICO na Kampuni ya Tancan waliingia makubaliano ya kufanya uchunguzi na uendelezaji kwa kuunda Kampuni ya Itetemia na STAMICO ilipewa asilimia kumi za hisa katika Kampuni ya Itetemia ambazo zina thamani ya Shilingi milioni 3. Tancan walitakiwa wailipe STAMICO Shilingi milioni 1 kwa ajili ya uhamishaji wa taarifa na kupata haki ya kuchukua madini. Pia, Tancan walipaswa kulipa kodi ya pango yenye thamani ya Dola za Kimarekani 7,200 wakati wa utafutaji madini na kiasi cha Dola za Kimarekani 10,000 wakati wa uchimbaji.

Hata hivyo, nilishindwa kupata thamani halisi ya taarifa za kitaalamu zilizohamishiwa Tancan pamoja na uhalali wa miamala iliyofanyika kati yao. Pia, Kampuni ya Dhahabu ya Itetemia haijarekodiwa kwenye vitabu vya hesabu vya STAMICO.

STAMICO wanapaswa kufanya tathmini ya thamani halisi ya taarifa za kitaalamu zilizohamishwa. Pia, waitambue Kampuni ya Dhahabu ya Itetemia kama kampuni tanzu kwenye vitabu vya hesabu ya shirika.

4.45 Ofisi ya Taifa ya Twakimu (NBS)

4.45.1 Viwanja visivyo na Hati miliki vyenye Thamani ya Shilingi bilioni 5.44

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ina maeneo/viwanja katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, na Kigoma vyenye thamani ya Shilingi bilioni 4.75, Shilingi bilioni 0.65 na Shilingi bilioni 0.04 mtawalia baada ya uthaminishaji wa maeneo ayo. Ukaguzi wangu umebaini kuwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu haina hati miliki ya maeneo tajwa.

Kwa upande wa ardhi ya Arusha, nilibaini kuwa Shirika la Nyumba la Taifa lilitoa ardhi hiyo kwa NBS na BOT kwaajili ya kujenga majengo 12, ambapo NBS inamiliki majengo 3. Hata hivyo, hati miliki ya kiwanja yenye namba 13367 inaonesha kuwa kiwanja hicho ni mali ya BOT. Katika mahojiano yangu na viongozi,

walikiri kuwapo kwa mabadiliko hayo ya umiliki. Hata hivyo, hakuna juhudi za kufuatilia suala la BOT kumiliki hati ya kiwanja.

Inashauriwa NBS kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha maeneo yote inayoyamiliki yanakua na hati miliki zake na Pia kufanya majadiliano na BOT ilikuweza kupata umiliki wa kiwanja cha Arusha.

4.46 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)

4.46.1 Mapato Yanayokosekana kutokana na kutotekelezwa Vifungu vya Mkataba.

Chuo Kikuu cha Dar es salaam kiliingia mkataba na M/s Seacom Tanzania Limited wa kukodisha kiwanja na 49 kilichopo Kunduchi Beach Dar es Salaam kwa muda wa miaka ishirini.

Makubaliano ya mkataba yanaitaka M/s Seacom Tanzania Ltd kutoa bure kwa UDSM njia ya faiba yenye uwezo wa STM -1 kwa haki ya matumizi ya miaka 20.

Chuo Kikuu kilikuwa na mpango wa kujenga Hospitali ya Apollo, Kijiji cha Teknolojia na Kituo cha Takwimu cha kisasa. Miradi hii yote haikuteklezwa na kutokana na M/s Seacom Tanzania Limited kushindwa kutekeleza makubaliano ya mkataba.

Zaidi ya hayo, M/s Seacom Tanzania Limited haikutimiza majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 5.0 makubaliano ya upangaji kama ifuatavyo:

- i. Haikutafuta maeneo ya kutandanzia nyuzi za mawasiliano kutoka Kunduchi Beach kwenda palipotarajiwa pawe na kituo cha data, kituo cha TEHAMA na Hospitali ya Apollo kwenye Kampasi ya Mlimani kinyume na masharti ya mkataba.
- ii. Haikufadhili ujenzi wa njia ya mawasiliano kwenda kwenye maeneo ambayo kituo cha data, kijiji cha teknolojia na mawasiliano na Hospitali ya Apollo yalitarajiwa kujengwa.

iii. Haikuwezesha kupatikana kwa mbia mzuri na mwenye uwezo wa kujenga kituo cha data cha kisasa.

Kwa M/s Seacom Tanzania Ltd kushindwa kutekeleza mahitaji ya mkataba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimepoteza mapato ya kodi. Hii ni kwa sababau mkataba ulitaka pesa hiyo ya kodi itolewe sambamba na usambazaji wa vifaa vya mtandao wa mawasiliano ndani ya chuo.

Kwa kuwa kipindi cha miaka 10 ya mkataba kinakaribia kufika mwisho, ninashauri mkataba kurekebishwa ili kuweza kubadili vifungu vya mkataba vinavyoelekeza kuwa kodi ya pango itafidiwa na huduma za mtandao. Hii itawezesha kupata malipo ya kodi badala ya utaratibu wa mwanzo.

4.46.2 Malipo ya awali Bila Mkataba Dola za Kimarekani 161,381.95

Vifungu Na. 60 (7) na (8) vya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, vinasema kwamba; Baada ya zabuni na mapendekezo kukubaliwa na Afisa Masuuli, pande mbili zitaingia mkataba rasmi wa utoaji wa huduma au kufanya kazi, na mkataba rasmi utakuwa na masharti kama ilivyo kwenye hati ya zabuni.

Nimebaini kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kililipia Vifaa vya Spectrometer na Vifaa vya Maabara kutoka Chemetrix (Pty) vyenye thamani ya Dola za Kimarekani 86,102.95 na Dola za Kimarekani 75,279 mtawalia. Hata hivyo, malipo hayo yalifanyika kabla mkataba rasmi kati ya pande mbili zilizousika.

Chuo Kikuu kipo kwenye hatari ya kupoteza fedha hizo kwa kutokuwepo kwa mkataba. Hii ni kwa sababu hakuna nyaraka yeyote inayotoa majukumu katika hizo pande mbili.

Chuo Kikuu kinatakiwa kuhakikisha kwamba mikataba yote imewekwa saini kabla malipo kufanyika. Pia, kufuatilia ili kupata hizo bidhaa cha kiasi malipo ya awali yaliyofanyika.

4.47 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB)

4.47.1 Makusanyo ya madeni ya Mikopo chini ya Malengo

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ilianzishwa mwaka 2005/2006. Bodi ilirithi mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 51.1 iliyotolewa kwa wanafunzi kabla ya kuanzishwa kwake. Bodi imetoa jumla ya Shilingi trilioni 2.9 tangu kuanzishwa hadi Juni 2016. Hadi tarehe 30 Juni 2017, jumla ya mkopo ilifikia Shilingi bilioni 464. Moja ya malengo katika mpango wake wa kimkakati 2014/2015 - 2016/2017 ilikuwa kuimarisha uwezo wa uendeshaji ambao Bodi ililenga kukusanya asilimia 80 ya mikopo inayotarajiwa ili kuhakikisha uendelevu wa kutoa mikopo kwa mwaka 2017.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wangu nilibainisha kuwa, kati ya jumla ya mikopo iliyowiva ya Shilingi bilioni 464, Bodi imeweza kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 221.12 tangu ilipoanzishwa. Mkusanyo haya ni sawa na asilimia 47.6 ya jumla ya mikopo iliyoiva, ambayo ni asilimia 80 chini ya malengo yaliyowekwa.

Bodi haitoweza kufikia malengo yake, ikiwemo lile la kuwa na uwezo na uendelevu wa kutoa mikopo mipya.

Ninashauri Bodi kushirikiana na waajiri ili kuweza kuwabaini watumishi wanaodaiwa.

4.47.2 Ukosefu wa Mkakati ya kuondoa Hatari juu ya Hasara itokanayo na Wanufaika Waliokufa au Wasio na Uwezo wa Kulipa

Sehemu ya 33 ya Kanuni za Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka 2009 inasema kuwa, ambapo imedhibitishwa na Bodi kuwa mnufaika wa mkopo amekufa wakati wa masomo yake au baada ya masomo, au wakati analipa mkopo, madeni yoyote ambayo anadaiwa yatafutwa.

Hadi wakati nafanya ukaguzi Bodi ilikuwa inadai Shilingi milioni 257.71 za wanufaika waliokwisha fariki dunia. Na nilibaini kuwa Bodi haina mkakati kamili wa kupunguza hatari hiyo.

Ukosefu wa mikakati ya kukabiliana na hatari unaweza kusababisha Bodi kuingia hasara kutokana na wafu au walemavu wanaopatikana. Kwa hiyo, nashauri Bodi ya kutafuta njia za kupunguza hatari ya kuwa na hasara kubwa kutokana na vifo vya walengwa wa mkopo au wanafunzi wenye ulemavu.

4.47.3 Ugumu wa Kupatikana kwa Wanufaika wa Mikopo

Aya ya 4 'g na h' ya Sheria ya Bodi ya Mikopo nambari 17 ya 2007, inahitaji Bodi kuanzisha ushirikiano wa misingi na manufaa na taasisi na mashirika kama vile serikali au mashirika yasiyo ya kiserikali, ya ndani, ya kigeni au ya kimataifa na waajiri wa walengwa wa mkopo kwa lengo la kuwezesha kurejeshwa mikopo.

Uchunguzi wangu wa ripoti za ulipaji na urejeshaji umebaini kuwa, Bodi ina wadaiwa ambao wameshindwa kuwapata. Deni lao ni Shilingi trilioni 1.46. Sehemu ya deni hilo imekuwapo tangu mwaka 1994/1995.

Ukosefu wa utaratibu sahihi wa kufuatilia walengwa unaweza kuzuia ufanisi wa Bodi katika kufuatilia wahalifu.

Ninashauri Bodi kuanzisha mfumo bora wa kufuatilia walengwa, hasa wale walio katika sekta isiyo rasmi.

4.48 Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania (TIRA)

4.48.1 Uthibiti hafifu kwenye makusanyo ya tozo ya malipo ya bima

Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania (TIRA) imepewa mamlaka ya kutoza na kukusanya tozo la asilimia 1.5 kutoka katika malipo ya bima yaliyokusanywa na makampuni ya bima ijulikanayo kama tozo ya malipo ya bima. Kwenye kuratibu ukusanyaji wa tozo hii, makampuni ya bima yanahitajika kufanya marejesho ya malipo ya

bima waliyokusanya kwenye kila robo ya mwaka. Kutokana na marejesho hayo, TIRA hukokotoa malipo stahiki ya tozo.

Ukaguzi wangu umebaini ya kuwa, TIRA haina mfumo wa kimawasiliano unaoweza kufuatilia moja kwa moja malipo yote ya bima yaliyokusanywa na makampuni ya bima ili kujiridhisha na kuthibitisha kiasi kilichowasilishwa kama makusanyo ya malipo ya bima na makampuni hayo.

Pia, TIRA haifanyi uhakiki wa uhalali wa malipo ya bima pacha yapunguzwayo toka kwenye makusanyo ya makampuni ya bima wakati wa kufanya marejesho. Wakati wa kufanya marejesho ya makusanyo ya bima, makampuni ya bima yanapunguza malipo ya bima yaliyofanyika kwa makampuni nyingine ya bima kwenye bima pacha. Kwa mfano, katika mwaka 2016/2017 jumla ya Shilingi bilioni 62.60 (Shilingi bilioni 39.00 kwa TANRE na Shilingi bilioni 23.60 kwa makampuni mengine ya bima) ilikatwa na makampuni ya bima 19 wakati wa kufanya marejesho ya makusanyo ya bima. Makato hayo hayakuweza kuonekana ulipofanyika ufuatiliaji wa malipo hayo.

Kutokuwepo kwa mkakati wa ufuatiliaji wa malipo ya bima kunaifanya TIRA kushindwa kuhakiki tozo ya malipo ya bima.

TIRA inashauriwa kuanzisha mfumo wa kimawasiliano utakaowezesha kufuatilia malipo ya bima yanayokusanywa na makampuni ya bima. Zaidi ya hayo, TIRA ifanye uchunguzi kutambua uhalali wa makato yanayofanywa na makampuni ya bima kwenye malipo ya bima pacha.

4.49 Mfuko wa Pensheni wa NSSF

4.49.1 Kutolewa kwa mikopo Zaidi ya kiasi cha Mkatiba Shilingi Bilioni 6.18

NSSF iliingia Mikatiba ya kutoa Mikopo kwa Taasisi nne kiasi cha Shilingi bilioni 60.69. Hata hivyo, nilibaini, NSSF ilizipatia taasisi hizo kiasi cha Shilingi bilioni 66.87 badala ya kiasi

walichokubaliana, hivyo kiasi cha Shilingi bilioni 6.18 kilitolewa nje ya makubaliano ya mikataba. *Angalia kiambatisho Na. II*

Kuna uwezekano wa Mfuko kupata hasara ya kutolipwa kiasi kilichotolewa nje ya makubaliano.

NSSF inashauriwa kuchunguza sababu za malipo zaidi kwa Taasisi hizo nne na kuhakikisha kunafanyika majadiliano juu ya urejeshwaji wa fedha hizo. Pia, Mfuko katika siku zijazo, uhakikishe hakuna malipo ya ziada yanayofanywa kinyume na mikataba.

4.49.2 Kutozingatiwa Miongozo ya Uwekezaji ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mwongozo Na.8 wa Miongozo ya Uwekezaji ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2015, iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, inaweka ukomo wa kiwango cha juu cha asilimia 10 katika uwekezaji wa mikopo kwa serikali kuu. Hata hivyo, mapitio yangu ya uwekezaji wa NSSF yalibaini kuwa mikopo kwa Serikali kuu hadi tarehe 30 Juni 2017 ilikuwa Shilingi bilioni 1.11, sawa na asilimia 31 zaidi ya kiwango cha juu cha asilimia kumi kilichowekwa.

Kutoa mikopo juu ya viwango vinavyokubalika, kunahatarisha uwezo wa Mfuko katika kutekeleza majukumu yake ya kisheria ya utoaji wa mafao kwa wakati.

Ninaushauri mfuko kuhakikisha unazingatia kikomo kinachokubalika katoka utoaji mikopo na kuzingatia sheria, kanuni na miongozo.

4.49.3 Kukinzana kwa Kiasi cha Uwekezaji Kilichiripotiwa katika Dhamana za Serikali Shilingi Bilioni 1.05

Nimebaini kuwa NSSF haifanyi usuluishi wa uwekezaji wake katika dhamana za Serikali mara kwa mara. Hiyo imetokana na uthibitisho uliopatikana kutoka Benki Kuu ya Tanzania ambao

ulibainisha kuwa Mfuko NSSF ulikuwa na uwekezaji wa thamani ya Shilingi bilioni 321.03 kinyume na rekodi za Mfuko za Shilingi bilioni 322.08 hivyo kusababisha tofauti ya Shilingi bilioni 1.05 ambayo haikuthibitishwa.

Kushindwa kufanyika kwa usuluhishi wa uwekezaji katika Dhamana ya Serikali kunaweza kusababisha mapungufu na tofauti, zinazoweza sababisha upotevu wa fedha za Mfuko.

NSSF unashauriwa kuchunguza kiasi cha fedha kilichowekezwa katika dhamana za Serikali, na pia kuhakikisha kuwa usuluhishi unafanyika mara kwa mara.

4.49.4 Kutofanyika kwa tathmini ya Kupungua Thamani kwa Mradi Uliosimamishwa wa Dege Kigamboni Shilingi Bilioni 220

NSSF iliingia katika Ubia na Azimio Housing Estate Limited (AHEL) kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Makazi katika eneo lenye ukubwa wa ekari 300 katika mji wa Dege Kigamboni.

Ubia umesajiliwa kama Hifadhi Builders Limited. Katika ubia huu NSSF inamiliki asilimia 45 na AHEL asilimia 55. Katika ya asilimia 55 za AHEL ,asilimia 20 ni thamani ya ardhi. Makadirio ya gharama ya mradi huo ni Dola za Kimarekani milioni 653.44 ambayo asilimia 20 (sawa na dola za kimarekani milioni 108.91) ni thamani ya ardhi.

Ukaguzi wangu wa mradi , ulibainisha kuwa mradi huo una thamani ya Shilingi bilioni 220 katika vitabu vya hesabu, Hata hivyo, utekelezaji wa mradi ulisimamishwa mwezi Januari 2016 kufuatia mapungufu ya mkataba, na kusababisha kushindwa kuelewana kati ya Mfuko na Azimio Housing Estates Limited.

Kusimamishwa kwa mradi huo kunachukuliwa kama kupungua kwa thamani chini ya Kiwango cha Kimataifa cha Hesabu na. 36 ambapo NSSF haikufanya tathmini kama thamani imepungua au la.

Ninapendekeza NSSF kufanya tathmini ya upungufu wa thamani ya mradi ili kuhakikisha kuwa mali zake zinarekodiwa kwa usahihi.

NSSF unahitaji kuchunguza umuhimu wa mradi huu uliosimamishwa, kwa kuzingatia kiasi cha fedha kilichowekezwa na kutafuta njia mbadala inayofaa na yenye ufanisi ili kuhakikisha kuwa fedha zake zilizowekezwa zinaleta manufaa kwa Mfuko.

4.50 Hoja za Jumla zilizojitokeza kwenye Mashirika Mengi

4.50.1 Haja ya kuhakikisha sheria ya kodi ya mwaka 2004 na sheria ya fedha ya mwaka 2015 zinaendana

Mapitio niliyofanya kwenye taarifa za fedha za mashirika matano (5) wakati wa kutathmini athari ya Mashirika ya Umma kufuata Sheria ya Fedha ya mwaka 2015, nilibaini kuwa sheria inaitaka Mashirika na Taasisi za umma kuchangia asilimia 15 ya mapato yake (gross revenue) kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Pia, nilifanya mapitio ya Jedwali la Kwanza la sheria ya kodi ya mwaka 2004 linaloyataka Mashirika, Kurugenzi kukatwa kodi ya asilimia 30 ya mapato yote baada ya kutoa matumizi.

Baada ya tathmini ya mashirika, tulibaini kuwa taasisi hizo zinachangia asilimia 15 ya jumla ya mapato yote kabla ya kutoa matumizi; na wakati huo huo, mchango wao haujazingatiwa kama moja ya makato yanayotambuliwa (allowable expenses) kabla ya kukata kodi.

Mashirika hayo ni Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa, Shirika la Nyumba Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa Arusha na Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa pamoja yamechangia kiasi cha Shilingi bilioni 151.7 kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali na kiasi cha kodi ya mapato kilicholipwa na mashirika hayo ni Shilingi bilioni 87.6. Hali hii inaongeza mzigo wa kifedha kwa mashirika hayo. Malipo

hayo ni kama yanavyooneshwa kwenye jedwali namba 4 hapa chini.

Jedwali 3: Makato ya kodi pamoja na michango kwenye Mfuko Mkuu

Taasisi	Mapato yanayokatwa asilimia 15 'Shilingi	Mchango kwenye mfuko mkuu wa hazina (Asilimia 15) 'Shilingi	Kodi ya Makampuni kama kwenye taarifa ya fedha (Asilimia 30) 'Shilingi
TANAPA	207,587,218,000	30,206,435,000	1,136,098,000
NHC	154,225,947,000	1,000,000,000	4,583,058,000
TPA	641,152,646,000	106,903,872,000	77,909,761,000
NCAA	101,774,817,000	13,000,000,000	3,490,320,000
AICC	14,437,121,544	607,948,935	54,764,863

Serikali inashauriwa kufanya tathmini ya kina kwenye sheria hizi mbili. Ikiwezekana, mapato yanayochangiwa kwenye mfuko mkuu wa serikali yatambuliwe kama moja ya makato kabla ya kukata kodi ya kampuni.

4.50.2 Madeni ya Serikali Yaliyozidi Muda wa Kulipwa Shilingi Bilioni 644.24

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 imebainika ya kwamba, serikali inadaikiwa Shilingi bilioni 644.24 yaliyozidi muda wake wa kulipwa kutoka katika taasisi tofauti sita (6). Madeni haya yanatokana na mikopo ya moja kwa moja, dhamana, na michango ambayo haikuwasilishwa kulingana na matakwa ya kisheria. Madeni ya Serikali yaliyozidi muda wa kulipwa yameorodheshwa kwenye *Kiambatisho Na. III*

Kutokulipwa kwa madeni hayo kwa taasisi husika kunaathiri nguvu za kifedha za taasisi zinazotarajia kupokea fedha hizo. Kwa upande mwingine, kunaathiri shughuli zao za kiutendaji.

Serikali inashauriwa kufanya juhudi za makusudi kuokoa hali hiyo kwa kulipa madeni hayo, kwani baadhi ya taasisi zimedhoofika kifedha kiasi kwamba haziwezi kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu na kwa ufanisi unaotakiwa.

4.50.3 Kutokuwapo kwa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma

Kwa mwaka huu wa ukaguzi, kulikuwa na Bodi za mashirika 20 ambazo zimemaliza muda wake; na hakuna Bodi mpya za kusimamia mashirika hayo zilizochaguliwa hadi ninakamilisha ukaguzi wangu mwezi Machi 2018. Baadhi ya taasisi zimekuwa zikiendelea na utendaji wa kazi bila ya Bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja. Taasisi ambazo hazina Bodi zimeonyeshwa kwenye *Kiambatisho Na. IV*.

Kutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi na Wadhamini kunazorotesha shughuli za kiutendaji za mashirika hayo.

Tunashauri serikali iteue Bodi za Wakurugenzi na wadhamini kwa wakati pindi zinapomaliza muda wake. Pia Bodi zipitie na kupitisha taarifa za hesabu kwa muda muafaka ili kuwezesha mchakato wa ukaguzi kuendelea na kukamilika kwa wakati.

4.50.4 Madeni ya Muda Mrefu ya Shilingi Bilioni 41.45

Ukaguzi ulibaini kuwa mashirika na taasisi mbalimbali zinawadaiwa ambao hawajalipa kwa muda mrefu.

Malimbikizo hayo ya madeni ya muda mrefu yanasababishwa na mashirika hayo kukosa ufanisi kwenye usimamizi wa madeni yake.

Madeni yaliyoorodheshwa kwenye *Kiambatisho Na. V* ni muhimu na yanaweza kuathiri shughuli za mashirika na taasisi husika kwa sababu fedha nyingi zipo katika mikono ya wadaiwa badala ya kulipwa ili ziweze kutimiza majukumu yaliyolengwa.

Menejimenti za Mashirika na Taasisi husika zinashauriwa kupitia upya taratibu na njia za usimamizi wa madeni kwa maboresho zaidi ili kuweza kukusanya madeni kwa wakati.

4.50.5 Ucheleweshaji na Kutopelekwa kwa Makato ya Kisheria Shilingi bilioni 42

Mapitio ya makato ya kisheria ilibaini kwamba, baadhi ya mashirika hayakupeleka makato yake kwa muda uliowekwa. Makato hayo ya kisheria ambayo hayakupelekwa yanajumuisha michango ya kodi ya VAT, PAYE, michango ya pensheni pamoja na kodi ya ujuzi na maendeleo yenye thamani ya Shilingi bilioni 42.

Madeni hayo yameendelea kuongezeka kwa miaka kadhaa. Hali hii huweza kupelekea kulipa faini, riba, na adhabu ambazo zitaathiri hali ya kifedha ya Taasisi/ Mashirika hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa.

Kutokulipa kwa kodi kunaweza kuaathiri kiasi cha mapato ambayo Serikali ingepata. Pia, kutolipa michango ya pensheni kwa wakati kunaathiri uwezo wa kulipa mafao kwa wafanyakazi wakati wa kustaafu. Mafao ya wafanyakazi na kodi ambayo haijapelekwa kwa wakati yameelezewa kwenye *Kiambatisho Na. VI*.

Taasisi husika zinashauriwa kufanya jitihada za ziada ili kuhakikisha makato yote ya kisheria yanapelekwa kwenye taasisi husika kwa wakati. Hali hii itasaidia kuepuka faini, riba na adhabu zisizokuwa za lazima.

SURA YA TANO

MAPITIO YA MIKAKATI NA UENDESHAJI WA KIUFANISI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

5.0 Utangulizi

Usimamizi wa kimkakati unajumuisha mipango endelevu, ufuatiliaji, uchambuzi, na tathimini ya shughuli zote muhimu kwa ajili ya shirika kuweza kufikia malengo na madhumuni yake. Usimamizi wa kimkakati unahusisha kuchambua uwezo na udhaifu wa ndani na nje; kutengeneza mipango na tathimini ya utekelezaji wake, pamoja na kutathimini mafanikio na kufanya mabadiliko ili kufikia malengo.

Kwa upande mwingine, uendeshaji wa kiufanisi una maana uwiano kati ya nyenzo zinazohitajika kwenye biashara na matokeo yanayopatikana. Uendeshaji wa kiufanisi unajumuisha mikakati mbalimbali inayotumika kukamilisha malengo ya msingi ya kutoa huduma na bidhaa kwa wateja ndani ya muda na zenye kiwango na gharama nafuu.

Ufanisi unahusisha kupata thamani kutoka kwenye rasilimali na kupunguza upotevu katika uzalishaji na hatimaye kuongeza uzalishaji.

Nilikagua ufanisi wa mikakati na uendeshaji katika Mashirika ya Umma yaliyoainishwa hapo chini:

- (i) Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)
- (ii) Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)
- (iii) Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA)
- (iv) Bohari Kuu ya Dawa (MSD)
- (v) Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

- (vi) Mradi wa Viuadudu
- (vii) Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)
- (viii) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)
- (ix) Mfuko wa Self (SELF Microfinance)
- (x) Shirika la Posta
- (xi) Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA)

5.1 Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)

5.1.1 Mapungufu katika Usimamizi wa Ardhi na Mipaka

Hifadhi za Taifa Tanzania ina jumla ya mbuga za wanyama 16, zikiwemo mbuga ya Arusha, Manyara na Tarangire, ambapo nilibaini kuwapo kwa migogoro ya ardhi na mipaka kama inavyoelezwa hapo chini:

- (i) **Eneo la Mbuga ya Arusha linalomilikiwa na mtu Binafsi**
 Nilibaini kuwa ndani ya mbuga ya Arusha, kuna hekta 100 za ardhi zijulikanazo kama ‘Halali Estate’ ambazo ni sehemu ya kitalu namba 398 katika eneo lililopimwa namba 12691 lenye hati namba 15942 ambazo zinamilikiwa na raia wa Ujerumani ajulikanaye kama Von Blumental, licha ya eneo hilo kutangazwa kuwa sehemu ya mbuga ya Arusha mnamo 1967.

Kamishina wa ardhi aliishauri Hifadhi za Taifa mnamo tarehe 16 Juni 2017 kuvuta subira kwa sababu suala hilo lilikuwa lipo chini ya vyombo vya sheria.

- (ii) **Makazi na Shughuli za Watu katika Ukanda wa Wazi wa Mbuga**
 Ukanda wa wazi unaruhusu wanyama kuwinda ili kuweka uwiano sahihi wa wanyama wa porini. Ukanda wa wazi wa King’ori na Simanjiro Kusini mwa mbuga ya Arusha, Ziwa

Momella, Lendoiyaa na Sanya Mashariki mwa mbuga ya Arusha na pia maeneo ya kutawanyikia (dispersal areas) ya Magharibi mwa eneo la Kilimanjaro, Olkungw'ado, longido, Ziwa Natron na Uwiro mpaka Ngabobo yamezibwa kutokana na kongezeka kwa makazi ya watu na shughuli za kilimo ambazo zinafanya maeneo hayo kuwa madogo.

Zaidi ya hayo, ukanda wa wazi wa Kisimiri katika mbuga ya Arusha ulikuwa wazi, ingawa violeza vilikuwa bado havijawekwa na jamii ilikuwa bado ina usimamizi wa ardhi hiyo. Hifadhi za Taifa walipanga kuulinda ukanda wa wazi kufikia Juni 2016 lakini ukanda huo bado haujalindwa.

(iii) Migogoro ya Muda mrefu kati ya Mbuga na Jamii Zinazoizunguka

Migogoro ya ardhi katika ziwa Manyara ilikuwepo tangu mwaka 2009 baada ya tamko la mipaka mipya ya mbuga. Kuna maeneo ya mbuga ambayo mipaka bado haijawekwa kutokana na migogoro kati ya mbuga na jamii zinazoizunguka. Hata hivyo, mbuga ya Manyara imesafisha takribani kilomita 96 kati ya kilomita 146.8 ya urefu wa mipaka.

Katika mbuga ya Tarangire, jumla ya hekta 22,694.8 za ardhi zilikuwa na migogoro kati ya mbuga na jamii zinazoizunguka, ambapo kati ya hizo, hekta 6,499.6 (asilimia 29) zilipatiwa usuluhisho na kuacha hekta 16,195.2 (asilimia 71) zikiwa bado katika migogoro licha ya Mbuga kuweka juhudi za kuthibitisha mipaka yake tangu 2004.

TANAPA inashauriwa:

- a) Kuweka mkazo na kuendelea kushirikiana na jamii na kuhakikisha kanda za wazi za Kusini na Mashariki mwa mbuga ya Arusha zinafunguliwa.

- b) Kuendelea kufuatilia kwa Kamishina wa Ardhi kuhakikisha ardhi yenye hati namba 15492 inakuwa chini ya miliki ya TANAPA kama ilivyo kwenye Sheria ya mbuga za wanyama na tamko la Rais.
- c) Kuharakisha uwekaji wa violezo kuzunguka mipaka ya mbuga na kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii zinazozunguka.

5.1.2 Hatari ya Kupotea kwa Ziwa Manyara

Katika kupitia taarifa ya ikolojia, nilibaini kuwa kuna hatari kubwa ya kupotea kwa ziwa Manyara na vivutio vyake kutokana na kuongezeka kwa watu, matumizi mabaya ya ardhi ikiwemo umwagiliaji, kilimo na malisho ya mifugo kwenye maeneo yanayozunguka ziwa, kupotea kwa misitu kutokana na ongezeko la maeneo ya kilimo, kukata miti kwa ajili ya ujenzi na mkaa. Shughuli zote hizi zinasababisha maeneo kuwa wazi na yenye ukame, hivyo kupelekea mmomonyoko wa udongo unaopunguza kina cha ziwa, kiasi kwamba, wakati wa kipindi cha kiangazi ziwa linakauka kufikia wastani wa kina cha sentimita chini ya 50 katika maeneo ya kina kirefu.

TANAPA inashauriwa kuongeza juhudi katika kuchukua hatua ambazo zitahakikisha hatari ya kupotea kwa ziwa Manyara inadhibitiwa.

5.1.3 Kupishana kwa Mkakati wa Jumla na Mikakati ya Mbuga na Hifadhi husika

Mkakati wa jumla wa hifadhi wa TANAPA ulioandaliwa katika ngazi ya juu unajumuisha kipindi cha miaka 5 kutoka 2013 hadi 2018, wakati mikakati ya mbuga na hifadhi husika inajumuisha kipindi cha miaka 10. Hivyo basi, ni vigumu kutathmini mikakati ya hifadhi na mbuga husika kwa kulinganisha na mkakati wa jumla wa hifadhi. Hii ni kwa sababu miaka inapishana na baadhi ya malengo yaliyopo katika mkakati wa jumla wa hifadhi hayakujumuishwa kwenye mikakati ya mbuga na hifadhi husika.

Ninaishauri TANAPA kuhakikisha kuwa mikakati ya mbuga ya hifadhi husika inaendana na mkakati wa jumla ya hifadhi ili kuweza kufanya tathmini ya utekezaji baina ya mikakati hiyo miwili.

5.2 Mamlaka ya udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)

5.2.1 Kutowasilishwa kwa mpango wa vipindi vinavyorushwa na vituo vya redio na runinga

Kipengele cha 22 (1)-(3) cha Kanuni za Huduma ya Habari (2005) kinahitaji vituo vya redio na runinga vyenye leseni kutangaza jedwali la mpango angalau mwezi mmoja kabla kwenye gazeti la kila siku ambalo linaenea sehemu kubwa ya Tanzania, pia kufuata jedwali hilo la mpango katika kurusha vipindi. Pia, vituo hivyo vinatakiwa kuwasilisha mambo yafuatayo kwa Mamlaka: kwanza, jedwali la mpango wa robo mwaka siku 14 kabla ya kuanza kwa robo mwaka; pili, kila mwisho wa mwezi kutoa taarifa ndani ya siku 7 inayoonesha vipindi halisi vilivyorushwa; na tatu, kila mwisho wa mwezi kutoa orodha ya miziki ndani ya siku 7 iliyorushwa hewani.

Katika kupitia vituo 10 vya redio na runinga kati ya vituo 128 vyenye leseni halisi, nilibaini kuwa vituo havikuwasilisha jedwali la mpango la robo mwaka kama kanuni zinavyohitaji.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Mamlaka haina miongozo ambayo inahitaji jedwali la mpango lililotangazwa, jedwali la mpango la robo mwaka linalotolewa kabla, taarifa ya vipindi halisi vilivyorushwa na orodha ya miziki iliyorushwa hewani kuhakikiwa baada ya kuwasilishwa.

Mamlaka inaweza isiwe kwenye nafasi ya kujua vipindi ambavyo vitarushwa hewani kiasi cha kuleta hatari kubwa ya maudhui ya vipindi vinavyorushwa.

Mamlaka inatakiwa kuhakikisha vituo vya habari vinatekeleza majukumu yao kwa kuwasilisha jedwali la mpango kama

ilivyoelekezwa kwenye kipengele 22 (1-3) cha Kanuni za Huduma ya Habari (2005).

5.2.2 Dhamana za Vifaa vya Kielektroniki vya Mawasiliano ambavyo Havijathibitishwa

Kipengele cha 39 cha kanuni ya kielektroniki na mawasiliano ya Posta (2011) kinahitaji waingizaji, wasambazaji au wauzaji wa vifaa vya kielektroniki vya mawasiliano kutokuingiza kwa ajili ya kuuza au, kusambaza vifaa vyovyote ambavyo dhamana yake ni chini ya miezi kumi na miwili.

Katika kupitia miongozo iliyowekwa na Mamlaka kuhakikisha kuwa vituo vinafuata kanuni tajwa hapo juu, nilibaini kuwa hakuna utaratibu wowote unaohakikisha kuwa kanuni hizi zinafuatwa.

Pia, nilibaini kuwa Mamlaka haina ushirikiano na wadau wengine kama Shirika la viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuwezesha ufuatiliaji wa kanuni hizo.

Haki za watumiaji zinaweza kuwa hazijalindwa kikamilifu kwa kukosekana kwa miongozo ya kuhakiki dhamana. Hivyo, mamlaka inapaswa;

- (i) Kutengeneza utaratibu ambao utaiwezesha kusimamia na kudhibiti ubora wa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vinavyoingizwa nchini.
- (ii) Kuwahusisha wadau wengine kama Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kusaidia kuhakikisha kuwa vifaa vyote vya kielektroniki vinakidhi ubora unaotakiwa.

5.2.3 Upungufu katika Kusimamia Yaliyomo katika Huduma ya Mawasiliano

Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania ina wajibu wa kudhibiti mawasiliano, habari, mawasiliano ya kielektroniki,

huduma za posta na usimamizi wa wigo wa mawimbi ya kitaifa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama mdhibiti, Mamlaka ina wajibu wa kuhakikisha kuwa leseni zinatolewa kwa vituo vyote vya habari na vituo hivyo vinaendeshwa bila kuathiri viwango vya ubora wa huduma.

Katika kupitia udhibiti wa utendaji wa yaliyomo katika huduma ya mawasiliano na habari, nilibaini kuwa hakuna kanuni za udhibiti wa habari kwa njia ya mtandao (online content Regulations). Pia, nilibaini kuwapo kwa watoa huduma ya habari kwa njia ya mtandao ambao hawajasajiliwa na Mamlaka.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa mfumo wa udhibiti wa maudhui uliopo sasa umepitwa na muda, na unahitaji kuboreshwa ili kuendana na maendeleo ya teknolojia yanayoendana na ulimwengu wa utandawazi katika mawasiliano.

Pia, kuna waajiriwa 6 tu ambao wanashughulika na udhibiti wa maudhui ya habari. Idadi hii haitoshi kukidhi ukubwa wa kazi ya udhibiti wa yaliyomo katika huduma ya habari ya redio na runinga kwa nchi nzima.

Katika ofisi za kanda, udhibiti wa yaliyomo haufanyiki wote na kwa muda unaotakiwa kwa sababu hakuna maofisa waliopewa kazi ya kudhibiti, pia hakuna vifaa vya kudhibiti huduma hizo. Nilibaini kuwa mara nyingi udhibiti wa maudhui unafanyika kufuatia malalamiko yanayoletwa na wateja.

Ili kufanikisha zoezi la udhibiti kwa vituo vya redio na runinga, Mamlaka inashauriwa kufanya yafuatayo:

- a) Kuharakisha mchakato wa kuandaa kanuni za udhibiti wa maudhui katika huduma ya habari kwa ajili ya udhibiti wa huduma hiyo.
- b) Kuziwezesha ofisi za kanda ili kuhakikisha kuwa udhibiti wa maudhui katika habari unafanyika kwa muda sahihi.

- c) Kuongeza idadi ya waajiriwa wanaoshughulika na udhibiti wa maudhui katika huduma ya habari
- d) Kuitaarifu Serikali umuhimu wa kuharakisha mchakato wa kusimika mfumo mpya wa kudhibitiwa maudhui katika huduma ya habari.

5.2.4 Udhibiti Usioridhisha wa Watoa Huduma

Kifungu cha 6 (1) cha Kanuni ya Mamlaka ya udhibiti wa Mawasiliano Tanzania ya mwaka 2003, Mamlaka ilianzishwa kwa lengo la kutoa, kuhuisha, na kusitisha leseni, kudhibiti viwango vya tozo na utendaji wa sekta zinazodhibitiwa.

Hata hivyo, nilibaini usimamizi wa watoa huduma haufanyiki kwa kiwango cha kutosha kiasi kwamba sio wasambazaji na waingizaji wote wa vifaa vya kieletroniki walikuwa na leseni inayotolewa na TCRA. Pia, nilibaini kuwa baadhi ya mabasi yanasafirisha vifurushi bila ya leseni ya kusafirisha vifurushi hivyo inayotolewa na Mamlaka.

Sambamba na hayo, nilibaini kuwa hakukuwa na utaratibu uliopangwa wa ukaguzi wa watoa huduma za Posta waliopo nje ya Dar es Salaam, hali hiyo imepelekea ukaguzi kufanyika kwa dharura, hasa baada ya kupokea malalamiko ya wateja au kulingana na ratiba ya ukaguzi wa ofisi za mikoa za Shirika la Posta Tanzania.

Pia, nilibaini kuwa Mamlaka haina kanzidata ya baadhi ya watoa huduma kama za posta, wasambazaji wa vifaa vya kieletroniki na wasimikaji na warekebishaji wa vifaa vya kielektroniki. Jambo hili linasababisha watoa huduma wengi kufanya kazi bila leseni hivyo kuleta hatari kwenye ubora wa huduma inayotolewa.

Mamlaka inatakiwa kuja na mpango ambao utasaidia kutilia mkazo kwenye usimamizi wa sheria, viwango vya ubora, na uelewa kwa jamii. Pia, Mamlaka inatakiwa kusisitiza watoa

huduma kufuata sheria na kuhakikisha vituo ambavyo havijasajiliwa vinasajiliwa kwa leseni sahihi. Pia, Mamlaka iwe na kanzidata ya watoa huduma wote ili kurahisisha ufuatiliaji wa shughuli wanazofanya.

5.2.5 Ucheleweshwaji wa Mchakato wa Kutoa Leseni

Mamlaka inatoa leseni binafsi, leseni za madaraja na vyeti. Leseni binafsi ni pamoja na leseni za vifaa vya mtandao, za huduma ya mtandao, za huduma ya mifumo ya mitandao, pamoja nazo huduma inayohusu maudhui. Leseni hizo ni zile zinazoleta mabadiliko makubwa kijamii, kiuchumi na kikanuni. Leseni za madaraja ni pamoja na huduma ya kusafirisha vifurushi vya habari, vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki. Hizi ni zile ambazo hazileti mabadiliko makubwa kijamii, kiuchumi na kikanuni. Kwa aina zote za leseni, muda unaokubalika kuanzia kuomba leseni hadi kutolewa ni siku 60.

Katika mwaka wa Ukaguzi, Mamlaka ilitoa jumla ya leseni 26 za kusafirisha vifurushi vya posta. Nilichukua sampuli ya leseni 22 na kubaini kuwa kuna ucheleweshaji wa utoaji wa leseni wa wastani wa siku 86 kutoka muda wa kuomba leseni hadi inapotolewa ambao muda huo ni zaidi ya ule wa kisheria wa siku 60.

Pia nilibaini kuwa tarehe ya kuisha muda wa leseni haufuutiliwi kwa utaratibu mzuri ili kumfahamisha mtoa huduma kuisha kwa leseni yake kabla ya muda.

Ucheleweshaji wa kutoa leseni unamaanisha kuwa, hakuna ufanisi kwa upande wa Mamlaka. Ninaishauri Mamlaka kuongeza ufanisi ili kutoa leseni katika muda unaotakiwa kisheria.

5.2.6 Kucheleweshwa kwa Ukamilishaji wa Mradi wa Mfumo wa Uhakiki wa Mapato ya Sekta ya Mawasiliano

Mamlaka inatekeleza mradi wa mfumo wa uhakiki wa mapato ya sekta ya mawasiliano ambao ni mfumo mdogo wa nyongeza ya

mfumo wa kuratibu mfululizo wa mawasiliano katika mfumo wa mawasiliano (TTMS) ambayo ina lengo la kutoa uhakika wa mfumo wa mapato ya sekta ya mawasiliano kwa Serikali.

Utekelezaji wa mradi huu utaongeza uwezo wa kiufundi wa Mamlaka pamoja na uwezo wa kuhakiki mfumo wa mapato wa vituo vya habari. Jumla ya maeneo 14 ya mbali yataunganishwa kuelekea kituo kikuu kwa kupitia kebo yenye muungano wa waya za kiojoo ili kuwezesha kusafirisha taarifa kutoka maeneo ya mbali kwenda kituo kikuu.

Mradi ulipangwa kukamilika kufikia tarehe 27 Septemba mwaka 2017, hata hivyo mpaka kufikia muda wa ukaguzi mwezi Oktoba 2017, mradi huo ulikuwa haujakamilika, na hapakuwa na tarehe nyingine ya kukamilisha mradi iliyokuwa imepangwa.

Aidha, hakuna tathmini ya tahadhari iliyofanyika kwenye mradi, na hivyo hakuna mikakati iliyowekwa ya kupambana na tahadhari.

Nilitaarifiwa na Mamlaka kuwa ununuzi wa TTMS, ambapo TRAS ni moja ya mfumo mdogo yake, hufanywa kupitia mfumo wa Unda, Tumia na Hamisha. Hivyo, tahadhari zote zinahamishiwa kwa Mkandarasi wa TTMS kuanzia mwanzo wa utekelezaji wa mradi hadi mradi unapokamilika.

Mamlaka inashauriwa kupitia tena mpango wa utekelezaji wa mradi na kufanya tathmini ya tahadhari ya mradi ili kuainisha tahadhari na kuweka mikakati ya kuepuka tahadhari hizo ili kupata mafanikio yatokanayo na mradi huo.

5.3 Chuo Kikuu Cha Sokoine (SUA)

5.3.1 Kukosekana kwa Mikakati na Mpango wa Kuhuisha Tafiti na Kutowekea mkazo Makubaliano

Mnamo mwaka 2014, Chuo Kikuu kiliuza tafiti 3 zenye hati miliki zijulikanazo kama MSHINDI, PESA na MWANGAZA kwa TANSEED

International kupitia makubaliano ya mimea 3 yenye leseni, ambapo mtoa leseni na mpokea leseni walikubaliana kuwa mpokea leseni atakuwa na haki ya kuuza tafiti hizo; pia, walikubaliana mrabaha na kodi ya kukimu ya mwaka zitalipwa na mpokea leseni.

Baada ya kuuza, mtoa leseni anatakiwa kumsaidia mpokea leseni katika kusasisha tafiti husika ili iendane na hali ya soko.

Nilibaini kuwa, Chuo hakina mkakati wala mpango wa kuhuisha tafiti zake ambazo tayari zipo sokoni. Hali hii inaweza kupelekea tafiti hizi kuwa zimepitwa na muda.

Zaidi ya hayo, kifungu 2.1 (c) cha makubaliano kinaeleza kuwa, kama kodi ya kukimu na mrabaha hazitalipwa kama ilivyoelekezwa kwenye mkataba, basi riba ya asilimia 18 itadaiwa pamoja na kodi ya kukimu ya kila mwaka na mirabaha ambayo haijalipwa kwa kipindi cha nyuma. Pia, kifungu 2.3 (a) kinahitaji mauzo ya mbegu za mimea zinazouzwa na mpokea leseni yalipiwe mrabaha katika kiwango cha asilimia 1 ya bei ya mbegu; na malipo yafanywe tarehe 30 mwezi Oktoba ya kila mwaka.

Hata hivyo, Chuo hakijakusanya kodi ya kukimu ya mwaka na mirabaha kwa kipindi cha miaka 3 kuanzia 2014/2015 hadi 2016/2017. Kutofuata makubaliano ya mkataba kunakiondolea Chuo haki ya kupata mapato kupitia kodi ya kukimu ya mwaka na mirabaha.

Chuo kinashauriwa kuwa na mkakati na mpango madhubuti wa kuhuisha na kuboresha tafiti zake; na pia, kuingia makubaliano na wapokea leseni ili kutoa msaada wa kiutaalamu. Zaidi, Chuo kinatakiwa kikusanye kodi ya kukimu ya mwaka pamoja na mirabaha ambayo haijalipwa.

5.3.2 Kukosekana kwa Usimamizi Unaoridhisha wa Tafiti zenye Hati Miliki (Patents)

Kifungu cha 5 (r) cha miongozo ya chuo ya 2007 kinahitaji Chuo kulinda na kutunza haki za tafiti vilizovumbuliwa kutokana na juhudi za Chuo katika kutimiza majukumu yake.

Nilibaini kuwa, Chuo kilitafuta hati miliki (patented) ya tafiti 14; kati ya hizo, 3 ziliuzwa na 11 zilizobaki hazijauzwa. Vumbuzi 11 ambazo bado hazijauzwa zimeorodheshwa hapo chini:

- (i) Jukwaa lenye pande mbili la kupasulia magogo
- (ii) Jinsi ya kutengeneza Poda ya ubuyu kama mbadala wa viambata vya kutengenezea Jamu;
- (iii) Matumizi ya viambata ghafi kutoka mmea wa *Synadenium glaucescens* kwa ajili ya kutibu magonjwa ya virusi vya kuku;
- (iv) Matumizi ya viambata ghafi kutoka mmea wa *Synadenium glaucescens* kwa uponyaji wa jeraha na Udhibiti wa magonjwa ya bakteria na ya fungasi
- (v) Matumizi ya viambata ghafi kutoka mmea wa *Commiphora swynnertonii* ili kudhibiti ugonjwa wa Newcastle katika kuku
- (vi) Ubunifu wa kutengeneza Vifaa vya umwagiliaji kwa njia ya drip
- (vii) Mfumo wa Umwagiliaji unaotumia Nishati ya jua isiyounganishwa na waya.
- (viii) Matumizi ya mkojo mkali kuzibiti panya kwenye mashamba

- (ix) Jinsi ya kuandaa udongo wa kuoteshea miti ya *Olea welwitschii* L. (Ironwood Olive) kwa kutumia kipandikizi cha Shina
- (x) Uuandaaji wa udongo wa kuoteshea miti ya *Olea welwitschii* L.(Ironwood Olive) kwa kutumia vipando vya kawaida

Pia, nilibaini kuwa tafiti 2 zenye hati miliki kati ya 11 zilizotajwa hapo juu zilikuwa zimewekwa kwenye mitandao ya kijamii bila ya ruhusa ya Chuo licha ya kwamba Chuo kilipewa haki ya tafiti hizo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Hali hii inaathiri uwezo wa Chuo katika kusimamia tafiti na vumbuzi zake.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa SUA NITRO ni moja ya vumbuzi za Chuo zenye soko zuri. Nilibaini kuwa SUA NITRO iliwekwa kwenye mitandao ya jamii kwa biashara bila ya kupata hati miliki kutoka mamlaka husika, hali iliyopelekea Chuo kupoteza mapato kutokana na vumbuzi zake.

Chuo kinashauriwa kuweka udhibiti kuhakikisha tafiti zake hazipelekwi kwenye mitandao ya jamii bila ya ruhusa, pia kuweka utaratibu wa kuuza tafiti hizo.

Chuo pia kinashauriwa kushirikiana na Mamlaka husika ili kupata hati miliki ya tafiti ambazo zipo sokoni na kuandaa utaratibu wa kuingia makubaliano na wasambazaji ili Chuo kipate mrabaha na kodi ya kukimu ya mwaka.

5.3.3 Usajili Usioridhisha wa kazi binafsi za Ushauri

Kifungu cha 6.1 cha sera ya Ushauri (Consultancy policy), Taratibu na Miongozo ya mwaka 2000 kinaelekeza mgawanyo wa mapato yanayopatikana kutokana na kazi zilizopatikana kwa Taasisi, Kitivo au juhudi binafsi kuwa kama ifuatavyo: asilimia 5 ya Kamisheni ya mapato ya kodi kwa watu binafsi waliofanikisha upatikanaji wa kazi; asilimia 80 kwa Washauri; asilimia 7 kwa

Chuo; asilimia 5 kwa kitengo kinachoongoza utoaji ushauri kutoka kwenye Kitivo/Taasisi; na asilimia 3 kwa SUACONSULT.

Katika majadiliano niliyofanya na Mkurugenzi wa Tafiti, Masomo ya Uzamili, Teknolojia na Ushauri, nilibaini kuwa sera ya utafiti haina kipengele kinachoelezea usajili wa kazi binafsi za ushauri. Watu binafsi wanatumia jina na vitendea kazi vya Chuo kufanya shughuli zao za ushauri, lakini Chuo hakifaidiki kutokana na kazi hizo.

Chuo kinashauriwa kupitia tena sera ya ushauri ili kuweka kipengele cha usajili wa kazi binafsi pamoja na zile zinazofanywa na washauri wa nje ya Chuo.

5.3.4 Kutoanzishwa kwa Mfuko wa Utafiti

Kikao cha baraza la Chuo cha 135 kilichofanyika tarehe 25 mwezi Septemba mwaka 2014 kiliidhinisha kuanzishwa kwa mfuko wa Utafiti ili uwe chanzo cha ndani cha mapato kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa tafiti. Mfuko huo utatumika kwa ajili ya watafiti wadogo kutekeleza tafiti zao kutokana na mada zitakazotangazwa na idara ya tafiti na masomo ya uzamili.

Vyanzo vya fedha kwa ajili ya mfuko vilipendekezwa kutoka katika asilimia 2 ya fedha za wafadhili wa utafiti, asilimia 2.5 ya fedha ya ada ya Shahada ya Kwanza na asilimia 3.5 ya ada ya Shahada ya Uzamili.

Mfuko huo haujaanza kufanya kazi licha ya Baraza kuidhinisha. Kutosimikwa kwa mfuko huo kunazuia nafasi ya watafiti wadogo kujenga uwezo.

Chuo kinashauriwa kuhakikisha kuwa mfuko unafanya kazi ili kusaidia watafiti wadogo.

5.3.5 Kuchelewa kuanza kazi kwa Kampuni ya Uwekezaji ya Chuo

Kanuni na Sera ya Uwekezaji ya Chuo ya mwaka 2005 inaelezea kuanzishwa kwa kampuni ya uwekezaji ya Chuo kwa njia za hisa,

ubia na ushirikiano na wawekezaji wengine. Mnamo mwezi Agosti 2010, kampuni ilisajiliwa na BRELA kama kampuni yenye kikomo kwenye hisa yenye cheti cha usajili namba 77800 na mtaji ulioidhinishwa wa Shilingi bilioni 3.

Nilipitia utendaji wa kampuni kuanzia 2010 hadi 2017 na nilibaini mapungufu yafuatayo:

- i. Hakuna uelekeo sahihi ambao unawakumbusha watekelezaji wajibu wao;
- ii. Bodi wa wakurugenzi iliundwa baada ya miaka 5, hali inayoishiria kuwa kampuni ilianzishwa kabla ya kukamilisha taratibu muhimu; na
- iii. Gharama za uendeshaji wa kampuni hazikuweza kujulikana kirahisi kwa sababu ya kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kutunza gharama.

Kuchelewa kuanza kazi kwa kampuni kunapelekea malengo ya kampuni kutofikiwa kwa muda. Pia malipo ya gharama za uendeshaji wa kampuni zinaweza kuwa juu na kuchukuliwa kutoka kwenye bajeti ya Chuo ambayo haihusiani na kampuni.

SUA kinashauriwa kutathmini sababu za kuchelewa kuanza kazi kwa kampuni na kuzifanyia kazi. Chuo pia kingeangalia uwezekano wa kushirikiana na vyuo vingine ili kupata uzoefu wa kuendesha kampuni za aina hii.

5.3.6 Matumizi ya Chini ya Kiwango ya Shamba la Biashara

Kutokana na sera na mwongozo wa uwekezaji wa Chuo 2005, lengo kubwa la kuanzisha sera ya uwekezaji ni kuzalisha kipato cha ziada ili kuongezea gawio kutoka Serikalini; vilevile, ni kutoa msaada kwa jamii ya Chuoni ili kuboresha miundombinu kwa ajili ya shughuli za kitaaluma. Mpango Mkuu wa Chuo wa 2016 unaeleza kuwa moja ya mikakati ya Chuo ni kuhahakisha matumizi stahiki ya ardhi kwa ajili ya kuboresha miundombinu.

Chuo kina mashamba ya biashara ambayo yana jumla ya hekta 1482; ambapo, hekta 854 zipo Mazimbu na hekta 628 zipo makao makuu. Mashamba hayo hayajatumika tangu sera ya maendeleo ya shamba ilipoanzishwa na hakuna mpango kazi wowote ulioidhinishwa.

Kushindwa kutumia mashamba ya biashara ya Chuo kunazuia Chuo kupata mapato ya ndani ambayo yangesaidia kwenye shughuli zake.

Chuo kinashauliwa kutumia mashamba kikamilifu na kuwa na mpango kazi kwa ajili ya mashamba hayo.

5.4 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

5.4.1 Matumizi ya Mfumo wa Mizania (Balanced Score Cards)

Bodi ya Wadhamini ya Bohari Kuu ya Dawa iliamua kuhama kutoka mfumo unaotegemea kwenye matokeo katika kuandaa mpango mkakati wa nusu kipindi kwa kipindi cha 2014-2020 kwenda mfumo wa mizania. Mfumo wa mizania ni mfumo unaotumika kupanga na kupima utendaji kwa kuzingatia dira, dhamira na mkakati. Mfumo huu una sehemu 4 ambazo hutoa muonekano wa Bohari Kuu; na matumizi yake yanahitaji uelewa wa kutosha wa sehemu hizo 4.

Nilifanya mahojiano na Mkurugenzi wa mipango na kubaini kuwa, mikakati ilikuwa hauwasilishwi na kushushwa kwenye ngazi za chini kwa kiwango kinachotakiwa. Pia, mfumo wa kutathmini utendaji wa waajiriwa hauna maelezo na mtiririko wa kutosha. Pia, nilibaini kuwa sio waajiriwa wote wa kitengo cha tathmini na usimamizi walihudhuria mafundisho ya mfumo wa mizania.

Bohari inajiweka kwenye hatari ya kushindwa kutimiza mkakati wake kikamilifu kwa sababu ya kukosa uelewa wa kutosha wa kutumia mfumo wa mizania katika kutengeneza, kuwasilisha na kutimiza mkakati wake katika ngazi zote za Shirika.

Bohari Kuu inashauriwa kuhakikisha kuwa mafunzo ya mfumo wa mizania yanafanyika kwa wafanyakazi wote, hasa wale wanaohusika na utengenezaji wa Mpango Mkakati.

5.4.2 Kutobuniwa kwa Njia Nafuu ya kusafirisha Madawa na Vifaa vya Matibabu

Moja ya gharama kubwa ambazo Bohari inaziingia ni za usambazaji wa dawa kiasi cha kusababisha bei za dawa ziwe juu. Kupungua kwa gharama ya usambazaji kutafanya bei ya dawa iweze kuingia kwenye ushindani, na hivyo, kuiwezesha Bohari kufikia dhamira yake ya kuwezesha upatikanaji wa dawa muda wote, katika ubora na bei nafuu. Utaratibu unaotumika sasa wa kusafirisha dawa ni wa kutumia magari. Utaratibu huu hautoi nafasi ya uvumbuzi ili kupunguza gharama za usafirishaji. Bohari itaweza kupunguza gharama za usafirishaji kwa kushirikisha taasisi zingine za Serikali.

Pia, Bohari inaweza kushirikiana na Shirika la Ndege Tanzania katika kusafirisha dawa; jambo hili litaliongezea mapato Shirika la Ndege na kupunguza gharama za usambazaji wa dawa. Jambo hili litaweza kufanikiwa kwa ndege kuenda njia mpya ambazo ilikuwa haiendi, lakini kwa kushirikiana na Bohari Kuu ya madawa na kukubaliana kiasi cha mizigo ambacho kitakuwa kinasafirishwa, ndege itaweza kwenda njia hizo ngeni.

5.4.3 Kushindwa Kuainisha Vigezo vya Vifaa vya Afya Vinavyotakiwa Kununuliwa

Kifungu cha 3.9 cha makubaliano ya kisheria (Memorandum of Understanding) kati ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Bohari Kuu ya tarehe 29 Aprili 2016 kinaelekeza Wizara kutoa vigezo vya dawa, vifaa, vipuli na nyenzo nyingine za afya kwa ajili ya kununuliwa na Bohari, na ikiwezekana, kutaja na wauzaji, kiasi kinachohitajika na wakati wa kuleta.

Nilipotembelea vituo vya kanda na hospitali nilibaini kuwa hospitali hizo zilikuwa na mashine ambazo mara kwa mara zilikuwa hazifanyi kazi kwa sababu ya kukosekana kwa kemikali ya utendanishi.

Bohari inashauriwa kuwasiliana na Wizara tajwa ili kupata idadi ya vifaa vya afya ambavyo havifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali kama vile kukosekana kwa matengenezo na kukosekana kwa kemikali ya utendanishi.

5.4.4 Mapungufu katika utekelezaji wa mradi wa “Drones”

Bohari ilisaini makubaliano na Kampuni iitwayo Zipline, iliyopo Marekani, kwa ajili ya kutumia mitambo ya “Drones” kwa ajili ya kusafirisha madawa kwenda vituo 1,000 vya afya katika mikoa nchini.

Katika kutathmini utayari wa Bohari Kuu wa kutumia chombo hicho kwa usambazaji, nilibaini mapungufu kadhaa, yakiwemo kukosekana kwa mpango wa kibiashara uliotakiwa kutengenezwa kuonyesha matumizi sahihi ya chombo hicho na faida zitakazopatikana kama vile kupunguza gharama na kuongeza ufanisi.

Ninaishauri Bohari kutengeneza mpango wa kibiashara (Business case) ili kuainisha faida zitakazopatikana kutokana na matumizi ya mtambo huo.

5.4.5 Kukosekana kwa Muumano wa Huduma ya Mtandao kati ya Duka la Dawa la Bohari na Hospitali

Bohari iliboresha huduma zake ili kuendelea kufanya shughuli zake bila kuathiri uwasilishaji wa dawa bora, kwa bei nafuu karibu na jamii. Bohari ilifanikisha hili kwa kutengeneza maduka ya dawa yajulikanano kama “Community Outlets (MCO)”. Kuna maduka ya dawa sita ambayo yanaendeshwa na Bohari Kuu ambayo yapo Chato, Mbeya, Arusha, Mwanza, Katavi, na Hospitali ya Taifa Muhimbili. Maduka ya dawa yapo karibu au

ndani ya mazingira ya hospitali na hayakubali maelezo yoyote ya mgonjwa bila kupata ruhusa kutoka hospitalini.

Nilibaini kuwa, hakuna muunganiko kati ya mfumo wa uhasibu wa maduka ya dawa ya Bohari na mfumo wa hospitali. Hospitali haziwezi kujua kwa njia ya mtandao dawa zinazopatikana katika maduka ya dawa ya Bohari. Nilitembelea Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kubaini kuwa maelekezo ya dawa yalikuwa yanatolewa kwa wagonjwa kwa njia ya mtandao baada ya daktari mhusika kuhakiki upatikanaji wa dawa katika ghala kupitia mfumo wa “MNH JEEVA”. Kukosekana kwa muunganiko kati ya mfumo wa uhasibu wa maduka ya dawa wa Bohari kuu na mfumo wa hospitali kunapunguza ufanisi katika kutoa huduma kwa wagonjwa.

Ninashauri Bohari Kuu ya dawa kuweka muunganiko kati ya maduka ya dawa ya Bohari Kuu na hospitali ili kuimarisha utoaji wa huduma.

5.4.6 Kukosekana kwa Mfumo hai wa Kuhakiki Ubora wa Dawa na Vifaa Tiba vinazopelekwa Hospitali

Mwongozo wa huduma kwa wateja wa Bohari Kuu unahitaji Bohari Kuu kuhakikisha kuwa wateja wake wanapata dawa sahihi zenye ubora unaokubalika na katika muda sahihi, zaidi katika bei inayokubalika. Pia, aya ya 4 ya mwongozo huo inaelekeza bidhaa zote zinazoletwa zikaguliwe na kitengo cha kuhakiki ubora wa bidhaa. Zaidi ya hapo, Bohari Kuu inawahusisha wadau kama Mamlaka ya Dawa na Chakula Tanzania (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), GCLA na BICCO katika kuchukua sampuli na kuhakiki ubora wa dawa.

Nilipitia kitabu cha usajili wa malalamiko ya wateja na kubaini kuwapo kwa malalamiko yanayohusu kiwango cha chini cha ubora wa POP yenye ukubwa wa 7.5 na “cut guts” katika hospitali kadhaa za Wilaya, vipimo vya malaria viitwavyo “Malaria Rapid Diagnostic Test” vilikuwa vinatoa majibu yasiyo sahihi, kipimo cha

kupima presha ya damu kiitwacho “Riester” kilikuwa kimeharibika ndani ya miezi 2 ya matumizi. Mapungufu yaliyoonekana hayakuweza kuoneshwa na timu ya ubora wala waidhinishaji wa TFDA na TBS.

Ubora wa chini wa dawa na vifaa vya afya unaathiri ubora wa huduma za hospitali na wakati mwingine, inaathiri huhatarisha maisha ya wagonjwa.

Bohari Kuu inatakiwa kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinazoletwa zinafanyiwa uchunguzi ili kuhakikisha bidhaa zinazosambazwa zinakidhi viwango.

5.4.7 Gawio la Fedha lisilotosheleza Kwa Shughuli za Bohari Kuu

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Bohari Kuu haikupewa fungu la kutosha kufanya shughuli zake. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipanga kupeleka Shilingi bilioni 251.5 Bohari Kuu, lakini kiasi halisi kilichopelekwa in Shilingi bilioni 121. 08 (asilimia 48), hivyo kusababisha upungufu wa Shilingi bilioni 130.42.

Zaidi ya hapo, Bohari ina kiasi kikubwa cha wadaiwa, ambapo mwisho wa mwaka kulikuwa na deni la Shilingi bilioni 165.2. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 152.08 zilikuwa ni deni la Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Ninashauri Bohari Kuu washirikiane na Serikali kuhakikisha kuwa inalipa deni lake ili kuimarisha mtaji wa Bohari, na hivyo kuongeza ufanisi.

5.5 Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

5.5.1 Mbia Binafsi Ambaye Hajachangia Mtaji Katika Kampuni ya Global Packaging (T) Limited (GPTL)

Shirika la NDC na Kampuni ya Wande Printing & Packaging waliingia katika makubaliano tarehe 31 Machi 2013 ili kutengeneza ubia wa Kampuni iitwayo GPTL kwa lengo la

kusimika Mtambo katika eneo la viwanda la TAMCO. Shirika la NDC linamiliki asilimia 6 ya hisa zenye thamani ya Shilingi milioni 12 na Kampuni ya Wande inamiliki hisa 94 zenye thamani ya Shilingi milioni 188.

Katika kupitia makubaliano ya ubia ilibainika kuwa mtaji wa Shirika la NDC wa asilimia 6 ulikuwa katika mfumo wa ardhi yenye eneo la mita za mraba 17,419 lenye thamani ya Shilingi 200 milioni katika eneo la TAMCO na kampuni ya Wande ilitakiwa kuweka mtaji wa hisa za asilimia 94 zenye thamani ya Shilingi bilioni 3.44.

Nilibaini kuwa Wande hakuweka mtaji wa Shilingi bilioni 3.44 kwenye Kampuni. Suala hili linafanya umiliki wa asilimia 94 wa hisa kuwa wa mashaka.

Katika kupitia zaidi dokezo la Bodi la tarehe 8 Julai 2015 nilibaini kuwa Benki ya Taifa ya Uwekezaji (TIB) ilitoa mkopo kwa Kampuni ya GPTL wenye kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 2.33 (sawa na Shilingi bilioni 5) kwa ajili ya kusimika mtambo na kuwezesha shughuli. Mkopo huo ulikuwa na kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 1.63 kama mkopo wa muda mrefu na Dola za Kimarekani milioni 0.7 kama mkopo wa muda mfupi wenye riba ya mwaka ya asilimia 17 na kutumia hati ya Shirika la NDC kama dhamana.

Kwa sababu Kampuni ya Wande haikuchangia chochote kwenye mtaji, hivyo haina umiliki wowote katika ubia vinginevyo mkopo upatikane na ulipwe na Kampuni ya Wande.

Ninalishauri Shirika la NDC kutathmini kiasi lilichoweka kama mtaji kwa mfumo wa ardhi kulinganisha na mchango wa Kampuni wa Wande na kusimika sura mpya ya mgawanyo wa hisa kulingana na mchango wa kila upande.

5.5.2 Kucheleweshwa kwa uzalishaji wa Megawati 950 za Makaa ya Mawe na Nishati Mbadala

Shirika la NDC liliingia katika makubaliano ya ubia tarehe 21 Septemba 2011 na Kampuni ya “Sichuan Hongda (Group) Limited” ili kuzalisha megawati 600 kutoka kwenye makaa ya mawe yaliyopo Mchuchuma. Na tarehe 3 Aprili 2008 Shirika la NDC liliingia katika makubaliano na kampuni ya Pacific Corporation East Africa Ltd ili kuzalisha megawati 200 kutoka makaa ya mawe ya Ngaka. Mkataba mwingine uliingiwa tarehe 7 Februari 2013 kati ya Shirika la NDC, Shirika la Umeme (TANESCO) na Kampuni ya Power Pool East Africa LTD ili kuzalisha megawati 150 kutoka kwenye nguvu ya upepo.

Ilidhamiriwa kwamba kufikia mwaka 2017, miradi ya uzalishaji wa nguvu ya umeme Mchuchuma, ujenzi wa mtambo Ngaka, uzalishaji wa nguvu ya umeme kwa kutumia upepo Singida, ilitakiwa iwe imekamilika. Hata hivyo nilibaini kuwa malengo hayo hayakufanikiwa.

Taratibu zote za maandalizi zilikuwa zimekamilika kwa miradi ya Mchuchuma na Liganga, na walikubaliana kuwa manunuzi ya nguvu ya umeme kwa miradi hii yatafuata utaratibu wa Tengeneza Miliki na Endesha (Build Own and Operate arrangement). Ucheleweshwaji ulitokana na muda wa ziada uliohitajiwa na Kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources LTD kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa kifedha kwa ajili ya kuzungumza na TANESCO.

Katika kupitia mradi wa Ngaka, nilibaini kuwa mkataba ulikuwa umesainiwa na kampuni ya Sinohydro Corporation Limited ya China kwa ajili ya usimikaji wa mradi. Upembuzi yakinifu ulifanyika na Tancoal pamoja na Sinohydro, na mradi unasubiri makubaliano ya manunuzi ya nguvu za umeme kujadiliwa na TANESCO.

Kuhusu mradi wa upepo wa Singida, taratibu za maandalizi zote zilikuwa zimekamilika na Bodi ya Shirika la NDC lilikuwa limeshachagua mwekezaji kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Kulikuwa na ucheleweshwaji wa kutoa sera mpya ya Serikali kuhusu uzalishaji wa nguvu ya umeme.

Ucheleweshaji katika kutekeleza mradi unaweza kupelekea mradi kuchelewa kurudisha fedha, hatimaye kupunguza matarajio ya Serikali ya kupata fedha. Serikali inashauriwa kuharakisha utoaji wa sera ili Shirika la NDC liweze kuvutia wawekezaji.

5.5.3 Changamoto Katika Utekelezaji wa Mradi wa “Engaruka Basin Soda Ash”

Shirika la NDC lilianzisha mradi wa Soda Ash katika Bonde la Engaruka Wilayani Monduli mwaka 2010. Kutokana na ripoti ya upembuzi yakinifu ya Disemba 2010, Shirika lilibaini kuwa Bonde la Engaruka lina takribani mita za ujazo bilioni 4.68 za Soda Ash, likiwa na uwezo wa kujaa tena mita za ujazo milioni 1.875 kwa mwaka. Pia kutokana na tathmini ya kihaidrolojia (hydrological assessment) iliyofanywa na Shirika mwezi Februari 2016, ilibainika kuwa inahitajika takribani lita milioni 3.4 za maji kwa siku ili mradi huu ufanikiwe.

Mpaka kufikia muda huu, wawekezaji 15 walikuwa na nia ya kuwekeza katika mradi huu lakini hakuna hata mmoja kati yao ambaye alisaini mkataba na Shirika la NDC kwa sababu ya uhaba wa maji.

Shirika la NDC linashauriwa kuandaa mazingira yanayovutia wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa chanzo cha maji karibu na mradi na kuharakisha mchakato wa kuwaalika wawekezaji.

5.6 Mradi wa Viuadudu

5.6.1 Deni la Shilingi Milioni 320 Inalodaiwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa Ajili ya Lita 100,000

Wakati anatembelea Kampuni ya Tanzania Biotech Products Limited mnamo mwezi Juni 2017, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza kuwa lita 100,000 za viuadudu zilizotakiwa kusambazwa katika Halmashauri mbalimbali zisambazwe haraka iwezekanavyo. Rais aliagiza Wizara ya Fedha kulipa Shilingi bilioni 1.32 kwa ajili ya lengo hilo.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, Shilingi bilioni 1 tu ndizo zilikuwa zimeshalipwa na Wizara ya Fedha na Mipango licha ya kwamba lita 100,000 zilikuwa zime sambazwa kwenye Halmashauri. Kiasi cha Shilingi milioni 320 kilikuwa bado hakijalipwa mpaka kufikia muda wa ukaguzi.

Kiasi ambacho hakijalipwa na Wizara ya Fedha na Mipango kinaathiri utendaji wa kiwanda. Hii ni kwa sababu fedha nyingi zinakuwa mikononi mwa wadaiwa.

Wizara ya Fedha na Mipango inatakiwa ilipe deni lililobakia ili kukiwezesha kiwanda kujiendesha kwa sababu kiasi kikubwa cha fedha kiliwekezwa kwenye mradi huu.

5.6.2 Udhibiti Usiotosheleza Katika Usimamizi wa Taarifa za Wateja

Nilibaini mapungufu kadhaa kuhusiana na utunzaji wa taarifa za wateja (za mauzo) katika Halmashauri ya Korogwe mjini na Wilaya ya Korogwe kama ifuatavyo:

Wilaya ya Korogwe mjini ilipokea jumla ya lita 340 wakati wa awamu ya pili, na ilitakiwa kulipia kwa awamu ile. Halmashauri ya Korogwe mjini ililipa Shilingi milioni 1.95 kwa Kampuni ya Tanzania Biotech Products Ltd (TBPL) kupitia akaunti ya benki ya Azania tarehe 15 Septemba 2017. Uongozi wa Kampuni ya TBPL unalalamika kuwa haujapokea kiasi chochote kutoka kwenye Halmashauri ambayo ilipokea viuadudu kwenye awamu ya pili.

Hali hii inaleta shaka kuhusu taratibu zinazofuatwa kwenye usimamizi wa fedha taslimu kwa kuwa imebainika kuwa Shilingi bilioni 1 ambayo ililipwa na Wizara ya Fedha na Mipango ililipwa moja kwa moja kwa Shirika la NDC, badala ya Kampuni ya TBPL.

Pia, ilibainika kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ilitozwa lita 5,560 badala ya lita 2,400 ambazo zilikuwa zimewasilishwa, hali iliyopelekea Halmashauri kutozwa Shilingi milioni 73.39 badala ya Shilingi milioni 31.68.

Mapungufu yaliyobainika yanaweza kuathiri ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja, na hivyo kuathiri ufanisi. Hii ni kwa sababu fedha taslimu inakusanywa na Shirika la NDC pamoja na Kampuni ya TBPL. Pia, kukosekana kwa usimamizi mzuri wa taarifa za mauzo kunaweza kusababisha utata kwa wateja, kiasi cha kuweza kuwafanya wachukue maamuzi yasiyo sahihi kutokana na taarifa zisizo sahihi.

Kampuni ya TBPL inashauriwa kuongeza udhibiti kwenye usimamizi wa fedha taslimu na mchakato wa mauzo ili kuwa na taarifa sahihi za fedha taslimu, malipo na mauzo. Pia, panatakiwa pawe na maelewano kuhusu nani anatakiwa kukusanya na kupokea fedha taslimu kutoka kwa wateja ili kuepuka mikanganyiko isiyo ya lazima.

5.6.3 Mkataba na Wizara ya Afya na Ustawi ya Jamii Ambao Haujatekelezwa

Mnamo tarehe 11 Machi 2015, Shirika la Maendeleo la Taifa liliingia mkataba na iliyokuwa inajulikana kama Wizara ya Afya na Ustawi ya Jamii ili kuuza viudadu kufuatia uanzishwaji wa mtambo kwa ajili ya uzalishaji.

Nilibaini kuwa licha ya uwepo wa mkataba, hakuna manunuzi yaliyofanywa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwa kuangalia tarehe sahihi ya mkataba, manunuzi yalitakiwa kuwa katika bajeti ya Wizara ya mwaka

2015/16, 2016/17 na 2017/18 lakini kulikuwa hakuna bajeti hiyo. Matokeo yake, ghala la viuadudu lilijaa mpaka Rais John Pombe Magufuli alipoenda kutatua tatizo hili kwa kuelekeza Halmashauri zote kununua viuadudu.

Kwa Wizara kushindwa kutimiza mkataba, imesababisha Kampuni ya TBPL kushindwa kufikia malengo yake. Juhudi za Serikali za kutokomeza Malaria zinaweza zisizae matunda.

Wizara ya Afya inashauriwa kutekeleza makubaliano ya mkataba kwa kuchukua viwatilifu na kunyunyizia kwenye mazalia ya mbu ili kusaidia kufikia lengo la Serikali la Kutokomeza Malaria. Hatimaye Serikali itaokoa fedha nyingi ambazo zitatumika kununulia dawa za Malaria.

5.6.4 Dawa ya Viuadudu Iliyowasilishwa Lakini Haikutumika

Jumla ya lita 236,420 zilisambazwa kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara kati ya mwezi Agosti and Novemba 2017, ambapo Kila Halmashauri iligawiwa lita kadhaa za viuadudu. Kutokana na kuendelea kuwapa kwa ugonjwa wa Malaria na idadi ya vifo vinavyosababishwa na ugonjwa huo, ilitegemewa kuwa zoezi hili lingepewa uzito mkubwa sana.

Wakati wa ukaguzi mnamo mwezi Januari 2018 nilibaini kuwa Halmashauri zilikuwa bado hazijatumia kiasi cha viuadudu ambacho zilikuwa zimegawiwa. Nilitembelea sampuli ya Halmashauri 57 na kubaini kuwa lita 25,609 tu zilikuwa zimenyunyiziwa kwenye mazalia ya mbu kati ya lita 92,080 ambazo zilisambazwa, hii ni sawa na asilimia 28 ya viuadudu iliyosambazwa.

Ilibainika kuwa Halmashauri 19 kati ya 57 hazijanyunyizia lita 29,060 zenye thamani ya Shilingi milioni 383.59 zilizogawiwa kwao; dawa ya viuadudu ilikuwa inawekwa kwenye ghala bila ya kuwa na ishara yoyote kwamba inatumika. Orodha ya sampuli ya

Halmashauri na kiwango cha matumizi ya viudadu kati ya kile ilichopewa inaonekana kwenye *Kiambatisho Na. VII*.

Kushindwa kutumia dawa ya viudadu iliyosambazwa kunazuia juhudi za Serikali za kutokomeza Maleria katika nchi ya Tanzania. Matokeo yake, Serikali itatumia fedha nyingi kila mwaka katika kununua dawa badala ya kutumia dawa ya viudadu kutokomeza ugonjwa huu.

Ofisi ya Rais, Uongozi wa Mkoa na Serikali za Mitaa inashauriwa kuhakikisha kuwa juhudi za dhati zinafanyika ili kuzielekeza Halmashauri zote kutumia viudadu ili kufikia lengo la Kitaifa la kuwa na Taifa huru lisilo na ugonjwa wa Maleria.

5.6.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Kushindwa kukata Malipo ya Viudadu Wakati Wanapeleka Fedha Halmashauri ya Wilaya

Rais John Pombe Magufuli alipotembelea kiwanda aliagiza Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika kwa ajili ya dawa ya viudadu iliyosambazwa kwenye Halmashauri. Rais aliagiza ofisi hiyo kukata malipo ya dawa ya viudadu kabla ya kupeleka mgawo wa bajeti kwenye Halmashauri husika.

Jumla ya lita 136,420 zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.8 zilisambazwa kwenye Halmashauri mbalimbali kuanzia Agosti 2017 mpaka Novemba 2017, lakini hakuna malipo yaliyofanywa na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenda kwa Kampuni ya TBPL.

Kutokana na hali hiyo, kiwanda kinapata hali ngumu ya kifedha ambayo ilipelekea kusimamisha uzalishaji mwezi Disemba 2017. Hatimaye, uwekezaji unakuwa hauna mantiki licha ya kwamba Serikali imetumia fedha nyingi.

Ofisi ya Raisi-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inashauriwa kuhakikisha malipo yanafanyika kwa kukata fedha kutoka kwenye gawio la bajeti la Halmashauri. Pia, Ofisi inatakiwa kuhakikisha bajeti ya kutosha inagawiwa kwenye Halmashauri ili kuziwezesha kununua na kulipia dawa ya viuadudu.

5.6.6 Zoezi la Kunyunyizia Dawa Kutokuwa Endelevu

Kutokana na mapitio yaliyofanyika, matumizi ya viuadudu ni mchakato ambao ni endelevu ambao unatakiwa ufanyike kila baada ya muda fulani ili kuhakikisha maleria inatokomezwa kabisa.

Nikitoa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, hakuna Halmashauri hata moja ambayo imeendelea kununua viuadudu kutoka kwenye Kampuni ya Tanzania Biotech Products Ltd licha ya kuwapo kwa agizo kwamba zoezi hili liwe endelevu.

Hali hii inakwamisha juhudi ya kutokomezwa Maleria katika Taifa kwa sababu mazalia ya mbu yataendelea kuwapo kama zoezi la kunyunyizia dawa halitakuwa endelevu.

Serikali, kupitia Ofisi ya Raisi-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inatakiwa kusisitiza uhitaji wa Halmashauri zote kuendelea kununua na kunyunyizia dawa ya viuadudu katika mazalia yote ya mbu ili kuhakikisha mbu wanatokomezwa katika maeneo yote.

5.7 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

5.7.1 Kuhamisha Ubungo Complex kwenda Songas Bila ya Kukokotoa Thamani Yake

Katika kupitia ufanisi wa utendaji wa Shirika la Umeme, nilibaini kuwa eneo la Ubungo Complex lililhamishwa kwenda Songas mwaka 2004 wakati Kampuni ya Songas ilipoanza kufanya kazi zake Tanzania. Kutokana na mkataba wa kuhamisha, uhamisho huo ulihusisha haki ya umiliki wa ardhi na mali zisizohamishika, umiliki wa mali zinazohamishika (pamoja na vipuli na injini ya

kufua umeme[turbines]), tafiti (intellectual properties) na haki yeyote kutoka kwa Shirika la Umeme ambayo itaiwezesha Kampuni ya Songas kumiliki, kufanya kazi na kudumisha Ubungo Complex.

TANESCO ilipewa hisa 10,000 katika mtaji wa Songas; pia kampuni ya Songas ilichukua madeni ya TANESCO ambayo yalitumika kununulia injini nne za maji zilizopo eneo la Complex. Kutokana na mkataba wa usimamizi kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Biashara ya Ulaya, mchango wa mtaji wa Shirika la Umeme na Shirika la Maendeleo la Mafuta Tanzania (TPDC) katika Kampuni ya Songas ni Euro milioni 5, ambapo Shirika la Maendeleo la Mafuta lilikuwa na hisa 20,000. Hii inafanya mchango wa TANESCO katika hisa za Songas kuwa na thamani ya Euro milioni 1.67.

Hata hivyo, kulikuwa hakuna ushahidi unaonesha kuwa eneo la Complex na mali zake ambazo zilihamishwa kwenda kampuni ya Songas zilikokotolewa thamani yake kabla ya kuhamishwa. Pia, hakuna kipengele katika makubaliano ya kuhamisha na mkataba wa mkopo kinachoonesha kiasi cha mkopo uliochukuliwa na Songas ambao uliotumika kununua injini za kufua umeme.

Kuna uwezekano kuwa TANESCO halikupata thamani ya fedha kwa mali zilizohamishiwa Songas, kiasi kwamba, thamani ya hisa lilizopewa TANESCO zinaweza kuwa za chini kuliko thamani halisi ya mali hizo.

Ninalishauri TANESCO kutathmini tena na kupitia mkataba wa kuhamisha mali uliosainiwa kuangalia kama mali zilizohamishwa zinaendana na thamani ya hisa Shirika lilizopewa na kampuni ya Songas.

5.7.2 Kiasi Kikubwa cha fedha Kutolewa na Serikali Katika Mradi wa Songas

Mkataba wa usimamizi wa fedha ambao ulisainiwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benki ya Biashara ya Ulaya na Kampuni ya Songas unaonesha kuwa jumla ya gharama ya mradi wa Songas ilikuwa ni Euro milioni 392 (sawa na Dola za Kimarekani milioni 346 kwa wakati ule). Hata hivyo, nilibaini kuwa Serikali ilifanya uwekezaji mkubwa katika mradi bila kuuthaminisha.

Kutokana na mkataba wa usimamizi wa fedha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitakiwa kukopa Euro milioni 235.1 na kuwekeza katika mradi, pia kutoa Euro milioni 0.6 kutoka kwenye vyanzo vyake. Zaidi ya hapo, Serikali ilichukua mkopo wa Euro milioni 50 ili kuikopesha Kampuni ya Songas. Jumla ya uwekezaji uliofanywa na Serikali kwenye mradi ni Euro milioni 285.7 ambao ni sawa na asilimia 73 ya gharama yote ya mradi.

Hakuna sehemu yoyote kwenye mkataba ambayo inaonesha umiliki wa Serikali kwenye mradi licha ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali.

Ninaishauri Serikali kupitia upya mpangilio wa mtaji wa mradi na kutathmini kama mkataba ulifanyika kwa kuangalia usawa wa pande zote mbili.

5.7.3 Usimamizi Usiotosheleza wa Mkataba wa Mkopo kwa ajili ya Uzalishaji wa Nguvu za Umeme

- i) Nilibaini kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilidhamini mkopo kwa Kampuni ya Maendeleo ya Usimamizi wa Fedha (Tanzania Finance Development Limited) kwa ajili ya kuchukua hisa katika kampuni ya Songas. Nilishindwa kujua uhusiano uliopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Maendeleo ya

Usimamizi wa Fedha, usajili na umiliki ambao uliishawishi Serikali kutoa dhamana hiyo.

- ii) Nilibaini kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilidhamini mkopo wa Euro milioni 50 kutoka Benki ya Biashara ya Ulaya ambao Serikali uliipa Songas kama mkopo. Makubaliano ya mkopo yalikuwa ni Serikali kukopa fedha ambayo ilikopwa kutoka Benki ya Biashara ya Ulaya na kuipa Kampuni ya Songas, na Serikali italipa deni hilo; na wakati huo, ikidai mkopo huo kutoka Kampuni ya Songas. Serikali italipwa na Kampuni ya Songas kwa Shilingi za Kitanzania na itailipa Benki ya Biashara ya Ulaya kwa Euro. Haijulikani kama kampuni ya Songas italipa deni lake, na kama Serikali haitaingia hasara kwa sababu ya tofauti ya sarafu wakati wa kulipa.
- iii) Pia, [kampuni ya Songas ilichukua deni la Shirika la Umeme linalohusiana na injini 4 za kufua umeme ambazo zilinunuliwa na Shirika la Umeme na kusimikwa eneo la Ubungo Complex. Ulipaji wa deni lililochukuliwa haueleweki sababu Serikali ina wajibu wa kulipa deni hilo licha ya kwamba limechukuliwa na Kampuni ya Songas. Zaidi ya hapo, kifungu cha 12 na 13 cha mikopo ya Serikali, dhamana na Sheria ya ruzuku ya mwaka 1974 kama ilivyorekebisha mwaka 2003 inahitaji Serikali kudhamini Mashirika ya Umma tu na sio kampuni binafsi.

Kutokana na maelezo hayo ya juu, sijaweza kutathmini mambo ambayo yameathiri au yataathiri hali ya kifedha ya Serikali kutokana na deni hili.

Ninaishauri Serikali kuchukua hatua madhubuti kuchunguza mahusiano kati ya kampuni mbili na kufahamu mambo ya kisheria, malipo, faida zilizopo kwenye kila mkataba na hatari kwa nchi sababu ya madeni haya.

5.7.4 Utegemezi Mkubwa kwa Wazalishaji wa Umeme Binafsi na Kukosekana kwa Mpango wa Kuzihifadhi Mali Zilizokwisha Muda

Katika kupitia mpango wa mitambo wa Shirika la Umeme, ilionyesha kuwa jumla ya megawati 9,707 zinatarijiwa kuzalishwa na kuunganishwa na gridi ya Taifa kuanzia mwaka 2016/2017 mpaka 2040. Kati ya megawati hizo, megawati 3,924 zinatarijiwa kutokea kwenye Wazalishaji wa Umeme Binafsi (Independent Power Producers). Pia, mitambo 14 ya uzalishaji wa umeme yenye megawati 1332 inatarajiwa kuzimishwa wakati huo huo. Jumla ya gharama za Dola za Kimarekani bilioni 49.40 zinatarijiwa kutumika ili kusimika mtambo mpya wa kuzalisha umeme, ambapo dola za kimarekani bilioni 14.82 zinatarijiwa kutolewa na Shirika la Umeme kutoka vyanzo vyake na dola za kimarekani bilioni 34.58 zitatoka kwenye mikopo.

Nilibaini kuwa kutakuwa na utegemezi mkubwa kwa wazalishaji wa umeme binafsi na mikopo katika kuzalisha nguvu ya umeme, kitendo ambacho kitaendelea kudhoofisha uwezo wa kifedha wa Shirika la Umeme kwa sababu ya kuongezeka kwa gharama katika mfumo wa gharama za nishati. Pia nilibaini kukosekana kwa mpango wa kuhifadhi mitambo baada ya muda wake kuisha mnamo mwaka 2040.

Serikali inashauriwa kupitia tena na kubadilisha mpango wa mitambo wa Shirika la Umeme, pia kupunguza utegemezi kwa wazalishaji wa Umeme binafsi na mikopo.

5.8 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

5.8.1 Kutofanya kazi kwa Baadhi Vituo vya Mafuta na Kuisha kwa Mikataba baina ya TPDC na Watoa Huduma ya Mafuta

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) linamiliki vituo sita vya mafuta katika maeneo ya Segera, Tarime, Makuyuni, Singida, Geita na Musoma kama sehemu ya uwekezaji.

Ukaguzi wa ufanisi wa vituo vya mafuta umebainisha kuwa vituo vya Segera, Tarime na Makuyuni vinatumika na vilikodishwa kwa watoa huduma binafsi. Hata hivyo, mikataba ya makubaliano ya ukodishaji iliisha tangu Desemba 2014. Huku vituo vitatu vya Geita, Musoma na Singida vilibainika kuwa havitumiki tena.

Ziara yangu katika vituo vya mafuta vilivyoko Tarime, Musoma na Geita ilibaini kuwa kuna gereji zinaendeshwa ndani ya vituo hivyo bila idhini ya TPDC, huku kituo cha Singida kikiwa na kituo cha kuosha magari. Nikiwa Makuyuni nilishuhudia kituo cha mafuta kikiwa na mashine za kuuzia mafuta zilizochakaa sana huku mpangaji wa kituo cha Segera alifunga mashine zake binafsi za kuuzia mafuta.

Ukosefu wa makubaliano ya ukodishaji unaweza kusababisha upotevu wa mapato na kuzua migogoro isiyo ya lazima huku TPDC ikiwa na uwezekano mkubwa wa kupata hasara.

TPDC inashauriwa kuingia katika makubaliano mapya ya ukodishaji na wapangaji wake, kurekebisha majengo yaliyo chakaa, na kupangisha majengo yasiyotumika kwa sasa ili kunufaika kiuchumi kama ilivyokusudiwa.

5.9 Mfuko wa Self (SELF Microfinance)

5.9.1 Mikopo isiyouzika katika Soko

Mfuko wa Self unatoa mikopo ya aina 5 iitwayo Anza, Flex , Line of credit, Kilimo na Incubator. Ukaguzi wangu umebaini kuwa tangu kuanzishwa kwa Self mwaka 2000, mikopo hii haijawahi kubadilika, hivyo kupelekea kati ya mikopo yote, mikopo 3 haikuwahi kuuzwa sokoni, nayo ni Flex, Line of Credit, na Incubator. Zaidi ya hayo, uchambuzi wa mikopo kipindi cha mwaka 2017 uligundua kuwa mkopo wa ANZA ndio unaoongoza kwa Shilingi bilioni 12.23 ikiwa ni asilimia 94, wakati mkopo wa kilimo ukifuatia kwa Shilingi milioni 780 ikiwa ni asilimia 6.

Hii inamaanisha kwamba, kwa miaka yote 17 Self imekuwa ikiuza mikopo 3 isiyohitajika sokoni bila kuhakiki wala kuchunguza mikopo inayohitajika sokoni; hivyo, kutokufikia malengo yaliyopangwa. Menejimenti imeniambia kwamba, kwa sasa, wameandaa mpango mpya wa kuingiza mikopo sokoni japokuwa itachelewa kwa sababu ya ukosefu wa Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya kuidhinisha.

Ninaushauri mfuko wa Self kutathmini hali ya soko juu ya mikopo kwa kulinganisha mahitaji ya wateja.

5.9.2 Kudorora kwa Mwenendo wa Biashara kuu (core business)

Mfuko wa Self una mamlaka ya kuboresha upatikanaji wa fedha kwa jumuiya zisizojiweza (underserved) za vijijini na mijini. Lengo kuu likiwa ni kufikia malengo kupitia uuzaji wa jumla wa mikopo na kukuza uwezo wa Taasisi za kati za kifedha kama vile SACCOS na Taasisi ndogo za fedha.

Ukaguzi wa Mali (assets) katika kipindi cha mwaka 2017 uligundua kuwa, kati ya jumla ya Shilingi bilioni 59.89 zilizowekwa kwa faida, Shilingi bilioni 11.34 ikiwa ni asilimia 19 zilielekezwa kuhudumia biashara kuu ya Mfuko ambayo ni utoaji wa mikopo; na kiasi kilichobaki cha Shilingi bilioni 48.56, ikiwa ni asilimia 81, kilielekezwa katika uwekezaji wa dhamana ambayo siyo biashara kuu ya Mfuko.

Mapitio mengine yalibainisha kuwa, asilimia 77 ya jumla ya mapato ya Shilingi bilioni 5.73 yalitokana na uwekezaji wa dhamana (non core business), wakati mikopo ya biashara (biashara kuu) ilipata Shilingi bilioni 1.75 ikiwa ni asilimia 23.

Zaidi ya hayo, Uchunguzi wangu wa mishahara ya wafanyakazi kila mwaka umebainisha kuwa jumla ya Shilingi bilioni 2.98 zimetumika kama gharama za mishahara ikiwa ni zaidi ya asilimia 18 ya mapato yanayotokana na biashara kuu (riba ya mikopo na Mapato mengine) ya Shilingi bilioni 1.75. Nilitambua kuwa

upungufu huo umefunikwa na mapato kutoka kwa uwekezaji wa dhamana.

Kuhusu suala hili, Nina wasiwasi na ufanisi wa Mfuko katika biashara yake kuu na uwezekano wa kutokufikia malengo yake ya kimbakati katika kuimarisha ufikiaji na utoaji wa huduma za kifedha kwa jamii zisizojiweza.

Mfuko unapaswa kufuatilia ufumbuzi wa kina na mbinu sahihi za usimamizi wa biashara kwa kuchambua kwa makini michakato yake ya biashara ili kufikia matokeo chanya katika shughuli zake za kila siku; na kuongeza utendaji katika biashara kuu badala ya kutegemea katika uwekezaji wa dhamana ambayo siyo biashara kuu ya mfuko katika uzalishaji wa kipato. Pia, Mfuko unatakiwa kuweka jitihada zaidi katika maendeleo ya biashara ili kuhakikisha Mfuko unafika maeneo mengi, unajulikana na unaongeza bidhaa mbalimbali ili kuvutia wateja kwenye soko.

5.9.3 Kutokufikiwa kwa baadhi ya maeneo na Mfuko wa Self

Shughuli za Mfuko zimeenea mikoa yote ya Tanzania kama ilivyokuwa katika makubaliano kati ya Benki ya Afrika na Serikali mwaka 2009. Ili kuhakikisha Self inafika nchi nzima ilizindua uendeshaji wa vituo vinne ambavyo ni Mbeya kwa mikoa ya kusini, Mwanza kwa Kanda ya Ziwa, Arusha kwa mikoa ya Kaskazini na Dar es Salaam kwa mikoa ya Mashariki. Kila mkoa una wafanyakazi watatu, akikumuishwa na dereva isipokuwa kwa mkoa wa Dar es salaam, ambao watatoa huduma kwa mikoa sio chini ya sita.

Hata hivyo, nilibaini kuwa SELF haijawahi kufikia mikoa ifuatayo: Singida, Tabora, Rukwa, Katavi, Kigoma, Mara, Mtwara, Lindi, Simiyu, Unguja na Pemba. Hii ilitokana na maeneo haya kuwa na changamoto mbalimbali kama vile: shughuli chache za kichumi, usimamizi duni, kiwango cha juu cha kutokujua maswala ya kifedha (financial illiteracy), miundombinu duni na teknolojia ya chini.

Ni mtazamo wangu kuwa vituo vimebeba mikoa mingi ikilinganishwa na rasilimali watu. Wafanyakazi watatu katika kila kituo kufanya kazi katika mikoa isiyopungua sita hawatoshelezi. Hivyo, naushauri mfuko kufanya jitihada ya kujenga uwezo wa kufika maeneo haya ambayo hadi sasa yanahudumiwa na Mfuko.

5.10 Shirika la Posta Tanzania

5.10.1 Utekelezaji hafifu wa Mpango Mkakati wa Shirika la Posta

Ukaguzi wa Mpango Mkakati wa Shirika la Posta wa mwaka 2014-2018 na utekelezaji wake ulibainisha kuwa malengo yaliyojumuishwa katika mpango wa mwaka ni kuongezeka kwa ukuaji wa biashara na faida, kuhamasisha rasilimali za fedha na uwekezaji, na kuanzishwa kwa kampuni tanzu. Malipo hayo yote hayakutekelezwa licha ya mipango kuingizwa kwenye mwaka wa fedha.

Pia, nilibaini kuwa Shirika la Posta lina biashara nyingi, na bidhaa zake za kifedha zimesambaa haraka ikilinganisha na rasilimali zake (rasilimali za kifedha na rasilimali watu) katika utekelezaji wake. Shirika limepanga utekelezaji wa kampuni tanzu nne nazo ni Posta Logistic, Posta Giro Financial Services, Posta Freight Forwarding na Posta Digital.

Pia, nilibaini ukosefu wa uhodari, vifaa vya ufundi na mikakati ya utekelezaji wa malengo. Niligundua pia kuwa mfumo wa Shirika na mpango wa huduma haukusaidia kuimarisha mpango mkakati. Kutokana na dosari hizo zilizobainika, Shirika limeendelea kutengeneza hasara ya Shilingi milioni 3.490 kwa mwaka 2015/2016 na Shilingi milioni 540 kwa mwaka 2014/2015. Pia Shirika liliendelea kuingia gharama kwenye biashara zisizofanya vizuri na zisizokuwa na thamani.

Hivyo, nalishauri Shirika:

- a. Kupitia upya mwenendo wa Biashara na bidhaa nyingine kwa kuzingatia zile zenye umuhimu na uwezo mkubwa wa kuleta matokeo chanya.
- b. Kupitia upya gharama zote kwa malengo ya kupunguza gharama za uendeshaji wa Shirika ili kutengeneza faida.
- c. Kuunganisha muundo wa Shirika na Mpango Mkakati, kupata idhini ya mpango wa huduma iliyopendekezwa kutoka kwa Serikali kwa ajili yautekelezaji wake; na
- d. Kuchukua hatua muhimu ili kuongeza uwezo na ujuzi kwa wafanyakazi, na kupata mifumo mipya na vifaa vya kutekeleza mkakati.

5.11 Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA)

5.11.1 Kutokuwapo na Ufuatiliaji na Tathmini bora kwenye vyuo vya VETA

Nilibaini kuwa, ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za mafunzo hufanyika ili kutambua kama taasisi za VETA zinaendeshwa kwa ubora na kwa kufuata na kuzingatia viwango vya mafunzo ya ufundi, kuwapo kwa miundombinu ya kutosha, vifaa sahihi, vitabu na walimu wenye ujuzi wa kutosha.

Mapitio ya mchakato wa Ufuatiliaji na tathmini wa taasisi za VETA, yalibaini yafuatayo:

- i. Katika Kituo cha mafunzo ya ufundi (RVTSC) cha mkoa wa Dodoma , niliba kuwa uwiano wa mwalimu na wanafunzi ni wa juu kuliko kawaida, Mwalimu mmoja hufundisha wanafunzi 113, badala ya uwiano unaokubalika wa mwalimu mmoja wanafunzi kati ya 16-20.
- ii. Vituo vyote vya kanda ya Magharibi havikuwasilisha taarifa zao za fedha za mwaka 2016/2017; na Kituo 1 tu kati ya 11 ambavyo vina usajili wa awali ndicho kilikaguliwa na timu ya uhakiki ubora.

iii. Tangu mwaka 2012, vituo 89 vya Mafunzo ya Ufundi kanda ya Ziwa vimekuwa chini ya usajili wa awali, ambapo ndani ya mwaka mmoja baaada ya usajili huo, vilitakiwa kuomba kibali, cha usajili wa kudumu. Vituo 25 kati yao viliomba kibali cha kuidhinishwa kupata usajiri wa kudumu kwa zaidi ya miaka miwili sasa (15 kati yao vimewasilisha ripoti za utendaji wao lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa). Vituo 8 tu (9%) kati ya vituo 89 vyenye usajili wa awali ndivyo vimekaguliwa ili viweze kupatiwa usajili wa kudumu.

Ukosefu wa mfumo bora wa ufuatiliaji na tathmini unaweza kuathiri ubora wa elimu ya ufundi inayotolewa na taasisi za VETA.

Ninashauri VETA kuhakikisha kwamba taasisi za VETA zinasimamiwa vizuri na kutathminiwa ili elimu inayotolewa kwa jamii kuwa bora.

5.11.2 Changamoto za kusimamia mradi jumuishi wa mafunzo ya kiufundi wa madini

VETA, Barick Gold Afrika, Anglo Ashanti Gold na Chama cha Madini na Nguvu Tanzania (TCME) walianzisha mafunzo ya kiufundi ya madini ili kukuza ujuzi kwa sekta ya madini na kushughulikia migogoro ya kijamii kwenye maeneo ya madini. Kulingana na Randama ya Makubaliano iliyosainiwa mnamo 2/1/2009, mafunzo hayo yangefanyika kwa muda usiozidi miaka 4. Nilibaini mapungufu yafuatayo katika mradi:

- i. Mradi ulianza kabla ya kusainiwa kwa randama ya makubaliano. Meneja wa Mradi wa kwanza alianza kazi mwezi Januari 2008 wakati makubaliano yalisainiwa mnamo 2/12/2009.
- ii. Aya 8.0 (a) ya Randama ya Makubaliano inahitaji meneja wa mradi kuwa Moshi kusimamia mradi na shughuli zake za kila siku. Ilibainika kuwa tangu Oktoba 2017 Meneja alihamishiwa

Ofisi za TCME Dar es Salaam; kwa zaidi ya miezi 6 kituo cha mradi hakina meneja.

- iii. Aya 8 (b) ya Randama ya Makubaliano inaitaji kuundwa kwa Baraza la Uendeshaji (RMC) ambalo ni ngazi ya juu ya maamuzi ya mradi, lakini Baraza hilo bado halijaundwa. Hii pia ni kinyume na Aya na 8 (b) ya randama ya makubaliano ambayo inalitaka Baraza kukutana mara mbili kwa mwaka kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba huo.

Ninashauri VETA kupitia Moshi RVTSC kuanzisha mkakati ambao utaimarisha uendeleu wa mradi huo.

SURA YA SITA

UKAGUZI MAALUM

6.0 Utangulizi

Sura hii inaangalia mambo muhimu zaidi yaliyojitokeza katika kaguzi maalum na kaguzi za uchunguzi wa kisayansi (wakiforensiki) katika Mashirika ya Umma. Kaguzi hizi maalum zimefanyika kwa mujibu wa Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na Kanuni ndogo Na. 1 ya Kanuni ya 79 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, zilifanyika kaguzi maalum zifuatazo;

- (i) Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)
- (ii) Mfuko wa Hisani wa Kuendeleza zao la Korosho (CIDTF)
- (iii) Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)
- (iv) Uendeshaji wa Ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Kampuni ya Intra Energy Tanzania Limited (IETL)
- (v) Mfuko wa Pesheni wa NSSF

6.1 Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)

6.1.1 Kutokuwapo kwa Mali zilizopatiwa Msamaha wa Kodi Shilingi 34.4 Billioni

Sehemu ya nne ya mkataba wa kazi kati ya Kituo Cha Uwekezaji (TIC) na Star Media (T) Ltd inataka vifaa vyote vilivyoombewa msamaha wa kodi vitumike kulingana na mradi husika.

Marejeo ya rejista ya mali ya mwaka 2014 kwa vifaa vya mawasiliano na mtandao vilivyoainishwa vilivyoagizwa vimefika na kufungwa kwa matumizi.

Hata hivyo, ukaguzi wetu umeshindwa kuthibitisha kuwepo kwa vifaa hivyo ingawa vimeorodheshwa kwenye rejista ya mali pia, vifaa hivyo havijawekwa alama maalum za utambuzi; hivyo, kuweka ugumu kwenye upatikanaji wake.

Nimeshindwa kujua kama vifaa vilivyoagizwa vimetumika kwa kazi iliyokusudiwa, hivyo inaweza kupelekea msamaha wa kodi kutotumika ilivyokusudiwa.

Shirika la Utangazaji la Taifa linapaswa kufuatilia mali zote zilizopata msamaha wa kodi; vinginevyo, Star Times wanahitajika kulipia gharama za vifaa na kodi stahili iliyopaswa kulipwa.

6.1.2 Kuzuiwa kuperuzi kwenye Mfumo wa Usaidizi wa Biashara (STARiBOSS)

Wakati wa ukaguzi, niligundua kuwa makusanyo ya kila siku katika mfumo wa STARiBOSS hurekodiwa katika mfumo wa kihasibu uitwao ERP. ERP ni mfumo ambao haupo kwenye majengo ya Star Media Tanzania na badala yake mfumo wa kielektroniki unaotumia mtandao ambapo seva yake ipo nchini China.

Mnamo tarehe 16 mwezi wa pili na tarehe 19 mwezi wa sita 2017, niliomba kuperuzi kwenye mfumo kwa lengo la kufanya marejeo na kuhakiki uhalali na usahihi wa mfumo ambao unatumika kukusanya taarifa za kihasibu. Tarehe 23 mwezi wa sita 2017 nilinyimwa uhalali wa kuperuzi taarifa hizo kwa madai kuwa ni za siri.

Kunyimwa kuperuzi na kuhakiki taarifa zilizopo kwenye mfumo kulinfanya kushindwa kupata uhalali na usahihi juu ya taarifa zinazoenda kurekodiwa kwenye mfumo wa kihasibu (ERP).

Kampuni ya Star Media inatakiwa itoe nafasi kwa ajili ya marejeo na kuperuzi wa mfumo, vinginevyo hilo ni moja ya jambo linalopelekea uvunjifu wa mkataba.

6.1.3 Kushindwa kwa Star Media kulipa Madeni yake hata ya Muda Mfupi

Wakati wa ukaguzi wangu kuhusiana na uwezo wa Kampuni kulipa madeni madogo madogo na majukumu mengineyo

ilibainika kuwa, kwa kipindi cha miaka minne mfululizo Kampuni imeshindwa kulipia baadhi ya majukumu yake kama inavyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali 4: Ukokotozi wa uwiano wa ukwasi

Mwaka wa Fedha unaoishia 31/12	2014 Kiasi kwa dola	2013 Kiasi kwa dola	2012 Kiasi kwa dola	2011 Kiasi kwa dola
Mali za muda mfupi	18,790,734	22,551,835	9,704,037	8,755,818
Madeni ya muda mfupi	73,671,668	62,761,231	35,328,057	13,998,107
Uwiano wa ukwasi	0.26:1	0.36: 1	0.27: 1	0.63: 1

Chanzo: Taarifa za Fedha kwa kipindi kinachoishia 2011, 2012, 2013 and 2014

Uwiano wa ukwasi wa Kampuni ni chini ya kiwango cha uwiano kinachohitajika ambayo ni 2:1, hivyo kuashiria kuwa Kampuni haiwezi kulipia madeni ya muda mfupi pindi tu inapohitajika kufanya hivyo.

Star Media wanahitajika kuweka uwekezaji, hususani rasilimali fedha ya kutosha, ili kuwezesha kuendesha shughuli zake za kila siku.

6.1.4 Udanganyifu wa Taarifa za Fedha katika Ukokotoaji wa Uchakavu kwenye Ving'amuzi

Kifungu namba 7.3.2 cha mkataba wa makubaliano ya uendeshaji wa pamoja kinalitaka Star Media kugawa faida baada ya kukokotoa mapato na matumizi ya shughuli zake kwa mwaka.

Imegundulika kuwa kwa kipindi cha miaka saba mfululizo Star Media limekuwa likiripoti hasara kwenye hesabu zao; hili ni moja ya mambo yanayochangia ni kuingiza gharama za uchakavu kwenye ving'amuzi kinyume kabisa na sera hata za makampuni mengine yaliyo katika mfumo mmoja wa kibiashara kama vile Azam Media na DSTV, ambapo, pindi kifaa kinapouzwa hakuna gharama yoyote ambayo Kampuni inaingia.

Jumla ya Dola za Kimarekani 30,108,004 ziliingizwa kama gharama za uchakavu kwa kipindi cha miaka sita kutoka 2010 mpaka 2015. Hii ilipelekea kuripoti taarifa zisizo sahihi na za udanganyifu kwenye taarifa za fedha ili kuweza kupunguza mapato, na hivyo, kulidanganya TBC ambalo ni mdau wenza. Kukokotoa uchakavu kwa ving'amuzi ni namna moja ya kuhamisha faida.

Star Times linapaswa kurudisha kiasi cha fedha kilichofichwa kwenye ukokotoaji; na Star Media linapaswa kurekebisha hesabu katika vitalu vyake.

6.1.5 Mkopo uliochukuliwa bila kuitaarifu TBC Dola za Kimarekani 10.5 Millions

Katika ukaguzi wangu nimegundua kuwa Star Media walijipatia mikopo miwili yenye jumla ya Dola za Kimarekani 10.5 milioni bila kuitaarifu TBC ambaye ni mbia wakibiashara, na kiasi hicho cha fedha kutoonyeshwa kwenye taarifa za fedha kwa mwaka 2014.

Wakati wa mahojiano, Mkuu wa Idara ya Fedha wa kampuni ya Star Media alitanabaisha kuwa huo haukuwa mkopo ila ni msaada wa kifedha kutoka kutoka Star Group, na hivyo, imeripotiwa kama wadai.

Hata hivyo, marejeo ya makubaliano ya mikataba ya mikopo yaligundua kuwa ni mkopo wa riba ya asilimia 8.5 uliotoka Star Times International Holding of China ambayo ni kampuni dada ya Star Times na mali za Star Media ndizo zilizotumika kama dhamana ya mkopo huo.

Imeshindwa kuthibitika kama riba iliyotozwa kwenye mkopo huo ni ile inayoendana na hali ya soko, hivyo inapelekea kuficha faida na makampuni yenye mahusiano na Star Times.

Star Times wanatakiwa kurudisha kiasi chote cha riba kilichochajiwa kwenye, mkopo kwani imethibitika kuwa mkopo umetokana na kampuni dada.

6.1.6 Star Times Kutochangia Mtaji kwenye Kampuni ya pamoja

Kifungu namba 1.4 na 1.5 cha Randama ya Makubaliano kati ya TBC na Star Times kinaeleza kuwa, mtaji utakuwa jumla ya Dola za Kimarekani 1,000,000; ambapo jumla ya hisa 10,000 ziligawiwa kwa bei ya Dola za Kimarekani 100 kwa kila hisa. Mgawanyo wa hisa kwa uwiano ni asilimia 35 kwa TBC na 65 kwa Star Times; ambapo, TBC itachangia Dola za Kimarekani 350,000 na Star Media itachangia Dola za Kimarekani 650,000.

Wakati wa ukaguzi, iligundulika kuwa Star Times hawakuchangia kwenye mtaji kama inavyohitajika kwenye makubaliano, kwani hakukuwa na uthibitisho wa mapokezi ya kiasi chochote cha fedha hata kwenye taarifa za fedha za Star Media.

Star Times wanatakiwa wachangie mtaji kwa kiasi walichokubaliana, vinginevyo, mkataba wa ushirika urekebishwe ili kuweka kiwango sahihi cha hisa kilichochangiwa na Star Times.

6.1.7 Uhamishaji wa Hisa 300 kwenda kwa Kampuni Tanzu iliyopo Mauritius

Imethibitika kuwa Star Times iliamisha hisa 300 za Star media kwenda kampuni tanzu ya SDTV iliyopo Mauritius.

Wakati wa ukaguzi na kupitia ripoti za uthibitisho wa kampuni, ilithibitika kuwa kampuni ya SDTV ni kampuni iliyosajiriwa nje ya nchi ambayo hairuhusiwa kufanya uwekezaji Mauritius wala Dubai.

Hisa zilizohamishwa ziliuzwa kwa jumla ya Dola za Kimarekani 300; hii inamaanisha kuwa kila hisa moja iliuzwa kwa dola moja. Kifungu namba 1.4 cha randama ya makubaliano kati ya TBC na Star Times kinaeleza kuwa hisa moja itauzwa kwa thamani halisi

ya Dola za Kimarekani 100. Kutokana na hisa kuuzwa kwa hasara, Serikali imeshindwa kukusanya kodi ya ongezeko la mtaji. Ni kiasi cha shilingi 5000 tu kilichopatikana kama gharama za stempu ambacho kililipwa mnamo tarehe 21 Septemba 2011.

Kufungua kampuni iliyo nje ya mipaka na kupunguza thamani na bei ya hisa kunamaanisha kuwa kuna udanganyifu wa kumbukumbu ili kurahisisha na kufanikisha udanganyifu.

TBC wanapaswa kufanya uchunguzi juu ya kampuni iliyoanzishwa nje ya mipaka ambayo ina uhusiano wa moja kwa moja na Star Media ili miamala na bei ya hisa ifahamike na ikubaliwe na pande zote.

6.1.8 Star Times Kutoza Riba kwa kiasi Ambacho Hakijalipwa kutokana na Kuuziwa bidhaa na Huduma kutoka kwenye Kampuni Tanzu ya SDTV inayoimiliki kwa asilimia 100

Kupitia marejeo ya taarifa za fedha, iligundulika kuwa Kampuni ya Star Media inachajiwa riba ya asilimia 8.5 kwa mwaka kutoka kwa kiasi ambacho hakijalipwa kutokana na kuuziwa bidhaa na Huduma kutoka kwenye Kampuni Tanzu ya SDTV ambayo inamilikiwa na Star Times kwa asilimia mia moja.

Yumkini hali hii huweza kusababisha udanganyifu, kwani hakuna mdai ambaye anatoza riba kwa madai ya Star Media isipokuwa SDTV ambayo ni kampuni mama ya Star Times.

Kutokana pia na ukaguzi wa nyaraka mbalimbali za uagizaji bidhaa kwa mwaka 2013 na 2014 ilibainika kuwa hakuna bidhaa wala huduma yoyote iliyotolewa na SDTV Holding Co. Ltd kwa Star Media. Mnamo tarehe 13 mwezi Disemba mwaka 2016, kupitia barua pepe, niliomba kupitia rejesta ya wadaiwa na wadai ambao wana mahusiano ya moja kwa moja lakini nilishindwa kupata ufafanuzi wala kutofautisha kiwango cha riba kilicholipwa kutoka Star Media kwenda SDTV Holding Co.Ltd

kutokana na kutokuwepo kwa vielelezo ambatishi vinavyohusiana na gharama.

Kutoza riba kwa madai hewa ya bidhaa na huduma ni kufanya udanganyifu wa kupunguza mapato na kutorosha faida kupitia miamala kwa makampuni yanayohusiana.

TBC wanapaswa kufanya uchunguzi wa kina kwa miamala yote iliyofanyika na Star Media kupitia makampuni mwenza yaliyo nje ya mipaka ili kujiridhisha kama miamala yote ilifanyika kukiwa na uelewa wa pande zote mbili, pia hakukuwa na uhamshaji wa faida kupitia makampuni hayo.

6.1.9 Kutoza zaidi Gharama za Uchakavu kwa Vifaa vya Kituo inayofikia Dola za Kimarekani 1.01 Milioni

Nilifanya mapitio ya rejista kwa mwaka 2014 na nikagundua kuwa mali zisizohamishika ambazo, kulingana na sera ya uchakavu ya kampuni, muda wake wa miaka mitatu ulikuwa umekwisha lakini bado gharama za uchakavu zilikuwa zinatozwa. Niligundua kuwa vifaa vya kuungia vilinunuliwa mwaka 2011, na mpaka mwaka 2014 tayari ilishapita miaka minne, ila ilibainika kuwa vifaa hivyo bado vinaendelea kutozwa gharama za uchakavu, ambapo kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 1.01 kilitozwa dhidi ya faida; hivyo kupelekea kupunguza faida ya mwaka.

Hili lilipelekea kutotoa taarifa sahihi ya fedha na ililenga kufanya udanganyifu kwa mbia mwenza ambaye ni TBC; hivyo, kufanikisha uhamishaji wa faida kupitia makampuni yenye mahusiano yaliyopo nje ya mipaka.

6.2 Mfuko wa Hisani wa Kuendeleza Zao la Korosho

6.2.1 Udhaifu Katika Ukusanyaji wa Michango Kutoka kwa Wakulima na Wabanguaji ajili ya Mfuko wa Uendelezaji zao la Korosho Shilingi 4.85 Bilioni

Vipengele vya 4(a)(i) na (ii) vya Randama ya Maelewano baina ya wawakilishi wa wakulima wa Korosho, Wabanguaji wa Korosho, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazolima Korosho na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwezi Machi 2010, vinaainisha kuwa kiasi cha Shilingi kumi kwa kilo ya korosho ghafi kitatozwa kwa wakulima na wabanguaji.

Ukaguzi maalum ulibaini jumla ya kiasi cha shilingi 4.85 bilioni hakikukusanywa kutoka Vyama vya Msingi licha ya fedha hizo kukatwa kwa wakulima katika kipindi cha Mwaka 2011/12 mpaka 2016/17.

Huenda fedha zilizokatwa kwa wakulima na kisha kubakizwa katika akaunti za vyama vya msingi zilitumiwa na viongozi wa vyama vya msingi husika, kinyume cha makusudio na hivyo kuathiri kazi za CIDTF na zao la korosho kiujumla.

Menejimenti ya CIDTF ihakikishe inakusanya kiasi cha shilingi 4.85 bilioni kwa kila chama cha msingi husika na kwa kiasi ambacho hakikuwasilishwa CIDTF.

6.2.2 Amana Zilizokaa Zaidi ya Muda Uliokubalika Bila Kupata Riba Shilingi Milioni 518.84

CIDTF ilikuwa ikiwekeza sehemu ya fedha kwenye amana za muda mfupi za benki (fixed deposit) kwenye benki za CRDB tawi la Mtwara (A/c Na.0150237061701) na tawi la Holland (0150237061700) ambapo muda na riba ulikubalika kati ya pande zate mbili. Kwa kawaida, muda wa uwekezaji unapomalizika ni jukumu la benki kuzirudisha fedha hizo pamoja na riba kwenye akaunti ya mteja.

Hata hivyo, ukaguzi maalum umebaini kuwa fedha ziliendelea kukaa kwenye akaunti za Amana zaidi ya muda uliokubalika. Kwa wastani, fedha zilikaa mpaka siku 60 bila kurejeshwa kwenye akaunti tajwa hapo juu baada ya muda wa uwekezaji kupita, na hivyo, kupoteza kiasi cha Shilingi milioni 518.84 kama riba.

CIDTF imepoteza jumla ya Shilingi milioni 518.84 kwa kuziacha fedha kwenye akaunti za amana bila makubaliano.

Mamlaka husika ichukue hatua stahiki kwa viongozi wa CIDTF kwa uzembe wa kutofuatilia fedha, na hivyo, kupoteza Shilingi milioni 518.84 ambazo mfuko ungepata kama muda huo ungehesabiwa kama uwekezaji.

6.2.3 Zabuni kwa Kampuni Ambayo Haikuwa na Vigezo

Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 Kifungu 31 (2) inazuia mtu/taasisi ya umma kusaini mkataba na mzabuni kabla ya tunzo husika kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa Kamati ya Tathmini ilikaa tarehe 1 Machi 2012 na kuiondoa kampuni ya Hammers Incorporation Ltd katika mchakato wa zabuni ya kuuza salfa ya ruzuku katika hatua za awali kwa kushindwa kuwasilisha kinga ya mkataba.

Katika mchakato huo, kampuni tatu (3) za M/s Export Trading Company, M/s Export Trading Company na M/s Mukpar (T) Ltd ziliingia katika upembuzi wa kina na gharama. Kampuni ya M/s Export Trading Company alitaja bei ya chini zaidi, Shilingi 800 kwa kilo moja; M/s Tanzania Fertilizer Company ilitaja bei ya Shilingi 960 kwa kilo moja, na M/s Mukpar (T) Ltd bei ya Shilingi 1,280 kwa kilo moja. Kamati ya Tathmini kupitia taarifa yake ya tarehe 1 Machi 2012 ilipendekeza kugawanya zabuni kwa M/s Export Trading Company na M/s Tanzania Fertilizer Company kwa tani 2,500 kila kampuni ili kupunguza uwezekano wa mzabuni kushindwa kuleta salfa yote.

Hata hivyo, ilibainika kuwa M/s Export Trading Company alipatiwa kazi yote ya kuuza tani 5,000 za salfa iliyotolewa kupitia Zabuni Na. ME012/2011-2012/CIDTF/P/04 kwa Shilingi 4.4 bilioni; ikielezwa kuwa kutozingatiwa kwa mapendekezo ya Kamati ya Tathmini kulitokana na bei ya chini iliyonukuliwa na M/s Export Trading.

Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 21 Juni 2012 M/s Export Trading Company haikuwa imeleta kiasi cha Salfa kwa kiasi walichokubaliana katika mkataba (Kipengele cha 25(1) na (2) (a)); na badala yake, M/s Hammers Incorporation Limited alipewa zabuni kwa tani zote 5,000 kwa makubaliano ya kupewa malipo ya awali ya asilimia 50 Shilingi bilioni 1.92. Hata hivyo, fedha hizo zililipwa kwa M/s Hammers Incorporation bila ya kuwapo kwa dhamana ya mkataba.

Ugawaji wa zabuni kwa kampuni isiyo na vigezo kukasababisha ishindwe kufikisha pembejeo kwa walengwa.

Wizara husika inapaswa ichukue hatua za kinidhamu kwa watumishi wote walioshiriki kuipa zabuni Kampuni ambayo haikuwa na vigezo na Kampuni kwa kushindwa kutimiza masharti ya makubaliano.

6.2.4 Kutowasilishwa kwa Dhamana ya Shilingi bilioni 7.63

Ilibainika wakati wa ukaguzi maalum kwamba CIDTF iliingia jumla ya mikataba minne (4) na M/s Hammers Incorporation Ltd na Mukper (T) Limited yenye thamani ya jumla ya Shilingi bilioni 7.63 bila kuwa na dhamana ya mkataba (performance security). CIDTF ilipata hasara baada ya Hammers Incorporation Ltd kushindwa kuleta salfa kwa wakati na kufanya udaganyifu kwenye idadi na ujazo wa mifuko.

Nashauri Uongozi wa CIDTF kufuata sheria ya manunuzi ya umma wakati wote wa mchakato wa manunuzi na hatua stahiki kwa

mujibu wa sheria ya manunuzi zichukuliwe kwa viongozi wa CIDTF kwa kukiuka sheria ya manunuzi.

6.2.5 Kutowasilishwa kwa tani 837 ya Salfa yenye thamani ya Shilingi 803.52 Milioni

CDTIF waliingia kwenye mkataba na M/s Hammers Incorporation Ltd kwa ajili ya usambazaji wa tano 3000 za sulphur. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa msambazaji alisambaza tani 2307 huku tani 693 zikiachwa. Nikagundua zaidi uzito wa baadhi ya mifuko iliyosambazwa ni pungufu kiasi cha kupelekea upungufu wa zaidi ya tani 144.

Udanganyifu huo uliogundulika umesababisha hasara ya tani 837 zenye thamani ya Shilingi milioni 803.52. Hivyo, naishauri Menejimenti ya mfuko, wakishirikiana na Serikali, kuwachukulia hatua kali watumishi ambao kwa namna moja au nyingine, walishiriki kwenye udanganyifu huo; pia hatua kali zichukuliwe dhidi ya kampuni/ Msambazaji.

6.2.6 Viatilifu vilivyokwisha muda wake wa Matumizi Shilingi milioni 594.03

Mnamo tarehe 31 Machi 2017 mpaka 7 Aprili 2017, ulifanyika uhakiki kwenye maghala ya Mtwara Mjini, Naliendele na Tandahimba na kubaini viatilifu vyenye thamani ya Shilingi milioni 594.03 vilivyohifadhiwa kwenye maghala hayo vimekwisha muda wake wa matumizi. Tropical Pesticides Research Institute (TPRI) ambao wamechukua sampuli ya dawa hizo kwa ajili ya kuzifanyia vipimo ili kuona kama itafaa tena kwa ajili ya matumizi.

Serikali inaweza kupata hasara ya jumla ya Shilingi milioni 594.03 kama sampuli zilizochukuliwa na TPRI zitabaini kuwa viatilifu hivyo havifai kwa matumizi; pia, Serikali italazimika kugharamia uteketezaji wa viatilifu endapo itaamuliwa viteketezwe kwa kuzingatia utaalumu.

Bodi ya Korosho iwasiliane na TPRI ili kupata majibu ya kitalaamu juu ya ubora wa viatilifu vilivyokwisha muda wake ili kubaini kama bado vinaweza kutumika kwa ajili kukinga na kutibu magonjwa ya mikorosho ili ziweze kugawiwa kwa wakulima katika msimu wa 2017/2018 ili kuiepushia Serikali hasara. Kama itabainika kuwa havifai kwa matumizi, hatua stahiki za uteketezaji wa viatilifu hivyo zizingatiwe ili kuepusha madhara.

6.2.7 Mikopo kutolewa kwa Makampuni ya ubanguaji bila Upembuzi yakinifu Uliosababisha kushindwa kurejeshwa Shilingi milioni 881.16

Ukaguzi maalum ulibaini kuwa jumla ya Shilingi milioni 881.16 zilikopeshwa kwa kampuni za ubanguaji wa korosho za Southern Jumbo Cashewnut Limited na Kikundi cha Kinamama Demros. Mpaka wakati wa ukaguzi huu, Mwezi Aprili 2017, kiasi cha Shilingi milioni 1.5 ndicho kilichokuwa kimerejeshwa na Demros, hivyo kubaki na jumla la deni la Shilingi milioni 881.16.

Kutokufuatwa kwa taratibu katika Mchakato wa ukopeshaji kulipelekea Mkopo huo kutorejeshwa kwa wakati, hivyo kukwamisha kazi za usimamizi wa korosho kwa kukosa fedha, kwani fedha zilikuwa bado hazijarejeshwa.

Mfuko uhakikishe unafuatilia fedha hizo na zirudishwe. Pia taratibu zifuatwe katika kutoa Mikopo; upembuzi yakinifu ufanywe na ufuatiliaji wa mikopo ufanyike mara baada ya kutolewa.

6.3 Kampuni ya Ndege Tanzania

Kampuni ya ndege iliingia mikataba na watoa huduma mbalimbali. Baadhi ya mikataba hiyo ilipelekea shirika kupata hasara kutokana na mapungufu yaliyomo katika mikataba hiyo. Mapungufu hayo ni kama yalivyoanishwa hapa chini;

6.3.1 Mkatoba wa Wallis Trading Inc. na shirika la ndege

Kampuni ya Ndege Tanzania iliingia mikatoba na makampuni mbalimbali, ikiwemo Wallis Trading Incorporation, kwa ajili ya kukodisha ndege aina ya AIR BUS A-320-214 AIRCRAFT. Ilibainika kuwa mkatoba umesainiwa tarehe 9 Oktoba 2007 lakini ndege ilikuja kukaguliwa tarehe 14 mpaka 22 Januari 2008, ambapo ni kinyume kabisa na kifungu namba 4.5 cha mkatoba kinachomtaka mkodishaji kumpa nafasi mkodishwaji kukagua ndege kabla ya kusaini mkatoba.

Ukaguzi uligundua kuwa ndege hiyo ina mapungufu na ubovu kiasi cha kuhitaji matengenezo makubwa na kwa muda wa miezi saba ya matengenezo, kampuni ililipa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 2.59 kwa sababu tu tayari kampuni ilishaingia kwenye mkatoba huo.

Mapitio zaidi yalibaini kuwa wakati wa usainishaji wa mkatoba ni Mkurugenzi Mkuu peke yake ndiye aliyekuwepo kwa upande wa kampuni pasi na kuwepo shahidi yeyote.

6.3.2 Kutowekwa Benki kwa Malipo yaliyofanyika kutokana na ukodishwaji wa eneo kutowekwa Benki

Kampuni iliingia mkatoba na Hoteli iitwayo Paradise Holiday Resort kwa ajili ya kukodisha eneo na kufanya ujenzi wa mgahawa uitwao City Garden kwa kipindi cha miaka kumi (10) kuanzia Mwezi Septemba 2006 mpaka Oktoba 2016.

Kulingana na makubaliano ya mkatoba, mkodishaji alipaswa kulipa kiwango sawa cha kodi ya pango na umeme kwa kipindi chote cha miaka kumi ya mkatoba bila kujali matumizi ya umeme au thamani halisi ya eneo kulingana na wakati, na Kampuni ya Ndege ndiyo ilipaswa kwenda kuwasilisha malipo kwa kampuni ya umeme (TANESCO).

Wakati wa ukaguzi iligundulika kuwa, jumla ya tozo ya kodi Shilingi milioni 101.3 na gharama za umeme Shilingi milioni 52.3

hazikuingizwa kwenye akaunti ya Kampuni ingawa Paradise Holiday Resort ametoa uthibitisho wa malipo ya madai hayo kupitia risiti namba 3836 kwa pango na risiti namba 3837 kwa gharama za umeme.

6.3.3 Malipo ya Huduma ya Mfumo wa Kihisibu hata kama Ndege zikiwa mbovu

Cashiering-Emirates HQ-UAE ni kampuni iliyokuwa ikitoa huduma ya mfumo wa uhasibu na mapato kwa Kampuni ya Ndege Tanzania. Kwa mujibu wa jedwali la orodha ya madeni ya Kampuni ya ndege Tanzania, kampuni ya Cashiering-Emirates HQ-UAE inaidai Kampuni ya Ndege Tanzania jumla ya Shilingi milioni 489.5 ikiwa ni gharama za kupokea huduma kutoka kwa kampuni hiyo.

Kwa mujibu wa mkataba, ilikadiriwa kuwa kiwango cha chini cha abiria 500,000 watahudumiwa kwa mwaka; na kwa kila abiria, ATCL italipa Dola za Kimarekani 0.39.

Ukaguzi ulibaini kuwa ATCL ilikuwa ikilipa kwa kila robo ya mwaka kiasi cha Dola za Kimarekani 48,750 (abiria 500,000 x \$0.39 ÷ 4) bila kujali kama ndege zinafanya kazi au hazifanyi kazi (yaani bila kujali idadi halisi ya abiria waliohudumiwa). Timu ya ukaguzi ilipitia mkataba huo na kubaini hauonyeshi ulianza lini na ungeishia lini. Pia, mkataba huo haukuwa umesainiwa na upande wa mdai, hali inayotilia shaka kama maslahi ya kampuni yalizingatiwa katika mkataba huu.

Timu ya ukaguzi ilimuomba mdai kuthibitisha na kutuma vielelezo na nyaraka za uthibitisho wa madai yake kwa Kampuni ya Ndege Tanzania kwa kumuandikia barua pepe mnamo tarehe 28 Machi 2017 na tarehe 18 Mei, 2017. Zaidi, iliwasiliana naye kupitia mawasiliano ya simu namba +971 4203 3551/971 4708 2767 bila mafanikio yoyote.

Kampuni ya Ndege inapaswa kulichukulia hatua jambo hilo ikiwemo kupitia upya mikataba ili uweze kunufaisha pande zote.

6.3.4 Kuendelea kupata Huduma za Kisheria bila kuingia mkataba upya

Kampuni ya Uwakili ya Octavian iliingia mkataba na Kampuni ya Ndege Tanzania tarehe 1 Juni 2007 ili kuwa wakili wa kampuni. Mkataba huo ni wa miaka miwili na unaweza kuongezwa tena kwa makubaliano ya pande mbili. Kampuni hiyo imekuwa ikiitoza ATCL Dola za Kimarekani 1,500 kwa mwezi na malipo mengine yamekuwa yakifanyika pindi kunapokuwa na kesi kortini.

Hata hivyo sikuweza kupewa uthibitisho unaoonyesha kuhuishwa kwa mkataba ingawaje kampuni husika inaendelea kutoa huduma za kisheria kwa ATCL.

Kampuni ya Ndege Tanzania wawasiliane na Kampuni ya uwakili kwa ajili ya kurudishiwa fedha ambazo walizilipa kama tozo ya huduma wakati kukiwa hamna mkataba kati yao.

6.3.5 Kutolipa Madeni yenye Riba kwa Wakati

Wakati wa ukaguzi imegundulika kuwa kampuni ya Ndege hailipi madai kwa wakati kutoka kwa watoa huduma wake, hivyo kupelekea kuzalisha madeni yenye riba na adhabu kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali 5: Kutolipa Madeni yenye Riba kwa Wakati (katika mamilioni ya Shilingi)

TAASISI	FEDHA	DENI HALISI	RIBA	GHARAMA ZA MAHAKAMA	VIWANGO VYA KUBADILI	JUMLA
AEROVISTA	USD	1.06	0.56	0.22	2,200.00	4,057.30
CO-ARCHITECTURE	SHILINGI	154.53	150.02	12.91	1.00	317.46
TIB	SHILINGI	2,478.00	739.19	0.00	1.00	3,217.19
KENYA KAZI	SHILINGI	30.93	31.86	0.00	1.00	62.79
PSPF	SHILINGI	39.20	15.70	0.00	1.00	54.89
PPF	SHILINGI	1,202.29	1,929.72	0.00	1.00	3,132.02
COMAIR	USD	0.38	1.29	0.00	2,200.00	3,653.60
TANZANIA MICROFINANCE LTD	SHILINGI	143.38	109.68	7.73	1.00	260.79
JUMLA			2,978.01	20.86		14,756.04

Kutokana na kuwapo kwa ongezeko la riba kwenye madeni yake. Kampuni ya Ndege inashauriwa kuyalipa madeni hayo kwa wakati ili kuepuka ongezeko na adhabu zisizo za lazima.

6.3.6 Kampuni kutokuwa na Takwimu Sahihi Zinazoonesha Viwango vya Madeni yaliyolipwa na ambayo bado

Katika zoezi la ukaguzi ilibainika kuwapo kwa madeni ambayo hati za madai zilirodheshwa kuwa bado hazijalipwa. Lakini baada ya timu ya ukaguzi kupokea mrejesho wa uthibitisho wa madai kutoka kwa wadai, ilibainika kuwa wadai walikiri kuwa baadhi ya hati hizo zilikuwa zimekwishalipwa; na baadhi ya wadai hawakuzitambua hati hizo kwa kuwa si miongoni mwa hati walizowasilisha kwa timu katika mirejesho ya uthibitisho wa madeni yao kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la hapa chini:

Jedwali 6: Udhaifu katika kusimamia madeni

Na .	Jina la mdai	Aina ya Fedha	Thamani ya deni katika orodha ya madeni	Thamani ya deni katika hati za madai	Deni lililothibitishwa na mdai
1	Law Advocate Associates	SHILINGI	25,830,200.00	25,830,200.00	0.00
2	Mwanza Handling Coy Limited	USD	385,682.80	385,682.80	258,667.40

Na .	Jina la mdai	Aina ya Fedha	Thamani ya deni katika orodha ya madeni	Thamani ya deni katika hati za madai	Deni lililothibitishwa na mdai
3	Tanzania microfinance Bank	SHILINGI	234,981,629.26	260,788,609.24	260,788,609.24
4	Moku security	SHILINGI	78,425,000.00	78,425,000.00	43,830,000.00
5	cemair	USD	300,750.00	1,457,283.76	1,457,283.76
6	Aerovista	USD	862,154.41	1,849,525.63	1,849,525.63
7	CO-Architecture (Architerial Services)	SHILINGI	134,532,837.00	317,416,678.00	317,461,678.00

Hali hii inaweza kusababisha Kampuni ya Ndege illipe madeni haya mara mbili au zaidi, au iwe na taarifa zisizo sahihi juu ya madeni yake. Pia, utaratibu dhaifu wa udhibiti madeni unatoa mianya ya udanganyifu na kupelekea upotevu wa fedha za umma.

Naishauri ATCL kuboresha utaratibu wa udhibiti wa madeni ya kampuni ili kuepuka kulipa madeni mara mbili na kuwa na taarifa za madeni zisizo sahihi ambazo zinaweza kupotosha maamuzi ya uongozi wa Kampuni na pia kuchunguza uhalali wa madeni haya ili kuona kama hakuna udanganyifu.

6.4 Ukaguzi Maalum wa Ubia wa Uendeshaji kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Kampuni yaa Intra Energy Tanzania Limited(IETL)

6.4.1 Matumizi Yasiyo Halisi Katika Utafutaji wa Madini Kiasi cha Shilingi Milioni 880.7 Yaliingizwa Katika Taarifa za Fedha za TANCOAL

Mapitio ya taarifa za fedha za TANCOAL kwa miaka Sita kuanzia 2011 hadi 2016 yalionyesha kwamba matumizi katika utafutaji wa madini ya jumla ya kiasi cha Shilingi bilioni 6.58 hayakustahili.

Uchambuzi wa taarifa za fedha pamoja na Ripoti ya Utafutaji wa Madini ulibainisha gharama za utafutaji wa madini za Shilingi bilioni 6.58; ambapo, kiasi cha Shilingi milioni 880.7 kati ya hizo kilijumuishwa isivyostahili.

Gharama hizi ziliainishwa katika taarifa za fedha kwa miaka minne kuanzia mwaka 2013 hadi 2016 isivyostahili, kwani utafiti wa madini uliisha mwaka 2012. Kuingizwa kwa gharama za aina hiyo katika taarifa za kifedha kumepunguza faida na kuonesha hasara kwa Kampuni ya TANCOAL, ambapo Serikali haikuweza kupokea gawio wala kukusanya kodi kwa kutoainishwa faida ya Kampuni.

NDC inapaswa kuimarisha usimamizi katika uendeshaji wa ubia ili kuhakikisha kuwa ripoti zote za fedha ni sahihi.

6.4.2 Gharama ya Kiasi cha Shilingi Milioni 940.34 na Dola za Marekani bilioni 3.35 zililipwa na TANCOAL Energy Ltd kwa Shughuli Zisizohusiana na Kampuni

Mapitio ya hati za malipo kwa miaka mitatu kuanzia 2014 hadi 2016 yalibaini kuwa TANCOAL imetumia kiasi cha Shilingi milioni 940.34 ambazo hazihusiani moja kwa moja na uchimbaji wa madini na shughuli nyingine za Mgodu kwa mujibu wa makubaliano ya Ubia. Uchambuzi wa kumbukumbu za malipo ulibainisha kuwa TANCOAL Energy Limited ilifanya malipo yasiyohusiana na shughuli za TANCOAL.

Kadhalika, uchambuzi umeonesha kuwa, jumla ya Dola za Marekani 3.35 zililipwa kwa TANCOAL nchini Malawi (Kampuni ya Tangu ya Intra Energy) kama gharama za shughuli za madini kama vile ada ya ushauri, gharama za kusafirisha, kukodisha mtambo, masoko, uhamisho wa fedha kwenda Intra Energy Malawi, pamoja na malipo mengine ya kampuni yote hayakuhusiana na shughuli za TANCOAL.

Matumizi ya jumla ya Shilingi milioni 940.34 na Dola za Kimarekani bilioni 3.356 yamesababisha TANCOAL Energy Ltd kutoripoti faida, hivyo, Kampuni kutotoa gawio na wala kustahili kulipa kodi.

Menejimenti ya NDC inapaswa kuhakikisha kuwa malipo yote yasiyofaa na kiasi kilichopatikana na TANCOAL Energy Ltd

kinarejeshwa tena na kurejea taarifa zao za kifedha kwa kuondoa malipo yasiyo ya lazima.

6.4.3 Gharama za Mchango wa Kampuni kwa Jamii Zilizidishwa kwa Jumla ya Kiasi cha Shilingi milioni 917.62

Mapitio ya taarifa za fedha za TANCOAL kwa miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka wa 2016 zilionesha kuwa Kampuni ya TANCOAL Energy Ltd ilichangia jumla ya Shilingi milioni 993 katika shughuli za maendeleo ya jamii huko Ngaka na Songea kama sehemu ya wajibu wake kwa Jamii (CSR).

Ukaguzi umebaini kuwa, ni kiasi cha Shilingi milioni 75.4 pekee ndicho kilitolewa na Kampuni ya TANCOAL Energy Ltd kama mchango kwa Jamii. Kiasi pekee kilicholipwa pia kilithibitishwa na Meneja wa Usalama, Afya na Mazingira (HSE) ambaye ndiye mwenye jukumu la kutekeleza shughuli za Kampuni kwa Jamii.

Menejimenti ya TANCOAL haikuwa na nyaraka zozote zinazothibitisha matumizi ya jumla ya kiasi cha Shilingi milioni 917.62 kwa mujibu wa taarifa za fedha. Kujumuishwa kwa kiasi hicho katika taarifa za fedha za Kampuni kunapotosha makusudi kwa taarifa za fedha.

TANCOAL Energy Ltd wanapaswa kurejesha kiasi kilicholipwa kwa ajili ya kurudisha faida kwa jamii ambacho hakina uthibitisho wa nyaraka na kufanya marekebisho ya hesabu katika vitabu vyao.

6.4.4 Malipo Yasiyo Sahihi kwa Shirika la Intra Energy Corporation (Australia) Kama Tozo ya Menejimenti Kiasi cha Shilingi Bilioni 1.47

Taarifa za fedha za TANCOAL kwa miaka mitano (5) kuanzia Juni 2013 hadi Machi 2017 zilionesha jumla ya shilingi 7.26 billioni kama ada za usimamizi wa Menejimenti. Matumizi hayo yalionyeshwa kama mkopo ambao ni deni kwa TANCOAL linalopaswa kulipwa.

Ulipaji wa mkopo kwa gharama za uendeshaji, matumizi ya mtaji na ada za usimamizi ulianza rasmi Mei 21, 2013 hadi Juni 2017 kwa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 1.81, ambapo kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 1.72 kililipwa kwa Intra Energy Corporation (IEC). Kati ya fedha hizo, kiasi cha Dola za Kimarekani 667,187,730 sawa na Shilingi bilioni 1.47 kililipwa kama Ada ya Menejimenti kinyume na maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi.

Mapitio ya Muhtasari wa Mkutano wa Bodi ya TANCOAL Energy Ltd wa tarehe 15 Novemba 2012 yalionesha kwamba Bodi ya Wakurugenzi TANCOAL iliamua kutokuwa na makubaliano ya huduma ya usimamizi (management service). Hivyo, kampuni ya Intra Energy Corporation (IEC) Australia ingepaswa kulipwa gharama halisi zinazoiingia badala ya kulipa Ada ya Menejimenti. Malipo ya Ada za Menejimenti yaliyo kinyume na idhini ya Bodi ya Wakurugenzi yamepunguza faida ya kampuni, hivyo kutokusanywa kwa kodi.

Inapendekezwa kuwa, shughuli zote zinazohusiana na ada za usimamizi wa Menejimenti za Shilingi bilioni 1.47 zilizolipwa kwa IEC zinapaswa kurejeshwa na TANCOAL Energy Ltd kutoka Intra Energy Corporation Australia.

6.5 TATHMINI YA MIRADI MBALIMBALI ILIYOTEKELEZWA NA NSSF

6.5.1 Kliniki ya Apollo

Mnamo tarehe 23 mwezi Septemba 2014, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii uliingia kwenye makubaliano na kusaini mkataba na Apollo Hospitals Enterprises Limited na Apollo Hospital Singapore PTE Ltd kwa ajili ya ujenzi wa hospitali; ambapo, kila mbaia atapaswa kuchangia asilimia hamsini (50). Kulingana na makubaliano ya mkataba, AHEL walipaswa kutoa vifaa vyote kwa vinavyohusiana na hospitali na kuiendesha kwa miaka 15 katika tozo waliyokubaliana. Mpaka sasa, mradi umeshatumia Shilingi bilioni 4.19.

Mwezi wa pili mwaka 2018 nilitembelea miradi kwa ajili ya ukaguzi na kubaini kuwa, mkandarasi ametelekeza mradi na hakuna kinachoendelea; pia, kijiografia mradi umekaa mazingira ambayo sio Rafiki, kwani ni ngumu kufikika. Hii ni kutokana na kuwapo kwa mradi wa mabasi yaendayo kasi ambapo magari binafsi hayaruhusiwi kupita kwenye miundombinu ya mradi huo. Hivyo, kukwaza ufikikaji wa kliniki hiyo.

Naishauri Menejimenti na Bodi ya wadhamini ya NSSF watafute mwekezaji ambaye uwekezaji wake utakuwa na manufaa kwa pande zote, kwani bado mahitaji makubwa ya huduma bora za afya hapa nchini ni makubwa.

6.5.2 Ujenzi wa Ofisi za Ubalozi na Jengo la Kibiashara mjini Nairobi
Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje ambaye wanamiliki eneo mjini Nairobi, waliingia makubaliano ya ujenzi wa jengo la kibiashara na ofisi za Ubalozi, ambapo mradi ungegharimu jumla ya Shilingi bilioni 1.05 za Kenya sawa na Shilingi bilioni 77.4 za Kitanzania.

Mpaka sasa jumla ya Shilingi milioni 854.28 zimetumika kwa ajili ya shughuli mblimbali zinazohusiana na mradi. Mpaka sasa, hakuna chochote kinachoendelea kuhusiana na mradi.

6.5.3 Mradi wa Kuzalisha Umeme Mkuranga
Shirika la Umeme Tanzania, Shirika la Maendeleo ya Petroli na baadhi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii walikutana kwa ajili ya kutafuta namna ya kukabiliana na tatizo la umeme kwa kipindi hicho wakati ufumbuzi wa kudumu wa tatizo ukitafutiwa majawabu. Kwa dharura hiyo, mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii wakaingia kwenye mradi wa uzalishaji umeme; ambapo mitambo ingewekwa eneo la Mponga wilayani Mkuranga. Gharama za mradi inakadiriwa kufikia Dola za Kimarekani milioni 490.

Katika maandalizi ya mradi, NSSF ilinunua eneo la hekari 100 huko Mponga kwa ajili ya uwekaji wa mitambo na mashine; pia, visima 11 vilichimbwa kwa ajili ya upatikanaji wa maji ili mitambo na mashine iweze kupoozwa. Mpaka sasa, jumla ya Shilingi bilioni 3 za Kitanzania zimeshatumika kwa shughuli mbalimbali.

Nilipotembelea eneo la mradi, niligundua kuwa eneo lililonunuliwa na NSSF kwa ajili ya mradi huo halijawekwa alama za utambuzi, hivyo kupelekea urahisi wa kuvamiwa na kusababisha mgogoro wa ardhi.

Pia, nilishindwa kupata taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi ili kuweza kujiridhisha kama mradi una manufaa kwa Taasisi.

6.5.4 Ujenzi wa Nyumba za Makazi katika Eneo la Njiro Kiwanja Namba 249 Kitalu D

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii uliingia makubaliano ya ununuzi wa viwanja katika eneo la Njiro mnamo tarehe 4 Novemba 2010 kwa makubaliano ya jumla ya Shilingi milioni 440 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi za kisasa ambazo zingeuzwa kwa jamii yote ya Watanzania ambapo malipo yalifanyika kwa awamu. Gharama za mradi zinakadiriwa kufikia Shilingi bilioni 14.7. Malipo ya mwisho ya jumla ya Shilingi milioni 308 yalifanyika mnamo tarehe 22 Machi 2011.

Nilipofanya ukaguzi eneo la mradi mnamo mwezi Januari mwaka 2018 niligundua kuwa eneo limevamiwa; kuna makanisa yamejengwa pamoja na shughuli nyingi za kibinadamu zinaendelea. Pia, kwenye ukaguzi wangu nimeshindwa kupata nyaraka za umiliki wa eneo na hati za kiwanja hicho.

Ni ngumu kwa NSSF kurejesha Shilingi milioni 440 ambazo zimeshatumika kwenye mradi.

6.5.5 Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Mwanza katika Eneo la Kiseke na Bugarika

Mwaka 2008 Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulipanga kujenga nyumba za gharama nafuu katika eneo la Kiseke na Bugarika kwa ajili ya kuuzwa kwa watumishi na jamii yote ya watanzania.

Mfuko uliingia kwenye makubaliano ya mauziano na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa ajili ya kununua viwanja 357 katika eneo la Bugarika na viwanja 299 katika eneo la Kiseke kwa jumla ya Shilingi bilioni 1.89, ambapo malipo yangefanywa kwa awamu tatu.

Shilingi bilioni 1.51 ililipwa ambayo ni asilimia themanini ya mradi. Kwenye ukaguzi wangu niligundua kuwa mpaka sasa sio viwanja vyote ambavyo vimeshagawiwa kwa mfuko kulingana na makubaliano; na hakuna uendelezaji wowote uliofanyika kwenye eneo lilikwishagawiwa. Pia, ilibainika kuwa viwanja vilichukuliwa bila kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuangalia faida za kiuchumi na kijamii zitokanazo na mradi.

Nilifanya mahojiano na Afisa Mtendaji wa Kata ya Buhongwa na akabainisha kuwa kuna baadhi ya wanakijiji bado hawajalipwa fidia na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa eneo lile la mradi. Pamoja na hayo, pia Mfuko haujafanya jitihada katika kulilinda eneo hilo, kwani kuna shughuli za kibinadamu zinaendelea.

Ni vigumu kwa Mfuko kudai viwanja ambavyo vimevamiwa na wakazi wa maeneo ya jirani.

6.5.6 Kituo cha Usafirishaji cha Kimataifa Mwandiga

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulipanga kuendeleza eneo la ekari 28 lililopo Mwandiga kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha usafirishaji cha kimataifa; na kati ya ekari hizo, mfuko tayari umeshachukua ekari 23 kwa thamani ya Shilingi billioni 1.85.

Mpaka sasa hakuna kinachoendelea kwenye eneo la mradi.

Ni ngumu kwa sasa Mfuko kuweza kurejesha kiasi cha Shilingi bilioni 1.85 ambazo tayari zimeshalipwa.

6.5.7 Ununuzi wa Ardhi kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii uliingia kwenye mradi wa ununuzi wa maeneo kwa ajili ya ugawaji wa viwanja. Maeneo hayo ni Madale (mita za mraba 76,633), Mlunga (ekari 1,496.8) Misugusugu (ekari 100), Mataya (mita za mraba 187,103) na Ngarambe (ekari 300) kwa ajili ya uhifadhi wa ardhi kwa matumizi ya baadae kama inavyoainishwa hapa chini:

- i. Mlunga - Kibaha (Mkoa wa Pwani)- Ujenzi wa Bandari kavu
- ii. Madale - Kinondoni - Ujenzi wa mji wa kisasa
- iii. Mataya - Bagamoyo - Ujenzi wa mji wa kisasa
- iv. Misugusugu - Kibaha (Mkoa wa Pwani) Ujenzi wa mji wa kisasa
- v. Ngarambe - Mkuranga (Mkoa wa Pwani) - Ujenzi wa makazi

Mpaka sasa, mradi umeshatumia kiasi cha Shilingi bilioni 15.8 kwa ajili ya ununuzi wa maeneo hayo.

Wakati wa ukaguzi wa eneo la mradi nilibaini kuwa mfuko umeshauza viwanja vya Madale vilivyopo wilaya ya Kinondoni. Hata hivyo, viwanja vilivyopo Wilaya ya Mkuranga havina alama, na ni eneo ambalo halijapimwa. Maeneo mengine yaliyobaki yapo mbali kibiashara.

Maeneo yote yalinunuliwa bila kufanyika kwa upembuzi yakinifu. Pia, hakuna baraka za kikao cha Bodi ya Wadhamini wala kikao cha Kamati ya Uwekezaji vilivyoidhinisha.

Pia, maeneo mengi yalinunuliwa kabla ya kupimwa, na hakuna ushahidi unaoonesha namna ambayo thamani ya Shilingi bilioni 15.8 ilifikiwa.

Nashauri Mfuko uuze viwanja hivyo ili kuweza kurudisha kiasi cha pesa kilichotumika; na pia kuweka ardhi kama akiba kuna gharama kubwa za uendeshaji kuliko faida itakayopatikana.

6.5.8 Kampuni Tanzu ya Mkulazi

Mnamo tarehe 6/9/2016 Mashirika mawili ya Pensheni ambayo ni Mfuko wa Pensheni wa NSSF na Mfuko wa Pensheni wa PPF yaliunda Kampuni Tanzu ya Mkulazi ambayo ni chombo maalum kilichoundwa kwa ajili ya ujengaji wa kiwanda cha Sukari na uendelezaji wa mashamba ya miwa ambapo kitakuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya tani laki mbili (200,000) kwa mwaka.

Kampuni Tanzu ya Mkulazi inaendeleza mashamba mawili, moja ni shamba namba 217 lilipo kata ya Mkulazi (Mkulazi I) wilaya ya Morogoro vijijini lenye ukubwa wa eneo la hekta 63,227 na jingine likiwa Mbigiri (Mkulazi II) lililopo Wilaya ya Mvomero Mkoa wa Morogoro lenye ukubwa wa hekta 4,856.

Mwezi Februari 2017 Kampuni Tanzu ya Mkulazi na Jeshi la Magereza Tanzania walisaini Randama ya Makubaliano kw ajili ya uendelezaji wa shamba la Mbigiri.

Mtaji wa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 76.87 zitatolewa kwa awamu nne kuanzia mwaka 2017/18 mpaka 2020/21.

Marejeo ya upembuzi yakinifu inaonyesha kuwa mradi utakuwa na marejesho ya faida katika uwekezaji ya asilimia 24.30 na kipindi cha malipo ya mtaji kitakuwa miaka 4 na nusu kutoka kwenye uwekezaji wa awali.

Pia, marejeo zaidi ya upembuzi yakinifu yamegundua mradi utakuwa na mauzo ya Dola za Kimarekani milioni 18.8 kwa mwaka wa kwanza (2018/2019) na yataongezeka mpaka Dola za

Kimarekani milioni 30.6 kwa mwaka wa 5 na Dola za Kimarekani Milioni 35.2 kwa mwaka wa 10 wa mradi faida itaongezeka mpaka kufikia Dola za Kimarekani milioni 39.5 kufikia mwaka wa 15.

Mradi unatarajiwa kuingiza faida ya Dola za Kimarekani milioni 5.4 kwa mwaka wa kwanza na inatarajiwa kuongezeka mpaka kufikia Dola za Kimarekani milioni 16.5 kwa miaka 5 na kuendelea.

Kwa mujibu wa Menejimenti, mradi una faida za kijamii na kiuchumi ambazo kati ya hizo ni kupunguza uhaba wa sukari, kuongeza upatikanaji wa ajira, ongezeko la vyanzo vya kodi kwa Serikali kuu na Serikali za Mitaa na kukuza ustawi wa jamii ya watu wanaouzunguka mradi.

Pia mradi wa Mkulazi II una changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kurekebishwa kabla mradi haujaanza kazi kikamilifu ambazo ni kama zifuatazo:-

- i. Ujenzi wa njia ya reli inayokwenda kwenye mradi unafanyika kwenye eneo ambalo linakabiliwa na mafuriko ya mara kwa mara;
- ii. Eneo la mradi katika shamba la Mbigiri halina hati miliki;
- iii. Miundombinu ya umwagiliaji ni ya zamani ambayo ilirithiwa kutoka shamba la zamani na haikidhi haja katika eneo la mradi;
- iv. Madaraja yaliyopo kwenye njia ya kuingia na kutoka kwenye mradi ni madogo yenye uwezo wa kubeba mpaka tani 30 tu hivyo hayakidhi mahitaji yaliyopo sasa
- v. Kunahitajika uwepo wa mafunzo kwa ajili ya kuwaongezea uwezo wakulima wadogo ambao ni washikadau muhimu kwa ustawi wa mradi; na

- vi. Eneo ulipo mradi ni mahali panapopata mvua nyingi mpaka kupelekea mafuriko ambapo inaleta ugumu kwa utekelezaji wa shughuli mbali mbali za mradi.

Naishauri Kampuni Tanzu ya Mkulazi kutilia mkazo na kuhakikisha changamoto zote zilizoainishwa zinapatiwa ufumbuzi wa haraka kwa ajili ya ustawi wa mradi.

SURA YA SABA

UKAGUZI WA UFANISI WA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA NCHINI

7.0 Utangulizi

Sekta ya madini, gesi na mafuta inahusu utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia. Nchi ya Tanzania imebarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa madini na gesi, lakini mchango wa sekta hii kwenye uchumi hauridhishi.

Katika mwaka huu wa fedha nimefanya ukaguzi katika sekta ya uchimbaji wa madini na gesi na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha mchango wa sekta kwenye uchumi.

Ukaguzi wangu umehusisha taasisi zote za Serikali nchini zinazohusika na sekta ya uchimbaji kama vile Wizara ya Madini, Tume ya Madini, Kampuni ya Uthamini wa madini vito Tanzania, Shirika la Taifa la madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Uratibu wa shughuli za Mafuta, na Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania.

7.1 Mapungufu ya Ujumla

(i) Kutokuwapo kwa kanuni za kuelezea sheria za Maliasili na Rasilimali

Serikali imedhamiria kulinda na kuhakikisha kuwa maliasili na rasilimali za nchi zinawanufaisha wananchi wa Tanzania kwa kuhakikisha mikataba na makubaliano yahasayo utafutaji, uchimbaji na usimamizi wa maliasili unalindwa.

Katika utekelezaji wa dhamira husika, Serikali imeanzisha sheria mbili: - Sheria za Maliasili na Rasilimali ya mwaka 2017 (Permanent Sovereignty) na Sheria ya Mkataba ya Maliasili na Rasilimali (Mapitio na Majadiliano juu ya vifungu hasi) ya mwaka 2017. Sheria hizi zimethibitisha haki ya umiliki wa Tanzania juu ya maliasili na rasilimali zote zipatikanazo ndani ya nchi, na

kulipa nguvu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweza kupitia mikataba na kubadilisha vifungu visivyo na maslai kwa taifa.

Hata hivyo, upembuzi wangu umebainisha ya kuwa licha ya kuwapo kwa sheria hizi, kanuni zinazoongoza utekelezaji wa vifungu vya sheria hizi hazijatayarishwa. Kutokuwapo kwa kanuni za kuongoza sheria kutadhoofisha utekelezaji wa sheria hizi na Serikali kutoweza kufikia dhamira yake juu ya sheria hizi.

Serikali, kupitia Wizara ya Madini, inashauriwa kutunga kanuni zitakazoongoza na kusimamia utekelezaji wa sheria za Rasilimali na Maliasili.

(ii) Ukomo wa wigo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika sekta ya Madini, Gesi na Mafuta

Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imempa mamlaka mdhibiti na makguzi mkuu wa Serikali ya kukagua na kutoa ripoti za Ukaguzi juu ya Hesabu za Serikali, Mahakama, na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kadhalika, kanuni namba 5 na 15 za Sheria za Ukaguzi za mwaka 2008 zimempa nguvu na uwezo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuweza kupata taarifa na nyaraka yeyote atakayohitaji katika utekelezaji wa majukumu yake.

Hata hivyo, mamlaka haya hayajatajwa katika sheria zinazoratibu sekta ya madini, mafuta na gesi. Kwa mfano, kifungu cha 26 katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kama ilivyorekebisha na Sheria ya Marekebisho namba 7 ya mwaka 2017 inazitaka kampuni za madini kutotoa nyaraka na taarifa kwa mtumiaji wa nje asiyetajwa kwenye sheria husika isipokua kwa maamuzi ya kampuni.

Zaidi ya hayo, kifungu cha 93 katika Sheria ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015 kinamtaka mmiliki wa leseni na vibali vya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi katika sheria hii kutotoa taarifa

na nyaraka za kampuni kwa mtu/taasisi yeyote ambayo siyo mamlaka ya usimamizi wa shughuli za mafuta na gesi (PURA) au mfanyakazi wa umma isipokuwa kwa kibali cha kampuni, ingawa ibara ya 18(k) ya MPSA 2013 inaeleza kuwa Serikali na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kupitia wawakilishi na wafanyakazi wake vitakua na haki ya kuingia kwenye eneo la uchimbaji na kufuatilia utelelezaji wa shughuli za mafuta na gesi kwa kukagua rasilimali, malighafi, taarifa na nyaraka husika.

Kutokana na kutokuwapo kwa mamlaka ya wazi, Ofisi yangu imelazimika kuihusisha Wizara ya Madini, kupitia tume ya madini na Shirika la Mafuta Tanzania, kuweza kuwafikia makampuni ya madini.

Mnamo tarehe 3 Januari 2018 Ofisi yangu ilijulisha Wizara ya Madini juu ya kusudi la Ofisi yangu kufanya ukaguzi juu ya gharama rejeshwa na upatikanaji wa mapato kwa makampuni haya kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2012 mpaka 2017. Hata hivyo, ni mpaka mwishoni wa mwezi Februari 2018 ndipo Ofisi yangu ilipokea barua toka Wizarani ikielezea kukubali kwa makampuni ya madini na mafuta kutembelewa na ofisi yangu.

Kitendo hiki kimechangia Ofisi yangu kushindwa kukagua misamaha ya gharama rejeshwa na mapato ya makampuni ya madini, gesi na mafuta.

Kutokana na umuhimu wa kuwapo kwa uwazi katika sekta ya madini, gesi na mafuta, kuna ulazima wa kurekebisha sheria mama za madini na mafuta ili ziweze kumtaja na kumpa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka ya wazi ya kupata taarifa zilizo na zisizo za kahasibu za makampuni ili kuboresha uwajibikaji wa kampuni hizi juu ya maliasili walizopewa kuziendeleza.

7.2 Taarifa ya Ukaguzi wa Sekta ya Madini

7.2.1 Tume ya Madini

Tume ya Madini imeundwa na Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Kufuatia kuvunjwa kwa iliyokuwa wakala wa ukaguzi wa madini Tanzania, shughuli zote zilizokuwa zinatekelezwa na wakala zimehamishiwa kwenye Tume ya Madini.

Yafuatayo ni mapungufu yaliyobainika kwenye ukaguzi wangu:

(i) Kutofanyika kwa uhakiki wa gharama za uwekezaji wa migodi

Kwa mujibu wa kifungu cha 41(4) (c) kwenye Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kama ilivyorekebisha na sheria ya marekebisho namba 7 ya mwaka 2017, miongoni mwa majukumu ya uliokuwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania, kwa sasa Tume ya Madini, ni kufanya uhakiki wa gharama za uwekezaji zinazotarajiwa ndani ya miezi kumi na mbili baada ya kutoa leseni ya wachimbaji wakubwa wa madini na kufuatilia utekelezaji wa ripoti ya upembuzi.

Uchambuzi wangu umebaini kuwa hakuna uthibitisho unaoonyesha kuwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini, kwa sasa Tume ya Madini, umefanya uhakiki wa gharama za uwekezaji tarajiwa wakati wa utoaji wa leseni ya uchimbaji madini.

Kutokuwapo kwa hatua stahiki za kuratibu uwekezaji hupelekea serikali kutoweza kutambua kwa uhakika gawio lake la mapato (mrabaha na kodi) toka kwenye makampuni ya madini kutokana na upandishwaji wa gharama kwa kulangua risiti au kutorosha faida na kutumia upangaji wa bei miongoni mwa makampuni yenye ubia.

Serikali, kupitia Tume ya Madini, inashauriwa kufanya uhakiki wa usahihi wa gharama za awali na muendelezo za uwekezaji katika migodi kuthibitisha usahihi wa taarifa za uwekezaji zilizotolewa

na makampuni ya migodi ili kuiwezesha serikali kukusanya mapato stahiki kupitia mrabaha na kodi.

(ii) Mauzo ya mali za migodi iliyopewa misamaha ya mitaji
Ibara 22(a) ya mfano wa mkataba wa uzalishaji wa gesi (MPSA) 2013 inaelekeza kuwa, mali zisizohamishika zinazomilikiwa na mkandarasi anayetokeleza shughuli za uchimbaji wa gesi na mafuta zitakuwa mali za TPDC kwa uamuzi wa TPDC baada ya kumalizika makubaliano au kuvunjika au wakati mkandarasi atakapokuwa amerejesha gharama za ununuzi wa mali hizo kupitia gharama za uendeshaji.

Kwa kuongeza, ibara ya 22(f) ya mfano wa Mkataba wa Uzalishaji Gesi (MPSA) 2013 imeeleza kuwa, iwapo gharama za mali zisizohamishika zitakuwa zimerejeshwa kwa asilimia 50 kulingana na vifungu vya makubaliano, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linaweza kumiliki mali hizo kwa shirika kulipia gharama za mali hizo zilizosalia.

Kinyume na mapendekezo ya mfano wa Mkataba wa Uzalishaji Gesi (MPSA) 2013, uchambuzi wangu wa mikataba ya madini umebaini kuwa mikataba haiipi serikali uwezo wa kumiliki mali za migodi baada ya wamiliki kurejesha gharama za ununuzi wa mali za migodi.

Kwa mfano, kupitia toleola tarehe 3 Machi 2018, Gazeti la Tanzania Daily News limechapisha tangazo lililotolewa na kampuni ya Harvest Tanzania Ltd ikishirikiana na kampuni za Slatery Auctions ya Australia na Liquidity Service ya South Africa kuwa watafanya mnada wa mali za mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi unaomilikiwa na Acacia ikiwa ni utekelezaji wa mikakati ya kufunga mgodi wa Buzwagi ifikapo mwaka 2020.

Pia, mnamo Novemba 2013 STAMICO ilinunua mgodi wa dhahabu wa Tulawaka kutoka kwa African Barrick Gold plc kwa dhamani ya dola za kimarekani milioni 4.5.

Imebainika ya kuwa misamaha ya mitaji inayotolewa kwa makampuni haya, kwa mfano, kurejeshwa kwa gharama za uwekezaji ambazo zinapunguzwa toka kwenye mapato ya migodi ni mapato ambayo yangeweza kukusanywa na serikali kama misamaha husika isingetolewa. Hii inaonyesha yakuwa kampuni za migodi zimesharejesha gharama zao za awali za uwekezaji zinazohusu ununuzi wa mali. Hivyo basi, mali hizi zinastahili kuwa za serikali baada ya kurejeshwa kwa gharama za uwekezaji zilizotumiwa na makampuni haya.

Zaidi ya hayo, hapakuwa na ushahidi wa kuwa misamaha ya uwekezaji inayotolewa kupitia misamaha ya kodi, mapumziko ya kodi, na marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani hayaendani na mchango wa migodi hii kupitia kodi na mirabaha kutokana na uchimbaji wa madini.

Serikali inashauriwa:

- a) Kutumia kifungu namba 4 cha sheria ya Mikataba ya Maliasili na Rasilimali ya mwaka 2017 kurekebisha mikataba ya migodi kuwezesha mali zote za migodi ambazo gharama zake zimesharudishwa kuwa mali ya serikali.
- b) Kuanzisha kamati maalum itakayochunguza na kulinganisha mimala inayohusiana na misamaha ya uwekezaji, misamaha ya kodi, na marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kutambua kama mapato haya yaliyosamehewa na serikali yanaendana na mchango wa sekta ya madini kwenye uchumi kupitia malipo ya mirabaha na kodi kutoka kwenye makampuni ya migodi.

7.2.2 Kampuni ya Uthamini wa Madini Vito Tanzania

Kampuni ya uthamini wa madini vito Tanzania ilianzishwa kufanya uthamini na upangaji bei wa dhahabu kwa ajili ya kutambua mrabaha na kodi zinazotakiwa kulipwa Serikalini.

Ukaguzi wangu katika kampuni hii ulibaini yafuatayo:

(i) Kutokuwepo kwa kanuni zilizopitishwa za upangaji na uthamini wa madini vito

Kulingana na kifungu cha 22(R) na (S) cha Sheria ya migodi ya mwaka 2010 kama ilivyorekebisha na Sheria ya marekebisha namba 7 ya mwaka 2017, tume ya madini imepewa majukumu ya kutambua thamani ya madini yaliyozalishwa, na kupanga bei elekezi za madini kwa kulinganisha na bei za masoko ya ndani na nje ya nchi kwa dhamira ya kukadiria mrabaha na kodi itayatakiwa kulipwa Serikalini. Kwa kuongezea kifugu namba 100(b) cha Sheria hii inaelekeza kuwepo kwa Afisa Mkazi wa Madini, Afisa wa Mamlaka ya Mapato, na maafisa toka kwenye taasis nyinginezo wakati wa uthaminishaji wa madini.

Kampuni ya uthamini wa madini vito Tanzania ambayo kwa sasa ipo chini ya tume ya madini imeandaa utaratibu na kanuni za kufuata wakati wa kutekeleza majukumu yake kama vile: kutumia viwango vya juu wakati wa kufanya uthamini, kutumia njia mbalimbali za kuthamini madini vito ghafi na yaliyosafishwa, na kutumia bei zilizopo sokoni kwenye kubaini thamani ya madini vito. Hata hivyo, hakuna ushahidi wa kuwa utaratibu huu umeidhinishwa na Wizara ya Madini.

Kutokuwapo kwa kanuni zilizoidhinishwa zitakazoongoza shughuli za upangaji na uthaminishaji kunasababisha kutokupatikana kwa matokeo linganifu wakati wa uthamini wa madini na kuwepo kwa makosa yatokanayo na matumizi ya mawazo binafsi ya kibinadamu wakati wa uthaminifu wa madini.

Serikali kwa kupitia Wizara ya Madini, inashauriwa kutunga na kupitisha kanuni zitakazoongoza shughuli za upangaji na uthaminifu wa madini.

(ii) Kutolipishwa kwa ada ya upangaji na uthamini wa madini vito

Kifungu namba 90 cha sheria ya madini ya mwaka 2010 kama ilivyorekebisha na sheria ya uwajibikaji na uwazi kwenye sekta ya madini na mafuta ya mwaka 2015, kinaelekeza ya kuwa kutakuwa na ada ya upangaji na uthamini wa madini vito itakayolipwa serikalini na mmiliki wa leseni ya uchimbaji wa madini vito wakati wa kuuza madini aliyozalisha au kununua kwa viwango vitakavyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali na Waziri.

Uchambuzi wa shughuli za Tume ya Madini umebaini ya kuwa, ada hii hailipishwi kutokana na Waziri husika kutochapisha viwango vya ulipaji wa ada kwa ilivyotakiwa na sheria.

Serikali, kupitia Wizara ya Madini, inashauriwa kutunga na kuchapisha ada elekezi za upangaji na uthamini wa madini ya vito.

7.2.3 Ufanisi hasi wa utendaji wa Kampuni ya madini bati ya Kyera.

Kampuni ya madini bati ya Kyerwa zamani STAMITRADE ilianzishwa tarehe 6 Februari 2014 kama kampuni huru inayomilikiwa na shirika la madini la taifa.

Upembuzi wangu wa utendaji wa kampuni umebaini mapungufu yafuatayo:

Uchambuzi na utambuzi wa viwango vya madini bati wakati wa ununuzi unafanyika kwa utambuzi wa macho na ukaguzi usiohusu mashine au teknolojia ya uchambuzi, Njia hii inapendelekea kufanyika makosa yatokanayo na utashi wa kibinadamu. Kwa mfano, mnamo mwezi Oktoba 2016 wakati wanauza madini bati kwa kampuni ya African Top Minerals, kampuni ya Kyera ilibainisha kununua madini bati yaliyosafishwa tani 26.739 lakini wakati wa kufanya mauzo, baada ya madini bati hayo kufanyiwa uchambuzi na uthamini ilibanika ya kuwa madini hayo yalikuwa na uzito wa tani 18.0652 tu. Hii inamaanisha kuwa kiasi cha tani

8.3138 ilikuwa ni madini bati yaliyochini ya viwango. Hii ilipelekea kampuni kupata hasara ya TZS 150 milioni kwa kutumia bei ya TZS 18,000 kwa kilo moja ya madini bati.

Kampuni inashindwa kufikia moja kwa moja soko la dunia la madini bati kwa kuwa nchi ya Tanzania haijasajiliwa katika shirikisho la International Tin Research Institute (ITRI) ambalo linasimamia uuzwaji, uwazi, na usafirishaji katika uchimbaji na usimamizi wa biashara ya madini bati katika nchi za Maziwa Makuu barani Afrika.

Mauzo ya madini bati katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2017 yalifanyika kwa upimaji kilo za makinikia ya madini bati badala ya viwango vya madini bati zinavyopatikana kwenye kilo za makinikia ya madini bati ambayo ndiyo sera ya mauzo ya kampuni na njia bora inayotumika duniani. Kwa kuongezea, bei zilizokuwa zinatumiwa na kampuni hazikuwa zinafanyiwa marejeo ili kuweza kuendana na ongezeko la thamani ya madini bati baada ya kuoshwa na kuwa na viwango bora. Pia bei hizo hazikuwa zinaendana na bei za dunia kama zinavyoonyeshwa kwenye soko kuu la vyuma mjini London-Uingereza. Kwa Mfano, mwezi Oktoba 2016 bei ya kampuni ya mauzo ya madini bati ilikuwa Shilingi 18,000 kwa kilo wakati bei ya manunuzi ilikuwa Shilingi 19,000 kwa kilo.

Kampuni inanunua madini bati toka kwa wachimbaji wadogo na madalali kwa kutumia fedha taslimu. Kwa kila mwezi, Kampuni inatoa wastani wa Shilingi milioni 40 fedha taslimu kufanikisha manunuzi hayo. Aidha, manunuzi ya madini bati toka kwa wachimbaji wadogo na madalali yalikuwa hayaambatishwi na vocha ya uuzwaji madini ambayo ndiyo stakabadhi inayotumiwa na serikali kudhibiti na kutambuwa uuzwaji wa madini bati nchi. Kwa ziada, pia hapakua na uangalizi na udhibiti wa manunuzi ya madini bati, mtumishi moja alikuwa anasimamia zoezi la ununuzi wa madini bati kuanzia upimaji wa uzito wa madini bati mpaka

kuja kufanya malipo kwa muuzaji bila ya kukaguliwa na afisa wa pili.

Shirika la Madini la Taifa linashauriwa:

- a) Kuchunguza na kuwachukulia hatua za kinidhamu maofisa walioisababishia kampuni hasara ya Shilingi milioni 150,
- b) Kutumia teknolojia na vifaa vya kisasa wakati wa kufanya uchambuzi na uthamini wa madini bati,
- c) Kujisajili na kupata uanachama wa taasisi ya kimataifa ya utafiti wa madini bati ili kuogeza wigo wa soko, na
- d) Kuboresha udhibiti wa uuzwaji na manunuzi ya madini bati.

7.2.4 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

(i) Kukosekana kwa mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za bei linganifu katika sekta ya madini

Kifungu namba 33 cha Sheria ya Kodi ya mapato ya mwaka 2004 kinahitaji mipango au makubaliano kati ya taasisi mbili zenye mahusiano ya umiliki kuchambua na kutenga kiasi ambacho kinatakiwa kujumuishwa au kupunguzwa wakati wa kukokotoa mapato ambayo yatatumika kwenye kukadiria kodi ya taasisi husika ambayo ingetozwa kama miamala baina ya taasisi hizo ilifanyika kwa kuzingatia usawa na bei elekezi.

Ukaguzi wangu umebaini kuwa, TRA haina mfumo wa kimtandao unaoiwezesha kuweza kufanya mlinganisho wa gharama ili kutambua kama gharama za miamala kati ya taasisi zenye ubia zina usawa wa kutumia bei elekezi au kamahazikuhusisha uratibu wa bei kwa nia ovyo ya kuhamisha faida au kuongeza gharama uzalishaji.

Kutokuwapo kwa mfumo wa kimtandao wa kulinganisha bei na gharama kinaipunguzia uwezo TRA kutambua kama bei za

miamala baina ya taasisi zenye ubia hazikuratibiwa kwa nia ya kupunguza faida ya taasisi au kuongeza gharama za uendeshaji.

Mamlaka ya mapato inashauriwa kutenga bajeti ya ununuzi wa mfumo wa kimtandao utakaoiwezesha kuweza kuchambua na kufanya mlinganisho wa bei na gharama za kampuni ya madini kutambua kama bei husika zilikuwa zenye usawa unaoendana na bei elekezi bila ya kuwapo kwa uratibu wa bei baina ya makampuni ya ubia kwa nia ya kufanya udanganyifu wa bei, au kuhamisha faida.

(ii) Mamlaka ya Mapato (TRA) kutokuwa na miongozo ya utekelezaji wa taarifa za ukaguzi wa kodi toka kwa Tume ya Madini.

Kifungu namba 22 cha Sheria ya Madini 2010 kama ilivyorekebisha na Sheria za marekebisho za mwaka 2017 inaelekeza kuwa miongoni mwa majukumu ya Tume ya Madini ni kufanya ukaguzi wa mitaji ya uwekezaji na utendaji wa migodi mikubwa na ya kiwango cha kati kwa madhumuni ya kukusanya taarifa za kikodi na kuziwasilisha kwa mamlaka ya kodi na taasisi nyingine husika kwa utekelezaji.

Kabla ya kuanzishwa kwa Tume ya Madini, Wakala wa Ukaguzi wa Mmadini Tanzania ilitoa ripoti kwenye migodi ya Geita (2014 na 2015), Bulyanhulu (2013 na 2014) na North Mara (2013), ingawaje uchambuzi wangu umebaini kuwa ripoti hizi hazikufanyiwa kazi na kuwekwa kwenye mipango ya Mamlaka ya Mapato.

Ufutiliaji hafifu wa ripoti za migodi zinazotolewa na Tume ya Madini unadhoofisha jitihada za serikali za kukuza ukusanyaji wa mapato na mchango sekta ya madini katika nchi.

Mamlaka ya mapato, kwa kushirikiana na Tume ya Madini, zinashauriwa kutunga miongozo itakayozisaidia katika kutekeleza majukumu yao juu ya utekelezaji wa ripoti za Tume.

(iii) Kutokuwapo kwa vifungu vya kodi katika sheria ya mapato vinavyoratibu kodi ya ziada

Uchambuzi wangu ibara ya 15 na 17 ya mkataba wa uzalishaji gesi (MPSA) wa mwaka 2008 na 2013 unaonyesha ya kuwa kodi ya ziada itakuwa inakotolewa kwa kila mwaka na itakuwa inatofautiana kutokana na kiwango cha faida atakachopata mkandarasi wa kampuni wa gesi na mafuta toka kwenye taaarifa ya mtiririko wa fedha ya eneo la uchimbaji. Kwa kuongeza, MPSA zimeelezea kuwa kodi italipwa kwa muda na utaratibu utakaopangwa na kamishina wa mamlaka ya mapato.

Kodi ya ziada ni kodi inayolipishwa kwenye baadhi ya sekta ambazo kutokana na mabadiliko ya hali ya kiuchumi, makampuni yanapata nafasi ya kupata faida maradufu zaidi ya faida ya kawaida inayopatikana kwenye sekta husika. Ili kuwa na usawa kwenye ugawo wa faida na kodi kwa Serikali, kodi ya ziada inatakiwa kulipishwa kwa makampuni ya kimataifa ya mafuta.

Ripoti yangu ya mwaka uliopita ilionyesha kuwa kuna baadhi ya makampuni ya gesi na mafuta yalishaanza kutambua kuwapo kwakodi hii kwenye vitabu vyao vya uhasibu, ila hakukuwa na mfumo wala muongozo wowote toka kwa Mamlaka ya Mapato wa jinsi ya kulipia kodi hii.

Mapitio ya ziada ya Sheria ya Mapato ya mwaka 2004 kama ilivyorekebisha na Sheria za Fedha za mwaka 2016 na 2017, hakuna kifungu kinachoelekeza ulipwaji wa kodi ya ziada kwa makampuni ya madini, gesi na mafuta.

Serikali inashauriwa, kurekebisha Sheria ya Mapato kwa kutunga vifungu vitakavyoiwezesha Mamlaka ya koMi kukusanya kodi ya ziada.

(iv) Kaguzi chache za Upangaji wa bei baina ya Makampuni bia katika Sekta ya Madini na Mafuta

Kifungu namba 33 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kinahitaji mipango au makubaliano kati ya taasisi mbili zenye mahusiano ya umiliki kuchambua na kutenga kiasi ambacho kinatakiwa kujumuishwa au kupunguzwa wakati wa kukokotoa mapato ambayo yatatumika kwenye kukadiria kodi ya taasisi husika ambayo ingetozwa kama miamala/mipango baina ya taasisi hizo ilifanyika kwa kuzingatia usawa na bei elekezi.

Serikali imetunga kanuni zinazosimamia upangaji wa bei kwa makampuni yenye ubia za mwaka 2014 ili kuratibu mipango ya upangaji wa bei baina ya makampuni yenye ubia kadhalika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeanzisha kitengo kinachosimamia utozaji wa kodi kwa shughuli za kimataifa kilichopewa majukumu ya kufanya ukaguzi na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania juu ya mambo yote ambayo yanahusiana na upangaji wa bei kwa makampuni yenye ubia.

Uchambuzi wangu wa kaguzi zilizofanywa na kitengoumebaini kuwa, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2014 mpaka mwezi Julai 2017, kitengo kimeweza kufanya kaguzi 28 pekee ambapo kati yake ni kaguzi 3 pekee ((PETROBRAS, SONGAS LTD na TANZANITE ONE MINING) ndizo zilikua zinahusiana na sekta ya madini na mafuta.

Ongezeko la usimamizi na ukaguzi katika upangaji wa bei baina ya makampuni wabia litapelekea kuongezeka kwa mapato ya serikalini na kuzuia uhamishwaji wa faida kati ya makampuni kupitia upangaji wa bei baina ya makampuni yenye uhusiano.

Mamlaka ya Mapato Tanzania inashauriwa kuongeza kaguzi zinazohusiana na upangaji wa bei katika sekta ya madini na mafuta kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba bei zilizopangwa baina ya kampuni tajwa yalikuwa na usawa na kutumia bei elekezi.

7.3 Taarifa ya Ukaguzi wa Sekta ya Gesi na Mafuta

7.3.1 Ucheleweshwaji wa kuendeleza vitalu Namba 4/1B/1C

Iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ilitenga vitalu namba 4/1B na 4/1C kwa ajili ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa kupitia tangazo la serikali namba 184 la tarehe 20 Mei 2016.

Shirika la mafuta liliwasilisha mpango mkakati wake pamoja na gharama za utekelezaji wa kufanya utafiti wa mafuta uliogawanyika katika sehemu mbili zenye utelezaji wa miaka 2 kwa kila sehemu zenye gharama za dola za kimarekani milioni 50 kwa kila kitalu cha mafuta.

Uchambuzi wangu juu ya maendeleo ya vitalu hivi umebaini ya kuwa, Wizara haijaipa TPDC leseni ya utafutaji wa mafuta katika vitalu hivi, pia hakuna fedha iliyotolewa kufanikisha utekelezaji wa mradi huu.

Ucheleweshwaji wa shughuli za utafiti wa mafuta katika vitalu hivi unachelewesha serikali kuweza kuvumbua maliasili itakayoinufaisha serikali kwa ujumla, pia kutotolewa kwa leseni ya utafiti kunalizuia Shirika la Mafuta kuingia kwenye mikataba na wawekezaji wenye nia ya kuendeleza vitalu.

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Wizara ya Nishati wanashauriwa:

- a) Kutunga na kusaini makubaliano yatakayoongoza shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta katika vitalu husika,
- b) Kuhakikisha leseni ya utafutaji wa mafuta inatolewa kwa Shirika la Mafuta ili kufanikisha uendelevu wa vitalu, na
- c) Kuwasiliana na Serikali pamoja na washirika wengine kuweza kupata fedha za kuendesha na kufanikisha mradi husika.

7.3.2 Kutokuendelezwa kwa Vitalu saba vya Mafuta kwenye kina kirefu cha Ziwa na Kitalu Kimoja katika Ziwa Tanganyika.

Mnamo mwezi wa Oktoba 2013, wakati wa Utoaji wa leseni za utafutaji na uchimbaji mafuta baharini (4th Tanzania Offshore Licensing Round), Serikali ilikaribisha zabuni za uendeleu wa vitalu 7 vya mafuta katika vina virefu vya maziwa na kitalu kimoja katika ziwa la Tanganyika kwa kutumia vifungu vya mfano wa mkataba wa uzalishaji gesi (MPSA) wa mwaka 2013 kwa ajili wa utafiti na uchimbaji wa mafuta. Makampuni mawili, China National Offshore Oil Corporation (CNOOC) na Ras Al Khaimah Gas LLC (RAKGAS) yalishinda zabuni na kukaribishwa kufanya mazungumzo ya mkataba.

Mazungumzo ya kimkataba yaliyofanyika mwezi Agosti 2015 yaliichagua kampuni ya RAKGAS kuendeleza kitalu kilichopo ziwa Tanganyika lakini kabla ya kukabidhiwa kitalu kwa ajili ya uendelezaji, kampuni ya RAKGAS ilijitoa kwenye makubaliano wakati makubaliano na kampuni ya CNOOC ya China iliyochaguliwa kuendelezaji kitalu namba 4/3A yalishindwa kufikiwa. Uchambuzi uliofanyika ulibaini kuwa, wawekezaji wengi wamekwazwa na vifungu vya mfano wa mkataba wa uzalishaji gesi (MPSA) wa mwaka 2013 vilivyotumika katika kuingia kwenye mikataba ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta katika vitalu tajwa.

Zaidi ya hayo, hapakuwa na tangazo la ziada lililofanyika tangu zabuni za awali ilipotangazwa, licha ya ukweli kuwamradi huu kuwa na matumaini makubwa ya upatikanaji wa mafuta katika vitalu tajwa.

Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania linashauriwa kuelekeza Serikali umuhimu wa kupitia vifungu vya mfano wa mkataba wa uzalishaji gesi (MPSA) wa mwaka 2013 ili kuhamasisha uwekezaji katika vitalu.

7.3.3 Kupingwa kwa kodi ya Ongezo la Mtaji Shilingi Trilioni 1.14 na Kampuni ya British Group Plc

Kifungu namba 51(5) cha Sheria ya Uongozi wa Kodi ya mwaka 2015 kinamtaka mtu yeyote ambaye hajakubaliana na maamuzi ya kikodi ya Kamishna Mkuu wa Kodi kuyapinga matokeo hayo kwa kutuma malalamiko hayo kwa Kamishna Mkuu wa Kodi ndani ya siku 30 tangu atarifiwe kuhusu maamuzi ya Kamishna Mkuu wa Kodi. Kwa kuongezea, kifungu namba 51(6) cha sheria hii kinaelezea kuwa mapingamizi ya kodi hayatapokelewa mpaka pale mlipa kodi atakapolipa kiasi cha kodi ambacho hakipingwi au moja ya tatu ya kodi iliyokadiriwa kimoja wapo kitachokua kikubwa.

Mnamo tarehe 27 Januari 2016 kampuni ya Royal Shell Plc ilinunua umiliki ya kampuni ya British Group Plc. Kutokana na mumala huu, Mamlaka ya Mapato ilipitia uuzwaji huu na mnamo tarehe 3 Mei 2016 ilitoza kampuni ya British Group Plc kodi ya ongezeko la mitaji kiasi cha Dola za Kimarekeni milioni 524.85 ambazo ni sawa na Shilingi trilioni 1.14.

Kampuni ya British Group Plc ilipinga kodi hii na kwenda kushtaki katika Bodi ya Usuluhishi wa Masuala ya Kikodi. Bodi ya usuluhishi ilielekeza kuwa Mamlaka ya Mapato iyasilikilize malalamiko ya mlipa kodi kulingana na Sheria za Kikodi, na mnamo tarehe 14 Juni 2017 Mamlaka ya Mapato ilitoa maamuzi yake ambayo hayakubadilisha kiasi cha kodi kilichotozwa hapo awali. Uamuzi huu ulipingwa tena na mlipa kodi.

Mamlaka ya Mapato imeshindwa kukusanya kiasi cha TZS 381 bilioni ikiwa ni sawa na moja ya tatu ya kodi ambayo imepingwa kama inavyotakiwa na sheria za kodi ya mapato.

Mamlaka ya Mapato inashauriwa kukusanya moja ya tatu ya kodi inayopingwa kiasi cha TZS 381 bilioni wakati ikisubiria maamuzi ya Bodi ya Usuluhishi wa Mambo ya Kikodi.

7.3.4 Tathimini wa Utendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

(i) Matumizi ya Mitambo ya Gesi chini ya Uwezo wake

Uchambuzi wangu wa mitambo ya utengenezaji wa gesi ya Madimba na Songosongo inavyomilikiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania umebaini kuwa, mitambo ina uwezo wa kutengeneza gesi kwa kiwango cha 350mmscfd lakini, kwa sasa mitambo hii inazalisha gesi kwa kiwango cha 85mmscfd tu ambacho ni sawa na asimili 24 ya uwezo wa uzalishaji wa mitambo. Matumizi ya mitambo ipo chini ya uwezo wake kwa asilimia 76 husababisha kushuka kwa faida itokanayo na uendeshaji wa mitambo hii kwa vile Shirika bado linahitajika kulipia gharama za kuendesha na kukarabati mitambo ambazo huwa hazibadiliki kutokana na uzalishaji.

Shirika la maendeleo ya mafuta Tanzania linashauriwa kutafuta wateja wapya watakaooongeza matumizi ya mitambo, ambapo itapelekea kuongezeka kwa faida ya jumla kwa shirika.

(ii) Umiliki wa Hisa za Ushiriki chini ya Asilimia 25

Kifungu namba 44(5) cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 kinaitaka Kampuni ya Taifa ya Mafuta ambayo pia ni Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuwa na umiliki usiopungua asilimia 25 ya haki za utafutaji wa petroli uliotolewa isipokuwa shirika la mafuta likiamua vinginevyo.

Ukaguziwangu wa baadhi ya stakhabathi za haki za utafutaji wa petroli zilizotolewa umebaini kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linaumiliki wa asilimia 20 katika visima vya gesi vya Mnazi Bay na haina umiliki kabisa katika visima vya gesi vya Songosongo na Kiliwani Kaskazini ambapo ni kinyume na matakwa ya kifungu namba 44(5) cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.

Serikali inashauriwa kutumia kifungu namba 4(1) cha Sheria ya Mikataba ya Maliasili na rasilimali ya mwaka 2017 kuchukua

umiliki katika visima vya gesi usiopungua asilimia 25 kama inavyotakiwa na sheria ya Petroli ya mwaka 2015.

(iii) Mrabaha kulipwa Kutoka kwenye Faida ya Serikali

Kifungu namba 113 cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 kinamtaka mmiliki wa leseni na mkandarasi kulipia serikalini mrabaha kwa asilimia 12.5 na 7.5 ya uzalishaji wa mafuta ghafi/gesi kabla ya kutoa kurejesha gharama za uzalishaji wa mafuta na gesi.

Hata hivyo, Mapitio ya kipengele XII cha mfano wa mkataba wa uzalishaji wa pamoja wa gesi wa Songosongo nimegundua kwamba aya 12.2(c) inaelekeza kwamba TPDC ndiyo itakayolipa mrabaha kwa Serikali kutokana na mgawo wake wa mapato unaotokana na faida kutoka kwenye eneo la uwekezaji. Hii ni kinyume na matakwa ya kifungu cha 113 cha sheria ya petroli ya mwaka 2015.

Kupitia mamlaka iliyopewa kwenye kifungu namba 4 cha Sheria ya Mikataba ya Maliasili na Rasilimali, Serikali inashuriwa kupitia na kubadilisha vifungu vya mkataba wa Songosongo ili kuwezesha mrabaha kuweza kulipwa na mmiliki wa leseni au mkandarasi kama ilivyoelekezwa kwenye sheria ya petroli ya mwaka 2015.

(iv) Kutokufanyika kwa Mapitio ya bei ya Gesi inayolindwa na Mkataba

Kulingana na kifungu namba 3.1(c) cha mkataba kati ya Serikali ya Tanzania, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, na Kampuni za Songas na PAET bei ya gesi ambayo inalindwa na mkataba itakuwa inapitiwa mara kwa mara kulingana na kanuni na mamlaka zinazosimamia bei za gesi na mafuta.

Mapitio yangu ya stakabadhi za malipo za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania umebaini ya kuwa, gesi inayolindwa na mkataba kutoka katika visima vya Songosongo inauzwa dolla za kimarekani 0.69 kwa mmBTU wakati ile inayotoka katika visima vya Mnazi

Bay inauzwa Dola za Kimarekani 3. Kwa kuongezea, mapitio ya bei hayawahi kufanyika kinyume na makubaliano ya mkataba.

Mmlaka inayosimamia upangaji wa bei ya petroli inashauriwa kuhakikisha bei ya gesi inapitiwa mara kwa mara kama inavyohitajika kwenye makubaliano ya uzalishaji.

(v) Kutokulipwa kwa Ankara za Mauzo ya Gesi Asilia kutoka TANESCO Kwenda TPDC kiasi cha Shilingi za Billioni 248

Mnamo Septemba 2015, Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (TPDC) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) walisainiana mkataba wa mauziano ya gesi ambapo, TPDC ilitakiwa kuuza gesi asilia kwa TANESCO kwa ajili ya kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi, Ubungo II na Symbion Power Plants.

Nimegundua kuwa, kati ya mwezi wa Septemba na Desemba 2017 jumla ya madai ya kila mwezi yalikuwa na gharama ya Shilingi bilioni 567.51, kutoka TPDC kwenda TANESCO kwa ajili ya gesi asili iliyopelekwa na kutumika na TANESCO.

Mpaka kufikia mwezi Disemba 2017, TANESCO ilikuwa imeshalipa kiasi cha Shilingi bilioni 318.90 ambayo ni sawa na asilimia 56 ya deni lote wanalodaiwa, na kubakiza deni la Shilingi bilioni 248.61.

Hali ya TANESCO kuchelewa kulipa TPDC, inasababisha sintofahamu kwenye ulipaji wa mkopo kutoka benki ya Exim ya China. Kuchelewa huku kwa malipo kunaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama zaidi kupitia riba ambayo itatakiwa kulipwa na TPDC. Kwa kuongezea, kushindwa kulipa mkopo kutasababisha uhamisho wa haki za TPDC kwenda kwa benki ya Exim-China kama ilivyoadhinishwa kwenye kipengele namba 2 cha mkataba wa makubaliano ya uuzwaji wa gesi kati ya TPDC na Benki ya Exim-China.

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati inashauriwa kuisadia TANESCO kuweza kufanikisha kulipa deni lake wanalodaiwa na TPDC ili kuliokoa shirika lisiweze kupokonya haki zake na benki ya Exim-China.

7.3.5 Uthamini wa Ununuzi wa Umiliki kwa asilimia 40 kutoka PAET kwenda Swala Oil & Gas Tanzania

(i) Ununuzi wa umiliki wa Pan African Energy Tanzania Ltd kwa asilimia 40 kwenda Swala Oil & Gas (Tanzania)

Pan African Energy Tanzania LTD (PAET) ni kampuni inayojishughulisha na utafutaji na uuzwaji wa gesi asilia kwa ajili ya uzalishaji nishati. Kampuni hii inamilikiwa kwa asilimia 100 na kampuni ya Pan African Energy Corporation (PAE) ambayo pia inamilikiwa jumla na kampuni ya Orca Exploration Group Inc (Orca).

Kampuni ya Orca Exploration Group ina mpango wa kuuza asilimia 40 ya hisa za kampuni Pan African Energy Tanzania LTD (PAET) kwenda kwa kampuni ya Swala Oil & Gas (Tanzania) kwa malipo ya Dola za Kimarekani milioni 130. Hata hivyo Serikali, kupitia barua ya tarehe 5 Januari 2018 toka Wizara ya Madini yenye kumbukumbu namba CBC105/294/01/50 iliamrisha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kusimamisha mchakato wa mauziano hayo mpaka pale Serikali itakapopitia mchakato mzima wa mauziano.

Katikanipoti yangu wa mwaka jana, nilibainisha ya kuwa mkataba wa PAET-Songosongo ulikuwa na mapungufu yafuatayo:

- **Kupungua Kwa Gawio la Faida kwa Serikali kadri Uzalishaji Unavyoongezeka**

Kifungu namba 10.4 cha ibara ya X cha makubaliano ya mgawanyo wa uzalishaji wa Songosongo (PSA) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TPDC na Pan- African Energy Tanzania Limited (PAET) yamekuwa kinyume ambapo gawio la Serikali hupungua wakati

uzalishaji unapongezeka.

- **Kutokuanzishwa Kwa Mfuko wa Urejeshaji wa Eneo la Uchimbaji Katika Hali ya Awali.**

Ikiwa imepita miaka 16 tangu mkataba wa Songosongo kuingiwa na kuanza kutekelezwa na ikiwa imebakia miaka 9 kwa mkataba kumalizika mnamo tarehe 10 Oktoba 2025, bado Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na kampuni ya Pan- African Energy Tanzania Limited (PAET) hawajaanzisha mfuko maalumu kwa ajili ya kutelekeza na kurejeshwa eneo la uchimbaji wa gesi.

- **Makadirio ya Kodi ya Mapato Kupunguzwa Moja kwa Moja Kutoka Kwenye Ankara za Mauzo ya Gesi**

Kulingana na aya ya 12(a) ya mkataba wa ushirikiano wa uchimbaji gesi ya Songosongo, makadirio ya kodi ya mapato yanayolipwa na kampuni ya PAET yanapunguzwa kutoka kwenye ankara za mauzo ya gesi kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Hii inaonesha kuwa, PAET hailipi kodi kabisa kwa kuwa kodi inatolewa moja kwa moja toka kwenye mauzo.

- **Mkataba wa Songosongo Kuruhusu PAET Kurudishiwa Gharama za Masoko na Utafiti wa Masoko**

Aya ya 2.6 ibara ya II na III kifungu kidogo D (Taratibu za Kihasiibu) ya mkataba wa Songosongo umeorodhesha gharama ambazo zinastahili kurejeshwa bila kuomba idhini ya Shirika. Katika gharama zilizoidhinishwa ni za utafiti wa masoko na utafutaji masoko. Gharama hizi hazistahili kuingizwa kwenye gharama za utafutaji na uendelezaji wa gesi, hivyo kukubaliwa kurejeshwa kunapunguza mapato ya Serikali.

- **Kutosuluhishwa kwa Mgogoro wa Kimkataba Kuhusu Gharama Zinazopaswa Kurejeshwa Kiasi cha USD milioni 34.**

TPDC na PAET bado wana mgogoro kuhusu usahihi wa gharama zinazopaswa kurejeshwa kiasi cha dola za kimarekani milioni 34 tangu tarehe 30 Novemba 2012.

Kutokana na mapungufu yaliyopo katika mkataba wa PAET na Serikali kwenye uzalishaji wa gesi, Serikali inashauriwa kusimamia msimamo wake wa kusimamisha mauziano ya hisa kwenda kwa Swala Oil and Gas T Ltd mpaka hapo tofauti na mapungufu yaliyoonekana yatakapotatuliwa ikiwemo kupitia upya mkataba husika na kujadili juu ya vifungu vya mkataba visivyoinufaisha nchi kwa kutumia kifungu cha 4 cha Sheria ya Mikataba ya Maliasili na Rasilimali ya mwaka 2017.

HITIMISHO

Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa menejimenti za Mashirika ya Umma niliyoyakagua kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha ukaguzi huu na hivyo kuwezesha kuwasilisha ripoti hii kwa Mheshimiwa Rais, Dk. John Pombe Joseph Magufuli.

Ni matumaini yangu kuwa, kupitia ripoti hii, Serikali itachukua hatua za haraka na muhimu kuhusiana na masuala yaliyojitokeza.

Hili litawezekana iwapo Serikali itaimarisha nyenzo kama vile sera mpya, taratibu na mfumo wa sheria ili kuboresha utendaji wa Mashirika ya Umma kama ilivyoshauriwa katika ripoti hii.

Kwa kuongezea, ni matarajio yangu kuwa Ofisi yangu itawezeshwa kwa kupewa mamlaka ya kupata taarifa zote zinazohusiana na sekta ya Madini, Gesi na Mafuta kupitia kufanya marekebisho ya Sheria mama za Madini na Petroli.

Kuhusiana na mapendekezo yangu yaliyopita na yanayojirudia mara kwa mara, naisisitiza Serikali kuongeza juhudi katika utekelezaji wa mapendekezo hayo ili kuleta ufanisi katika Mashirika husika.

VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Mchanganuo wa Maoni ya Ukaguzi

Na.	Shirika/Taasisi ya Umma	Hati
1	Chuo Kikuu cha Ardhi	Hati Inayoridhisha
2	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha	Hati Inayoridhisha
3	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha	Hati Inayoridhisha
4	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati	Hati Inayoridhisha
5	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba	Hati Inayoridhisha
6	Taasisi ya Saratani (Ocean Road)	Hati Inayoridhisha
7	Mamlaka ya Udhhibiti wa Soko la Mtaji (CMSA)	Hati Inayoridhisha
8	Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CARMATEC)	Hati Inayoridhisha
9	Chuo cha kidiplomasia (CFR)	Hati Inayoridhisha
10	Chuo cha Wanyama Pori - Mweka	Hati Inayoridhisha
11	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB)	Hati Inayoridhisha
12	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam (DMI)	Hati Inayoridhisha
13	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	Hati Inayoridhisha
14	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam	Hati Inayoridhisha
15	Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO)	Hati Inayoridhisha
16	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma	Hati Inayoridhisha
17	Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Maji (EWURA)	Hati Inayoridhisha
18	Udhhibiti wa Nishati na Maji (EWURA CCC)	Hati Inayoridhisha
19	Mamlaka ya Kanda Maalum ya kuzalisha Bidhaa za Nje (EPZA)	Hati Inayoridhisha
20	Tume ya Ushindani (FCC)	Hati Inayoridhisha
21	Baraza la Ushindani (FCT)	Hati Inayoridhisha
22	Bodi ya Bahati Nasibu Tanzania	Hati Inayoridhisha
23	Mfuko wa mafao ya kustaafu wa GEPF	Hati Inayoridhisha
24	Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA)	Hati Inayoridhisha
25	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP)	Hati Inayoridhisha
26	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)	Hati Inayoridhisha
27	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa	Hati Inayoridhisha
28	Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)	Hati Inayoridhisha
29	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga	Hati Inayoridhisha
30	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama	Hati Inayoridhisha
31	Mfuko wa Pensheni wa LAPF	Hati Inayoridhisha
32	Mamlaka ya Maji Makambako	Hati Inayoridhisha
33	Mamlaka ya Maji Masasi nachingwea	Hati Inayoridhisha
34	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Hati Inayoridhisha
35	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya	Hati Inayoridhisha
36	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa	Hati Inayoridhisha

Na.	Shirika/Taasisi ya Umma	Hati
37	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro	Hati Inayoridhisha
38	Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi	Hati Inayoridhisha
39	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi	Hati Inayoridhisha
40	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara	Hati Inayoridhisha
41	Hospitali ya Taifa Muhimbili	Hati Inayoridhisha
42	Chuo cha Afya na Teknolojia Muhimbili	Hati Inayoridhisha
43	Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere	Hati Inayoridhisha
44	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza	Hati Inayoridhisha
45	Chuo cha Mzumbe	Hati Inayoridhisha
46	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)	Hati Inayoridhisha
47	Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)	Hati Inayoridhisha
48	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)	Hati Inayoridhisha
49	Shirika la Nyumba Tanzania	Hati Inayoridhisha
50	Chuo cha Usafirishaji (NIT)	Hati Inayoridhisha
51	kampuni ya Uwekezaji ya NHC na PPF	Hati Inayoridhisha
52	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Njombe	Hati Inayoridhisha
53	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT)	Hati Inayoridhisha
54	Mfuko wa Pesheni PPF	Hati Inayoridhisha
55	Bodi ya Wataalam wa Manunuzi na Ugavi (PSPTB)	Hati Inayoridhisha
56	Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA)	Hati Inayoridhisha
57	Mfuko wa Pesheni wa PSPF	Hati Inayoridhisha
58	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Same	Hati Inayoridhisha
59	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga	Hati Inayoridhisha
60	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida	Hati Inayoridhisha
61	Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA)	Hati Inayoridhisha
62	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira songea	Hati Inayoridhisha
63	Bodi ya Sukari Tanzania (TSB)	Hati Inayoridhisha
64	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira sumbawanga	Hati Inayoridhisha
65	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Mjini (SUMATRA)	Hati Inayoridhisha
66	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora	Hati Inayoridhisha
67	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga	Hati Inayoridhisha
68	Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)	Hati Inayoridhisha
69	Tume ya Nguvu za Nyuklia Tanzania (TAEC)	Hati Inayoridhisha
70	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	Hati Inayoridhisha
71	Shirika la Viwango Tanzania (TBS)	Hati Inayoridhisha
72	Baraza la Walaji la Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA-CC)	Hati Inayoridhisha
73	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)	Hati Inayoridhisha
74	Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)	Hati Inayoridhisha

Na.	Shirika/Taasisi ya Umma	Hati
75	Baraza la Walaji la Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA-CC)	Hati Inayoridhisha
76	Bodi ya Pamba Tanzania (TCB)	Hati Inayoridhisha
77	Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)	Hati Inayoridhisha
78	Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)	Hati Yenye Mashaka
79	Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)	Hati Inayoridhisha
80	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)	Hati Inayoridhisha
81	Benki ya Biashara ya TIB	Hati Inayoridhisha
82	Benki ya Rasilimali ya TIB	Hati Inayoridhisha
83	Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)	Hati Inayoridhisha
84	Benki ya Posta Tanzania (TPB)	Hati Inayoridhisha
85	Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)	Hati Inayoridhisha
86	Taasisi ya Utafiti wa Wanyama Pori (TAWIRI)	Hati Inayoridhisha
87	Benki ya Wanawake Tanzania (TWB)	Hati Inayoridhisha
88	Bodi ya Rufaa ya Mapato ya Kodi (TRAB)	Hati Inayoridhisha
89	Baraza la Usuluhishi la Mapato ya Kodi (TRAT)	Hati Inayoridhisha
90	Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM)	Hati Yenye Mashaka
91	Benki ya Maendeleo ya TIB	Hati Inayoridhisha
92	Shirika la Kuendeleza Miradi na Miundombinu UTT (UTT-PID)	Hati Inayoridhisha
93	Kampuni ya Nyumba za Watumishi (WHC)	Hati Inayoridhisha
94	Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)	Hati Yenye Mashaka
95	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Chalinze (CHAUWASA)	Hati Inayoridhisha
96	Kituo cha Elimu Kibaha (KEC)	Hati Inayoridhisha
97	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)	Hati Inayoridhisha
98	Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)	Hati Inayoridhisha
99	Mfuko wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo (SELF)	Hati Inayoridhisha
100	Chuo kikuu cha Dar es salaam (UDSM)	Hati Inayoridhisha
101	Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda (TIRDO);	Hati Inayoridhisha
102	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)	Hati Inayoridhisha
103	Mamlaka ya Uendelezaji wa Biashara Tanzania (TTDA)	Hati Inayoridhisha
104	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB)	Hati Inayoridhisha
105	Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)	Hati Yenye Mashaka

Kiambatisho Na. II: Mikopo Iliyotolewa Zaidi ya Kiasi Kilichopo kwenye Mkataba Shilingi Bilioni 6.18

Mkopo	Bei ya Mkataba TZS	Kiasi Kilichotolewa TZS	Tofauti TZS
Mkopo wa riba ya asilimia 15 kwa JWTZ kwa ajili ya manunuzi ya mashine na vifaa vya ujenzi	23,120,000,000	26,221,927,476	3,101,927,476
Nyumba	20,000,000,000	20,216,942,986	216,942,986
Mkopo wenye riba ya asilimia 15 kwa TAKUKURU kwa ajili ya makao makuu Kiwanja Na. 339, 340 na 341, Upanga, Dar es Salaam.	4,160,698,188	5,044,802,325	884,104,137
Kituo cha Biashara Ilala	13,409,792,000	15,390,653,189	1,980,861,189
TOTAL	60,690,490,188	66,874,325,976	6,183,835,788

Kiambatisho Na. III: Madeni ya Serikali Yaliyozidi Muda wa Kulipwa

Na.	Taasisi inayokopesha	Asili ya mkopo	Muhusika/mkopwaji	Kiasi 'Shilingi bilioni
1	PPF	Tofauti tofauti	Taasisi za serikali	264
2	PSPF	Tofauti tofauti	Taasisi za serikali	127.8
3	LAPF	Tofauti tofauti	Hazina	165.8
4	LAPF	Back purchases	Taasisi za serikali	75.34
5	GEPF	Tofauti tofauti	Taasisi za serikali	10.51
6	SOUWASA	BBili za maji	Taasisi za serikali	0.79
Jumla ya Deni				644.24

Kiambatisho Na. IV: Taasisi zisizo na Bodi

Na.	Taasisi/Shirika la Umma
1	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA)
2	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TSLB)
3	Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC)
4	Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)
5	Bohari Kuu ya Dawa (MSD)
6	Kampuni Hodhi ya Kusimamia Ralisilimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)
7	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA)
8	Mamlaka ya Udhhibiti ya Hifadhi za Jamii (SSRA)
9	Bodi ya Chai Tanzania (TBT)
10	Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)
11	Baraza la Sanaa la Taifa (NAC)
12	Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)
13	Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB)
14	Wakala wa Uendelezaji wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)
15	Shirika Tija la Taifa (NIP)
16	Chuo cha Ufundi Arusha (ATC)
17	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)
18	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)
19	Bodi ya Bima ya Amana (DIB)
20	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)

Kiambatisho Na. V: Madeni ya Muda Mrefu

Na.	Taasisi	Kiasi (Shilingi Bilioni)
1	MWAUWASA	5.99
2	EWURA	3.53
3	NHC	18.00
4	N.I.C	6.70
5	T.C. U	1.87
6	UTT Project and Infrastructure Development Plc.	1.09
7	Mbeya Urban Water Sanitation Authority	0.20
8	Moshi Urban Water Supply and sanitation Authority	1.48
9	STAMICO	0.67

Na.	Taasisi	Kiasi (Shilingi Bilioni)
10	National Institute of Transport	0.71
11	EPZA	0.30
12	Mwalimu Nyerere Memorial Academy	0.91
	Jumla	41.45

Kiambatisho Na. VI: Ucheleweshaji na Kutopelekwa kwa Makato ya Kodi

Shirika	Kodi (W/Tax)	Kodi ya Mafunzo na Maendeleo (SDL)	Kodi kadri ya kipato chako (PAYE)	Pensh eni	Makat o ya fidia	Jumla Kwa bilioni
Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Songea	0.00	0.00	0.10	0.12	0.00	0.22
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	0.00	0.00	0.05	0.00	0.00	0.05
Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete	0.00	0.00	0.00	0.53	0.00	0.53
Kituo cha Uwekezaji Tanzania	0.01	0.00	0.13	0.06	0.00	0.20
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	0.00	1.24	5.36	0.00	0.41	7.01
Shirika la Maji safi na Maji Taka Dar es Salaam	0.00	0.69	0.00	0.00	0.04	0.73
Shirika la Posta Tanzania	0.00	29		2.70	0.00	31.70
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania	0.05	0.00	0.00	0.00	0.00	0.05
Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Songea		1.51				1.51
Jumla						42.00

Kiambatisho Na. VII: Hali ya Matumizi ya Viududu katika Halmashauri mbalimbali

HALMASHAURI	VILIVYOPOKEL EWA (LITA)	VILIVYOTUM IKA (LITA)	VILIVYOB AKI (LITA)
Halmashauri ya Jiji la Arusha	620	180	440
Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	440	140	300
Halmashauri ya Wilaya ya Bahi	4,420	0	4,420
Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	1,740	1,740	0
Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba	840	540	300
Halmashauri ya Wilaya ya Bunda	680	0	680
Halmashauri ya Mji wa Bunda	660	0	660
Halmashauri ya Wilaya ya Butiama	960	0	960
Halmashauri ya Wilaya ya Chato	1,320	1,320	0
Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma	20,480	1,280	19,200
Halmashauri ya Wilaya ya Gairo	460	380	80
Halmashauri ya Wilaya ya Geita	2,100	2,100	0
Halmashauri ya Wilaya ya Hai	200	0	200
Halmashauri ya Wilaya ya Handeni	320	0	320
Halmashauri ya Mji wa Handeni	320	0	320
Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi	1,680	0	1,680
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela	440	100	340
Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	560	560	0
Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	4,000	2,800	1,200
Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	1,260	220	1,040
Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu	960	635	325
Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe	2,400	0	2,400
Halmashauri ya Mji wa Korogwe	340	0	340
Halmashauri ya Wilaya ya Lindi	1,800	80	1,720
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi	1,080	260	820
Halmashauri ya Wilaya ya Longido	240	42	198
Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	1,140	0	1,140
Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	1,060	0	1,060
Halmashauri ya Mji wa Masasi	580	300	280
Halmashauri ya Wilaya ya Meru	280	200	80
Halmashauri ya Wilaya ya Misugwi	1,300	260	1,040
Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga	860	800	60
Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	480	120	360
Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	960	440	520
Halmashauri ya Wilaya ya Moshi	1,140	0	1,140
Halmashauri ya Manispaa ya Moshi	1,760	1,090	670

HALMASHAURI	VILIVYOPOKEL EWA (LITA)	VILIVYOTUM IKA (LITA)	VILIVYOB AKI (LITA)
Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	780	340	440
Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani	720	60	660
Halmashauri ya Wilaya ya Muheza	740	0	740
Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	2,580	740	1,840
Halmashauri ya Wilaya ya Musoma	680	680	0
Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero	1,020	500	520
Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga	1,220	0	1,220
Halmashauri ya Manispaa ya Mwaza	440	0	440
Halmashauri ya Manispaa ya Nanyumbu	680	480	200
Halmashauri ya Mji wa Newala	540	440	100
Halmashauri ya Wilaya ya Newala	800	580	220
Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji	680	680	0
Halmashauri ya Wilaya ya Same	400	380	20
Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	1,240	380	860
Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga	820	820	0
Halmashauri ya Wilaya ya Siha	200	0	200
Halmashauri ya Wilaya ya Singida	1,260	0	1,260
Halmashauri ya Manispaa ya Singida	1,080	20	1,060
Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba	1,440	1,000	440
Halmashauri ya Manispaa ya Tanga	9,880	0	9,880
Halmashauri ya Manispaa ya Temeke	5,000	2,922	2,078
Jumla Kuu	92,080	25,609	66,471